NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

BUNGE LA TANZANIA

_____

MAJADILIANO YA BUNGE

_____

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Thelathini na Nane – Tarehe 27 Mei, 2021

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaweza tukakaa.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mkutano wetu wa Tatu, leo ni Kikao cha thelathini na Nane, Katibu.

NDG. NENELWA MWIHAMBI – KATIBU WA BUNGE:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

MHE. JANEJELLY J. NTATE (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Janejelly Ntate, Katibu.

NDG. NENELWA MWIHAMBI – KATIBU WA BUNGE:

MASWALI KWA WAZIRI MKUU

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu karibu. Tunaanza kipindi cha maswali na Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mbunge wa Makete.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza swali ambalo limejikita kwenye usalama. Siku za karibuni hapa nchini kumekuwa na changamoto ya wimbi la ujambazi ambalo linaendelea hasahasa Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Mbeya, Mwanza na Arusha kitu ambacho kimekuwa kikihatarisha usalama wa wafanyabiashara wetu lakini mali pamoja na usalama wa wananchi wetu. Je, ipi ni kauli na maelekezo ya Serikali dhidi ya hivi vitendo viovu ambavyo vinaendelea kwenye Taifa letu?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhali.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mheshimiwa Sanga kwa swali hili zuri na muhimu kwa usalama wa nchi yetu. Serikali inao wajibu wa kulinda raia wake kwa usalama wao, mali zao lakini pia kuhakikisha kwamba wanaendesha shughuli zao za kila siku kwa amani na utulivu. Kazi hii inafanywa vizuri na vyombo vyetu vya dola lakini pia kazi hii mara kadhaa tumewaomba Watanzania kushiriki kwenye ulinzi wa nchi yetu pale kila Mtanzania anapopaswa kujilinda yeye mwenyewe, jamii

inayomzunguka na hatimaye jamii kubwa kwa ukubwa wake ili kujiridhisha kuwa usalama wa nchi unakuwa imara.

Mheshimiwa Spika, Jeshi letu la Polisi linafanya kazi nzuri sana na siku mbili/tatu hizi nimesikia kazi nzuri wameifanya Jijini Dar es Salaam na Watanzania wote wamesikia na wameona kazi ambayo wameifanya kudhibiti majambazi hawa. Nataka nikuhakikishie kwamba Serikali inaendelea na kazi hiyo ya kuhakikisha kwamba usalama wa raia na mali zao unaendelea. Watanzania wote wanajua kwamba hata Mheshimiwa Rais Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kupitia moja ya hotuba zake Kitaifa ameweza kuwaonya wale wote wanaofikiria kwamba huu ni wakati wa kufanya maovu nchini na amewataka wale ambao walikuwa wanafikiria kufanya hivyo waache mara moja. Anapoagiza haya maana yake anaagiza vyombo vya ulinzi na usalama kuchukua hatua kali dhidi ya wale wote ambao wanasababisha madhara ya usalama kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni jukumu letu sote kuhakikisha kuwa tunashiriki kikamilifu kwenye ulinzi wa nchi na kila Mtanzania pale anapohisi/anapoona kwamba kuna dalili za upotevu wa amani ni vyema kutoa taarifa kwenye vyombo vya sheria ili hatua kali ziweze kuchukuliwa. Kwa hiyo, bado tunaendelea na jukumu hilo la kulinda nchi, watu wake, mali zao na usalama wao ili nchi hii iendelee kuwa na tunu yake ya amani wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwasihi Watanzania sasa kuhakikisha kuwa tunatoa taarifa pale ambapo tunaona kwamba kuna tatizo linaloweza kutokea mahali ili majeshi yetu yafanye kazi inayokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwatwe.

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitenga mazao ya kimkakati na miongoni mwa mazao haya kahawa ni mojawapo. Hata hivyo, zao hili ambalo ni muhimu limekuwa na changamoto ya kukosa soko la uhakika, wananchi kucheleweshewa malipo pale wanapouza kahawa lakini pia wananchi kukosa pesa ya kuwasaidia pale wanapokuwa wanaelekea kuvuna. Nini kauli ya Serikali juu ya changamoto hizi ambazo zinamfanya mwananchi kukata tamaa juu ya zao hili muhimu? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu tafadhali

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu imedhamiria kusimamia kilimo kwa ujumla wake kwa mazao ya chakula pamoja na ya biashara. Haya mazao ya kibiashara usimamizi wake ni kuhakikisha kwamba kuanzia kilimo hiki kinapoanza kwa kuandaa shamba mpaka mavuno na hatimaye masoko yanaratibiwa vizuri. Tumejitahidi sana kufanya hivyo wakati wote ili kuhakikisha tunaleta tija kwa mkulima anayeshiriki kilimo kila siku kwenye zao ambalo linalimwa kwenye eneo lake kulingana na jiografia yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kahawa ni miongoni mwa mazao tena ni mazao ya kimkakati ambayo yanalimwa na jamii pana. Kwa hiyo, Serikali tumehakikisha kwamba zao hili nalo tunalisimamia.

Mheshimiwa Spika, zao hili kwenye masoko tunaliuza kwenye mfumo wa mnada kupitia Ushirika. Zao hili pia kwenye maeneo yote yanayolima ikiwemo na kule Kyerwa, Karagwe na maeneo mengine ya Mkoa wa Kagera lakini pia kule Ruvuma maeneo ya Mbinga, Kilimanjaro, Arusha tunaona Tarime kule Mkoani Mara zao hili linaleta manufaa sana kwa wakulima. Tunaendelea kuratibu masoko yake na kama ambavyo Wizara ya Kilimo ilivyomaliza bajeti yake juzi na kutoa maelezo bayana ya kuimarisha masoko, bado

nataka niwahakikishie wakulima wa kahawa tunaendelea kusimamia Ushirika, tutaendelea kusimamia masoko yake na pale ambapo masoko haya yanaleta tija tutahakikisha mkulima analipwa kwa wakati ili aweze kupata fedha ajipange tena kwa kilimo msimu ujao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Bilakwate kwa sababu hata wakati wa Bajeti ya Kilimo hapa alisimama kueleza haya na Wizara ikamjibu. Wizara ilipokuwa inamjibu yeye maana yake ilikuwa inajibu wananchi wanaolima kahawa wakiwemo wale wa kule Kyerwa. Kwa hiyo, niwahakikishie wakulima wote kwa mazao yote ikiwemo kahawa kwamba Serikali itaendelea kusimamia bei nzuri ya mazao haya lakini pia tutahakikisha baada ya kuuzwa fedha za mkulima zinalipwa katika kipindi kifupi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaendelea kuhuisha sheria na mifumo na zile Kanuni za kutoka siku ya mnada na kipindi cha kulipwa na hatimaye fedha kumfikia mkulima. Tukishafanikiwa hapo kila mmoja atafarijika kuendelea na kilimo hiki wakati wote.

Mheshimiwa Spika, nataka nisisitize tu kwamba pamoja na kuleta masoko yaliyo bora, malengo yetu hasa ni kuanzisha viwanda vya ndani ili zao hili liweze kuongezwa ubora na ubora ule ndio utakaoleta masoko. Pia zao hili mnada wake ulikuwa Moshi pekee kwa hiyo utamuona mwananchi wa kule Kyerwa, Mbinga hata waliopo kule Mbozi wanapeleka kahawa Moshi. Tumeamua sasa kuweka vituo vya karibu na wakulima hukohuko walipo ili minada hii ifanywe huko walipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumefungua kituo cha mnada wa kahawa Kagera, Makambako pamoja na Mbozi ili wale wanaolima mikoa ya jirani kwenye maeneo haya waende kwenye minada ile. Minada hii itakuwa ya wazi, mtu yeyote aliyepo ndani na nje ya nchi anakaribishwa kuja kununua. Kahawa ya Tanzania ni nzuri sana na ina thamani kubwa, kwa hiyo, tunawashawishi wanunuzi wote wa

kahawa kuitumia kahawa ya Tanzania ikiwemo kahawa inayolimwa kule Mkoani Kagera kwenye Wilaya ya Kyerwa na Karagwe kwa ujirani.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje, uliza swali lako.

MHE. NUSRAT S. HANJE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nimuulize Waziri Mkuu swali.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa kuna ugumu wa kupata ajira kwa vijana hasa waliomaliza darasa la saba kwenye taasisi za Serikali hata kama wamepata mafunzo katika fani mbalimbali kwenye vyuo vyetu vya ufundi hata vinavyotambuliwa na Serikali kwa kigezo cha cheti cha *form four*. Vyuo hivi vinatambuliwa na *NACTE* na Serikali kwa ujumla, je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba ina-*recognize* vijana wetu hawa wa *standard seven* ambao wanaulizwa kigezo cha *form four* wakati wamepatiwa mafunzo na wana uwezo wa kufanya kazi hizo? Serikali ina mkakati gani kuwatambua na kuhakikisha kwamba inawasaidia?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhali.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nusrat, Mbunge kutoka Mkoa wa Singida, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika mazingira ya kawaida ni kweli upo ugumu wa upatikanaji ajira na changamoto ya ajira iko duniani kote ikiwemo na hapa kwetu Tanzania lakini kila Serikali inaweka utaratibu mzuri wa kukabiliana na changamoto hii. Kwetu nchini Tanzania kupitia Serikali yetu inayoongozwa na Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu

Hassan imeendeleza mkakati wa Awamu ya Tano wa kupanua wigo ambao unaruhusu Watanzania kupata ajira bila ya kuangalia elimu yao; muhimu ni ujuzi na hasa anapozungumzia wale wamepata ujuzi kwenye vyetu vya ufundi vinavyotambulika na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mkakati wa ujenzi wa viwanda ndiyo jibu sahihi la kupunguza changamoto hii ya ajira kwa ngazi zote; uwe umemaliza darasa la saba, kidato cha nne, una *degree* hata ukiwa Profesa unaweza kufanya kazi kwenye viwanda kwa sababu kazi za kufanya zipo nyingi. Kwa hiyo, mkakati wetu wa ujenzi wa viwanda ni miongoni mwa njia moja muhimu ya kuwezesha kupata ajira watu wa kada zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbili; tunaendelea pia kuimarisha vyuo vyetu vinavyotoa ufundi stadi kwa sababu unaposoma kwenye vyuo vya ufundi stadi unapata ujuzi, ukipata ujuzi unaweza kujiajiri, unaweza pia ukaanzisha taasisi ukawaajiri wenzako na kuajirika pia kwenye sekta nyingine. Nataka niwaongezee kuwajulisha kwamba hata Ofisi ya Waziri Mkuu tunao mkakati wa kutoa mafunzo ya watu wa ngazi zote ili waweze kupata ujuzi huo wapate nafasi ya kujiajiri, kuajiriwa lakini pia na wale wanaopata ujuzi wakaanzisha kampuni yao na kuweza kuwaajiri wengine; kwa utaratibu huu tumefanikiwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika miaka mitatu iliyopita tuliwahi kukusanya vijana wa taaluma mbalimbali zaidi ya 35,000 tukawapeleka kwenye sekta mbalimbali; kilimo, madini lakini pia utoaji huduma na maeneo mengine, tumewapeleka *VETA* na Chuo cha Don Bosco, tumewapeleka kwenye mahoteli na maeneo mbalimbali ya utoaji huduma. Wanapokuwa kule asilimia 40 ya muda ni nadharia, asilimia 60 ya muda wao unatumika kwa ajili ya vitendo. Wanapokamilisha mafunzo hayo ya miezi sita wanakuwa tayari wana ujuzi na wengi wamepata mafanikio wameajiriwa na wengine wamejiajiri. Kwa hiyo, huo ndiyo mkakati ambao Serikali inautumia ili kuwezesha kila mmoja kwa ngazi yake kuweza kupata ajira.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, uliza swali lako.

MHE. HAWA M. CHAKOMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nimuulize Mheshimiwa Waziri Mkuu swali.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya mbegu ya *hybrid* kwa mazao kama mahindi, maharage, mchele na mengine mengi yamefanya mazao hayo kupoteza ladha lakini pia yanahitaji matumizi makubwa ya mbolea na viuatilifu. Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha inawekeza katika uzalishaji wa mbegu za asili kibiashara ili kuwawezesha wakulima kuzinunua lakini pia kufanya kilimo cha gharama nafuu na ku-*maintain* afya za Watanzania?

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhali.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Mchafu, Mbunge kutoka Mkoa wa Pwani, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli ameeleza kwamba yapo baadhi ya mazao ambayo tunatumia mbegu zile tunaita *hybrid,* zile mbegu ambazo zinakuzwa kwa kutumia madawa ambazo mazao yake yanaweza kuwa yanapoteza ladha kama ambavyo amesema. Hata hivyo, sisi ndani ya Serikali yetu kupitia Wizara ya Kilimo tumeweka Sera ya kuimarisha vitengo vyetu vinavyozalisha mbegu hizi ambazo ni za asili ambazo pia zinaweza zikazalisha kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunavyo vyuo vya utafiti vinaendelea na tafiti mbalimbali kwa mbegu hizi zinazozalishwa na kuona kuwa tunazalisha kwa kiasi kikubwa

tuweze kukipeleka kwa wananchi. Pia tumehakikisha kwamba kila tunapolima zao hilo ambalo limetokana na mbegu hizi ambazo tumezitafiti na tumezilima kutokana na uasili wetu, tunatenga kiasi cha mbegu ambacho kitasaidia kulima pia msimu ujao. Tumefanya hivyo kwenye zao la pamba, korosho na mazao ya mahindi na mpunga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tusingependa sana kuingiza mbegu hizi ambazo zimekuzwa kwa mfumo mwingine kwa sababu zina athari mbalimbali kama mahitaji ya mbolea na vitu vingine. Pia bado tunaendelea kufanya tafiti ya udongo tulio nao ili tuone udongo huo kama unaweza kuzalisha bila ya kutumia mbolea nyingi ili tuweze kuhakikisha kuwa uzalishaji wetu unapanda na unasaidia pia wakulima kupata tija kutokana na mazao wanayozalisha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hatua ambayo tunaichukua ni ile ya kuimarisha vyuo vya utafiti na kuongeza idadi ya wataalam, kuwapa fursa ya kufanya tafiti nyingi zaidi ili kupata mbegu. Tunayo taasisi ya mbegu ambayo pia nayo tunaitumia kuhakikisha kwamba inahakikisha tunapata mbegu za kutosha kwa kila zao linalolimwa hapa nchini na vituo hivi tumeviweka vingi kwa kanda ndani ya nchi ili kila kanda waweze kutafiti mbegu zinazolimwa kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, hizi ndiyo jitihada za Serikali ambazo tunazifanya na tutaendelea kufanya hilo ili Serikali na watu wake kwa maana ya Watanzania wapate manufaa kwa mbegu ambayo tunaizalisha sisi wenyewe na kusimamia kilimo kilicho bora kitakachovuna mazao mengi zaidi kama ambavyo mmejadili hapa kwenye Bajeti ya Wizara ya Kilimo. Kwa hiyo, huo ndiyo mkakati wetu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, uliza swali lako.

MHE. AIDA J. KHENAN: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi nami niweze kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa magonjwa sugu ambayo yanakuja kwa kasi ni pamoja na ugonjwa wa Kisukari. Madaktari bingwa wanapatikana kuanzia Hospitali za Mikoa, Kanda pamoja na Taifa kulingana na Sera yetu ya Afya; na wagonjwa hawa wa Kisukari wapo maeneo yote nchini:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujua, kwa kuwa wagonjwa hao wa vijijini, wengi wanashindwa kujua kwamba wana ugonjwa huo na hawana uwezo wa kutoka vijijini na kwenda mpaka Hospitali ya Mkoa; Serikali ina mkakati gani wa ziada kulingana na uzito wa tatizo hili hivi sasa kuweza kutoa huduma kwenye Hospitali za Wilaya pamoja na ngazi ya Kata?

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhali.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aida, Mbunge wa Nkasi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nami naungana naye kwamba tunayo magonjwa mengi nchini na ambayo tunaendelea kutafuta tiba sahihi ili Watanzania waendelee kuwa na afya njema zitakazowawezesha kufanya shughuli zao za maendeleo. Ugonjwa wa Kisukari ni miongoni mwa magonjwa ambayo kwa sasa yamesambaa sana nchini. Kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, ni kweli mengine yapo mpaka kwenye Vitongoji.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu imepanua wigo wa utoaji huduma za afya. Wigo huu umeanzia kwenye ngazi ya huko huko vijijini ambapo kuna zahanati. Vile vile katika ngazi ya Kata kama rufaa ya zahanati, tuna vituo vya afya

vinavyotoa huduma nzuri sana sasa hivi na tumejenga vituo vya afya vingi sana na tunaendelea kuvijenga. Pia tuna Hospitali za Wilaya, Mkoa na Rufaa mpaka zile za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ugonjwa wa Kisukari ni miongoni mwa magonjwa ambayo sasa tunatoa huduma mpaka kule kwenye zahanati. Kwenye Sera yetu imeelekeza zahanati na zenyewe zinunue madawa ya Kisukari ili wawe wanapata huduma kule. Pale ambapo anaweza kupimwa kwenye Hospitali ya Kata ambayo ipo kwenye maeneo hayo hayo, lakini upatikanaji wa dawa sasa unakwenda mpaka kwenye zahanati.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni jukumu la zahanati na nataka niagize Halmashauri ambazo ndiyo zinasimamia zahanati kuhakikisha kwamba wanaagiza dawa za Kisukari na ziende katika zahanati, kwenye kituo cha afya na kwenye kila ngazi ya kutoa huduma ili wale Watanzania walioko kule kijijini kabisa wapate huduma hiyo bila usumbufu wa kusafiri na kulipa nauli kwenda mahali pengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kupitia Mheshimiwa Aida, nikuhakikishie kwamba Serikali tumejipanga vizuri kwenye sekta ya utoaji huduma kwenye ngazi zote na bado tunaendelea na maboresho ya utoaji huduma kwa magonjwa yote. Mkakati wetu sasa ni kuhakikisha tunapunguza ukali wa magonjwa haya ili Watanzania wawe na afya njema na kila Mtanzania afanye kazi yake vizuri. Tunataka tuone tija ikipatikana kwa Watanzania kuwa na fya njema.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi ya kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na nitauliza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara 52A, Waziri Mkuu ametajwa

kuwa ndio mdhibiti, msimamiaji wa shughuli za Serikali za kila siku. Idara za Serikali Kuu na Serikali za Mitaa zimekuwa zikitekeleza mpango, wakati huo huo zinajifanyia tathmini zenyewe. Mfano, hai ni Wizara ya Fedha na Mipango imekuwa na kitengo cha tathmini ndani ya Idara ya Mipango.

Mheshimiwa Spika, sasa ili tuweze kuisimamia na kuidhibiti Serikali ipasavyo: Je, hatuoni haja ya kuwa na taasisi inayojitegemea ya kuisimamia Serikali na kufanya tathmini, kutunga mifumo ya ufuatiliaji na tathmini nchini?

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Bado nalitafakari hilo swali lako. Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu tafadhali. Kwa sababu taasisi inayojitegemea yaani ilikuwa inanipa taabu, kwa sababu mihimili si mitatu; sasa taasisi inayojitegemea itakayoisimamia Serikali, maana yake uunde mhimili wa nne au! Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu tafadhali.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Mbunge wa Mkoa wa Tanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo umepata shida kulielewa vizuri lakini niseme suala la tathmini na kuona mwelekeo wa kazi hiyo baada ya tathmini, mbali ya kwamba tumeipa Wizara ya Fedha na tukaiita Wizara ya Fedha na Mipango, lakini bado kila Wizara na kila sekta yenyewe tunaitengea bajeti hapa Bungeni kwa ajili ya kujiwekea mpango wake na kwenda kufanya tathmini yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanapokuja awamu ya pili, wanaweza kuweka mipango yao kutokana na tathmini waliyoifanya msimu uliopita. Kwa hiyo, hatujaishia Wizara ya Fedha na Mipango pekee, kila Wizara na kila sekta tumeipa mamlaka hiyo na utakuta pia hata kwenye maombi ya fedha ya bajeti ya miradi kuna *element* ya usimamizi.

Mheshimiwa Spika, tunaposema usimamizi, maana yake wanakwenda kuikagua mipango waliyoiweka katika kipindi cha mwaka na kuitekeleza ili kupata mwelekeo wa kama: Je, wamefanikiwa au hawajafanikiwa? Kama hawajafanikiwa inawawezesha kuweka mpango ule kuwa endelevu kwa msimu ujao. Kwa hiyo, hiyo tumeishusha mpaka Wizarani na kwenye sekta zetu, hatujaishia kwenye Wizara ya Fedha pekee.

Mheshimiwa Spika, nalichukua hilo, tutafanya mapitio huku kuona swali lako limetokana na nini? Je, kazi hiyo inafanywa na Wizara ya Fedha pekee? Hapo baadaye naweza kukupa majibu kwa namna nyingine ili uweze kupata uelewa mpana juu ya wajibu huo na kama huko kuna udhaifu, basi tutaangalia na kuweza kuboresha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla wake, suala la mipango na tathmini lipo katika kila sekta.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa *Engineer* unaweza ukaliandikia vizuri wazo lako hilo na ukali-*present* kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ufafanuzi zaidi na hata mimi ukanipa nakala ili tuweze kuona unafikiri nini?

Mheshimiwa Lemomo Steven Kiruswa.

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kumwuliza Waziri Mkuu swali.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo unafahamu mwaka huu nchi yetu ilivamiwa na nzige wa jangwani na ikanipelekea kupenda kufahamu mkakati wa Serikali katika kupambana au kudhibiti majanga yanayoweza kuathiri usalama wa chakula na mazao mengine ya kiuchumi katika nchi yetu ikiwemo mifugo. *(Makofi)*

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhali.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Kiruswa, Mbunge wa Longido, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anataka kujua mkakati wa Serikali wa namna ya kukabiliana na majanga. Amezungumzia chakula, lakini majanga yapo mengi. Mkakati huo upo ndani ya Serikali, pale ambapo Ofisi ya Waziri Mkuu kimeanzishwa Kitengo cha Maafa. Kitengo hiki ambacho kipo Ofisi ya Waziri Mkuu, tumekishusha pia kipo ngazi ya Mkoa, kiko Kamati ya Maafa; ngazi ya Wilaya tuna Kamati ya Maafa na pia ngazi ya Tarafa ina Kamati ya Maafa.

Mheshimiwa Spika, wajibu wetu ni kuhakikisha kwamba tunaepusha utokeaji wa majanga haya. Wakati mwingine huwezi kuyaepusha, ila ni kushughulikia majanga haya yanapojitokeza. Kwa hiyo, eneo la chakula nako pia linapotokea janga ambalo linapoteza vyakula ambavyo wananchi walikuwa wanavitegemea, nayo pia tunashughulikia.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Kiruswa atakumbuka siku za hivi karibuni kule Longido na maeneo mengine tulivamiwa na nzige, nami niliwenda pale, nikaenda mpaka Monduli kwenda kuona hali ya nzige. Ndiyo majanga hayo, wadudu wamekuja kutoka huko, wameruka wanakuja kushambulia chakula, lakini tulikabiliana nao kabla hawajaanza kushughulikia chakula chetu. Kwa hiyo, hiyo ndiyo njia mojawapo ambayo tunaitumia kukabiliana na majanga. Tulienda kuwakabili kabla hawajaanza kula chakula chetu na tukamudu kuwapoteza wote.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumeimarisha kitengo hiki kwa kuweka vifaa, watalaam na pia pamoja na utaalam huo tumeendelea kushusha elimu hii kwa wananchi wenyewe

waanze kushughulikia majanga pindi tu inapotokea majanga haya. Vile vitengo husika na vyenyewe vikikaa na kuratibu, vinashughulikia, lakini pale wanaposhindwa ngazi ya Kata, wanajulisha Wilaya, janga linapokuwa kubwa zaidi ya ngazi ya Wilaya wanajulisha Mkoa na Mkoa unaposhughulikia janga hilo likionekana limeshindikana, wanajulishwa Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Waziri Mkuu imekuwa ikifanya kazi hiyo vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwahakikishie Watanzania kuwa na uhakika na Serikali yao na kuiamini kwamba pia tumejipanga kwenye eneo hilo la kupambana na majanga mbalimbali ili kuhakikisha kwamba shughuli zote za Watanzania zinaenda vizuri na tuweze kuwa na akiba ya kutosha kwenye chakula na pia usalama wa maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Jesca Jonathani Msambatavangu, uliza swali lako.

MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. nashukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni tumekuwa na matatizo na vijana wetu wanaotoa huduma za usafiri mijini ikiwemo bajaji, bodaboda na daladala na hasa kutokana na kugombania ile miundombinu ya barabara. Nilichokiona sasa pale, pamoja hiyo *crisis* iliyopo ni kwamba kuna shida katika ku-*co-ordinate* namna ya kufanya kazi zetu kati ya Serikali za Mitaa na Wizara. Mzigo mkubwa...

SPIKA: Ukichukua muda mrefu, hutajikuta umeuliza swali.

MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Swali lenyewe lilivyo, kidogo linahitaji ufahamu. Samahani.

Mheshimiwa Spika, jinsi ilivyo sasa tunapata shida kwa sababu unakuta kwa mfano *TARURA* wapo TAMISEMI wakati Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ndiyo inayohusika na masuala ya ujenzi na miundombinu. Sasa unapofika wakati wa kufanya *co-ordination,* hawa Ujenzi wanakuwa kwa mfano wamejenga barabara kubwa imepita katikati ya mji, lakini *TARURA* hawakuwa *aware* kutengeneza *alternative way* kuhakikisha kwamba ule mzigo mzito wa *traffic* unaokuja kuingia kwenye ule mji unapitishwa kwenye barabara nyingine. Labda ni kwa sababu *TARURA* wapo chini ya Wizara nyingine. Haya yanatukuta pia kwenye masuala ya afya...

SPIKA: Swali lako ni nini sasa? Maana unachangia.

MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU: Mheshimiwa Spika, ahsante. Haya yanatukuta pia kwenye Wizara ya Afya kwenye kupandisha hospitali zetu kutoka vituo kwenda Hospitali za Wilaya.

Mheshimiwa Spika, sasa swali langu ni hivi: Je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kuona kwamba hizi Wizara zinachukua mzigo wake mzima; kwa mfano, Ujenzi na Uchukuzi wanaichukua na *TARURA,* Wizara ya Afya wanachukua na vituo vyake vya zahanati ili wanapotaka kupandisha madaraja washughulike wenyewe, kusiwe na *contradiction* na kuleta ugumu pale katika kurahisisha kazi hiyo? *(Makofi)*

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri Mkuu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Msambatavangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali lake limegusa mambo mengi; limegusa bodaboda, *TARURA, TANROAD* baadaye akahama tena akaja kwenye hospitali. Kwa hiyo, halina mwelekeo sahihi sana, lakini nataka niseme tu, ndani ya Serikali vyombo vyote ni vya Serikali na tumetoa miongozo ya kila mmoja. Miongozo hii tumejitahidi lazima izungumze

Pamoja. Ninaposema lazima miongozo izungumze, maana yake mipango ya *TANROADS* hata kama inaenda kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa, lazima pia kama ni ya kisheria iende i-*fit in;* iweze kuwa ndani ya mipango ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, wanapojenga barabara kukatiza humo, ni lazima barabara hiyo ijengwe kwa vipimo vilevile na Mamlaka ya Serikali za Mitaa ziruhusu hawa wapitishe barabara hiyo ili iweze kutumika na wote. Hata kwenye matumizi, kila mmoja atatumia na kama barabara hiyo inahitaji kuwa na njia za waenda kwa miguu, lazima ziende hivyo.

Mheshimiwa Spika, sasa tunapokuja kwenye Sekta ya Afya na yenyewe ambayo inaongozwa na Wizara ya Afya ambapo pia miundombinu inajengwa kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa, ni lazima Wizara hizi zizungumze, zihakikishe kwamba zinasimamia ujenzi wa miundombinu hiyo ili iweze kutoa huduma kwa Watanzania. Mwisho wa yote haya tunawahudumia hawa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, sasa tunapokuja hapa ndani ya Serikali, tunaweka sawia katika mambo ya kisheria ambapo kila mmoja atatumia miundombinu yote ya kila Wizara kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni zilizopo na zinazotuongoza. Kwa hiyo, niseme tu kwamba taasisi zote hizi pamoja na kwamba zipo huko kwenye mamlaka mbalimbali, lakini lazima ziwe zinazungumza lugha moja ili Mtanzania anapotumia asiwe na mgongano wa matumizi ya maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama nilivyosema swali lako lilijikita kwenye mambo mengi, lilikuwa pana, nilichofanya ni kuchukua maeneo hayo yote na kazi wanazozifanya kuwa zote ni za Serikali na kila mmoja anapotaka kutekeleza lazima kuwe na mawasiliano na taasisi nyingine ambayo ni ya Serikali. Kwa hiyo, Serikali lazima izungumze lugha moja na utoaji huduma lazima uende wa

aina moja ili wananchi waweze kupata huduma kwenye maeneo hayo, kila mmoja na eneo ambalo analolihitaji. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana. Muda wa Maswali kwa Waziri Mkuu umekwisha, tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Tulikuwa na waombaji 11, tumeweza kupata tisa; wawili imeshindikana, lakini mtaona kwamba tukienda kwenye swali moja kwa moja na kumpa nafasi Mheshimiwa Waziri Mkuu kujibu, tunaweza tukawapata wote bila wasiwasi. Naamini tunavyoendelea tutazidi kuzoea; na maswali mengine kwa kweli ni maswali ambayo inatakiwa upeleke Serikalini kwa *nature* yake lilivyo au upate dakika za kuchangia humu Bungeni ili Serikali ikusikie ukifafanua hoja yako vizuri zaidi kuliko kuweka katika swali hoja ambayo ni *a little bit complex,* linahitaji mtazamo wa peke yake. Tutazidi kujua ni jambo gani ulipeleke wapi na kwa wakati gani *as we go.*

Tunaendelea na maswali sasa. Katibu.

NDG. NENELWA MWIHAMBI – KATIBU WA BUNGE: Maswali ya Kawaida.

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Maswali ya kawaida, tunaanza na Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mbunge wa Moshi Mjini.

Na. 316

Halmashauri Nchini Kuwezesha Kina Baba

MHE. PRISCUS J. TARIMO aliuliza:-

Je, ni nini mpango wa Serikali kuwawezesha akina baba kiuchumi baada ya mpango wa Halmashauri wa

kuwawezesha akina mama, vijana na watu wenye ulemavu kuwa na mafanikio makubwa?

SPIKA: Majibu ya swali hili muhimu Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, Serikali ina mpango gani na wanaume wa nchi hii? Majibu tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mbunge wa Jimbo la Moshi Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeendelea kuwezesha wananchi kiuchumi kwa kutoa mikopo isiyo na riba kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Mikopo hiyo hutolewa kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 kifungu cha 37A inayoelekeza kutenga 10% ya mapato yanayokusanywa na Halmashauri kwa ajili ya mikopo ya 4% kwa wanawake, 4% kwa vijana na 2% kwa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, lengo la mikopo hii ni kusaidia makundi maalum katika jamii ambayo hayawezi kupata mikopo katika mabenki ya biashara na taasisi za fedha kwa sababu ya masharti magumu ikiwemo dhamana na riba kubwa. Hivyo, Serikali ilitoa kipaumbele kwa makundi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa kuwa wengi wao hawakopesheki katika mabenki na taasisi za fedha. Kwa sasa Serikali haikusudii kuanzisha mpango wa kuwawezesha wanaume au akina baba katika mikopo hii.

SPIKA: Mheshimiwa Tarimo, swali la nyongeza.

MHE. PRISCUS J. TARIMO: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Wizara; na kwa kuwa katika kundi la vijana wanakopeshwa vijana wa kiume na wa kike; na kutokana na Katiba yetu tunawatambua kwa umri wa miaka

18 mpaka 35; na kwa kuwa kuna wanaume wengi ambao ndiyo *bread winner* kwenye familia zao na ni wazalishaji kati ya miaka 36 – 45; na kwa sababu ni suala la kisera: Je, Serikali ipo tayari kuongeza umri angalau mpaka miaka 45 katika kundi hili la vijana ili wanaume waweze kufaidika na mikopo hiyo? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA – (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mbunge wa Moshi Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Serikali imeweka utaratibu huu wa mikopo kwa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu. Na katika kundi la vijana asilimia kubwa wanaonufaika na mikopo hii ni vijana wa kiume, lakini *definition* kwa maana ya tafsiri ya vijana kwa mujibu wa taratibu zetu ni wale wenye umri wa miaka 18 hadi 35. Kwa hivyo, kwa maana ya tafsiri hii ya kisheria Serikali bado haijaweka mpango wa kuongeza umri kwa sababu, lengo la mikopo hii ni kwa vijana na kwa maana ya tafsiri ya vijana ni chini ya miaka 35. Kwa hivyo tunachukua wazo lake, lakini kwa sasa sheria hii itaendelea kutekelezwa wakati tunafanya tathmini ya kuona uwezekano wa kuongeza eneo hilo.

SPIKA: Swali hili pamoja na kwamba, linawahusu wanaume, naona wanaume wote mmekaa chini. Basi kwa niaba ya wanaume Mheshimiwa Sophia Mwakagenda. *(Kicheko/Makofi)*

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ni kweli kwamba, katika halmashauri zetu kunatengwa fedha asilimia 10 kwa maana ya mbili, nne na nne kwa wanawake, lakini ufuatiliaji wa mkopo huu baada ya kupewa hivyo vikundi unakuwa ni mgumu sana kurudisha fedha kwenye halmashauri. Serikali ina mkakati gani wa kudai

madeni hayo ili fedha zirudi zikopeshe wanawake wengine kwa wakati unaofuata? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa, swali linahusu wanaume nao watapataje *access* ya hizo fedha?

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Spika, wanaume tunaomba wapate, lakini wanapokwenda kukopa huwa hawaelezi wake zao kama wamekwishakopa mkopo?

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Sophia. Jibu swali la msingi la Mheshimiwa Sophia, Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali. Nyie wanaume mtaachwa kila mahali, shauri yenu. *(Kicheko)*

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MITAA NA SERIKALI ZA MITAA – (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mpango huu wa kukopesha asilimia kumi kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu Serikali imeboresha utaratibu kupitia Sheria Na. 12 ya Mikopo kwa maana ya fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, kuhakikisha sasa siku za nyuma hatukuwa na asilimia kwa ajili ya ufuatiliaji wa marejesho ya mikopo hii. Kwa hivyo, ilikuwa ni ngumu kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii kufuatilia vikundi ambavyo vimekopeshwa kwa ajili ya kurejesha mikopo ile ili vikundi vingine vinufaike zaidi.

Mheshimiwa Spika, lakini kuanzia mwaka wa fedha ujao tumeweka kifungu cha ufuatiliaji katika vikundi hivyo kuwawezesha Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Maafisa Maendeleo ya Jamii kufuatilia vikundi vile pamoja na kuviwezesha kuhakikisha marejesho yanafanyika ipasavyo.

SPIKA: Tunaendelea na Mifugo na Uvuvi. Swali la Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, Mbunge wa Donge.

Na. 317

Wasafirishaji wa Dagaa Wanaotozwa Ushuru Zanzibar na Tunduma

MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH aliuliza:-

Je, Serikali itawasaidiaje Wafanyabiashara wa Dagaa wanaofuata Masoko nchi jirani ambao hutozwa ushuru Zanzibar na Tunduma kwa upande wa Tanzania Bara?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Mifugo na Uvuvi. Mheshimiwa Abdallah Ulega tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, Mbunge wa Donge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mazao ya uvuvi yanayosafirishwa kwenda nje ya nchi au yanayoingizwa nchini kwa upande wa Tanzania Bara yanalipishwa ushuru stahiki wa Serikali kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Uvuvi pamoja na Sheria nyingine za Nchi. Aidha, dagaa wanaotoka Zanzibar kwenda nchi jirani kupitia mpaka wa Tunduma hawalipishwi ushuru wowote katika Bandari ya Dar es Salaam na wanapokuwa wamefikishwa Tunduma kuelekea nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeweka Maafisa katika Bandari ya Dar es Salaam na maeneo ya mipakani kwa ajili ya kudhibiti utoroshaji na biashara haramu ya mazao ya uvuvi nchini. Hata hivyo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kuona umuhimu wa kulinda na kuendeleza rasilimali za uvuvi, itakutana na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili kuangalia namna bora ya kuweka mazingira rafiki kwa wafanyabiashara wa Tanzania Bara na Tanzania Visiwani katika kutatua changamoto zinazohusu masuala ya uvuvi.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge wa Donge uliza swali lako la nyongeza.

MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu yasiyoridhisha ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, Mheshimiwa Naibu Waziri ana mpango gani wa kuhakikisha kwamba, malalamiko haya ambayo yamedumu kwa kipindi kirefu sasa yanafikia mwisho?

Mheshimiwa Spika, swali namba mbili, je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza akaji-*committ* ni lini atakutana na wadau wa biashara ya dagaa wanaosafirisha kutoka Zanzibar kwenda Tunduma, ili kuhakikisha kwamba, anazungumza nao kuhusu hizi kadhia na kuzimaliza? Ahsante.

SPIKA: Majibu ya swali hilo muhimu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, naomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge wa Donge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, lini yatafika mwisho malalamiko haya ya wafanyabiashara wa dagaa. Nataka nimhakikishie kwamba, tumeweka utaratibu mzuri wa kufunga lakiri. Dagaa wanaotoka Zanzibar kupita katika Bandari ya Dar – es - Salaam wanapita katika utaratibu wa magunia yaliyo wazi. Tumeweka utaratibu ndani ya Serikali kwamba, wanapifika katika Bandari ya Dar - es - Salaam ni lazima tuyafunge lakiri ili kuthibitisha kama huu mzigo tayari ulishalipiwa ushuru kwa upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, nakiri yawezekana wako watumishi, baadhi, wasio waaminifu wanaoleta vitendo visivyokuwa vya kiungwana. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wafanyabiashara wote, tutashughulikia jambo hilo hatua kwa hatua na vyombo

vyetu vya dola vitakuwa vikifuatilia ili hao watumishi watakaokuwa wanabainika kufanya vitendo visivyokuwa vya kinidhamu tuwachukulie hatua na kuwarahisishia wafanyabiashara wetu kazi yao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu lini nitakwenda kukutana na wadau wetu. Nataka nimhakikishie kwamba, mara baada ya Bunge la Bajeti, ikimpendeza yeye na Wabunge wengine wanaoguswa na jambo hili niko tayari kuandaa mkutano huo kwa ajili ya kukamilisha zoezi hili. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Soud Mohamed Jumah, leo na kesho ni Mifugo na Uvuvi. Kama utahitaji muda wa kuchangia na kufafanua tatizo hili nakuhakikishia tutakupa nafasi hiyo kwa hiyo, badaye.

Tunahamia Mambo ya Ndani ya Nchi. Swali la Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka.

Na. 318

Kikosi Maalum Kupambana na Ubakaji na Ulawiti

MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA aliuliza:-

Jeshi la Polisi linao uwezo wa kukomesha tatizo sugu la ubakaji na ulawiti kwa watoto wadogo nchini:-

Je, ni kwa nini Serikali isiunde Kikosi Maalum cha kuwashughulikia watu wanaojihusisha na vitendo vya ubakaji na ulawiti?

SPIKA: Mheshimiwa Angelina hili swali, hili tatizo ni kubwa kiasi cha kuunda kikosi cha polisi?

Mheshimiwa Naibu Waziri majibu, tafadhali. Mheshimiwa Hamza Khamis Khamis.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Kaskazini Unguja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kupambana na tatizo sugu la ubakaji na ulawiti Jeshi la Polisi limejiwekea mikakati thabiti inayohusisha ufuatiliaji wa vyanzo vya makosa na kuyatafutia ufumbuzi. Moja miongoni mwa mikakati hiyo ni kutoa elimu kwa kushirikisha jamii kupitia madawati ya unyanyasaji wa jinsia yaliyopo kwenye vituo vya polisi. Aidha, hutoa elimu ya mapambano dhidi ya makosa ya aina hii katika shule za msingi na sekondari, maadhimisho pia ya kitaifa na matamasha mbalimbali. Aidha, wale wote wanaobainika kutenda makosa hayo huchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

Mheshimwa Spika, kwa sasa mikakakati ya jeshi la polisi inatosheleza kukabiliana na tatizo hilo bila ya kuhitaji kuanzishwa kwa kikosi maalum kwani yote ya jinai ikiwemo udhalilishaji yana adhabu zake kisheria. Aidha, makosa haya yanatendeka miongoni mwa jamii hivyo, ni lazima jamii nzima ishirikiane kuyapinga na kuyakataa kwa kutoa taarifa vituo vya polisi na kuwa tayari kwenda kutoa ushahidi mahakamani, ili adhabu stahiki zitolewe kwa wahalifu hao, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Malembeka, kwanini unahitaji kikosi maalum?

MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuongeza maswali mawili ya ziada. Swali langu la kwanza, nataka nijue kwa kuwa, suala la ubakaji na ulawiti na unyanyasaji kwa watoto haliko Tanzania pekee, lipo katika nchi mbalimbali. Nilitaka kujua Serikali inashirikiana na mashirika gani, ili kuhakikisha suala hili linakomeshwa?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, kwa kuwa, kuna maafisa wa madawati katika maeneo kadhaa, ili kusaidia kupambana na masuala ya ulawiti, ubakaji na unyanyasaji kwa watoto, nilitaka kujua wanawawezeshaje maafisa wale, ili waepukane na rushwa, lakini pia waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi? Ahsante.

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Hamza Khamis Khamis, Naibu Waziri Mambo ya Ndani ya Nchi.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, anataka kujua ni mashirika gani ya kimataifa au mashirika gani ambayo tunashirikiananayo katika kupambana na jambo hili. Kwa kweli, niseme tu kwamba, yapo mashirika mengi ambayo tunashirikiananayo. Yapo ya ndani na nje ya nchi ambayo tunashirikiananayo katika kupambana dhidi ya matukio haya ya uhalifu, hasa ya udalilishaji wa kijinsia. Kwa upande wan je huko tuna mashirika kwa mfano ya *UNICEF,* kuna shirika La *WHO (World Health Organization),* tuna *UN Women,* tuna *USAID,* tuna *Save the Children,* hapa tuna akina taasisi zile zinazoshughulikia masuala ya kisheria. Kwa hiyo, kwa ufupi tuna taasisi nyingi ambazo tunashirikiana nazo katika kuhakikisha kwamba, tunapambana dhidi ya haya matukio ya udhalilishaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vipi tunawawezesha hawa maafisa wa madawati; maafisa wa madawati tuna mambo mengi. La kwanza tuna mfumo maalum ambao upo kwa ajili ya uwezeshaji na ufuatiliaji wa matukio ya udhalilishaji, lakini pia tumekuwa tunawapa elimu ya kisheria, tunawapa elimu ya *protections,* tunawapa elimu ya kijamii. Elimu ambazo zinawasaidia wao kuweza kuchukua hatua pale tukio linapotokea, lakini zaidi tumeanzisha kwenye vituo pamoja na kwamba sio vyote, lakini vipo vituo ambavyo tumewawekea usafiri ambao huwa wanatumia kwa ajili ya kufuatilia hayo matukio mara tu yanapotokea. Nakushukuru.

SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Madini, Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya muda, mtaona bado tuna maswali mawili; swali la Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mbunge wa Ndanda.

Na. 319

Utafiti wa Madini ya *Graphite* – Ndanda

MHE. CECIL D. MWAMBE aliuliza:-

Je, nini mpango wa Serikali baada ya kukamilika kwa Mradi wa Utafiti wa Madini ya *Graphite* Kata ya Chiwata?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Profesa Manya, Naibu Waziri madini. Naomba Waheshimiwa Wabunge tulisome hilo swali na tusikilize majibu yake.

NAIBU WAZIRI WA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mbunge wa Jimbo la Ndanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nipende kulieleza Bunge lako tukufu kuwa, Mikoa ya kusini mwa Tanzania ikiwemo Lindi na Mtwara imebarikiwa kuwa na hazina kubwa ya madini ya kinywe ambayo kitaalam inaitwa g*raphite* ambayo ni madini ya kimkakati yanayohitajika sana duniani kwa sasa kutokana na matumizi yake kama malighafi za viwandani.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uwepo wa hazina ya madini hayo, yapo makampuni mengi yanayomiliki leseni za utafutaji na uchimbaji madini ya kinywe katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo mikoa ya Lindi na Mtwara. Hadi sasa kwa nchi nzima kuna jumla ya leseni 68 za utafutaji, leseni 24 za uchimbaji wa kati na leseni moja ya uchimbaji mkubwa wa madini ya kinywe.

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Chiwata ambayo ipo Jimbo la Ndanda, Wilayani Masasi kuna leseni mbili za uchimbaji wa kati zilizotolewa kwa Kampuni ya *Volt Graphite Tanzania Limited* na leseni hizo zilitolewa mwaka 2018 baada ya kuwa kampuni hiyo imekamilisha shughuli za utafiti. Na kinachosubiriwa ni Kampuni hiyo kuanza uchimbaji na hatimaye uchakataji wa madini ya kinywe katika leseni hizo.

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali ni kuona kuwa makampuni yanayomiliki leseni za utafutaji madini yanakamilisha shughuli za utafiti na kuomba leseni za uchimbaji mkubwa na wa kati. Kuwepo kwa leseni za uchimbaji wa madini katika maeneo hayo kutasababisha kuanzishwa kwa miradi ya uchimbaji ambayo italeta mapinduzi makubwa ya kiuchumi katika Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Spika, aidha, uanzishwaji wa miradi hiyo utaiwezesha Serikali kukusanya mapato zaidi, kutoa fursa za ajira kwa Watanzania hasa wanaoishi katika maeneo yanayozunguka miradi, uhaulishaji wa teknolojia, fedha za kigeni, lakini pia na manufaa mengine kwa jamii kupitia *local content* pamoja na *CSR*.

SPIKA: Ndio maana niliwaambia msome swali na tuangalie majibu. Sidhani kama Mheshimiwa Mwambe una haja ya kuuliza swali la nyongeza kwa sababu, kwa kweli, swali hili halijajibiwa Profesa. Kwa hiyo, nalirudisha tena Wizara ya Madini mlijibu hili swali, tutalipangia tarehe nyingine ambayo mtatakiwa mjibu swali hili. *(Makofi)*

Tujibu maswali. Tujibu maswali Waheshimiwa Mawaziri, swali ni rahisi tu kwamba, mradi wa utafiti wa madini ya *graphite* Chiwata umekamilika. Sasa Serikali ina mpango gani? Sasa mmepiga maneno wee, jibu haliko. Kwa hiyo, tunalipangia wakati mwingine swali hili.

Tunaendelea na Wizara ya Maji. Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, Mbunge wa Busega.

Na. 320

Mradi wa Maji Busega – Bariadi

MHE. SIMON S. LUSENGEKILE aliuliza:-

Je, ni lini Mradi mkubwa wa Maji wa Ziwa Victoria kutoka Busega mpaka Itilima kupitia Bariadi utaanza kutekelezwa?

SPIKA: Majibu ya swali hili, Mheshimiwa Naibu Waziri Maji. Eng. Winfrida Mahundi.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Simon Songwe Lusengekile, Mbunge wa Busega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la *KFW* la Serikali ya Ujerumani imekamilisha taratibu za kupatikana kwa wataalam washauri ambao watasimamia utekelezaji wa mradi huu mkubwa wa maji kutoka Ziwa Victoria kupeleka Mkoa wa Simiyu. Mradi huu unahusisha ujenzi wa bomba kuu kilomita 195, matenki 8 yenye ujazo wa lita milioni 11.9 na mabomba ya usambazaji kilomita 49.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa mradi unatarajia kuanza mwezi Agosti 2021 na miji mikuu ya Wilaya itakayonufaika ni Busega, Bariadi, Itilima, Maswa, Meatu na vijiji vilivyoko pembezoni mwa bomba kuu umbali wa kilomita 12 kila upande. Mradi umepangwa kutekelezwa kwa miaka minne.

SPIKA: Mheshimiwa muuliza swali.

MHE. SIMON S. LUSENGEKILE: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa Serikali tayari imemaliza kushauriana na wenzetu wa *KFW* na tayari kwenye bajeti ya mwaka 2021/2022 Serikali imetenga bilioni 19 za

ndani kwa ajili ya kuanza mradi huu. Je, ni kiasi gani kimetengwa kwa kutoka kwa hawa marafiki zetu wa *KFW* kwa ajili ya mradi huu kwa mwaka wa fedha 2021/2022?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa, miradi mingi ya maji imekuwa ikitengenezwa kwa ajili ya matumizi ya binadamu tu na Mkoa wetu wa Simiyu wananchi walio wengi ni wakulima na wafugaji. Je, Waziri anawahakikishiaje wananchi wa Mkoa wa Simiyu kwamba, mradi huu utaenda kuwasaidia katika zoezi zima la umwagiliaji na matumizi ya mifugo?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, je, maji haya pia yatawezesha umwagiliaji na mifugo kupata maji?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Simon Lusengekile, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza anahitaji kufahamu ni kiasi gani kimetengwa na hawa wenzetu wa Serikali ya Ujerumani:-

Mheshimiwa Spika, kwa majibu ya rahisi ni kwamba, sisi tumetenga hiyo milioni 19 ambavyo imesomeka kwenye bajeti yetu na kwa Serikali ya Ujerumani wametenga bilioni 55 kwa ajili ya mradi huu. Na huu mradi ni mradi mkubwa ambao utakwenda kugharimu zaidi ya bilioni 444, fedha za ndani zitakazotumika zitakuwa ni bilioni 124 na fedha za *KFW* 320.

Mheshimiwa Spika, kwa suala la kuzingatia umwagiliaji na ufugaji, sisi kama Wizara tumezingatia na tumeweza kuona kwamba tunaenda kuhakikisha kukabiliana na mabadiliko ya tabia-nchi katika Mkoa wa Simiyu. Na shughuli kubwa ambazo zitaendelea kufanyika ni ujenzi wa mabwawa ambayo yatatumika katika umwagiliaji, lakini vilevile malambo katika namna ambavyo tutaendelea kupata fedha katika miaka ya fedha ya mwaka 2021/2022 pia malambo kwa ajili ya mifugo yatajengwa.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mtaona *time* yetu ya kumaliza maswali imefika, sasa tuendelee na matangazo ya wageni waliopo katika majukwaa yetu. Tuanze na wageni waliopo katika Jukwaa la Spika ni wageni wanne ambao ni madaktari kutoka Hospitali ya Mkoa wa Dodoma, nitawatambulisha mmoja mmoja; Ndugu Danford Katenda, Ndugu Michael Mhando, Ndugu Ninael Uriyo na Ndugu Tulibaki Mwandunga. Hawa ni Madaktari wetu wa Mkoa wa Dodoma wamekuwa wakiwahudumia Waheshimiwa Wabunge wengi na wananchi kwa ujumla katika hospitali yetu ya Mkoa wa Dodoma (*General Hospital). (Makofi)*

Wageni wengine 112 wa Mheshimiwa Spika ambao ni Umoja wa Madiwani wa CCM Tanzania (UWAMA) wakiongozwa na Mwenyekiti wao Mheshimiwa Bogomba Chichake na Katibu Mheshimiwa Hilda Kadunda. Karibuni sana Waheshimiwa Madiwani, tunafarijika sana kuwa nanyi, ni heshima kubwa sana kututembelea na Waziri wenu Mheshimiwa Ummy Mwalimu yupo hapa ndani. *(Makofi)*

Hoja yenu kubwa tunaifahamu na tunazidi kumkumbusha Mheshimiwa Waziri ya zile posho za mwezi kulipwa kutoka Serikali Kuu badala ya kutegemea makusanyo ya Halmashauri peke yake. Mheshimiwa Waziri analo sana jambo hilo mara kwa mara anaendelea kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Wageni 32 wa Mheshimiwa Mashimba Ndaki, Waziri wa Mifugo na Uvuvi ambao ni viongozi wa Wizara na Watendaji Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo ni pamoja na Katibu Mkuu wa Mifugo Prof. Elisante Ole Gabriel. Ahsante Profesa karibu sana, mifugo ipo mikono salama maana ipo chini ya Katibu Mkuu mchunga ng'ombe. *(Makofi)*

Wengine ni Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Maabara ya Veterinari Tanzania-*TVLA,* Dkt. Stella Bitanyi; Kaimu Meneja Mkuu wa Kampuni ya Ranchi za Taifa, Ndugu Maselle Shilaji; Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Vyuo vya Mifugo, Dkt. Pius Mwambene; Msajili wa Bodi ya Maziwa Tanzania, Dkt. George Msalya; Msajili wa Bodi ya Nyama Tanzania, Dkt. Daniel Mushi;

Mwenyekiti wa Bodi ya *LITA*, Prof. Zacharia Masanyiwa; Mwenyekiti wa Bodi ya *TALIRI,* Prof. Sebastian Chenyambuga; na Mwenyekiti wa Bodi ya *NARCO, Senator* Paul Kimiti. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, *Senator* Paul Kimiti yeye nimtambulishe peke yake alikuwa ni mmoja wa Wabunge ambao sisi tuliwakuta hapa Bungeni, ni Mbunge ambaye alitumikia Ubunge kutoka mwaka 1980 hadi mwaka 2010, kwa miaka 30 kwa ujumla wake. Sasa hivi ni Mwenyekiti wa Bodi ya *NARCO* na wale mliokuwa kwenye Bunge la Katiba mtakumbuka alikuwa Mwenyekiti wa Kamati Namba 12. Pia wakati anaapishwa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu kama nakumbuka vizuri alikuwa ni mmoja wa wale wazee walioshiriki katika uapisho huo. Kwa hiyo, ni katika wazee wetu wa Taifa letu, tunakushukuru sana, tunaona una afya nzuri, karibu sana Bungeni. *(Makofi)*

Upande wa Sekta ya Uvuvi tunaye Katibu Mkuu Uvuvi, Dkt. Rashid Tamatamah; Meneja wa *TAFICO,* Ndugu Ester Mulilya; Mkurugenzi wa *DSFA,* Dkt. Emmanuel Sweke; Mwenyekiti wa Bodi ya *FETA,* Dkt. Blandina Lugendo; Mwenyekiti wa Bodi ya *TVLA,* Ndugu Selina Lyimo; Mwenyekiti wa Bodi ya *TAFIRI,* Ndugu Yahaya Mgawe; na Mwenyekiti wa Bodi *MPRU,* Dkt. Boniventure Baya. *(Makofi)*

Tunaye pia Mkuu wa Mkoa Mstaafu Mheshimiwa Meck Sadick. Karibu sana Mheshimiwa Meck Sadick kutoka kule Mwanza mtani wangu huyu. Mheshimiwa Meck Sadick mjini hapa magari mengi uwe makini maana Dodoma ni kubwa kuliko Mwanza. *(Makofi/Kicheko)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wageni 65 wa Mheshimiwa Abdallah Ulega, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi ambao ni Madiwani kutoka Jimbo la Mkuranga wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri Ndugu Mohammed Mwera. Karibuni sana Waheshimiwa Madiwani, hili Baraza hatari watu wanapendeza wapo vizuri. Mbunge wenu anafanya kazi nzuri karibuni sana lakini pia nawaona na Viti Maalum wapo vizuri pia, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 14 wa Mheshimiwa Godwin Mollel, Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kutoka Taasisi ya *PUNCHWMI* Marekani na wengine kutoka katika Mkoa wa Kilimanjaro wakiongozwa na Mwenyekiti wa Bodi kutoka Marekani Ndugu Gerald Thames. Karibuni sana wageni wetu hapa Bungeni.

Hawa wageni wanashirikiana na Mkurugenzi wa kule Siha ambapo wageni wetu kutoka Marekani kupitia kwa Askofu Mafie ambaye baba mlezi kiroho wa Mheshimiwa Mollel wanategemea kuichangia Halmashauri ya Siha zaidi ya bilioni 6 kujenga shule ya mfano ambayo itasaidia sana katika maendeleo ya wananchi wa kule. Tunawapongeza wadau wote mnaoshiriki katika jambo hilo mwendelee nalo vizuri. *DED* wa kule Stephen Ndaki yupo wapi, ahsante sana karibu uendelee kufanya *coordination* hiyo vizuri. Ahsante sana. *(Makofi)*

Wageni 28 wa Mheshimiwa Margaret Sitta ambao ni kutoka Taasisi ya *Patriotic Youth Association* iliyopo Urambo Mkoa wa Tabora wakiongozwa na Ndugu Esther Mitinangi. Karibuni sana kutoka Urambo mama yupo anapiga kazi. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Jackson Kiswaga ambao ni wapiga kura wake kutoka Jimbo la Kalenga: Ndugu Daniel Mwangili; Ndugu Editha Tesha na Ndugu Aziz Mkwawa. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi ambao ni walimu wa Shule ya Sekondari ya Kakanganga ya Kigoma ambao ni Ndugu Abduljalilu Mustapha; Ndugu Zaitun Kachwamba; na Ndugu Mahfudhi Abdulmaliki. Karibuni sana walimu. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Fredy Mwakibete wawekezaji kutoka Ufaransa; Ndugu Thomas Debertrand na Ndugu Stephen Philemon. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 32 wa Mheshimiwa Maryprisca Mahundi, Naibu Waziri Wizara ya Maji, ambao ni *Tanzania Sickle Cell Warriors Organization-TASWA* kutoka Jijini Mwanza wakiongozwa na Mkurugenzi Ndugu Paskazia Mazeze. Karibuni sana wale mnaopambana na *sickle cell,* hongereni sana.

Mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Joseph Mhagama ambaye ni Mhadhiri Mwandamizi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, Ndugu Joel Mmasa. Karibu sana ndugu Mmasa. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Tunza Malapo ambao ni rafiki zake kutoka Mkoani Mtwara wakiongozwa na Ndugu Ahmad Watanga. Karibuni sana wale wa kutoka Mtwara. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Judith Kapinga ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Ruaha *Catholic University-RUCU*, wakiongozwa na Rais wa chuo hicho Ndugu Charles Thomas. *RUCU* karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Stephen Byabato ambao ni Mstahiki Meya na viongozi wengine kutoka Bukoba, Mkoani Kagera wakiongozwa na Meya wa Bukoba Mheshimiwa Godson Gibson. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Eng. Kundo Mathew, Naibu Waziri wa Mawasiliano ya Teknolojia ya Habari kutoka Bariadi ambaye ni Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Simiyu, Ndugu Shemsa Mohamed na Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya Ndugu Mary Misangu. Karibuni sana Dodoma Wanyantuzu. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo ambao ni Madiwani Viti Maalum kutoka Arumeru Mkoani Arusha ambao ni Ndugu Glory Kaaya na Ndugu Severa Minja. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni watatu kutoka Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania ambao wamekuja kujifunza namna Bunge linavyofanya kazi ni Dkt. Mboni Ruzegea, Ndugu Abdallah Sudi na Ndugu Judith Lugongo. Karibuni sana nimewaona pale. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda ambao ni wawekezaji wa Kiwanda cha Samaki cha *West Side Fishimans* kutoka Mkoa wa Mwanza; Ndugu Yusuph Yanda, Ndugu Lin Cheung na Ndugu Sadi Kawemba. Karibuni sana. *(Makofi)*

Baada ya maswali baadaye wataingia wageni 152 wa Mheshimiwa Fatma Toufiq, ambao ni Walimu 10 na wanafunzi 142 wa Shule ya Sekondari ya Umonga iliyopo jijini Dodoma wakiongozwa na Mkuu wa Shule hiyo Ndugu Leticia Singo. Ahsante sana. *(Makofi)*

Huo ndio mwisho wa matangazo ya wageni. Kuna tangazo moja kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii linawatangazia Waheshimiwa Wabunge Wajumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii pamoja na Waheshimiwa Wabunge 53 wanaotoka katika Majimbo yenye migongano kati ya wanyamapori na binadamu kwamba leo tarehe 27 kutakuwa na mafunzo mchana Msekwa pale kuanzia saa 7.00 mchana hadi saa 10.30. Wale mnaotoka kwenye maeneo ambayo yana mgongano mkubwa wa wanyama na binadamu mnaombwa kuhudhuria semina hii. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, semina hizi hazimaanishi kuwanyamazisha, kama kuna mgongano huko semina hii haikufanyi kesho kutwa kwenye Wizara ya Maliasili usiongee. Mmenielewa Waheshimiwa Wabunge, semina inawezesha tu lakini kama kuna matatizo unafanya kazi yako ya Ubunge ili Serikali iweze kuchukua hatua na kurekebisha matatizo hayo kwa nia njema.

Ahsante sana, tunaendelea, Katibu.

NDG. NENELWA MWIHAMBI – KATIBU WA BUNGE

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 - Wizara ya Mifugo na Uvuvi

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Mashimba Ndaki sasa ni wakati wa kuwasilisha hotuba yako, tafadhali, una nusu saa.

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea na hotuba yangu, naomba hotuba yangu yote iingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge yaani *Hansard.*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoka hoja kwamba kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge inayosimamia Kilimo, Mifugo na Maji iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi; Fungu 99 – Mifugo na Fungu 64 – Uvuvi, Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2020/2021. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha hotuba yangu siku ya leo. Kwa heshima na unyenyekevu mkubwa, namshukuru sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini kuendelea kushika wadhifa huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilipokea kwa masikitiko makubwa taarifa ya kifo cha Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais aliyeiongoza nchi yetu kwa uhodari na umahiri mkubwa

wakati wa uhai wake tangu alipoingia madarakani. Napenda kuchukua nafasi hii, kumuombea kwa Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuapishwa kuwa Rais wa Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Watanzania wana matumaini makubwa na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu. Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango kwa kuteuliwa na kisha kuthibitishwa na Bunge lako Tukufu kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Husein Ally Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa kushika nafasi hiyo. Vilevile nampongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge wa Jimbo la Ruangwa kwa kuendelea kuaminiwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kukupongeza wewe binafsi kwa kuliongoza vizuri Bunge letu Tukufu kwa weledi na umahiri mkubwa. Wewe pamoja na Naibu Spika umewezesha Bunge la Kumi na Mbili kutekeleza majukumu yake kikamilifu kwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo ambayo imewekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum na Makamu wake Mheshimiwa Almas A. Maige, Mbunge wa Jimbo la Uyui kwa ushirikiano, maelekezo na ushauri mzuri walioutoa wakati wa kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2020/2021 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Aidha, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchaguliwa kuwawakilisha wananchi katika Bunge lako Tukufu hili la Kumi na Mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kwa mara nyingine tena niwapongeze na kuwashukuru wananchi wa Jimbo ninaloliwakilisha, yaani Jimbo la Maswa Magharibi, kwa kunichagua na kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa katika kuwawakilisha na kuwatumikia katika Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, masuala tuliyozingatia katika mpango wa bajeti wa mwaka 2021 ni pamoja na maelekezo yaliyomo kwenye mwongozo wa Mpango na Bajeti wa mwaka 2021/2022 uliozingatia maeneo ya kipaumbele vya kitaifa kama yalivyo kwenye Dira ya Taifa ya Maendeleo; Malengo Endelevu ya Maendeleo (*Sustainable Development Goals);* Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano kwa kipindi cha 2021/2022 hadi mwaka 2025/2026; na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020/2025. Aidha, Mpango na Bajeti vimezingatia Progamu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo ya II *(ASDP II)*.

Mheshimiwa Spika, sasa nieleze kidogo kuhusu utekelezaji wa Mipango na Bajeti kwa mwaka 2020/2021. Katika mwaka 2020/2021 idadi ya mifugo hapa nchini inakadiriwa kuongezeka ikilinganishwa na mwaka 2019/2020 ambapo idadi ya ng'ombe imeongezeka kutoka milioni 33.4 hadi milioni 33.9, mbuzi kutoka milioni 21.29 hadi milioni 24.5 na kondoo kutoka milioni 5.65 hadi milioni 8.5.

Mheshimiwa Spika, aidha, kuku wameongezeka kutoka milioni 83.28 hadi milioni 87.7 ikiwa kuku wa asili wameongezeka kutoka milioni 38.7 hadi milioni 40.36, kuku wa kisasa wameongezeka kutoka milioni 44.51 hadi milioni 47.34 na nguruwe kutoka milioni 2.14 hadi milioni 3.2. Aidha, Sekta ya Mifugo katika mwaka 2020 ilikua kwa asilimia 5.0 na kuchangia asilimia 7.1 katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa maziwa umeongezeka kwa 3% kutoka lita bilioni 3.01 mwaka 2019/ 2020 hadi kufikia lita bilioni 3.1 mwaka 2020/2021. Aidha, usindikaji wa maziwa umeongezeka kutoka lita milioni 74.3 mwaka 2019/2020 hadi lita milioni 75.9 mwaka 2020/2021 sawa na ongezeko la asilimia 2.2. Ongezeko hili limetokana na

viwanda kuongeza usindikaji ambapo sasa usindikaji umeongezeka kutoka asilimia 20 hadi asilimia 30 ya uwezo uliosimikwa wa viwanda.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa zao la nyama umeongezeka kutoka tani 701,679.1 mwaka 2019/2020 hadi tani 738,166 mwaka 2020/2021 sawa na ongezeko la asilimia 5.2. Pia katika mwaka 2020/2021 uzalishaji wa mayai umeongezeka kutoka mayai bilioni 3.58 mwaka 2019/2020 hadi mayai bilioni 4.5 mwaka 2020/2021 sawa na ongezeko la asilimia 26. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2021 vipande vya ngozi milioni 11.77 vyenye thamani ya shilingi bilioni 25.93 vimezalishwa ikilinganishwa na vipande milioni 11.23 vyenye thamani ya shilingi bilioni 22.8 vilivyozalishwa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, aidha, jumla ya Wakaguzi wa Ngozi 60 kati ya 113 walioteuliwa wamejengewa uwezo pia wachunaji ngozi 423 wamepatiwa mafunzo. Vile vile tumeweza kugawa visu maalum 131 kwa wachunaji ngozi katika Mikoa ya Kagera na Simiyu. Aidha, upatikanaji wa ngozi bora katika viwanda viwili vikubwa vinavyozalisha bidhaa za ngozi umeongezeka kutoka asilimia 30 hadi asilimia 80. Kwa mwaka 2021/2022 Wizara kwa kushirikiana na wadau wa tasnia ya ngozi itaendelea kusimamia wingi na ubora wa ngozi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021, ili kuboresha mifugo hapa nchini, Wizara imeendelea kukiboresha Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji *(NAIC)* kwa kukipatia madume bora nane ya mbegu na kufikia jumla ya madume 37. Katika njia ya asili dume moja linaweza kupanda majike 25 kwa mwaka lakini kwa mpango wa uhimilishaji dume moja anaweza kuzalisha dozi za mbegu kwa ajili ya majike 150,000 kwa mwaka. Kwa muktadha huo, madume manane yaliyonunuliwa kwa mwaka 2021 yataweza kuzalisha dozi za mbegu kwa ajili ya majike milioni 1.2 kwa mwaka. Kwa ujumla wake madume 37 yanaweza kuzalisha dozi za mbegu kwa ajili ya majike milioni 5.6 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2021/2022 Wizara itaendelea kuimarisha Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji na Vituo vyetu saba vya Uhimilishaji vilivyoko kwenye kanda na kuwezesha uendelezaji na uanzishaji wa kambi za uhimilishaji kwa lengo la kuhimilisha ng'ombe zaidi ya 1,000,000. Katika mwaka 2020/2021 jumla ya mitamba 18,012 ya maziwa na nyama kutoka katika mashamba ya Serikali na binafsi imezalishwa na kusambazwa kwa wafugaji ikilinganishwa na jumla ya mitamba 16,809 iliyosambazwa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/2022 Wizara itanunua mitamba bora 300 ya ng'ombe wazazi aina ya Borani kwa ajili ya mashamba ya Serikali ili kuboresha uzalishaji wa mitamba katika mashamba hayo. Aidha, Wizara itasambaza kwa wafugaji mitamba 1,000 kwa bei ya ruzuku kutoka katika mashamba ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2020/2021, jumla ya vifaranga vya kuku milioni 88.3 vimezalishwa na kusambazwa nchini. Kati ya hivyo, vifaranga milioni 52 ni vya nyama, vifaranga milioni 29 ni vya kuku chotara milioni 7.4 ni wa kuku wa mayai ikilinganishwa na vifaranga milioni 70.3 vilivyozalishwa kwa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2021/2022 Wizara itaendelea kushirikiana na wazalishaji wa vifaranga vya kuku ili kuhakikisha wafugaji wanapata vifaranga bora katika ukuaji na ustahimilivu wa magonjwa ili kujikomboa kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/2021 hadi tarehe 30 Aprili, 2021 jumla ya ng'ombe 1.8, mbuzi 2.1, kondoo 360,745 na punda 191,656 wenye thamani ya shilingi trilioni 1.5 waliuzwa katika minada hapa nchini ikilinganishwa na ng'ombe 1.5, mbuzi 1.7, kondoo 299,157 na punda 198,000 wenye thamani ya shilingi trilioni 1.06 waliouzwa hapa nchini mwaka 2019/2020. Sababu za kuongezeka kwa biashara ya mifugo kwa soko la ndani limetokana na Serikali kutengeneza mazingira rafiki ya biashara ya mifugo na kutoa elimu juu ya utaratibu na kanuni za biashara ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/2022 Wizara itaendelea kujenga na kukarabati minada ya mifugo ya upili na mipakani ili kuwezesha biashara ya mifugo ndani na nje ya nchi pamoja na kuimarisha vituo vya doria vya kimkakati.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2020/2021 Halmashauri za Wilaya 17 zimetenga jumla ya hekta 271,661.11 kwa ajili ya malisho ya mifugo. Hivyo maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya malisho yameongezeka kufikia hekta milioni 3.1 mwaka 2020/2021 ikilinganishwa na hekta milioni 2.8 mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/2022 pia Wizara kwa kushirikiana na mamlaka za Serikali za Mitaa itaendelea kutenga maeneo kwa ajili ya malisho kuimarisha miundombinu ya maji kwa ajili ya mifugo kwa kuchimba malambo na visima virefu hususan katika maeneo yaliyo na uhitaji mkubwa wa maji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/2021 viwanda vya kutengeneza vyakula vya mifugo vimeongezeka na kufikia 154 kutoka viwanda 105 mwaka 2019/2020. Hivyo, kuongeza uzalishaji wa vyakula vya mifugo kutoka tani 900,000 mwaka 2019/2020 hadi tani 1.2 mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/2022, Wizara itaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika uzalishaji malisho na vyakula bora vya mifugo; kusimamia na kudhibiti ubora na usalama wa vyakula vya mifugo; kutoa mafunzo rejea kwa wakaguzi wa vyakula vya mifugo na maeneo ya malisho; na kuimarisha mashamba ya Serikali ya kuzalisha malisho na mbegu. Aidha, Wizara imeandaa mpango wa kuendeleza malisho aina ya Juncau katika mashamba ya taasisi za Serikali na baadhi ya Halmashauri na sekta binafsi kwenye eneo lenye ukubwa wa hekta 1,250.

Mheshimiwa Spika, Ugonjwa wa Homa ya Nguruwe; aina ya ugonjwa huu inaitwa *African Swine Fever (ASF)* ulilipuka kwa vipindi mbalimbali kwa mwaka 2020/2021 na kusababisha jumla ya vifo 5,428 katika Halmashauri 18 Tanzania Bara. Ugonjwa huu hauna tiba wala chanjo. Hivyo

nitoe wito kwa Halmashauri zote nchini kutoa elimu ya namna ya kujikinga na ugonjwa na pia pale kunapotokea mlipuko, kutoa taarifa mapema kwa Wizara na kupulizia dawa ya kuuwa virusi ili kuzuia hasara inayoweza kuwapata wafugaji. Aidha, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu na wananchi kuwa ugonjwa huo kwa sasa umedhibitiwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/2022 Wizara itaendelea kuimarisha mfumo wa upatikanaji wa taarifa za magonjwa ya mifugo, kuwezesha uchanjaji wa wanyama 25,000,000 dhidi ya magonjwa ya kipaumbele 13 yenye chanjo.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutoa mafunzo rejea kwa Wafugaji katika Halmashauri 21 na pia kuwajengea uwezo Maafisa Ugani kutoka katika Halmashauri za mikoa hapa hapa Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/2022 Wizara itaendelea kuwezesha utoaji wa huduma za ugani kwa kununua pikipiki 300 kwa ajili ya Maafisa Ugani, kuwezesha pia Halmashauri 20 ili ziweze kuanzisha mashamba darasa 60 ya malisho ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa kukabiliana na changamoto ya uzalishaji wa ng'ombe na upatikanaji wa malisho, nitazungumzia kwa kifupi sana kuhusiana na kampuni ya *NARCO*. Kampuni ya *NARCO* ina eneo la malisho lenye ukubwa wa hekta 480 kwa nchi nzima, hivyo kuwa na uwezo wa kutunza *units* za mifugo 240,000 kwa uwiano wa kitaalamu wa hekta 2 kwa *unit* moja ya mifugo. Kwa sasa kwenye *unit* za mifugo 157,000, kunakuwa na eneo lililobakia lenye uwezo wa kutunza *unit* za mifugo 83,000 tu.

Mheshimiwa Spika, asilimia 75 ya eneo la ranchi limekodishwa kwa wafugaji binafsi wadogo wadogo, wa kati na wakubwa, hivyo *NARCO* imebakiwa na asilimia 25 ya eneo kwa ajili ya mafunzo, utafiti, biashara na biashara

za kampuni. Baadhi ya ranchi za kampuni za NARCO zina mifugo mingi Zaidi ya uwezo wake hivyo watahamishiwa katika ranchi nyingine.

Mheshimiwa Spika, Wizara imefanya mapitio ya tozo zinazoathiri uwekezaji katika biashara ya mifugo, lengo likiwa ni kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji na kuongeza mauzo ya mazao ya mifugo nje ya nchi. Maboresho yaliyofanyika yatawasilishwa na Waziri wa Fedha na Mipango wakati akiwasilisha Muswada wa Sheria ya Fedha *(Finance Bill)* ya mwaka 2021/2022. Hatua hiyo itawezesha viwanda vya ndani ikiwemo *Tanchoice*, *Elia Food Overseas Ltd*, Chobo *Investment*, *Alfa Choice*, Machinjio ya Dodoma na wengine kuuza nyama nje ya nchi kwa ushindani.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2021/2022, Wizara itaendelea kutathmini tozo na ada mbalimbali zitakazoonekana kuwa kero kwa wazalishaji na wafanyabiashara wa mifugo na mazao yake ili kuzifuta au kuzifanyia marekebisho.

Mheshimiwa Spika, nijielekeze sasa kwenye Sekta ya Uvuvi. Sekta ya Uvuvi ni miongoni mwa sekta muhimu za kiuchumi inayochangia katika kuondoa umasikini na kukuza uchumi. Sekta hii imegawanyika katika tasnia za uvuvi kwenye maji ya asili na ukuzaji viumbe maji. Katika mwaka 2020 Sekta ya Uvuvi ilikuwa kwa asilimia 6.7 na kuchangia asilimia 1.7 katika pato la Taifa. Sekta imeajiri wavuvi 195,435, wakuzaji viumbe maji 30,064 na zaidi ya Watanzania milioni 4.5 kwenye mnyororo wa thamani. Vile vile samaki huchangia asilimia 30 ya protini inayotokana na wanyama.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Aprili, 2021 takribani tani 422,859.78 za samaki zenye thamani ya shilingi trilioni 2.62 zilivunwa katika maji ya asili na jumla ya vifaranga vya samaki 20,040,000 zilizalishwa pamoja na tani 22,793.2 zilivunwa kupitia ukuzaji viumbe maji. Aidha, idadi ya mabwawa imeongezeka kutoka 27,979 hadi kufikia 30,032 na vizimba kutoka 431 mwaka 2019/2020 hadi 473.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa majukumu yetu kwa mwaka 2020/2021 kwa kuangalia kodi, ada na tozo, katika sekta hii, Serikali imepunguza viwango vya tozo na ada mbalimbali katika uzalishaji na usafirishaji wa mazao ya uvuvi nje ya nchi kupitia kanuni iliyotangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 491A la tarehe 29 Juni, 2020 iliyoanza kutumika Julai, 2020 ili kupunguza gharama ya kuhimili ushindani wa kibiashara ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya viwango vya tozo vilivyopunguzwa na kuanza kutumika ni kama ifuatavyo: tozo ya usafirishaji wa dagaa nje ya nchi kutoka Ziwa Tanganyika imepungua kutoka Dola za Marekani 1.5 hadi Dola za Marekani 0.5 kwa kilo. Tozo ya usafirishaji wa dagaa nje ya nchi kwa dagaa wa bahari, Ziwa Nyasa na Ziwa Victoria, toka Dola za Marekani 1 hadi Dola za Marekani 0.16.

Mheshimiwa Spika, ada ya leseni ya kusafirisha dagaa nje ya nchi kwa wafanyabiashara wadogo imepungua kutoka Dola za Marekani 1,000 hadi Dola za Marekani 250 na kwa wafanyabiashara wakubwa kutoka Dola za Marekani 1,800 hadi Dola za Marekani 500.

Mheshimiwa Spika, ada ya leseni ya mazao mengine ya bahari kama Pweza, Kambakoche na Kaa imepungua kutoka Dola za Marekani 2,500 hadi Dola za Marekani 500 kwa wafanyabiashara wadogo na kutoka Dola za Marekani 2,700 hadi Dola za Marekani 1,000 kwa Wafanyabiashara wakubwa. Tozo ya usafirishaji wa samaki aina ya migebuka kwenda nje ya nchi imepungua kutoka Dola za Marekani 0.5 hadi Dola za Marekani 0.3 kwa kilo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2020/2021 kwa kuzingatia mkakati shirikishi wa usimamizi na udhibiti wa rasilimali za uvuvi Wizara imefanya ulinzi na usimamizi shirikishi katika Ziwa Victoria, Tanganyika, Nyasa na Bahari ya Hindi. Juhudi hizi zimewezesha kupungua kwa uvuvi haramu kwa asilimia 80 katika maji baridi na asilimia 100 katika matumizi ya vilipuzi kule baharini.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2021/2022 Wizara itaendelea kutekeleza Mkakati Shirikishi wa Usimamizi na Udhibiti wa Rasilimali za Uvuvi. Kuhusiana na uboreshaji wa miundombinu ya mialo na masoko kwa mwaka 2021 Serikali ilipanga kufanya ukarabati na ujenzi wa mialo na masoko. Hata hivyo utekelezaji wake umekabiliwa na changamoto ya kuwepo kwa mvua kubwa zilizonyesha katika msimu wa mwaka 2020 na hivyo kusababisha baadhi ya miundombinu kuharibika na mingine kufunikwa na maji, hususan katika mialo ya Ziwa Tanganyika na Ziwa Victoria. Hali hii imechelewesha utekelezaji wa kazi katika mialo ya Muyobozi Uvinza, Kasanga Kalambo, Kirando Nkasi katika Ziwa Tanganyika na Kigangama Magu, Gana Ukerewe, Nyamikoba Busega, na Marehe Bukoba katika ziwa Victoria ambapo jumla ya shilingi 589,068,327/= zilitengwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Wakala wa Majengo *(TBA)* inafanya ukarabati wa maeneo tisa yaliyoathirika kwa gharama ya shilingi 1,490,931,673/=. Maeneo hayo ni pamoja na mialo ya Ihale (Busega), *New Igombe* na Kayenze kule Ilemela, Igabilo (Bukoba), Chifunfu/ Kijiweni (Sengerema), soko la MbambaBay kule Nyasa) na Ofisi za Vituo vya Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi vya Busega, Sengerema na Sota.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usimamizi wa mazao ya uvuvi nje ya nchi, hadi kufikia Aprili, 2021 jumla ya tani 32,962.79 za samaki hai wa mapambo 141,592 wenye thamani ya shilingi bilioni 335.25 ziliuzwa nje ya nchi na kuliingizia Taifa mrabaha wa shilingi bilioni 15.55 ikilinganishwa na tani 35,329.36 na samaki hai wa mapambo 102,458 yenye thamani ya shilingi bilioni 436 yaliyouzwa nje ya nchi katika kipindi kama hiki kwa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, kiasi cha mazao ya uvuvi yaliyouzwa nje ya nchi kimepungua kwa asilimia 6.70 ikilinganishwa na kiasi kilichouzwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2019/2020. Kiasi cha mrabaha kilichokusanywa kutokana na mauzo hayo kimepungua kwa asilimia 25.27 hali hii imechangiwa na kuyumba kwa soko la mazao ya

uvuvi nje ya nchi kutokana na mlipuko wa homa kali ya mapafu UVIKO 19. Vilevile upungufu huo umesababishwa na kupungua kwa kiasi cha samaki kinachochakatwa viwandani ambacho ndicho kinachosafirishwa nje ya nchi. Aidha, upungufu wa malighafi viwandani unachangiwa na kuibuka kwa biashara ya mabondo ambapo bondo pekee lina bei kubwa kuliko bei ya samaki mwenye bondo ndani yake.

Mheshimiwa Spika, katika usimamizi wa uvuvi katika bahari kuu, ninayo furaha kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa tarehe 23 Februari, 2021 Sheria ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu Sura 388 ya mwaka 2020 iliwasilishwa katika Baraza la Wawakilishi Zanzibar na kuorodheshwa kulingana na masharti ya Ibara ya132 ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 toleo la 2010. Hali hii italiwezesha mamlaka ya kusimamia uvuvi wa bahari kuu *DSFA* Kuongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, Kanuni mpya za Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu zimetayarishwa na kutangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 334 ya tarehe 23 Aprili, 2021. Kanuni hizi zitawezesha kutekeleza kikamilifu Sheria ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu, Sura 388 ya mwaka 2020 ambayo pamoja na mambo mengine imeweka mazingira bora ya uwekezaji kwenye uvuvi wa Bahari Kuu kwa kutoa vivutio kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi, masharti nafuu ya leseni kwa wazawa ili kuongeza ushiriki wa sekta binafsi katika uchumi wa *bluu*.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Aprili 2021 jumla ya vifaranga vya samaki hii ni katika ukuzaji viumbe maji 2040 vilizalishwa katika vituo 34 vya Serikali na Sekta binafsi ililinganishwa na vifaranga 1,4531,487 vilivyozalishwa mwaka 2019/2020 sawa na ongezeko la asilimia 37.9. Katika Mwaka wa 2020/2021 Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imepandikiza samaki 101,500 katika malambo Kongogo (Dodoma - 20,000), Mwanduigembe (Singida - 15,000), Mwalusho (Simiyu - 20,000), Mahiga (Mwanza -20,000), Igigwa (Tabora 10,000), Mpera

(Shinyanga - 1,500), Wanging'ombe (Njombe - 5,000) na Kitanda (Ruvuma - 10,000) ikilinganishwa na samaki 1,500.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/2022, Wizara itawezesha kutambua na kufanya upembuzi yakinifu kwa maeneo yanayofaa kwa ufugaji samaki kwenye vizimba (*Strategic Environmental Impact Assessment*) kwa lengo la kupunguza gharama za uwekezaji. Zoezi hili litaanza na kanda mbili (2) katika Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, pia, Wizara imepanga kuanzisha mashamba darasa 40 katika halmashauri 40 nchini kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI. Aidha, Wizara itaanza ujenzi wa vituo vipya viwili (2) vya ukuzaji viumbe maji katika Mikoa ya Mtwara na Dar es Salaam ili kuhamasisha ufugaji wa viumbe maji bahari, katika ukanda wa Pwani. Aidha, Wizara itaendelea na ukarabati na upanuzi wa vituo vitano ili kuongeza uzalishaji wa faranga vya samaki na huduma za ugani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, chini la uvuvi pia tunazo Taasisi zilizo chini yake nimeziainisha kwenye aya 108, 207. Lakini nizungumzie habari ya *TAFICO* kidogo, katika mchakato wa za kufufua Shirika la Uvuvi Tanzania *(TAFICO)* wizara imekamilisha Muundo wa shirika na kuwasilishwa kwenye mamlaka husika na inaendelea na ukarabati wa majengo ya Ofisi ya utawala na karakana ya ukarabati wa zana za uvuvi.

Mheshimiwa Spika, mwaka wa 2021/2022 chini ya ufadhili wa Serikali ya Japan *TAFICO* inatarajia kuanza uzalishaji wa barafu na uhifadhi wa barafu na uhifadhi wa samaki ambao utatumika kwa ajili ya shirika na wavuvi wadogo ili kuongeza dhamani na kupunguza upotefu wa mazao ya uvuvi. Vile vile shirika litaanza wa bahari kuu kwa kutumia meli ya kwanza ambao inatarajiwa kuwasili mwezi Januari, 2022 ambayo pia imefadhiliwa na Serikali ya Japan.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020 mradi wetu wa *SWIOFish* ukijumuisha ujenzi wa mahabara ya utafiti wa

uvuvi Dar es Salaam na Ofisi tano za uvuvi wa usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi katika wilaya tano za ukanda wa habari ya Indi ambazo Mkinga, Pangani, Chalinze, Bagamoyo na Lindi Vijijini;

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/2022 Serikali kupitia *program AFDP* imepata mkopo wenye masharti nafuu kutoka Mfuko wa Kimataifa wa Kuendeleza kwa ajili ya kununua meli nne za kuvua katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu chini ya *TAFICO*. Ili kuchochea uwekezaji katika uvuvi wa bahari kuu katika mwaka 2021/2022 Serikali itaanza ujenzi wa bandari ya uvuvi katika eneo la Mbegani Bagamoyo. Uwepo wa bandari utawezesha meli zinazovua bahari kuu kuja kushusha samaki na hivyo kuchochea fursa za uwekezaji ikiwepo kujenga viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi na mitambo ya kuzalisha barafu.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, kabla ya kuhitimisha hotuba yangu napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wale wote waliochangia kwa namna moja au nyingine katika...

SPIKA: Malizia sasa Mheshimiwa Waziri, omba fedha.

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/2022, Wizara inaomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ya jumla ya shilingi169,194,996,810.00 Kati ya fedha hizo, shilingi 47,844,949,810 kwa ajili ya Sekta ya Mifugo na shilingi 121,350,047,000 kwa ajili ya Sekta ya Uvuvi. Mchanganuo wa fedha zinazoombwa kwa kila Fungu ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Wizara inaomba kutumia jumla ya shilingi 47,844,949,810 kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Sekta ya Mifugo. Kati ya fedha hizo, shilingi 30,973,208,810 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 16,871,741,000 ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Mgawanyo wake ni kama ifuatavyo; Matumizi ya Kawaida Mishahara shilingi 19,269,097,810 Matumizi Mengineyo shilingi 11,704,111,000, Fedha za Matumizi ya Maendeleo shilingi Fedha

za Ndani, shilingi 16,871,741,000; na Fedha za Nje hakuna kwa sekta ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Uvuvi katika mwaka 2021/2022 Wizara inaomba jumla ya shilingi 121,350,047,000 kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Sekta ya Uvuvi. Kati ya fedha hizo, shilingi 22,205,681,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 99,144,366,000 ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Fedha za Matumizi ya Kawaida ni shilingi 22,205,681,000, Mishahara ni shilingi 11,575,270,000; na Matumizi Mengineyo ni shilingi10,630,411,000.00. Fedha za Maendeleo za Ndani: shilingi 62,550,000,000; na Fedha za Nje: shilingi 36,594,366,000.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe shukrani zangu za dhati sana kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara: *www.mifugouvuvi.go.tz*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

HOTUBA YA WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI MHESHIMIWA MASHIMBA MASHAURI NDAKI (MB) KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NAMATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI KWAMWAKA 2021/2022 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

A. UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika*,** naomba kutoa hoja kwamba, kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge inayosimamia Kilimo, Mifugo na Maji iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Fungu 99 – Mifugo na Fungu 64 – Uvuvi) Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2020/2021. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha hotuba yangu siku ya leo. Kwa heshima na unyenyekevu mkubwa namshukuru sana **Mhe. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini kuendelea kushika wadhifa huu. Aidha, Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilipokea kwa masikitiko makubwa taarifa ya kifo cha **Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli,** Rais aliyeiongoza nchi yetu kwa uhodari na umahiri mkubwa wakati wa uhai wake tangu alipoingia madarakani. Katika kipindi chake, tumeshuhudia maendeleo makubwa ya kiuchumi na kijamii, tumeuona umahiri na uhodari wake katika kuiongoza nchi yetu ukigusa na kusisimua nchi na taasisi za Afrika na hata kimataifa. Hii ndiyo kusema, alikuwa kiongozi wa mfano katika nchi yetu, Afrika na duniani kwa ujumla. Napenda kuchukua nafasi hii, kumuombea kwa Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi, AMINA.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kuchukua nafasi hii kumpongeza **Mhe. Samia Suluhu Hassan** kwa kuapishwa kuwa Rais wa Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Watanzania wana matumaini makubwa na **Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan** kwamba ataifanya nchi yetu ipige hatua kubwa za maendeleo ya kiuchumi na kijamii na sisi katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi tunaahidi hatutamwangusha katika kufikia matumaini hayo ya Watanzania. Aidha, napenda kumpongeza **Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango** kwa kuteuliwa na kisha kuthibitishwa na Bunge lako tukufu kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nachukua nafasi hii kuwaombea viongozi wetu kwa Mwenyezi Mungu, wawe na afya njema, Mungu awape hekima, busara na ufunuo katika kuiongoza nchi yetu.

4. ***Mheshimiwa Spika*****,** nichukue fursa hii pia, kumpongeza **Mhe. Dkt. Husein Ally Mwinyi**, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa kushika nafasi hiyo. Vile vile nampongeza **Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa,** Mbunge wa Jimbo la Ruangwa kwa kuendelea kuaminiwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri Mkuu wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

5. ***Mheshimiwa Spika*****,** aidha, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru na kumpongeza, Mhe. Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwasilisha hotuba yake iliyotoa mwelekeo wa utendaji wa sekta zote ndani ya Serikali. Pia, nichukue fursa hii kumpongeza **Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb**) kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Fedha na Mipango. Aidha, nampongeza pia **Mhe. Mohamed Mchengerwa (Mb)** kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala Bora.

6. ***Mheshimiwa Spika*****,** napenda pia kukupongeza wewe binafsi, kwa kuliongoza vizuri Bunge letu Tukufu kwa weledi na umahiri mkubwa. Wewe pamoja na Naibu Spika umewezesha Bunge la **12** kutekeleza majukumu yake kikamilifu kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo iliyowekwa.

7. ***Mheshimiwa Spika*****,** naomba kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji chini ya Mwenyekiti wake **Mhe. Dkt. Christine Ishengoma,** Mbunge wa Viti Maalum na Makamu wake **Mhe. Almasi A. Maige**, Mbunge wa Jimbo la Uyui kwa ushirikiano, maelekezo na ushauri mzuri walioutoa wakati wa kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2020/ 2021 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Aidha, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchaguliwa kuwawakilisha wananchi katika Bunge lako Tukufu la 12.

8. ***Mheshimiwa Spika*****,** Wizara ilipokea kwa masikitiko makubwa taarifa za kifo cha **Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad**, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar. Nachukua nafasi hii kuwapa pole familia na wananchi wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla kwa kuondokewa na kiongozi wetu mpendwa. Pia, Wizara yangu ilipokea kwa masikitiko taarifa za vifo vya **Mhe. Atashasta Nditiye**, Mbunge wa Jimbo la Muhambwe na **Mhe. Martha Umbulla,** Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Manyara; **Mhe. Khatib Said Haji,** Mbunge wa Jimbo la Konde,

Naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa salaam za pole kwa familia za marehemu, ndugu na wananchi ambao walikuwa wanawatumikia. Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi, AMINA.

9. ***Mheshimiwa Spika*****,** pia nichukue nafasi hii kumpongeza **Mhe. Abdallah Hamis Ulega**, Mbunge wa Mkuranga kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi na nimshukuru kwa kunisaidia kutekeleza majukumu ya Wizara. Aidha, napenda nimshukuru aliyekuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi **Mhe. Pauline Philip Gekul**, Mbunge wa Jimbo la Babati Mjini kwa jinsi alivyonisaidia katika kuiongoza Wizara hii. Pia, nawashukuru Makatibu Wakuu wa Wizara **Prof. Elisante Ole Gabriel** (Mifugo) na **Dkt. Rashid Adam Tamatamah** (Uvuvi) kwa kuwa kiungo muhimu kati yangu na watumishi na kuwezesha kutekeleza majukumu ya Wizara kwa ufanisi. Aidha, ninawashukuru kwa dhati na kuwapongeza watumishi wote wa Wizara yangu kwa kazi nzuri wanayofanya.

10. ***Mheshimiwa Spika***, naomba kwa mara nyingine tena niwapongeze na kuwashukuru wananchi wa Jimbo ninaloliwakilisha, yaani jimbo la Maswa Magharibi, kwa kunichagua na kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa katika kuwawakilisha na kuwatumikia katika Bunge hili Tukufu.

B. SEKTA YA MIFUGO (FUNGU 99)

HALI HALISI YA SEKTA YA MIFUGO

11. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2020/2021 idadi ya mifugo hapa nchini inakadiriwa kuongezeka ikilinganishwa na mwaka 2019/2020 ambapo idadi ya ng'ombe imeongezeka kutoka **milioni 33.4** hadi **milioni 33.9,** mbuzi kutoka **milioni 21.29** hadi **milioni 24.5** na kondoo kutoka **milioni 5.65** hadi **milioni 8.5.** Aidha, kuku wameongezeka kutoka **milioni 83.28** hadi **milioni 87.7** ikiwa kuku wa asili wameongezeka kutoka **milioni 38.77** hadi **milioni 40.36**, kuku wa kisasa wameongezeka kutoka **milioni 44.51** hadi **milioni**

47.34 na nguruwe kutoka **milioni 2.14** hadi **milioni 3.2 (**Taarifa ya Sensa ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, 2020**)**. Aidha, Sekta ya Mifugo katika mwaka 2020 ilikua kwa asilimia **5.0** na kuchangia asilimia **7.1** katika Pato la Taifa ikilinganishwa na kukua kwa asilimia **5** na kuchangia asilimia **7.4** katika Pato la Taifa mwaka 2019.

12. ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa maziwa umeongezeka kwa asilimia **3** kutoka lita **bilioni 3.01** mwaka 2019/2020 hadi kufikia lita **bilioni 3.1** mwaka 2020/2021 **(**Taarifa ya Sensa ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, 2020)**,** ambapo kati ya hizo, lita **bilioni 2.17** zilitokana na ng'ombe wa asili na lita **bilioni 0.93** zilitokana na ng'ombe wa kisasa (**Kiambatisho Na. 1**). Aidha, kati ya ng'ombe **milioni 33.9** waliopo nchini ng'ombe wa maziwa ni **milioni 1.2** (Taarifa ya Sensa ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, 2020).

13. ***Mheshimiwa Spika,*** usindikaji wa maziwa umeongezeka kutoka lita **milioni 74.3** mwaka 2019/2020 hadi lita **milioni 75.9** mwaka 2020/2021 sawa na ongezeko la asilimia **2.2**. Ongezeko hili limetokana na viwanda kuongeza usindikaji ambapo sasa usindikaji umeongezeka kutoka asilimia 20 hadi asilimia 30 ya uwezo uliosimikwa (*installed capacity*). Aidha, hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2021 kuna jumla ya viwanda vya kusindika maziwa **99** kati ya hivyo, viwanda **96** vinafanya kazi na viwanda **3** havifanyi kazi kutokana changamoto mbalimbali ikiwemo ushindani wa kibiashara (**Kiambatisho Na. 2**).

14. ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa zao la nyama umeongezeka kutoka tani **701,679.1** mwaka 2019/2020 hadi tani **738,166** mwaka 2020/2021 sawa na ongezeko la asilimia **5.2 (Kiambatisho Na. 1)**. Kati ya hizo, tani **508,355.17** ni za nyama ya ng'ombe; tani **102,137.22** za nyama ya mbuzi na kondoo; tani **86,205.78** za nyama ya kuku na tani **41,467.82** za nyama ya nguruwe.

15. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021 uzalishaji wa mayai umeongezeka kutoka mayai **bilioni 3.58** mwaka 2019/2020 hadi mayai **bilioni 4.5** mwaka 2020/2021 sawa na

ongezeko la asilimia **26 (Kiambatisho Na. 1)**. Ongezeko hilo limesababishwa na kuongezeka kwa vituo vya kutotolesha vifaranga vya kuku kutoka 26 mwaka 2019/2020 hadi 28 mwaka 2020/2021 na wananchi kuhamasika kufuga kuku ili kujikomboa kiuchumi.

16. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2021 vipande vya ngozi milioni **11.77** (ng'ombe milioni **4.17,** mbuzi milioni **5.96** na kondoo milioni **1.64)** vyenye thamani ya shilingi **bilioni 25.93** vimezalishwa ikilinganishwa na vipande milioni **11.23** (ng'ombe – milioni – **4.03**, mbuzi milioni - **5.6** na kondoo milioni - **1.6** vyenye thamani ya shilingi **bilioni 22.8** vilivyozalishwa mwaka 2019/2020.

17. ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2021 jumla ya vipande vya ngozi milioni **1.50** vyenye uzito wa kilo **7,951,004** (ng'ombe kilo **7,250,879,** mbuzi/kondoo kilo **119,654** na punda kilo **580,480**) vyenye thamani ya shilingi bilioni **16.1** viliuzwa nje ya nchi katika nchi za Ghana, Nigeria, Italy, Ethiopia, Indonesia, Vietnam, Kenya na China ikilinganishwa na vipande vya ngozi vyenye uzito wa kilo **6,747,011** (ng'ombe – **5,948,791**; mbuzi/kondoo – **114,904** na punda – **683,317**) vyenye thamani ya shilingi bilioni **12.9** vilivyouzwa nje katika nchi za Ghana, China, Pakistan, Indonesia, Ethiopia, Nigeria na Italy mwaka 2019/2020 kipindi kama hicho. Sababu za kuongezeka kwa mauzo ya ngozi nje ya nchi ni kuongezeka kwa mahitaji ya ngozi katika nchi za Ghana na Nigeria.

UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2020/2021 NA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2021 /2022

Maeneo ya Kipaumbele katika Mwaka 2020/2021

18. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021 maeneo ya kipaumbele katika Mpango na Bajeti ya Wizara kupitia Idara Kuu ya Mifugo (Fungu 99) yaliyotekelezwa ni pamoja na:-

(i) Kuimarisha afya ya mifugo;

(ii) Kuwezesha upatikanaji endelevu wa rasilimali za vyakula vya mifugo na maji kwa ajili ya mifugo;

(iii) Kuboresha kosaafu ya mifugo ili kuongeza tija na uzalishaji:

(iv) Kuboresha biashara ya mifugo ndani na nje:

(v) Kuimarisha huduma za utafiti wa mifugo, huduma za ugani na mafunzo kwa wafugaji na maafisa ugani;

(vi) Kuanzisha na kuimarisha vikundi na vyama vya ushirikavya mazao ya mifugo;

(vii) Kusimamia na kuratibu shughuli za taasisi zilizo chini ya Wizara;

(viii) Kuboresha masuala ya rasilimali watu;

(ix) Kuboresha utekelezaji wa sera, sheria na kanuni katika sekta ya mifugo; na

(x) Kuimarisha uratibu na usimamizi wa wataalamu wa sekta ya mifugo.

Makusanyo ya Maduhuli

19. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Fungu 99 ilitarajia kukusanya kiasi cha shilingi **50,000,000,000.00**. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2021 kiasi cha shilingi **32,779,275,605.06** kimekusanywa sawa na asilimia **66** ya lengo la makusanyo kwa mwaka 2020/2021. Hata hivyo, makusanyo hayo ni sawa na asilimia **75** ya makusanyo yaliyolengwa kukusanywa ndani ya kipindi cha miezi kumi na nusu (**10.5**) ambayo ni shilingi **bilioni 43.8.** Makusanyo hayo hadi tarehe 15 Mei, 2021 (**32,779,275,605.06**) yamepungua kwa shilingi **7,235,716,790.19** ikilinganishwa na kipindi kama hicho

mwaka 2019/2020 ambapo makusanyo yalifikia shilingi **40,014,992,395.25**. Upungufu huu kwa kiasi kikubwa umechangiwa na kupungua kwa biashara ya mifugo na mazao yake nje ya nchi na mwenendo wa biashara ya ngozi. Mathalani katika mwaka wa fedha 2019/2020 hadi 15 Mei, 2020 makusanyo yatokanayo na mauzo ya mazao ya mifugo nje ya nchi yalikuwa shilingi **1,568,282,255.95**, huduma za ukaguzi wa mifugo shilingi **11,055,137,530.56** na Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo shilingi **8,656,640,195.00** ikilinganishwa na shilingi **352,534,255.67**; shilingi **9,736,208,360.25**; na shilingi **7,313,159,738.00** zilizokusanywa hadi tarehe 15 Mei, 2021 mtawalia. Hii ni pungufu ya shilingi **3,629,377,306.92** kutoka katika vyanzo tajwa kutokana na athari za COVID 19.

Fedha Zilizoidhinishwa kwa Ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo 2020/2021

20. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Fungu 99 ilitengewa jumla ya shilingi **38,929,091,304.01.** Kati ya Fedha hizo, shilingi **28,587,804,438.76** ni fedha za Matumizi ya Kawaida na shilingi **10,341,286,865.25** ni fedha kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

Matumizi ya Bajeti ya Kawaida

21. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021, Fungu 99 lilitengewa jumla ya shilingi **28,587,804,438.76**. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2021, jumla ya shilingi **23,524,701,194.23** zilikuwa zimetolewa, ambazo ni sawa na asilimia **82** ya bajeti iliyotarajiwa kwa miezi kumi na miwili, ikiwa ni sawa na asilimia **94** ya kipindi cha miezi kumi na nusu (yaani hadi 15 Mei, 2021). Kati ya hizo, shilingi **13,686,921,045.71** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara (PE) na shilingi **9,837,780,148.52** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

Matumizi ya Bajeti ya Maendeleo

22. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Fungu 99 ilitengewa jumla ya shilingi **10,341,286,865.25** kwa ajili ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo zikiwa ni fedha za ndani ili kutekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya

Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II). Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2021 kiasi cha shilingi **6,902,623,129.68** (sawa na asilimia **67**) kilipokelewa kutoka Wizara ya Fedha na Mipango. Hii ni sawa na asilimia **80** kwa kipindi cha miezi 10.

Sera, Sheria na Kanuni Katika Sekta ya Mifugo

Sera, Mikakati na Programu

23. ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2020/2021 Wizara imeendelea kutoa elimu kuhusu Sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006 na Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta ya Mifugo Tanzania (Tanzania Livestock Master Plan - TLMP). Jumla ya wadau **6,172** walipata elimu hiyo kupitia Maonesho ya Sabasaba, Nanenane na Siku ya Chakula Duniani. Aidha, Wizara imesambaza nakala **120** za Sera ya Taifa ya Mifugo na nakala **80** za Fursa za Uwekezaji kwa wadau katika Sekta ya Mifugo. Pia, Wizara imeanza mapitio ya Sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006 ili kubaini uhitaji wa kuboresha Sera hiyo. Vilevile, Wizara imefanya mapitio na kuboresha Mpango Mkakati wa Muda wa Kati (Medium Term Strategic Plan - MTSP) ambao ni wa miaka mitano kuanzia 2021/2022 hadi 2025/ 2026.

24. ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2021/2022, Wizara itaendelea kutekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili *(Agriculture Sector Development Programme – ASDP II)* na kukamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006 na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya mifugo, Wakala, Bodi na Taasisi zilizo chini ya Wizara.

Sheria na Kanuni

25. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kupitia Sheria za sekta ya mifugo kwa ajili ya kuboresha mazingira na kuwezesha ukuaji wa sekta ya mifugo ambapo kanuni mpya nne (**4**) zimeandaliwa na kutangazwa katika Gazeti la Serikali ambazo ni; *Hides, Skin and Leather Trade* (*Appointment of Inspector) Notice, 2020 GN No.619* chini ya Sheria ya Biashara

ya Ngozi SURA 120; *Animal Welfare (Impounded Animal) Regulations, 2020 GN. No.724* chini ya Sheria ya Ustawi wa Wanyama SURA 154; *The Veterinary (Internship for Veterinarians) Regulations, 2020 GN. No.725* na *The Veterinary (Internship for paraprofessionals) Regulations, 2020 GN. No.726* Chini ya Sheria ya Veterinari SURA 319.

26. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya kanuni sita (6) zimefanyiwa marekebisho Chini ya Sheria ya Tasnia ya Maziwa SURA 262 ambazo ni:-

(i) *The Dairy Industry (Registration of Dairy Industry Stakeholders) (Amendment), Regulations 2020 GN No.540;*

(ii) *The Dairy Industry (Raw Milk Transportation) (Amendment) Regulations,2020 GN No.535;*

(iii) *The Dairy Industry (Treatment and Disposal of Unfit Milk)(Amendment) Regulations,2020 GN No.539;*

(iv) *The Dairy Industry (Duties and Powers of Inspector and Analysts) (Amendment) Regulations, 2020 GN No.537;*

(v) *The Dairy Industry (Raw Milk Grading and Minimum Quality and Safety Requirements) (Amendment) Regulations, 2020 GN No.534; na*

(vi) *The Dairy Industry (Import and Export of Milk and Milk Products (Amendment) Regulations, 2020 GN No.536*

27. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya kanuni tatu (3) zimefanyiwa marekebisho Chini ya Sheria ya Tasnia ya Nyama SURA 421 ambazo ni:-

(i) *The meat industry (registration of meat industry Stakeholders) (amendment) regulations, GN. No. 183;*

(ii) *The meat industry (inspection of meat industry stakeholders' activities) (amendment) regulations, GN. No. 184;* na

(iii) *The Meat Industry (Import and Export of Livestock, Meat and Meat Products) (Amendment) Regulations, GN. No.185.*

28. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021,Wizara imekamilisha Kanuni (3) chini ya Sheria ya Nyanda za Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Mifugo ambazo ni:-

(i) *Import and Export of Animal Feeds Resources;*

(ii) *Registration and Movement of Animal Feed Resources and Products;* na

(iii) *Packaging, Branding, Labelling and Sealing.*

29. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022 Wizara itaendelea kuratibu na kuboresha Sheria, Kanuni na Taratibu kuhusu usimamizi na
uendelezaji wa sekta ya mifugo nchini

Uzalishaji wa Mifugo na Masoko

Huduma ya Uhimilishaji

30. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji (NAIC) kwa kushirikiana na Halmashauri na Sekta Binafsi imeendelea kuwezesha utoaji wa huduma ya uhimilishaji kwa wafugaji hapa nchini ambapo hadi tarehe 30 Aprili, 2021 jumla ya ng'ombe **77,375** wamehimilishwa (Kiambatisho Na.3) ikilinganishwa na ng'ombe **76,612** waliohimilishwa mwaka 2019/2020.

31. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuboresha mifugo hapa nchini Wizara imeendelea kukiboresha Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji (NAIC) kwa kukipatia madume bora nane (**8**) ya mbegu kutoka nchini Afrika Kusini. Madume yaliyonunuliwa ni Fresian (**2**), Ayrshire (**2**), Jersey (**1**), Simmental (**1**) na Flckvieh (**2**). Vilevile, vituo vitatu (**3**) vya Uhimilishaji vya Kanda ya Mashariki (Kibaha Pwani), Kanda ya Kati (Dodoma) na Kanda ya Kusini (Lindi) vimeendelea kuwezeshwa ili kutoa huduma endelevu ya uhimilishaji katika maeneo ya kanda tajwa.

32. ***Mheshimiwa Spika*,** Wizara kupitia Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji (NAIC) kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya na Sekretarieti za Mikoa imeanzisha na kuendeleza kambi za uhimilishaji katika Mikoa ya Dodoma (Kongwa), Katavi (Sumbawanga), Simiyu (Meatu), Geita (Chato na Bukombe), Kagera (Misenyi na Kyerwa), Pwani (Mkuranga na Kisarawe), Lindi (Ruangwa), Mara (Butiama, Musoma, Bunda na Serengeti), Morogoro (Kilosa na Mvomero) na Tanga (Muheza, Tanga Jiji na Korogwe). Aidha, hadi Machi, 2021 jumla ya ng'ombe **7,896** wamehimilishwa bure kwa gharama za Serikali kupitia kambi hizo (Kiambatisho Na.4). Vilevile, jumla ya wahimilishaji **118** katika maeneo ya kambi wamejengewa uwezo juu ya utoaji wa huduma ya uhimilishaji kwa vitendo.

33. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022 Wizara itaendelea kuimarisha Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji, Vituo saba (**7**) vya Uhimilishaji vya kanda na kuwezesha uendelezaji na uanzishaji wa kambi za uhimilishaji kwa lengo la kuhimilisha ng'ombe **1,000,000** pamoja na kuwajengea uwezo wahimilishaji **150** katika Halmashauri za Wilaya.

Uzalishaji na Usambazaji wa Mitamba

34. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021 jumla ya mitamba **18,012** ya maziwa na nyama imezalishwa na kusambazwa kwa wafugaji. Kati ya hiyo, mitamba **3,460** imezalishwa katika Mashamba ya Serikali (Kiambatisho Na.5) na mitamba **14,562** imezalishwa kutoka katika mashamba binafsi ikilinganishwa jumla ya mitamba **16,809** iliyosambazwa mwaka 2019/2020 ambapo kutoka katika Mashamba ya Serikali ilikuwa mitamba **2,349** na kutoka kwa wafugaji binafsi ilikuwa mitamba**14,460.**

35. ***Mheshimiwa Spika*,** ili kuboresha uzalishaji wa mitamba katika mashamba ya Serikali, katika mwaka 2020/ 2021 Wizara imeliwezesha shamba la mifugo Nangaramo kwa kulipatia mitamba **53** ili kuongeza ng'ombe wazazi (*parent stock*) katika shamba hilo. Uboreshaji kama huo utaendelea kufanyika katika mashamba mengine ya Kitulo, Ngerengere, Mabuki na Sao Hill.

36. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022 Wizara itanunua mitamba bora **300** ya Borani kwa ajili ya mashamba **4** ya kuzalisha mifugo ya Serikali ili kuboresha uzalishaji wa mitamba katika mashamba hayo. Pia, Wizara itasambaza mitamba **1,000** kwa bei ya ruzuku kutoka katika mashamba matano (5) ya Serikali. Aidha, Wizara inatoa wito kwa wadau binafsi kuendelea kuwekeza katika tasnia ya uzalishaji wa Mitamba bora ya Maziwa na Nyama kutokana na fursa kubwa iliyopo katika eneo hili inayosababishwa na uhitaji mkubwa wa mitamba bora hapa nchini.

Uzalishaji wa Kuku na Mayai

37. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/2021, vituo vya kutotolesha vifaranga vimeongezeka kutoka vituo **26** mwaka 2019/2020 hadi kufikia vituo **28** (**Kiambatisho Na.6**). Vituo hivyo vipo katika mikoa ya Dar es Salaam (9), Iringa (2), Njombe (1), Pwani (11), Kilimanjaro (2), Arusha (1), Mbeya (1) na Mwanza (1). Aidha, mashamba ya kuku wazazi nchini yameongezeka kutoka 20 hadi 22 (**Kiambatisho Na.7**) katika kipindi hicho yenye uwezo wa kutunza zaidi ya kuku wazazi 1,300,000.

38. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka **2020/2021**, jumla ya vifaranga **88,348,000** vimezalishwa na kusambazwa nchini. Kati ya hivyo, vifaranga **52,000,000** ni wa nyama, vifaranga **28,964,000** ni vya kuku chotara ambapo Sasso ni **15,600,000** na Kroiler **13,364,000** na vifaranga **7,384,000** ni wa kuku wa mayai ikilinganishwa na vifaranga **70,323,000** vilivyozalishwa mwaka 2019/2020.

39. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022 Wizara itaendelea kushirikiana na wazalishaji wa vifaranga vya kuku ili kuhakikisha wafugaji wanapata vifaranga bora katika ukuaji na ustahilivu wa magonjwa ili kujikomboa kiuchumi. Aidha, Wizara kupitia Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (TALIRI) itaendeleza tafiti za uzalishaji wa kuku wa kienyeji (*dual purpose*) aina ya Horasi kwa wafugaji nchini. Matoke tarajiwa ya mradi huu wa kuku wa asili aina ya horasi ni:-

i. Kuwezesha Tanzania kuwa na aina yake ya kuku wa asili wazazi;

ii. Kuwezesha nchi kujitegemea katika tasnia ya kuku kwa kuwa na mashamba ya kuku wa asili wazazi;

iii. Upatikanaji wa kuku wa asili mwenye uzito mkubwa kutoka gramu 500 -750 kwa sasa hadi kufikia kilogramu 1.5 akiwa na umri wa miezi 4.

iv. Kuongeza umbo na uzito wa yai la kuku wa asili kutoka gramu 25-45 ya sasa hadi kufikia gramu 50-60.

v. Kuongeza kiwango cha utagaji wa mayai toka 40-60 ilivyo sasa hadi kufikia 150-200 kwa kuku kwa mwaka

Uzalishaji wa Nguruwe

40. ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2020/201 Wizara kwa kushirikiana na Chama cha Wafugaji wa Nguruwe Tanzania (TAPIFA) imeratibu uingizaji nchini wa mbegu bora ya nguruwe **91** wenye umri mbalimbali. Aina za nguruwe zilizoingizwa ni Cambo, TN70 (*latest version of Large white*). Mbegu hii bora ya Nguruwe kutoka Zambia imesambazwa kwa Wanachama wa TAPIFA waliopo katika Mikoa ya Iringa, Morogoro, Pwani na Dar es Salaam. Kuletwa kwa mbegu bora ya nguruwe kumesaidia kupunguza changamoto kubwa ya vizazi/koo za nguruwe waliopo nchini kupandana (*inbreeding)*. Aidha, Wizara inampongeza mwekezaji binafsi wa *Phema Piggery Breeding Farm* aliyopo Bagamoyo kwa kuanzisha uhimilishaji wa nguruwe ambapo hadi tarehe 31 Machi, 2021 wafugaji **40** wamefikiwa na huduma hiyo katika mikoa ya Arusha, Morogoro, Pwani na Dar es Salaam na jumla ya nguruwe **160** wamehimilishwa.

41. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021 jumla ya tani **41,467.82** za nyama ya nguruwe zimezalishwa ikilinganishwa na tani **38,377.4** zilizozalishwa mwaka 2019/ 2020 sawa na ongezeko la asilimia **8**. Aidha, Wizara

inahamasisha wafugaji wa nguruwe kutumia mbegu bora kwa teknolojia ya uhimilishaji pamoja na kuzitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa kutenga maeneo kwa ajili ujenzi wa machinjio za nguruwe.

42. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022 Wizara itaendelea kushirikana na TAPIFA katika uingizaji na uzalishaji wa ndani wa mbegu bora za nguruwe pamoja na ufugaji wa kisasa wa nguruwe.

Haki Miliki za Waboreshaji Mbari za Wanyama

43. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021, Wizara imeendelea kuimarisha uwezo wake wa uchambuzi na utambuzi wa koo **12** za ng'ombe wa asili zilizopo nchini na zilizopo katika hatari ya kutoweka. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2021, Wizara imetoa mafunzo elekezi kuhusu uchambuzi wa mbari za mifugo ya asili kwa wataalam **18**. Pia, Wizara imeendelea kuhamasisha wafugaji kuhusu utambuzi wa mbari za mifugo ya asili, ambapo jumla ya wafugaji **107** wamehamasika kushiriki katika zoezi la utambuzi wa koo za mifugo ya asili katika Mikoa ya Singida (**45**), Iringa (**52**) na Dodoma (**10**).

44. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022 Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itafanya tambuzi na tathmini za mbari za wanyama (*characterization*) zilizopo nchini na kusajili mbari, wanyama wa mbegu na waboreshaji mbari katika mikoa mitatu (**3**) ya Mara, Shinyanga na Kagera; na kusimamia eneo la utoaji huduma ya uhimilishaji mifugo.

Biashara ya Mifugo na Mazao Yake

Biashara ya Mifugo

45. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/2021 hadi tarehe 30 Aprili, 2021 jumla ya ng'ombe **1,843,904** mbuzi **2,081,233** kondoo **360,745** na punda **191,656** wenye thamani ya shilingi Trilioni **1.5** waliuzwa katika minada mbalimbali hapa nchini ikilinganishwa na ng'ombe 1**,513,926**, mbuzi **1,733,463,**

kondoo **299,157** na punda **198,000** wenye thamani ya shilingi Trilioni **1.06** waliouzwa hapa nchini mwaka 2019/2020 kipindi kama hicho. Sababu za kuongezeka kwa biashara ya mifugo hapa nchini imetokana na serikali kutengeneza mazingira rafiki ya biashara ya mifugo na kutoa elimu juu ya taratibu na kanuni za biashara ya mifugo kwa wadau mbalimbali. Hadi tarehe 30 Aprili, 2021, jumla ya Shilingi **12,247,233,701.81** zilikusanywa kutoka katika minada ya awali, upili na mpakani kama Maduhuli ya Serikali ikilinganishwa na jumla ya shilingi **7,945,676,541.20** zilizokusanywa kutoka katika minada ya awali, upili na mpakani mwaka 2019/2020 kwa kipindi kama hicho.

Udhibiti wa Biashara ya Mifugo na mazao yake

46. ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2020/2021 Wizara imeongeza idadi ya vituo vya doria vya kimkakati kutoka vitatu (**3**) vya Lamadi (Busega), Nderema (Handeni) na Makuyuni (Monduli) hadi vituo **10** katika maeneo ya Kyaka (Missenyi), Wasso (Loliondo), Makambako (Njombe), Msolwa (Chalinze), Tunduma (Momba), Darajani (Serengeti) na Buhigwe (Buhigwe) kwa lengo la kurahisisha biashara na kudhibiti utoroshwaji mifugo na mazao yake. Aidha, kati ya mwezi Machi na Mei, 2021 jumla ya shilingi **629,328,500** zimekusanywa kupitia vituo hivyo.

47. ***Mheshimiwa Spika****,* katika mwaka 2021/2022 Wizara itaendelea kujenga na kukarabati minada ya mifugo ya upili na mipakani ili kuwezesha biashara ya mifugo ndani na nje ya nchi pamoja na kuimarisha vituo vya doria vya kimkakati.

Kodi, Ada na Tozo Katika Sekta ya Mifugo

48. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imekuwa ikipokea malalamiko kutoka kwa wadau wa sekta ya mifugo kuhusu ada na tozo mbalimbali hususan tozo ya asilimia 1 ya thamani ya mzigo (*FOB Value*) kwa nyama zinazouzwa nje ya nchi na ada ya ukaguzi wa mazao ya mifugo. Kufuatia hali hiyo Wizara imefanya mapitio ya tozo hizo ili kuzibadilisha lengo likiwa ni kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji na kuongeza mauzo ya mazao ya mifugo nje ya nchi. Maboresho

yaliyofanyika yatawasilishwa na Waziri wa Fedha na Mipango wakati akiwasilisha Muswada wa Sheria ya Fedha (Finance Bill) ya mwaka 2021/2022.

49. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/2022, Wizara itaendelea kutathmini tozo na ada mbalimbali zitakazoonekana kuwa kero kwa wazalishaji na wafanyabiashara wa mifugo na mazao yake ili kuzifuta au kuzifanyia marekebisho.

Zao la Ngozi

50. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara inaendelea kusimamia ubora wa ngozi zinazozalishwa hapa nchini kwa kutumia Sheria ya Biashara ya Ngozi Na. 18 ya mwaka 2008 na Kanuni zake za mwaka 2010. Katika mwaka 2020/2021, Wizara imeteua na kuwatangaza kwenye Gazeti la Serikali Na**. 619** la tarehe 7 Agosti, 2020 wakaguzi wa ngozi **113** kutoka Mikoa **11** ya kimkakati.

51. ***Mheshimwa Spika***, katika mwaka 2020/2021 jumla ya Wakaguzi wa ngozi **60** kati ya **113** walioteuliwa wamejengewa uwezo kwa kupatiwa mafunzo; vitambulisho na nakala ya Sheria ya Biashara ya Ngozi na Kanuni zake katika Mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Pwani; Mwanza; Shinyanga; Simiyu na Mara. Pia, Wachunaji Ngozi **423** wamepatiwa mafunzo katika machinjio za Jiji la Dar es Salaam; na leseni **666** zimetolewa kwa wachunaji ngozi wa Mikoa ya Dar es Salaam, Manyara, Mwanza, Simiyu, Shinyanga, Kagera, Arusha na Kilimanjaro. Vilevile, visu maalum **131** vimetolewa kwa wachunaji ngozi za wanyama wa Mikoa ya Kagera na Simiyu.

52. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imefanya tathmini na ufuatiliaji wa upatikanaji na ubora wa ngozi kupitia Kiwanda cha *ACE Leath*er cha Morogoro na *Kilimanjaro International Leather Company Limited* na kubaini kuwa kati ya mwaka 2019 na 2021 ubora wa ngozi zinazozalishwa katika Machinjio hizo umeongezeka kutoka asilimia **30** hadi **80** kutokana na mafunzo ya uchunaji ngozi na matumizi ya visu maalum vya kuchunia ngozi.

53. ***Mheshimiwa Spika*;** katika mwaka 2021/2022, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa tasnia ya ngozi itaendelea kusimamia ubora wa ngozi zinazozalishwa hapa nchini na kuhakikisha kuwa ngozi zote zinapangwa katika madaraja kabla ya kuuzwa; kufanya mapitio ya Sheria ya Biashara ya Ngozi Na. 18 ya mwaka 2008 na Kanuni zake za mwaka 2010; na kufanya mapitio na kuhuisha Mkakati wa Kuendeleza Tasnia ya Ngozi (*Tanzania Leather Sector Develepment Strategy 2016 – 2020*).

Machinjio ya Dodoma

54. ***Mheshimiwa Spika,*** Machinjio ya Dodoma inaendelea na shughuli za uchinjaji wa mifugo kwa soko la ndani na nje ya nchi. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2021 jumla ya ng'ombe **41,020** na mbuzi **23,004** walichinjwa. Aidha, katika kipindi hicho, Machinjio ilianzisha huduma ya kuchakata nyama kulingana na mahitaji ya wateja ambapo jumla ya kilo **18,943.6** za nyama ya ng'ombe zilichakatwa kwa ajili ya masoko maalum ya ndani ikiwemo Kampuni ya Ujenzi wa SGR ya Yapi Merkez.

55. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa soko la nje, jumla ya mbuzi na kondoo **17,732** walichinjwa na kuzalisha jumla ya kilo **159,588** (tani **160**) kwa ajili ya wateja mbalimbali waliosafirisha nyama kwenda nchi za Oman, Qatar na Vietnam zikiwa zimepozwa (*Chilled*), zimegandishwa (*Frozen*) na zimenyonyolewa (*Shoats with skin*). Pia, jumla ya ng'ombe **45** sawa na kilo **5,400** (tani **5.4**) wamepokelewa, kuchinjwa na kugandishwa kwa ajili ya kuuzwa nje ya nchi (Oman).

56. ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2020/2021 baada ya Serikali kuchukua Machinjio ya Dodoma ni pamoja na:-

(i) Kuongezeka kwa wastani wa idadi ya ng'ombe wanaochinjwa kwa mwezi kwa ajili ya soko la ndani, kutoka wastani wa ng'ombe **1,950** hadi ng'ombe **4,050**; na

(ii) Wastani wa mbuzi wanaochinjwa kwa ajili ya soko la nje imefika mbuzi **2,217** kwa mwezi ambapo katika mwaka 2019/2020 hakukuwa na mbuzi waliochinjwa.

57. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022 Machinjio ya Dodoma itaendelea kuimarishwa kwa kupatiwa vitendea kazi na kukarabatiwa ili itumike kikamilifu katika kuwezesha biashara ya nyama ndani na nje ya nchi.

Rasilimali za Malisho, Vyakula na Maji kwa Mifugo

Malisho, Vyakula na Maji kwa Mifugo

58. ***Mheshimiwa Spika*****,** Wizara inaendelea kutekeleza Mkakati wa Upatikanaji wa Uhakika wa Malisho na Maji kwa Mifugo. Katika mwaka 2020/2021, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya na Sekta binafsi imeendelea kuboresha miundombinu ya maji kwa ajili ya mifugo ambapo ujenzi wa visima virefu viwili (**2**) katika Halmashauri ya Wilaya ya Iringa (Usolanga) na Mpapa (Manyoni) vimefikia asilimia **70** na asilimia **30** mtawalia. Pia, ukarabati wa mabwawa matatu (**3**) ya Chamakweza (Chalinze), Kimokoua (Longido) na Narakauo (Simanjiro) umefikia asilimia **100**, asilimia **100** na asilimia **100** mtawalia.

59. ***Mheshimiwa Spika*****,** Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Mipango na Matumizi ya Ardhi na Halmashauri za Wilaya, imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria na Kanuni zinazohusu utengaji na upimaji wa maeneo kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo malisho ya mifugo. Katika mwaka 2020/2021 Halmashauri za Wilaya kumi na saba(17) zimetenga jumla ya Hekta **271,661.11** kwa ajili ya malisho ya mifugo. Hivyo, maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya malisho yameongezeka kufikia hekta **3,060,562.27** mwaka 2020/2021 ikilinganishwa na hekta **2,788,901.17** katika mwaka 2019/2020 (**Kiambatisho Na**. 8).

60. ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2021/ 2022,Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa itaendelea kutenga maeneo kwa ajili ya malisho, kuimarisha

miundombinu ya maji kwa ajili ya mifugo kwa kuchimba malambo na visima virefu hususan katika maeneo yenye uhitaji mkubwa wa maji.

61. ***Mheshimiwa Spika*****,** ili kuongeza upatikanaji wa malisho na mbegu za malisho, jumla ya marobota ya hei **81,188** yamezalishwa kutoka katika mashamba ya Serikali ya Vikuge (**14,194**), Langwira (**3,773**), TALIRI (**21,388**), Sao Hill (**20,000**), Mabuki (**13,343**), LITA (**5,391**) na NARCO (**3,094**). Pia, jumla ya kilo **3,874.5** za mbegu bora za malisho na vipandikizi **8,255** zimezalishwa katika mashamba ya Serikali ya Vikuge **(**mbegu kilo **267)** na (vipandikizi **255**); Langwira (mbegu kilo **328**); TALIRI (mbegu kilo **1,550** na vipandikizi **8,000**); LMU Sao Hill (mbegu kilo **1,500**), LMU Mabuki (mbegu kilo **154**) na LITA (mbegu kilo **76**).

62. ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2020/2021 viwanda vya kutengeneza vyakula vya mifugo vimeongezeka na kufikia **154** kutoka viwanda **105** mwaka 2019/2020 **(Kiambatisho Na. 9).** Hivyo, kuongeza uzalishaji wa vyakula vya wanyama kutoka tani **900,000** mwaka 2019/2020 hadi tani **1,200,000** mwaka 2020/2021.

63. ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2020/2021 Wizara imeongeza idadi ya wakaguzi wa vyakula vya mifugo na maeneo ya malisho kufikia **176** kutoka **165** mwaka 2019/2020. Ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi jumla ya wakaguzi **66** wamepatiwa mafunzo rejea kwa ajili ya kuhakikisha ubora na usalama wa vyakula vya mifugo**.** Aidha, maeneo **45** ya kuzalisha, **78** kuuza na **18** kuhifadhia rasilimali za vyakula vya mifugo yamesajiliwa (**kiambatisho Na.10**).

64. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/2022, Wizara itaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika uzalishaji wa vyakula bora vya mifugo; kusimamia na kudhibiti ubora na usalama wa vyakula vya mifugo; kutoa mafunzo rejea kwa wakaguzi **79** wa vyakula vya mifugo na maeneo ya malisho; na kuimarisha mashamba ya Serikali ya kuzalisha malisho na mbegu kwa kuyapatia vitendea kazi ili kuongeza

uzalishaji wa mbegu pamoja na marobota ya hei. Tayari Wizara imewasiliana na ofisi ya ubalozi wa Tanzania China na wadau wa sekta binafsi kwa ajili ya mkakati maalum wa kuzalisha mbegu za majani ya Juncau kutoka China. Mpango huu utakuwa mkombozi kwa wafugaji. Nachukua fursa hii kuikaribisha sekta binafsi kuwekeza katika uzalishaji wa mbegu za malisho na malisho.

Ustawi wa Wanyama

65. ***Mheshimiwa Spika,*** matukio ya ukamataji mifugo yasiyofuata utaratibu kwenye maeneo ya hifadhi kwa mwaka 2020/2021 yamepungua ambapo mifugo **6,245,356 (kiambatisho Na. 11)** ilikamatwa ikilinganishwa na mifugo **14,668,323** iliyokamatwa kwenye kipindi cha mwaka 2019/ 2020. Hali hii imetokana na wadau mbalimbali kuelewa Sheria ya Ustawi wa Wanyama Na. 19 ya mwaka 2008; na Sheria ya Magonjwa ya Wanyama Na. 17 ya mwaka 2003. Aidha, Wizara imetengeneza Kanuni za *Animal Welfare (Impounded Animal) Regulation 2020 GN No. 724* ambazo zimeanza kutumika na hivyo kupunguza matukio ya ukamataji mifugo kiholela.

Utatuzi wa Migogoro Baina ya Wafugaji na Watumiaji Wengine wa Ardhi

66. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/2021, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, imeendelea kutatua migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi ambapo utatuzi umefanyika katika Wilaya **5** za Mikoa **4 (Kiambatisho Na. 12)**. Pia, utatuzi wa migogoro umefanyika baina ya vijiji na Kituo cha Karantini cha Kwala mkoani Pwani ambapo jumla ya Hekta **3,139.2** zimegawiwa kwa vijiji vya Dutumi (Hekta **1,600**), Madege (Hekta **400**), Kwala (Hekta **400**), Mwembengozi (Hekta **400**) na Eneo la Mkuza Chicks (Hekta **179.2**) na Kitongoji cha Kisogo (Hekta **160**).

67. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/2022 Wizara itaendelea kutatua migogoro ya ardhi kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa rasilimali ardhi ikiwemo kutoa elimu

ya ufugaji bora wa mifugo unaozingatia maeneo ya malisho; kuratibu na kusimamia haki na ustawi wa wanyama kwa mujibu wa Sheria zilizopo.

Huduma ya Afya ya Mifugo

Magonjwa ya Mifugo

68. ***Mheshimiwa Spika,*** magonjwa mbalimbali ya mifugo yameendelea kuwa kikwazo katika uzalishaji na biashara ya mifugo na mazao yake. Magonjwa haya yanaathiri aina zote za wanyama na baadhi ya magonjwa huathiri binadamu.

69. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na wadau wa mifugo inaendelea kutekeleza mikakati ya kudhibiti magonjwa ya mifugo yaenezwayo na wadudu. Katika mwaka 2020/2021 mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

(i) Wizara ilizindua kampeni ya tatu ya kuogesha mifugo ambayo ilifanyika tarehe 10 Oktoba 2020 katika Wilaya ya Bahi Mkoani Dodoma.

(ii) Jumla ya lita **15,579.25** ya dawa za kuogeshea mifugo zenye thamani ya shilingi **592,804,625** zilisambazwa kwenye majosho **1,983** katika Halmashauri **162** zilizoko kwenye mikoa **25** Tanzania Bara.

(iii) Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2021 jumla ya michovyo ya kuogesha mifugo **446,997,857** sawa na asilimia **110** ya lengo la kuogesha mifugo **405,000,000** ambapo michovyo ya ng'ombe ni **342,968,774** mbuzi **89,649,306** na kondoo **14,364,827** (**Kiambatanisho Na. 13**).

70. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imefanya mapitio na kuboresha Kanuni na Mwongozo wa Uogeshaji ambao unatoa maelezo ya namna ya uogeshaji mifugo. Kanuni na Mwongozo huo umeainisha majukumu mbalimbali ya wadau ikiwemo bei elekezi ya kuogesha mifugo ya shilingi **50** kwa ng'ombe na shilingi **10** kwa mbuzi au kondoo.

71. ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za kudhibiti magonjwa ya mifugo**,** tarehe 22 Januari, 2021 Wizara ilizindua rasmi mwongozo wa uchanjaji mifugo. Mwongozo huo umeainisha majukumu ya Serikali Kuu, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekta Binafsi katika uchanjaji mifugo. Aidha, mwongozo huo umetoa bei elekezi wa kila chanjo inayozalishwa nchini. Lengo la Mwongozo huo ni kuhakikisha wafugaji wanapata huduma bora za chanjo na wanashiriki kikamilifu katika mazoezi ya uchanjaji mifugo.

72. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na wadau iliendelea kutekeleza mikakati ya kudhibiti magonjwa ya mifugo ya mlipuko na yanayovuka mipaka kwa kutumia chanjo, kutoa elimu kwa wafugaji, kufuatilia magonjwa na tiba. Katika mwaka 2020/2021 mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

(i) Utoaji wa chanjo umefanyika kwa mbuzi na kondoo **3,280,661** dhidi ya Ugonjwa wa Sotoka ya Mbuzi na Kondoo; ng'ombe **5,479,270** dhidi ya Ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya Ng'ombe (CBPP); na ng'ombe **2,518,600** dhidi ya Ugonjwa wa Miguu na Midomo.

(ii) Jumla ya dozi **35,474,800** za Chanjo ya Matone ya Ugonjwa wa Mdondo (I_2) zimezalishwa na kusambazwa katika mikoa yote. Aidha, jumla ya kuku **57,773,685** walichanjwa dhidi ya ugonjwa wa mdondo kwa chanjo ya Matone (**35,474,800**) ambapo kuku **22,298,885** walichanjwa kwa kutumia chanjo ya maji (Lasota) inayonunuliwa na kusambazwa na sekta binafsi.

(iii) Chanjo mpya (Tatu Moja) iliyogunduliwa na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine inayotumika kuzuia magonjwa matatu ya kuku (Mdondo, Ndui ya Kuku na Mafua ya Kuku) imegunduliwa na kuanza kutumika kuanzia tarehe 01 Machi 2021 kwa gharama ya shilling **6,800** kwa chupa inayochanja kuku **200** sawa na wastani wa shilingi **34**kwa dozi.

73. ***Mheshimiwa Spika***, napenda kuchukua nafasi hii kulitaarifu Bunge lako tukufu kuhusu mlipuko wa Homa ya Nguruwe (African Swine Fever - ASF) ambao ulilipuka kwa vipindi mbalimbali katika mwaka 2020/2021 na kusababisha jumla ya vifo **5,428** katika Halmashauri **18** Tanzania Bara (**Kiambatisho Na.14**). Ugonjwa huu hauna tiba wala chanjo hivyo nitoe wito kwa Halmashauri zote nchini kutoa elimu ya namna ya kujikinga na ugonjwa na pia pale kunapotokea mlipuko kutoa taarifa mapema kwa Wizara na kupulizia dawa ya kuuwa virusi ili kuzuia hasara inayoweza kuwapata wafugaji.

74. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo kama vile FAO na WHO iliandaa na kuhuisha mikakati ya kuzuia magonjwa mbalimbali yanayoambukiza binadamu kutoka kwa wanyama kwa kutumia dhana ya Afya Moja ili kukabiliana na magonjwa ya wanyama yanayoathiri binadamu. Katika mwaka 2020/ 2021 mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

(i) Jumla ya ng'ombe **1,036,769**, mbuzi **680,906** na kondoo **192,906** walichanjwa dhidi ya Ugonjwa wa Kimeta katika mikoa ya Arusha, Songwe, Manyara na Kilimanjaro.

(ii) Jumla ya mitamba **162,843** imechanjwa dhidi ya Ugonjwa wa Kutupa Mimba katika Wilaya za Arusha, Karatu, Babati, Dodoma Jiji, Simajiro, Iringa na Njombe.

(iii) Jumla ya matukio **210** ya Ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa yalifuatiliwa na sampuli **610** zilichukuliwa ambapo mbwa **812,712** na paka **4,152** walichanjwa dhidi ya Ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa.

(iv) Ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa umeendelea kufuatiliwa kwa kukagua na kuchukuwa sampuli kwa wanyama wote wanaotupa mimba kutokana na mwaka huu kuwa na mvua nyingi. Napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa nchi yetu bado ipo salama.

75. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/ 2022 Wizara itaendelea kusimamia utekelezaji wa kanuni za uogeshaji na chanjo ili kudhibiti magonjwa ya mifugo kwa kununua dawa za ruzuku za kuogeshea mifugo lita **13,880,** kujenga majosho **129** ili kuwezesha kuongeza uogeshaji wa mifugo kutoka lengo la michovyo **milioni 405** hadi michovyo **milioni 600**. Pia, itakarabati Kliniki **18** za mifugo na kuzipatia vitendea kazi ikiwemo mnyororo baridi kwa ajili utunzaji wa chanjo. Vilevile, katika udhibiti wa Ugonjwa wa Homa ya Nguruwe, Wizara itaendelea kutoa elimu ya ufugaji bora wa nguruwe. Pia, Wizara itasimamia uzalishaji, usambazaji na utoaji wa chanjo kulingana na miongozo iliyopo.

Kuimarisha Uchunguzi na Upatikanaji wa Taarifa za Magonjwa ya Mifugo

76. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2021 jumla ya matukio **449** ya magonjwa mbalimbali ya mifugo yalitolewa taarifa yakilinganishwa na matukio **586** yaliyotolewa taarifa katika mwaka 2019/2020 kipindi kama hicho. Pia, katika matukio hayo mifugo **520,901** ikiwemo ngómbe **472,006** mbuzi **29,456,** kondoo **13,807** na nguruwe **5**,**632** ilipatwa na magonjwa na mifugo **243,112** ilikufa kutokana na magonjwa hayo. Mifugo iliyokufa kwa magonjwa ni ngómbe **210,932**, mbuzi **24,131,** kondoo **2,657** na nguruwe **5,428** ikilinganishwa na mifugo **617,621** iliyopata magonjwa ikiwemo ng'ombe **442,432** mbuzi **141,605** kondoo **32,062** ambapo mifugo **221,783** ilikufa kutokana na magonjwa katika mwaka 2019/2020.

77. ***Mheshimiwa Spika,*** **k**atika mwaka 2021/2022 Wizara itaendelea kuimarisha mfumo wa upatikanaji wa taarifa za magonjwa ya mifugo, kuwezesha uchanjaji wa wanyama **25,000,000** dhidi ya magonjwa ya kipaumbele **13**yenye chanjo.

Baraza la Veterinari Tanzania

78. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Baraza la Veterinari Tanzania, imefanya ukaguzi wa vituo **1,225** vya kutolea huduma ya afya ya wanyama katika mikoa **18**. Kati ya vituo vilivyokaguliwa vituo **61** vilifungwa

kwa muda ili kurekebisha kasoro zilizobainiwa. Pia, madaktari wa wanyama **11** wameonywa kwa kukiuka maadili ya taaluma na watu wengine sita **(6)** wasio na sifa walikamatwa kwenye maeneo mbalimbali nchini wakitoa huduma ya afya ya wanyama na kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria ya Veterinari.

79. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Baraza la Veterinari imesajili madaktari wa wanyama **16** kati ya **70** waliotarajiwa kusajiliwa na kufanya idadi yao kufikia **1,021** kati ya hao wanaume **924** na wanawake **97**. Aidha, wataalam wasaidizi wa afya ya wanyama **297** kati ya **1,000** waliotarajiwa kuandikishwa na kuorodheshwa, wameandikishwa na kuorodheshwa katika kipindi hicho na kufanya idadi ya wataalam wasaidizi hao kufikia **4,111** kati ya hao wanaume **2,894** na wanawake **1,217**. Idadi ya wataalam waliosajiliwa na kuorodheshwa imekuwa chini ya lengo kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa COVID 19 ambapo wataalam waliolengwa walihitimu mwezi Desemba, 2020 badala ya Julai, 2020. Vilevile, vituo **159** vya kutolea huduma za afya ya wanyama vilisajiliwa na kufanya jumla ya vituo vyote vilivyosajiliwa kufikia **1,869.**

80. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/2022 Baraza la Veterinari litaendelea kufanya ukaguzi wa vituo vya huduma ya afya ya wanyama na maadili ya watoa huduma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa **184**; kukagua vyuo vinane (**8**) vinavyotoa na vinavyotaka kutoa mafunzo ya afya ya wanyama; kusajili Madaktari wa Wanyama **70** na vituo vya huduma ya afya ya wanyama; kuandikisha na kuorodhesha wataalam wasaidizi **3,000**; na kutoa leseni kwa wakaguzi wa nyama, wahimilishaji na wataalam wa maabara za veterinari **500**.

Utafiti, Mafunzo na Ugani

Uratibu wa Utafiti wa Mifugo

81. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia shughuli za utafiti wa mifugo nchini. Katika mwaka 2020/2021, Wizara imeandaa miongozo mitatu (**3**) ya utekelezaji wa Kanuni za Utafiti wa Mifugo GN. **462** ya

Mwaka 2020 ambayo inatekeleza Agenda ya Utafiti ya mwaka 2020-2025. Miongozo hiyo ni:-

(i) Mwongozo wa Kamati ya Maadili ya Utafiti wa Mifugo Nchini;

(ii) Mwongozo wa Masomo ya Ziada kwa Wahitimu wa Shahada ya Uzamivu (*Post Doctorial Guideline*); na

(iii) Mwongozo wa Haki Miliki ya Matokeo ya Tafiti (*Intellectual Property Rights – IPR*).

Miongozo hii itawezesha utekelezaji wa utafiti kwa kuzingatia vipaumbele vya Sekta, kusimamia matokeo ya Tafiti na kuwafikia wananchi kwa maendeleo badala ya kufungiwa makabatini.

82. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2020/ 2021,Wizara imeratibu vituo (7) vya Taasisi ya Utafiti TALIRI na Taasisi ya Wakala ya Maabara ya Veterinary zilizo chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Aidha, Wizara kupitia Idara ya Utafiti Mafunzo na Ugani inashirikiana na Taasisi za vyuo Vikuu zinazofanya tafiti za Mifugo ili kujua Taafiti zinazofanyika na matokeo ya Tafiti na kuainisha namna ya kusambaza teknolojia bora kwa wadau. Taasisi ambazo zimekuwa zikifanya Tafiti mbalimbali za Mifugo nchini ni pamoja na Taasisi ya Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Chuo Kikuu cha Nelson Mandela (NM-AIST), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

83. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022 Wizara itaendelea kuratibu vituo nane (**8**) vya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (TALIRI) na tafiti zinazofanywa na Wakala ya Maabara ya Veterinary (TVLA). Aidha, Wizara itaendelea kushirikiana na Taasisi zinazofanya utafiti wa mifugo nchini kwa kuhakikisha tafiti zote zinafanywa kwa kufuata Agenda ya Kitaifa ya Utafiti wa Mifugo na Kanuni zake, na hivyo kunufaisha jamii, wadau na Sekta ya Mifugo.

Huduma za Ugani wa Mifugo

84. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/2021, jumla ya wadau wa sekta ya mifugo **35,961** wamepatiwa elimu kuhusu ufugaji bora, uzalishaji, usindikaji wa mazao yatokanayo na mifugo, hifadhi ya malisho pamoja na mbinu za kupata masoko kupitia maonesho ya Saba Saba (**8,442**), Nane Nane (**22,287**) na maadhimisho ya Siku ya Chakula Duniani (**4,962**). Aidha, jumla ya vipeperushi **9,920** na vitabu **747** vya ufugaji bora vilisambazwa kwa wadau.

85. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kutoa mafunzo rejea kwa Wafugaji katika Halmashauri **21** na pia kuwajengea uwezo (ToT) Maafisa Ugani kutoka katika Halmashauri za mikoa ya Dodoma na Singida (**20**); Arusha, Kilimanjaro na Manyara (**21**) na Washauri wa Mifugo wa Mikoa yote Tanzania bara (**26**). Mafunzo yaliyotolewa yalihusu; uendelezaji wa kosaafu na uboreshaji wa mbari za mifugo; udhibiti wa magonjwa na tiba kwa mifugo; upatikanaji wa maeneo ya malisho, maji na vyakula vya mifugo; uanzishwaji wa mashamba darasa ya Mifugo; utambuzi wa Sheria, Kanuni na Miongozo ya Wizara. Aidha, idadi ya Mashamba Darasa ya malisho imeongezeka kutoka **88** mwaka 2019/2020 hadi **103** mwaka 2020/2021.

86. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022 Wizara itaendelea kuwezesha utoaji wa huduma za ugani kwa kununua pikipiki 300 kwa ajili ya Maafisa Ugani, kuwezesha Halmashauri 20 kuanzisha mashamba darasa 60 ya mifugo, kuwezesha uhuishwaji Mwongozo wa utoaji huduma za ugani na kuandaa mfumo wa kielektroniki kwa ajili ya kuratibu utoaji wa huduma za ugani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Taasisi Zilizo Chini ya Sekta ya Mifugo

Kampuni ya Ranchi za Taifa

87. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa takwimu za tarehe 30 Aprili, 2021 Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) ina jumla ya

ng'ombe **16,725**, mbuzi **3,307**, kondoo **3,155** na farasi **31** ikilinganishwa na mifugo iliyokuwepo tarehe 30 Aprili, 2020 ambayo ni ng'ombe **14,708**, mbuzi **2,9**12, kondoo **2,880** na farasi **30**. Katika mwaka 2020/2021 Wizara kupitia NARCO imetekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuzalisha na kukuza ndama **4,963** ikilinganishwa na ndama **3,056** waliozalishwa na kukuzwa katika mwaka 2019/2020.

(ii) Kununua ng'ombe **2,793** wenye thamani ya shilingi **1,675,800,000** kutoka kwa wafugaji wa asili kwa ajili ya kunenepesha kwa kutumia vyakula vya ziada ili kuzalisha nyama bora na hivyo kuwa sehemu ya soko la uhakika kwa wafugaji nchini ikilinganishwa na ng'ombe **3,327** walionununuliwa katika mwaka 2019/2020.

(iii) Kukamilisha uwekaji mpaka unaoonekana katika Ranchi ya Uvinza.

(iv) Kukamilisha upimaji, utengaji wa vitalu **89** na kumega hekta **11,772.152** katika ranchi ya Mwisa II iliyopo Wilayani Muleba.

88. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022 Kampuni ya NARCO itaendelea kuongeza uzalishaji wa ng'ombe bora wa nyama kwa ajili ya soko la ndani na nje.

Bodi ya Nyama Tanzania

89. ***Mheshimiwa Spika*****,** Bodi ya Nyama Tanzania (TMB) imeendelea kuratibu na kusimamia biashara ya nyama ndani na nje ya nchi kwa kutoa vibali**148** vya kusafirisha nje ya nchi nyama tani **1,774.29** (mbuzi tani **551.64,** ng'ombe tani **365.77**, kondoo tani **181.51**, kuku tani **0.37** na punda tani **675**) yenye thamani ya dola za Marekani milioni **4.29** sawa na shilingi **bilioni 9.91** katika nchi za Kuwait, Oman, Qatar, Hongkong na Zanzibar ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia **156.27** (tani za nyama) ikilinganishwa na vibali **102** vilivyotolewa kuuza nyama nje ya nchi tani **692.36** yenye thamani ya dola za

Marekani milioni **1.29** sawa shilingi bilioni **2.99** katika mwaka 2019/2020. Ongezeko hilo limechangiwa na kuanza kwa uzalishaji kwa viwanda viwili vipya vya Tan Choice Ltd (kilichopo mkoa wa Pwani) na Elia Food OverSeas Co. Ltd (kilichopo mkoa wa Arusha).

90. ***Mheshimiwa Spika*****,** Bodi imesimamia uingizaji wa bidhaa za nyama nchini kwa kutoa vibali **59** vya kuingiza bidhaa za nyama tani **319.27** (nguruwe tani **185.02** na ng'ombe tani **134.25**) zenye thamani ya dola za Marekani **milioni 1.06** sawa na shilingi **bilioni 2.44** ikilinganishwa na vibali **36** vilivyotolewa kuingiza bidhaa za nyama tani **243.65** (ng'ombe tani **195.12** na nguruwe tani **48.53**) vyenye thamani ya dola za Marekani **milioni 1.76** sawa na shilingi **bilioni 4.06** katika mwaka 2019/2020.

91. ***Mheshimiwa Spika*****,** Wizara kupitia Bodi ya Nyama Tanzania (TMB) imeendelea kusimamia tasnia ya nyama ambapo wadau **2,092** (Machinjio/Viwanda **12,** Makaro **21,** Bucha **2,075**) wamekaguliwa katika mikoa ya Pwani (Kibaha na Ruvu), Dar es Salaam (Temeke, Ilala, Kinondoni, Ubungo na Kigamboni), Dodoma (Dodoma Jiji na Chamwino DC); Arusha (Longido, Arusha Jiji, Arusha DC); Mwanza (Mwanza Jiji, Ilemela na Magu); Shinyanga (Shinyanga Manispaa) na Kilimanjaro (Moshi Manispaa).

92. ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2020/2021 Wizara kupitia Bodi ya Nyama Tanzania imefanya kikao cha wazalishaji kuku ambapo wadau **423** walishiriki na kusikilizwa kero zao. Aidha, Bodi imeendelea kutafuta masoko ya nyama katika nchi mbalimbali ikiwemo nchi ya Komoro ambapo ilimualika Balozi wa Komoro ili ajionee ubora wa nyama inayozalishwa nchini hususan katika kiwanda cha nyama cha *Eliya Foods Overseas Limited*.

93. ***Mheshimiwa Spika*****,** Bodi ya Nyama Tanzania imeendelea kutoa elimu ya ufugaji bora wa mifugo ya nyama, kuzalisha na kuuza nyama katika mazingira safi, kusafirisha nyama na kuhamasisha ulaji wa nyama nchini. Elimu hii

imetolewa kupitia vyombo vya habari vikiwemo televisheni, radio, magazeti na mitandao ya kijamii ikiwemo *Facebook, Instagram* na *twitter.*

94. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022 Bodi ya Nyama Tanzania itaendelea kuendeleza tasnia ya nyama kwa kuhamasisha uzalishaji, biashara na ulaji wa nyama bora na kusimamia tasnia ya nyama kwa kuzingatia Sheria.

Bodi ya Maziwa Tanzania

95. ***Mheshimiwa Spika*****,** Bodi ya Maziwa Tanzania (TDB) imewezesha kuingizwa nchini bidhaa za maziwa kwa kutoa vibali **308** vya jumla ya lita **5,336,955.16** (Liquid Milk Equivalent**-** LME) zenye thamani (Freight on Board - FoB) ya Shilingi **12,052,434,895.86** ikilinganishwa na vibali **443** vilivyotolewa mwaka 2019/2020 ili kuingiza maziwa yenye ujazo wa lita **11,725,859.84** vikiwa na thamani (FOB) ya Shilingi **15,199,487,699** kutoka nchi za Afrika Kusini; Uganda; Kenya; Emirates; Uholanzi; na Ireland sawa na upungufu wa asilimia **21.9**. Kupungua kwa kiasi cha maziwa kinachoingizwa nchini kumetokana na kuongezeka kwa uzalishaji na ukusanywaji wa maziwa na kuendelea kuimarika kwa viwanda vya ndani katika usindikaji wa bidhaa za maziwa. Aidha, katika mwaka 2020/2021 kulikuwa na viwanda **96** vya kusindika maziwa vinavyofanya kazi na viwanda **3** vimesimamisha uzalishaji kutokana na changamoto mbalimbali (**Kiambatanisho Na. 2**).

96. ***Mheshimiwa Spika*****,** Wizara kupitia Bodi ya Maziwa Tanzania imeendelea kusimamia, kuratibu na kuendeleza tasnia ya maziwa nchini. Katika mwaka 2020/2021 jumla ya wafanyabiashara wa maziwa **238** walikaguliwa katika mipaka ya Tunduma, Namanga, Mtukula, Kasumulo na Bandari ya Dar es Salaam na hatua kuchukuliwa kwa makosa yaliyobainishwa likiwemo kosa la kuingiza maziwa bila kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo.

97. ***Mheshimiwa Spika*****,** ili kudhibiti na kuendeleza tasnia ya maziwa nchini, Bodi ya Maziwa Tanzania imesajili jumla

ya wadau wa maziwa **315** wakiwemo wazalishaji **20**, wasindikaji **42**, wafanyabiashara **145**, waingizaji wa maziwa nchini **34**, wasambazaji **26**, wakusanyaji **5** pamoja na maghala ya kuhifadhia maziwa **42**. Katika zoezi hilo, elimu kuhusu Sheria ya Tasnia ya Maziwa SURA 262 na Kanuni zake ilitolewa kwa wadau hao. Pia, Bodi iliendesha mafunzo kwa wafugaji **195** wa ng'ombe wa maziwa kutoka wilaya za Mkuranga **93**, Mvomero **47**, Ubungo **43** na Kongwa **12**, kwa lengo la kuwawezesha ufugaji bora wa kibiashara.

98. ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2020/2021 Bodi ya Maziwa Tanzania imezindua Mpango wa Unywaji Maziwa katika Ofisi za Serikali. Lengo la Mpango huo ni kuunga mkono Sera ya Uchumi wa Viwanda. Hivyo kupitia mpango huu tunatarajia kiwango cha usindikaji wa maziwa na bidhaa za maziwa nchini kuongezeka; kuongezeka kwa masoko ya maziwa na bidhaa za maziwa na kuongezeka kwa unywaji wa maziwa na bidhaa zake nchini. Nitoe wito kwa viongozi wote wa ofisi za Serikali kuunga mkono juhudi za Wizara kwa kutumia maziwa yanayozalishwa na viwanda vyetu vya ndani kwani kwa kufanya hivyo tutakuza soko la ndani la unywaji wa maziwa na hivyo kuongeza kipato kutokana na uuzaji wa maziwa kwa wafugaji wetu hapa nchini.

99. ***Mheshimiwa Spika*****,** Bodi ya Maziwa Tanzania imeshiriki katika maonesho na promosheni mbalimbali ili kuhimiza unywaji wa maziwa kupitia maonyesho ya Sabasaba na Nanenane, pamoja na promosheni za unywaji wa maziwa shuleni. Aidha, Bodi iliratibu na kusimamia maadhimisho ya wiki ya unywaji maziwa shuleni ambayo kitaifa yalifanyika mkoani Kilimanjaro, mwezi Septemba, 2020. Vilevile, jumla ya lita za maziwa **5,096.8** ziligawiwa kwa shule za msingi **45** zenye wanafunzi **10,254**. Pia, mwezi Desemba, 2020 Bodi iliandaa na kufanya bonanza la maziwa katika Mkoa wa Dar es salaam kwa kushirikisha vyama vya michezo ambapo jumla ya wanamichezo **1,700** walishiriki.

100. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi ya Maziwa Tanzania kwa kushirikiana na wadau wa tasnia ya maziwa inaendelea na majaribio ya mpango wa unywaji wa maziwa shuleni kwa

mikoa ya kanda ya Kaskazini. Jumla ya shule za msingi **66** zenye wanafunzi **41,922** katika mikoa ya Arusha shule **13** wanafunzi **12,000**, Kilimanjaro shule **25** wanafunzi **10,722** na Manyara shule **28** wanafunzi **19,200**.

101. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2021/ 2022 Wizara kupitia Bodi ya Maziwa Tanzania itaanzisha programu ya mashamba ya kibiashara ya ufugaji wa ng'ombe wa maziwa (Small Scale dairy farms); itaanzisha programu ya majaribio ya unywaji wa maziwa shuleni; kujenga vituo vya ukusanyaji maziwa **25**; na kuendelea kuimarisha udhibiti wa uingizwaji holela wa maziwa kutoka nje ya nchi.

Wakala wa Maabara ya Veterinari

102. ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2020/2021 Wizara kupitia Wakala wa Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) imetekeleza yafuatayo:-

(i) Kuzalisha chanjo za magonjwa ya kimkakati aina sita (**6**) ambapo jumla ya dozi **48,883,825** za chanjo zilizalishwa na kusambazwa katika Halmasahuri **184** nchini zikijumuisha dozi **45,982,900** za chanjo dhidi ya Ugonjwa wa Mdondo TEMEVAC, dozi **504,500** dhidi ya Ugonjwa wa Kimeta, dozi **54,300** dhidi ya Ugonjwa wa Chambavu, dozi **1,830,100** dhidi ya Ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya Ng'ombe, dozi **13,275** dhidi ya Ugonjwa wa Kutupa Mimba na dozi **309,950** mchanganyiko wa Kimeta na Chambavu ikilinganishwa na dozi **49,008,325** za chanjo zilizozalishwa mwaka 2019/2020.

(ii) Uzalishaji wa chanjo ya Homa ya Mapafu ya Mbuzi (CCPP) uliosubiriwa kwa hamu umeanza na hivyo kufanya chanjo zinazozalishwa nchini kuongezeka kutoka sita (**6**) na kufikia saba (**7**). Uzinduzi wa chanjo hiyo utafanyika mwezi Mei, 2021.

(iii) Ujenzi wa jengo jipya la utengenezaji wa chanjo za bakteria umekamilika kwa asilimia **98**. Aidha, baadhi ya vifaa vitakavyotumika katika jengo hilo vikiwemo *Autoclave, Biosafety cabinets, Hot air oven* na *incubator* vimenunuliwa.

103. ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2021/2022 Taasisi ya Chanjo Tanzania (TVI) itazalisha jumla ya dozi milioni **123**; kukamilisha utengenezaji wa chanjo ya nane (**8**) ya Sotoka ya Mbuzi na Kondoo (PPR) na kuanza uzalishaji wake; pia Wizara itaendelea kusimamia uzalishaji, usambazaji na utoaji wa chanjo; na kukamilisha ujenzi wa kiwanda cha chanjo cha Kibaha na kukinunulia vifaa.

Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (TALIRI)

104. ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (TALIRI) inamiliki aina mbalimbali ya mifugo kwa ajili ya utafiti na kusambazwa kwa wafugaji. Hadi tarehe 30 Aprili, 2021 TALIRI ilikuwa na ng'ombe maziwa **1,576**, Mbuzi **1,110**, Kondooo **264** na Punda **22.**

105. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2020/2021 TALIRI ilitekeleza jumla ya miradi ya utafiti **58** katika nyanja mbalimbali za utafiti. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:-

(i) Kufanya tafiti na tathmini za teknolojia bora saba (**7**) za ng'ombe chotara wa maziwa wenye mchanganyiko wa damu za Friesian na Fipa; Mpwapwa na DanishRed; Friesian, Mpwapwa na Boran; Mpwapwa na Sahiwal; Mpwapwa, Boran na Sahiwal; DanishRed na Mpwapwa pamoja na ¾DanishRed na ¼Mpwapwa. Utafiti huu uliwezesha kuzalishwa kwa ng'ombe bora chotara wa maziwa**97** wanaotumika kutathmini ulinganifu wa uzito wa kuzaliwa, ukuaji na utoaji wa maziwa.

(ii) Jumla ya ng'ombe chotara **11** wa maziwa walisambazwa kwa ajili ya mbegu kwa wadau wa mifugo katika mikoa minne (**4**) ya Dodoma, Morogoro, Tanga na Mbeya.

(iii) TALIRI kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Utafiti wa Mifugo (ILRI) inatekeleza awamu ya pili ya mradi wa utafiti wa ng'ombe wa maziwa (Maziwa- Zaidi II) katika mikoa ya Kilimanjaro na Tanga ambao unatarajiwa

kukamilika mwaka 2026. Lengo la tafiti hizo ni kuzalisha na kusambaza teknolojia bora nne (**4**) zilizotokana na utafiti wa awamu ya kwanza ya mradi. Teknolojia hizo ni matumizi ya nyasi bora za malisho aina ya *Brachiaria* zilizotokana na uchaguzi wa nyasi za asili; matumizi na utunzaji wa samadi; uhimilishaji wa ng'ombe wa maziwa; na chanjo ya Ndigana Kali.

(iv) Teknolojia bora sita (**6**) za ng'ombe chotara kwa ajili ya uzalishaji wa nyama zilifanyiwa utafiti na kuzalisha ng'ombe **23** waliotokana na kuchanganya damu za Sahiwal, Mpwapwa na Boran; Boran na *BeefMaster*; *Bosimara* na Mpwapwa; Musi na *Singidawhit*e; Musi na Mpwapwa; na ¾*Boran* na ¼*BeefMaster*.

(v) Jumla ya madume ya mbegu bora ya ng'ombe chotara wa nyama **13** walisambazwa kwa wananchi kwa ajili ya kuboresha uzalishaji nyama katika mikoa mitatu (**3**) ya Kilimanjaro, (Moshi vijijini), Mwanza (Nyamagana), na Dodoma (Bahi).

(vi) Teknolojia bora tatu (**3**) za mbuzi zilifanyiwa utafiti kwa ajili ya uzalishaji wa nyama na maziwa. Jumla ya mbuzi chotara **100** aina ya *MalyaBlended* na *Gogowhit*e; Buha, *Norwegian* na *Parewhite* walizalishwa kwenye vituo vya TALIRI ambapo mbuzin**58** walisambazwa kwa wafugaji katika maeneo ya Tanga, Pwani, Morogoro, Katavi, Nyamagana, Meatu, Misungwi, Siha na Dodoma.

(vii) Mafunzo ya unenepeshaji wa mbuzi kibiashara yametolewa kwa vijana **20** kutoka Mikoa ya Mtwara, Mara, Mwanza, Simiyu, Kigoma, Iringa, Dodoma, Katavi, Pwani, Tanga, Morogoro, Tabora na Dar es Salaam. Aidha, jumla ya Mbuzi **1,059** walinunuliwa na kunenepeshwa.

(viii) Majaribio ya urasimishaji wa mbegu za malisho aina sita (**6**) za mikunde na nne (**4**) za nyasi yanafanyika kwenye vitalu **90** kwa awamu ya pili katika Kanda tatu za kitafiti kwenye vituo vya Mpwapwa, Uyole na Tanga.

106. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2021/2022 TALIRI itaendelea kuimarisha miundombinu ya utafiti kwa ajili ya kuwezesha tafiti za mifugo zenye lengo la kuongeza mchango wa sekta ya mifugo katika ukuaji wa uchumi na maendeleo ya viwanda.

Wakala ya Mafunzo ya Mifugo (LITA)

107. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2020/2021, Wakala ya Mafunzo ya Mifugo (LITA) imedahili jumla ya wanafunzi **3,574** katika ngazi ya Astashahada na Stashahada ikilinganishwa na wanafunzi **3,634** waliodahiliwa mwaka 2019/2020. Idadi hii ni pungufu ya wanafunzi **60**, sawa na takriban asilimia **2**. Aidha, idadi ya wanachuo wanaotarajiwa kuhitimu katika mwaka wa masomo 2020/2021 kutoka Vyuo vya Serikali ni **922** ukilinganisha na wanafunzi **689** waliohitimu mwaka 2019/2020. Idadi hii ni ongezeko la wanafunzi **233** sawa na asilimia **33.8**.

108. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021, LITA imewezesha jumla ya wafugaji **2,078** kupata mafunzo katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mpango wa utoaji mafunzo ya muda mfupi kwa vitendo ukilinganisha na wafugaji **2,062** waliopatiwa mafunzo kama hayo mwaka 2019/2020, ikiwa ni ongezeko la wafugaji **16** sawa na asilimia **0.8**.

109. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuboresha mazingira ya kusomea kwa wanafunzi waliodahiliwa katika mwaka wa masomo 2020/2021, miundombinu mbalimbali imeendelea kuboreshwa, ikiwemo Hosteli kumi (**10**); Madarasa matatu (**3**); Kumbi mbili (**2**) za mihadhara; Maabara nne (**4**) na Chumba cha Kompyuta kimoja (**1**). Miundombinu iliyojengwa upya ni pamoja na bweni moja katika Kampasi ya Tengeru, na vyoo vitatu (**3**) vya wanafunzi katika Kampasi za Morogoro, Mabuki na Kikulula.

110. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2021/2022 LITA inategemea kudahili wanafunzi **4,000** na kuendelea kuboresha miundombinu ya mafunzo ya mifugo katika

Kampasi nane (**8**) za LITA ili kuongeza udahili wa wanafunzi na kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

C. SEKTA YA UVUVI (FUNGU 64)

HALI YA SEKTA YA UVUVI

111. ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Uvuvi ni miongoni mwa sekta muhimu za kiuchumi inayochangia kuondoa umasikini na kukuza uchumi. Sekta ya Uvuvi imegawanyika katika Tasnia za uvuvi kwenye maji ya asili na ukuzaji viumbe maji. Tasnia hizo ni muhimu katika kutoa ajira, kipato, chakula na lishe bora pamoja na kukuza Pato la Taifa. Katika mwaka 2020, Sekta ya Uvuvi ilikuwa kwa asilimia **6.7** na mchango wake katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia **1.71** Sekta ya Uvuvi imetoa ajira za moja kwa moja kwa wavuvi wapatao **195,435** na Wakuzaji Viumbe Maji **30,064** katika mwaka 2020/2021. Aidha, zaidi ya Watanzania **Milioni 4.5** wameendelea kupata mahitaji yao ya kila siku kutokana na shughuli mbalimbali zinazohusiana na Sekta ya Uvuvi zikiwemo kuunda na kutengeneza boti, kushona nyavu, biashara ya samaki na mazao yake pamoja na Baba na Mama lishe. Pia, samaki huchangia takriban asilimia **30** ya protini inayotokana na wanyama.

112. ***Mheshimiwa Spika,*** kulingana na taarifa za tafiti zilizofanyika katika Ziwa Victoria mwaka 2020 kiasi cha samaki katika ziwa hilo kimeongezeka kutoka tani **2,681,165** mwaka 2019 hadi tani **3,465,913** kwa ziwa zima**,** sawa na ongezeko la asilimia **29.27.** Ongezeko hilo limechangia kiasi cha samaki kilichopo katika maji yote kufikia tani **4,058,913** (**Kiambatisho Na. 22**). Kutokana na kuwepo kwa rasilimali hii ni wazi kuwa Sekta ya Uvuvi inayo mchango katika kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na Pato la Taifa.

113. ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli za uvuvi kwenye maji asili kwa kiasi kikubwa hufanywa na wavuvi wadogo kwenye maji yote baridi na maji ya Kitaifa katika Bahari ya Hindi. Shughuli za wavuvi wadogo huchangia takriban asilimia **95** ya samaki wote wanaovuliwa nchini na asilimia **5** iliyobaki

huchangiwa na wavuvi wakubwa. Hadi kufikia Aprili, 2021, jumla ya wavuvi wadogo wapatao **195,435** walishiriki moja kwa moja katika shughuli za uvuvi kwa kutumia vyombo vya uvuvi vipatavyo **58,231** na kuwezesha kuvuna takriban tani **422,859.78** za samaki zenye thamani ya shilingi **trilioni 2.62** (**Kiambatisho Na. 23**). Kati ya hizo, tani **356,853.90** sawa na asilimia **84.39** ni kutoka maji baridi na tani 6**6,005.88** sawa na asilimia **15.61** ni kutoka maji chumvi.

114. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/2021 Wizara imeendelea kuhamasisha shughuli za Ukuzaji Viumbe Maji ambapo jumla ya vifaranga vya samaki **20,040,000** (**Kiambatisho Na. 24**) vimezalishwa hadi Aprili, 2021. Aidha, uzalishaji wa mazao ya Viumbe Machi Maji umefikia tani **22,793.2** hadi Aprili, 2021. Kati ya hizo, tani **20,258** ni za samaki, tani **97** za kambamiti, kilo **115** za majongoo bahari na tani **2,438** za mwani. Vilevile, vipande **360** vya lulu vilizalishwa katika kipindi hicho.

115. ***Mheshimiwa Spika,*** uvuvi wa kibiashara hufanywa na meli kubwa katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari ambazo nyingi ni kutoka nchi za kigeni na zinalenga samaki aina ya Jodari na Uvuvi wa Kambamiti unaofanywa na meli za Wazawa katika Maji ya Kitaifa. Katika mwaka 2020/2021, jumla ya meli sita (**6**) zilipata leseni ya kuvua Ukanda wa Uchumi wa Bahari. Kati ya hizo, meli tatu (**3**) ni za kigeni na meli tatu **(3**) ni za Wazawa. Meli hizo zimewezesha kuvuna jumla ya tani **437** za samaki.

116. ***Mheshimiwa Spika,*** uvuvi wa kambamiti ulifungwa mwaka 2007 baada ya Serikali na wadau kukubaliana kufuatia kiwango cha mavuno ya kambamiti kushuka hadi kufikia wastani wa kilo **17** kwa saa mwaka 2007 na hivyo uvuvi huo kutokuwa na tija. Pamoja sababu nyingine kushuka kwa mavuno hayo kutokana na kuongezeka kwa nguvu ya uvuvi ambayo ilitishia kutoweka kwa rasilimali hiyo. Aidha, taarifa za utafiti zilionesha kuongezeka kwa wastani wa mavuno kutoka kilo **23.70** kwa saa mwaka 2009 hadi kilo **31.09** kwa saa mwaka 2016. Kufuatia ongezeko hilo, uvuvi huo ulifunguliwa tena mwaka 2017 baada ya makubaliano

kati ya Serikali na wadau. Aidha, iliazimiwa kuwa uvuvi ufanyike kwa msimu usiozidi miezi sita (**6**) na idadi ya meli isizozidi **12** kwa kila mwaka. Katika msimu wa mwaka 2021 jumla ya meli sita (**6**) zimekidhi vigezo na kupatiwa leseni za kuvua kambamiti.

117. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea kuboresha mazingira ya uzalishaji, uchakataji na uhifadhi wa samaki na mazao ya uvuvi na kuimarisha miundombinu ya uvuvi ikiwemo mialo ya kupokelea samaki na masoko. Kutokana na juhudi hizo, hadi kufikia Mwezi Aprili, 2021, jumla ya tani **32,962.79** za mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo **141,592** waliuzwa nje ya nchi. Aidha, Serikali imeendelea kuratibu uingizaji wa samaki ndani ya nchi kutoka nchi mbalimbali ambapo hadi kufikia Mwezi Aprili, 2021 jumla ya tani **5.48** za samaki ziliingizwa nchini.

118. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza Mkakati wa Usimamizi na Udhibiti wa Rasilimali za Uvuvi Nchini kwa lengo la kuongeza ufanisi katika usimamizi, ulinzi na udhibiti wa uvuvi na biashara haramu ya mazao ya uvuvi. Katika kutekeleza Mkakati huo, Wizara imeimarisha Kanda **4** na Vituo **35** vya Ulinzi na Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi kwa kuvipatia vitendea kazi na watumishi. Kutokana na juhudi hizo vitendo vya uvuvi na biashara haramu imepungua hadi kufikia asilimia **80** katika maji baridi na uvuvi wa milipuko kwa asilimia **100** katika maji chumvi.

MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2020/2021

Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka 2020/2021

119. ***Mheshimiwa Spika*****,** Katika mwaka wa fedha 2020/ 2021 Wizara ilipanga kukusanya **Shilingi 33,000,000,000** kupitia Fungu 64. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2021 Shilingi **18,534,461,827.62** sawa na asilimia **56.2** ya lengo la mwaka zilikusanywa kutoka Sekta ya Uvuvi sawa na **asilimia 83.3** ya lengo la kukusanya **Shilingi 27,500,000,000** hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2021. (**Kiambatisho Na. 25).**

120. ***Mheshimiwa Spika,*** fedha hizi zimekusanywa kutoka vyanzo vifuatavyo: leseni za kusafirisha samaki na mazao yake (*Export Licences*); leseni za uingizaji mazao ya uvuvi (*Import Licences*); ushuru wa mrabaha (*Export Royalty*); mrabaha wa kuingiza mazao ya uvuvi nchini (*Import Royalty*), leseni za uvuvi katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu, tozo ya maabara; leseni za uvuvi wa kambamiti, mauzo ya vifaranga vya samaki na faini kwa makosa mbalimbali ya ukiukwaji wa sheria za uvuvi (***Kielelezo Na. 1***). Miongoni mwa sababu za kushuka kwa makusanyo ni pamoja na mlipuko wa ugonjwa wa Uviko - 19 (Covid – 19) ambao umeathiri mauzo ya mazao ya uvuvi katika nchi za Ulaya; kuimarika kwa soko la ndani la samaki ambalo ushuru wake hutozwa na Halmashauri; na kuendelea kuwepo kwa utoroshaji wa mazao ya uvuvi kwenda nje ya nchi.

Kielelezo Na. 1: Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021



Makadirio ya Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka 2021/2022

121. ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2021/2022 Wizara kupitia Fungu 64 inatarajia kukusanya kiasi cha Shilingi

40,000,000,000. Hili ni ongezeko la asilimia **21** ya makusanyo ya mwaka 2020/2021**.** Vyanzo vikuu vya fedha hizo ni pamoja na; leseni za kusafirisha samaki na mazao yake nje ya nchi *(Export Licences*); leseni za uingizaji mazao ya uvuvi (*Import Licences*); mrabaha wa kuuza mazao ya uvuvi nje ya nchi (*Export Royalty*); mrabaha wa kuingiza mazao ya uvuvi nchini (*Import Royalty*), leseni za uvuvi katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu, tozo za maabara; leseni za uvuvi wa kambamiti, mauzo ya vifaranga vya samaki na faini kwa makosa mbalimbali ya ukiukwaji wa sheria za uvuvi.

Fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa Mwaka 2020/2021

122. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/ 2021 Wizara kupitia Fungu 64 ilitengewa jumla ya Shilingi **34,721,321,000.00.** Kati ya fedha hizo, Shilingi **21,662,107,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **13,059,214,000.00** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

Matumizi ya Bajeti ya Kawaida

123. ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka wa fedha 2020/ 2021 Fungu 64 lilitengewa jumla ya Shilingi **21,662,107,000.00.** Kati ya fedha hizo, Shilingi **12,031,696,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara (PE) na Shilingi **9,630,411,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC). Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2021, jumla ya Shilingi **17,074,256,595.63** zilikuwa zimetolewa, sawa na asilimia **78.82** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo Shilingi **8,332,914,095.63** ni fedha za Mishahara ya Watumishi (PE) na shilingi **8,741,342,500** ni fedha za Matumizi Mengineyo.

Matumizi ya Bajeti ya Maendeleo

124. ***Mheshimiwa Spika*****, k**atika mwaka 2020/2021 Wizara kupitia Fungu 64 ilitengewa kiasi cha Shilingi **13,059,214,000.00** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo ikiwa ni fedha za ndani na nje. Kati ya fedha hizo Shilingi **5,976,856,000.00** ni

fedha za ndani na Shilingi **7,082,358,000.00** ni fedha za nje. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2021, jumla ya Shilingi **4,617,183,863.59** sawa na asilimia **35.36** kutoka vyanzo vya ndani na nje zilitolewa kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi **1,055,829,927.16** ni fedha za ndani na shilingi **3,561,353,936.43** ni fedha za nje.

UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KATIKA MWAKA 2020/2021 NA MPANGO WA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

Usimamizi wa Sera na Sheria

125. ***Mheshimiwa Spika*****,** Serikali imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uvuvi ya Mwaka 2015 kwa kutoa elimu kuhusu Ukuzaji Viumbe Maji, usimamizi, uendelezaji, uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi pamoja na utunzaji wa mazingira kwa wadau mbalimbali kupitia huduma za ugani, mafunzo rejea, semina, mikutano, elimu kwa umma (vipindi vya televisheni na redio) na maonesho ya Kitaifa. Aidha, Wizara imesambaza nakala **1,502** za Sera hiyo kwa wadau wa Sekta ya Uvuvi ili kuwajengea uelewa.

126. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kutekeleza Sera kupitia Sheria na Kanuni mbalimbali za kusimamia Sekta ya Uvuvi zikiwemo Sheria ya Uvuvi Na.22 ya Mwaka 2003 na Kanuni zake za mwaka 2009 pamoja na Marekebisho yake ya mwaka 2020; Sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Na. 29 ya mwaka 1994; Sheria ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu Na. 5 ya Mwaka 2020 na Kanuni zake za mwaka 2021 na Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania Na. 11 ya mwaka 2016.

127. ***Mheshimiwa Spika*****,** Wizara inaendelea kutunga na kuboresha sheria na kanuni mbalimbali zinazosimamia Sekta ya Uvuvi kulingana na mahitaji yaliyopo kwa sasa. Sheria na Kanuni zilizotungwa na kufanyiwa marekebisho na utekelezaji wake ni kama ifuatavyo:-

(i) Kufanya mapitio ya Sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Na. 29 ya mwaka 1994 ili kutunga Sheria mpya ya kuanzisha Mamlaka ya Kusimamia uhifadhi katika maji chumvi na maji baridi ambapo hatua iliyofikiwa ni kuandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri kwa ajili ya kutunga Sheria hiyo;

(ii) Kuendelea kufanya maboresho ya Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya Mwaka 2003 kwa lengo la kuondoa upungufu uliopo ili kukidhi mahitaji halisi ya sasa ambapo hatua ya kukusanya maoni ya wadau imekamilika;

(iii) Marekebisho ya Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2020 ambazo zilitangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 492 la tarehe 3 Julai, 2020;

(iv) Marekebisho ya Kanuni za Uvuvi za mwaka 2020 kuhusu ada za leseni na tozo za kusafirisha mazao ya uvuvi nje ya nchi ambayo ilitangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 491A la tarehe 29 Juni, 2020; na

(v) Kuandaa Rasimu ya Kanuni ya Ukuzaji Viumbe Maji ili kuwasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mapitio.

128. ***Mheshimiwa Spika*****,** Wizara inakamilisha kutafsiri Sheria, Kanuni na Miongozo ya Sekta ya Uvuvi kutoka lugha ya Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili ili kurahisisha uelewa kwa wadau.

Kodi, Ada na Tozo katika Sekta ya Uvuvi

129. ***Mheshimiwa Spika*****,** Serikali imepunguza viwango vya tozo na ada mbalimbali katika uzalishaji na usafirishaji wa mazao ya uvuvi nje ya nchi kupitia Kanuni iliyotangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 491A la tarehe 29 Juni, 2020 iliyoanza kutumika Julai 2020 ili kupunguza gharama na kuhimili ushindani wa kibiashara ndani na nje ya nchi. Baadhi ya viwango vya tozo vilivyopunguzwa na kuanza kutumika ni kama ifuatavyo:-

(i) Tozo ya usafirishaji wa dagaa nje ya nchi kutoka Ziwa Tanganyika imepungua kutoka Dola za Marekani **1.5** hadi Dola za Marekani **0.5** kwa kilo;

(ii) Tozo ya usafirishaji wa dagaa nje ya nchi kwa dagaa wa bahari, Ziwa Nyasa na Ziwa Victoria kutoka Dola za Marekani **1** hadi Dola za Marekani **0.16**;

(iii) Ada ya leseni ya kusafirisha dagaa nje ya nchi kwa wafanyabiashara wadogo imepungua kutoka Dola za Marekani **1,000** hadi Dola za Marekani **250** na kwa Wafanyabiashara wakubwa kutoka Dola za Marekani **1,800** hadi Dola za Marekani **500**;

(iv) Ada ya leseni ya mazao mengine ya bahari kama Pweza, Kambakoche na Kaa imepungua kutoka Dola za Marekani **2,500** hadi Dola za Marekani **500** kwa Wafanyabiashara wadogo na kutoka Dola za Marekani **2,700** hadi Dola za Marekani **1,000** kwa Wafanyabiashara wakubwa; na

(v) Tozo ya usafirishaji wa samaki aina ya migebuka kwenda nje ya nchi imepungua kutoka Dola za Marekani **0.5** hadi Dola za Marekani **0.3** kwa kilo.

130. ***Mheshimiwa Spika***, Katika mwaka 2021/2022 Serikali itaendelea kutoa elimu kuhusu Sera, Sheria na Kanuni za Sekta ya Uvuvi kwa wadau wa Sekta ya Uvuvi katika Kanda ya Ziwa Victoria, Kanda ya Pwani, Kanda ya Ziwa Tanganyika na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na kuhuisha Sheria na Kanuni za uvuvi ili kufikia malengo ya Uvuvi endelevu na Ukuzaji Viumbe Maji.

Usimamizi wa Takwimu za Uvuvi

131. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuratibu na kuhamasisha jamii za wavuvi na wadau mbalimbali kuhusu njia endelevu na uvunaji wa rasilimali za uvuvi zinazozingatia Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu zinazosimamia Sekta ya Uvuvi. Upatikanaji wa takwimu sahihi ni muhimu kwa

usimamizi endelevu wa uvuvi. Katika mwaka 2020/2021 jumla ya wavuvi **195,435** wanaotumia vyombo vya uvuvi vipatavyo **58,231** walishiriki katika shughuli za uvuvi ikilinganishwa na wavuvi **202,053** waliotumia vyombo vya uvuvi **58,930** mwaka 2019/2020. Aidha, hadi kufikia mwezi Aprili 2021, jumla ya tani **422,859.78** za samaki zenye thamani ya shilingi **trilioni 2.62** zilivunwa ikilinganishwa na tani **434,036.18** za samaki zenye thamani ya shilingi trilioni **2.04** zilizovunwa katika kipindi kama hiki mwaka 2019/2020. Kati ya tani hizo, tani **234,849.99** sawa na asilimia **55.54** ni kutoka Ziwa Victoria, tani **96,876.02** sawa na asilimia **22.91** ni kutoka Ziwa Tanganyika, tani **11,560.56** sawa na asilimia **2.73** ni kutoka Ziwa Nyasa, tani **13,567.33** sawa na asilimia **3.21** ni kutoka maji madogo na tani **66,005.88** sawa na asilimia **15.61** ni kutoka Ukanda wa Bahari ya Hindi (*Kielelezo Na. 2*). Sababu za upungufu huo wa mavuno ya samaki wa asilimia **2.57** kati ya mwaka 2019/2020 na 2020/2021 unatokana na kupungua kwa idadi ya wavuvi na vyombo vya uvuvi.

Kielelezo Na. 2: Mlinganisho wa uvunaji wa Samaki kwa mwaka 2019/2020 na 2020/2021 hadi Mwezi Aprili



132. ***Mheshimiwa Spika,*** Ili kuboresha upatikanaji wa taarifa na takwimu sahihi, Serikali kwa kushirikiana na Taasisi ya Usimamizi wa Uvuvi Ziwa Victoria (*Lake Victoria Fisheries Organisation LVFO*) ilifanya Sensa ya Uvuvi katika Ziwa Victoria Mwaka 2020. Matokeo ya sensa hiyo yanaonesha kupungua kwa idadi ya mialo ya kupokelea samaki, vyombo vya uvuvi na idadi ya wavuvi katika Ziwa hilo. Aidha, Serikali imefanya ufuatiliaji na tathmini ya ukusanyaji wa takwimu za uvuvi katika Halmashauri **17** za Ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi na Halmashauri Tatu (**3**) zinazozunguka Bwawa la Nyumba ya Mungu (**Kiambatisho Na. 26).** Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na LVFO inaendelea kuboresha Mfumo wa Ukusanyaji wa Takwimu za Uvuvi eCAS (*Electronic Catch Assessment Survey*) ambapo maboresho yanatarajiwa kukamilika mwaka 2021/2022. Pia, Wizara kwa kushirikiana na LVFO imekamilisha Tathmini ya uwingi wa samaki katika Ziwa Victoria ambapo kiasi cha samaki kilichopo ni tani **3,465,914,** kati ya hizo samaki aina ya Sangara ni tani **1,024,624,** Dagaa tani **950,714**, Furu tani **517,850** na Uduvi tani **972,726**(**Kiambatisho Na. 2**7). Kwa ujumla tathmini hiyo imeonesha kuwa Samaki wameongezeka kwa upande wa nchi za Tanzania na Uganda kutokana na juhudi za Serikali za kudhibiti uvuvi haramu wakati nchi ya Kenya uwingi wa samaki umepungua.

133. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2021/2022, Wizara itaendelea kusimamia uvunaji endelevu wa rasilimali za uvuvi nchini. Aidha, itafanya sensa za uvuvi katika maeneo matatu (**3**) ya Bwawa la Mtera, Bwawa la Nyumba ya Mungu na Ziwa Babati. Vilevile, Wizara itaendelea na ukusanyaji wa takwimu za uvuvi (*Catch Assessment Survey*) na ufuatiliaji katika maeneo ya Ukanda wa Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa, Bahari ya Hindi na mabwawa ya Nyumba ya Mungu na Mtera. Pia, itaendelea kushirikiana na *LVFO* kutekeleza mikakati mbalimbali ya usimamizi wa rasilimali za uvuvi katika Ziwa Victoria.

Usimamizi na Udhibiti wa Rasilimali za Uvuvi

134. ***Mheshimiwa Spika*****,** Wizara imeandaa Mkakati Shirikishi wa Usimamizi na Udhibiti wa Rasilimali za Uvuvi nchini wenye

lengo la kuongeza wigo wa ushirikishwaji wadau wa uvuvi katika usimamizi ili kuondoa kero na malalamiko ya wananchi katika udhibiti wa uvuvi haramu na utoroshaji wa mazao ya uvuvi nje ya nchi. Mkakati huu utaongeza uwazi na ufanisi katika usimamizi endelevu wa rasilimali za uvuvi. Aidha, Wizara imeweka mfumo wa kudhibiti uingizaji, utengenezaji na usambazaji wa zana zote za uvuvi nchini.

135. ***Mheshimiwa Spika*****,** Kwa kuzingatia Mkakati Shirikishi wa Usimamizi na Udhibiti wa Rasilimali za Uvuvi, katika mwaka 2020/2021 hadi kufikia Aprili, 2021 Wizara imefanya kaguzi na ufuatiliaji wenye siku kazi **6,911** za ulinzi na usimamizi shirikishi katika Ziwa Victoria, Tanganyika, Nyasa na Bahari ya Hindi. Juhudi hizi zimewezesha kupatikana kwa zana haramu na vyombo vilivyokuwa vikitumika katika uvuvi haramu, na hivyo kuchangia kupungua uvuvi haramu kwa asilimia **80** katika maji baridi na asilimia **100** ya matumizi ya vilipuzi baharini (**Kiambatisho Na. 28)**

136. ***Mheshimiwa Spika***, pia, Wizara kwa kushirikiana na Kikosi Kazi cha Kupambana na Uhalifu wa Mazingira (*National Multi-Agency Task TeamNMATT*) imeendesha doria maalumu mbili (**2**) za ulinzi na usimamizi shirikishi na ufuatiliaji katika maeneo ya Mikoa ya Mara (Bunda, Rorya na Musoma), Pwani (Bagamoyo), Mbeya (Kasumulu), Ruvuma (Songea na Mbamba Bay), Songwe (Tunduma), Dodoma (Mtera na Chimendeli), Manyara, Kilimanjaro (Nyumba ya Mungu) na Kigoma. Matokeo yalikuwa ni kupatikana kwa makokoro **179**, nyavu za timba **709**, nyavu za makila **55**, nyavu za dagaa vipande **100**, mtando **07**, vilipuzi (*explosives*) sita (**6)**, gari moja (**1)**, pikipiki tatu (**3)**, injini za boti **54**, tanki za mafuta mbili (**2),** samaki wachanga kilo **1,131** na watuhumiwa **176** pamoja na kufunguliwa kwa kesi **39** mahakamani.

137. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi kwa kutoa elimu kwa Wanachama wa Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi **520** kuhusu uanzishwaji wa Maeneo ya Pamoja ya Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi (*Collaborative Fisheries Management Areas* - CFMA) katika Ukanda wa

Bahari ya Hindi. Kufuatia mafunzo hayo, jumla ya CFMAs **12** zimeanzishwa katika Halmashauri za Tanga mjini (**1**), Mkinga (**2**), Pangani (**3**), Lindi vijijini (**3**) na Bagamoyo (**3**) ili kuwa na usimamizi wa pamoja. Aidha, CFMAs hizo zimewezeshwa kuandaa Rasimu za Mipango ya Usimamizi wa Maeneo ili kuimarisha usimamizi katika maeneo yao.

138. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2021/2022 Wizara itatekeleza kazi zifuatazo ili kuimarisha usimamizi, ulinzi na udhibiti wa rasilimali za uvuvi nchini:-

(i) Kuimarisha ulinzi na usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi kwa kushirikiana na mikoa husika ili kudhibiti uvuvi na biashara haramu katika maeneo ya Maziwa Makuu ya Ziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa, Ukanda wa Bahari ya Hindi, maji madogo pamoja na maeneo ya mipakani na vizuiani kwa kufanya sikukazi **7,800**;

(ii) Kuimarisha utekelezaji wa sheria kwa kushirikiana NMAT maeneo ya Maziwa Makuu ya Ziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa na Ukanda wa Bahari ya Hindi;

(iii) Kuimarisha vituo nane (**8**) vya Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi vya Bwawa la Nyumba ya Mungu, Bukoba, Tanga, Musoma, Ukerewe, Kipili, Kigoma na Mbamba Bay kwa kuvipatia watumishi na vitendea kazi;

(iv) Kufanya mafunzo kwa wadau **350** kuhusu Usimamizi wa Uvuvi unaozingatia Ikolojia na Mazingira na utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Uvuvi; na

(v) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya uvuvi haramu kwa kutumia zana za kisasa na TEHAMA.

Uthibiti wa Ubora na Usalama wa Mazao ya Uvuvi

139. ***Mheshimiwa Spika*****,** Katika mwaka 2020/2021 Serikali imeendelea kutekeleza jukumu la Kusimamia Ubora, Usalama na Viwango vya mazao ya uvuvi kwa ajili ya kuvutia masoko ya ndani, kikanda na kimataifa kwa kufanya jumla ya kaguzi

6,473 za kuhakiki ubora, usalama na viwango vya samaki na mazao ya uvuvi yanayosafirishwa. Kaguzi hizo zinalenga kutoa vibali na vyeti vya afya kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Uvuvi.

140. ***Mheshimiwa Spika***, Jumla ya kaguzi **4,482** zilifanyika kwenye miundombinu ya uvuvi ikiwemo viwanda vya kuchakata samaki, mialo, masoko na maghala. Kati ya kaguzi hizo, kaguzi **2,096** zimefanyika kwenye viwanda **51** vya kuchakata mazao ya uvuvi; kaguzi **297** zimefanyika katika mialo iliyoboreshwa ya kupokelea samaki **33**; kaguzi **681** kwenye maghala **90** ya kuhifadhi mazao ya uvuvi; kaguzi **279** katika masoko **31** ya kuuzia mazao ya uvuvi; na kaguzi **1**,**129** kwenye vyombo vya kusafirisha mazao ya uvuvi ikiwemo magari **517** na boti **31**. Matokeo ya kaguzi hizo yameonesha kuwa miundombinu hiyo inakidhi matakwa ya ubora na usalama kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za uvuvi.

141. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2020/2021 Serikali ilipanga kufanya ukarabati na ujenzi wa mialo na masoko. Hata hivyo, utekelezaji wake ulikabiliwa na changamoto ya kuwepo kwa mvua kubwa zilizonyesha katika msimu wa mwaka 2020 na hivyo kusababisha baadhi ya miundombinu kuharibika na mingine kufunikwa na maji, hususan katika mialo ya Ziwa Tanganyika na Ziwa Victoria. Hali hii imechelewesha utekelezaji wa kazi katika mialo ya Muyobozi (Uvinza), Kasanga (Kalambo) na Kirando (Nkasi) katika Ziwa Tanganyika na Kigangama (Magu), Ghana (Ukerewe), Nyamikoma (Busega) na Marehe (Bukoba) katika Ziwa Victoria ambako jumla ya Shilingi **589,068,327** zilitengwa. Hata hivyo, Wizara kwa kushirikiana na Wakala wa Majengo (TBA) imefanya tathmini na kuainisha jumla ya maeneo **9** ambapo ujenzi na ukarabati unafanyika kwa gharama ya Shilingi **1,490,931,673**. Maeneo hayo ni pamoja na mialo ya Ihale (Busega), New Igombe na Kayenze (Ilemela), Igabilo (Bukoba), Chifunfu/Kijiweni (Sengerema), soko la MbambaBay (Nyasa) na Ofisi za Vituo vya Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi vya Busega, Sengerema na Sota. Mikataba ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu hii imesainiwa na Wakandarasi wameanza kazi.

142. ***Mheshimiwa Spika***, Katika mwaka 2020/2021 katika kuimarisha ubora na usalama wa mazao ya uvuvi kwa ajili ya masoko ya ndani, kikanda na kimataifa, Wizara kupitia Maabara ya Taifa ya Uvuvi imetekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuhakiki ubora na usalama wa mazao ya uvuvi kwa kufanya chunguzi za kimaabara kwenye sampuli **3,066** za samaki, minofu ya samaki, dagaa, maji na vyakula vingine ili kuhakiki ubora na usalama. Matokeo ya chunguzi hizo yalionesha kutokuwepo kwa vimelea, kemikali na madini tembo na hivyo kukidhi viwango vya usalama na ubora kwa ajili ya kulinda afya za walaji (binadamu, wanyama na mazingira);

(ii) Kufanya zoezi la uchunguzi wa sampuli **22** maalumu za ustadi (*Proficiency Testing-PT*) kutoka Shirika la Viwango la Botswana (*National Quality Control Sample Exchange Scheme - NQCSES*), SADC Cooperation in Measurement Traceability - *SADCMET*, *Laboratory of Government Chemistry (LGC*) la Uingereza, *Proficiency Testing Australia* (*PTA*) la Australia ili kuhakiki mfumo wa utendaji wa maabara. Kutokana na uhakiki huo Maabara imefaulu kwa kiwango cha asilimia **100**;

(iii) Kufanyiwa ukaguzi kwa mara ya kwanza kwa kiwango kipya cha **ISO/IEC 17025:2017** kwa njia ya mtandao kupitia Taasisi ya Ithibati ya Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (*SADC Accreditation Services* SADCAS). Kufuatia ukaguzi huo, Maabara imepata ufaulu na hivyo kuendelea na hadhi ya ithibati kwa kuwa na wataalam mahiri **10** na njia **20** za uchunguzi zenye ithibati (**13** za vimelea na **7** za kemikali);

(iv) Kusimamia maabara ndogo za viwanda vya kuchakata samaki na kufanya kaguzi **13** za maabara hizo katika Mikoa ya Mwanza, Mara na Kagera; na

(v) Kuimarisha Maabara ndogo ya Uvuvi Dar es Salaam kwa kuipatia vitendea kazi ikiwemo Mitambo ya kisasa ya kiuchunguzi.

143. ***Mheshimiwa Spika*****,** Wizara imeongeza juhudi za kuhakiki ubora na usalama wa mazao ya uvuvi yanayozalishwa nchini. Hadi kufikia jumla ya tani **32,962.79** za mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo **141,592** wenye thamani ya shilingi **Bilioni 335.25** ziliuzwa nje ya nchi na kuliingizia Taifa mrabaha wa shilingi **Bilioni 15.55** *(***Kiambatisho Na. 29**) ikilinganishwa na tani **35,329.36** na samaki hai wa mapambo **104,524** yenye thamani ya shilingi **Bilioni 460.26** yaliyouzwa nje ya nchi katika kipindi kama hiki mwaka 2019/2020. Kati ya tani zilizouzwa katika mwaka 2020/ 2021, tani **28,838.89** zenye thamani ya shilingi **Bilioni 272.51** sawa na asilimia **87.49** zilitoka Ukanda wa Ziwa Victoria (**Kiambatisho Na. 30***).*

144. ***Mheshimiwa Spika*****,** Kiasi cha mazao ya uvuvi yaliyouzwa nje ya nchi kimepungua kwa asilimia **6.70** ikilinganishwa na kiasi kilichouzwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2019/2020. Kiasi cha mrabaha kilichokusanywa kutokana na mauzo hayo kimepungua kwa asilimia **25.27.** Kupungua kwa kiasi cha mazao ya uvuvi yaliyosafirishwa nje ya nchi na mrabaha kimechangiwa na kuyumba kwa soko la mazao ya uvuvi nje ya nchi kutokana na mlipuko wa Homa Kali ya Mapafu (UVIKO 19). Vilevile, upungufu huo umesababishwa na kupungua kwa kiasi cha samaki kinachochakatwa viwandani ambacho ndicho kinachosafirishwa nje ya nchi. Aidha, upungufu wa malighafi viwandani, unachangiwa na kuibuka kwa biashara ya mabondo ambalo lina bei kubwa kuliko samaki mwenye bondo ndani yake. Kutokana na hali hiyo, wavuvi wanashawishika kutenganisha bondo na samaki ambapo bondo huuzwa kwenye viwanda vya kuchakata mabondo na samaki kwenye soko la ndani, na hivyo kupelekea kupungua kwa samaki wazima (*whole fish*) wanaouzwa kwenye viwanda vya kuchakata samaki.

145. ***Mheshimiwa Spika*****,** Serikali imeendelea kuratibu uingizaji wa samaki ndani ya nchi kutoka nchi mbalimbali ambapo hadi kufikia mwezi Aprili mwaka 2021, jumla ya tani **5.48** za samaki wenye thamani ya shilingi **Milioni 170.26**zimehakikiwa na kuingizwa nchini ikilinganishwa na

tani **8.18** zenye thamani ya shilingi **Milioni 161.03** zilizoingizwa nchini katika kipindi kama hiki mwaka 2019/2020 **(Kiambatisho Na.31).** Hali hii imetokana na kuimarika kwa soko la ndani na kuongezeka kwa uzalishaji wa samaki kutoka kwenye ukuzaji wa viumbe maji.

146. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2021/2022 Serikali itaimarisha na kuviwezesha vituo vya Uthibiti wa Ubora wa Mazao ya Uvuvi kufanya kaguzi **8,080** za kuhakiki ubora na usalama wa samaki na mazao ya uvuvi na kufanya kaguzi **120** za kina kwenye viwanda vinavyochakata samaki, maghala ya kuhifadhi mazao ya uvuvi na vyombo vya kusafirisha samaki na mazao yake. Aidha, Serikali itaendelea kufanya ukarabati wa miundombinu ya uvuvi na kuhamasisha Sekta Binafsi kuwekeza katika viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi, utengenezaji wa zana za uvuvi na matumizi ya teknolojia sahihi katika shughuli za uvuvi. Katika mwaka 2021/2022, Wizara itakutanisha wafanyabiashara wa mazao ya samaki aina ya Sangara ili wajadiliane na kukubaliana namna bora ya kuendesha biashara hizo.

147. ***Mheshimiwa Spika***, Katika mwaka 2021/2022 Wizara kupitia Maabara ya Taifa ya Uvuvi itatekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kufanya uhakiki wa ubora na usalama wa mazao ya uvuvi kwa kufanyia uchunguzi jumla ya sampuli **5,200** za samaki, minofu ya samaki, dagaa, maji na vyakula vingine ili kuhakiki athari za uwepo wa vimelea, kemikali na madini tembo kwa ajili ya kulinda afya za walaji (binadamu, wanyama
na mazingira);

(ii) Kuhakikisha Maabara zinakidhi kigezo cha **ISO/IEC 17025:2017** hivyo kubakia na hadhi yake ya Ithibati na wataalam mahiri/bingwa **10** na kuongeza wigo wa njia za uchunguzi zenye ithibati kwa vimelea (njia **13** hadi **14**) na kemikali (**7** hadi **9**) kama inavyotakiwa na kuthibiti ubora katika bidhaa za mazao ya uvuvi kwenye Soko la Jumuiya ya Ulaya;

(iii) Kufanya zoezi la uchunguzi wa sampuli maalumu za ustadi (*Proficiency testing scheme* – PTs) za uhakiki wa mfumo wa utendaji wa maabara;

(iv) Kusimamia maabara ndogo za viwanda vya kuchakata samaki na kufanya kaguzi **30** katika Ukanda wa Ziwa Victoria, Pwani na Tanganyika.

148. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2021/2022 Serikali itaendelea kuhamasisha Sekta binafsi katika uzalishaji wa mazao ya uvuvi nchini kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa mazao hayo ili kupunguza uagizaji wa mazao hayo nje ya nchi na kupunguza matumizi ya fedha za kigeni katika uagizaji wa mazao ya uvuvi.

Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu

149. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (*Marine Parks and Reserves Units* - MPRU) imeendelea kusimamia na kuratibu shughuli za uhifadhi katika maeneo **18** yaliyohifadhiwa katika Bahari ya Hindi. Maeneo hayo ni Hifadhi za Bahari tatu (**3**) katika mikoa ya Mtwara (Hifadhi ya Ghuba ya Mnazi na Maingilio ya Mto Ruvuma), Pwani (Hifadhi ya Bahari ya Kisiwa cha Mafia) na Tanga (Hifadhi ya Bahari ya Silikanti Tanga) pamoja na Maeneo Tengefu (**15**) katika mikoa ya Dar es Salaam saba (**7**), Pwani matatu (**3**) na Tanga matano (**5**).

150. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2020/2021 Serikali imesimamia maeneo ya kipaumbele yafuatayo:-

(i) Kuimarisha ulinzi wa rasilimali za bahari na usimamizi wa sheria kwa kushirikiana na jamii katika maeneo yaliyohifadhiwa;

(ii) Kuimarisha ushirikishwaji wa jamii katika usimamizi endelevu wa rasilimali za bahari ikiwa ni pamoja na uperembaji wa rasilimali za bahari;

(iii) Kutekeleza Mkakati wa Kutangaza shughuli za uhifadhi na Kuongeza Mapato kwa kusimamia na kuboresha ukusanyaji wa mapato; na

(iv) Kuendeleza utangazaji wa vivutio vya utalii kwa kutumia fursa mbalimbali za kujitangaza zikiwemo maonesho ya ndani na nje ya nchi.

151. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kutekeleza vipaumbele hivyo yafuatayo yamefanyika:-

(i) Kusimamia ulinzi na usimamizi shirikishi kwa kufanya siku kazi **625** kwa lengo la kusimamia matumizi endelevu ya bioanuwai na mifumo ya ikolojia ya Bahari pamoja na uvunaji na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi na utunzaji wa mazingira ndani ya maeneo yaliyohifadhiwa kwa kuzingatia Sheria ya hifadhi. Matokeo ni pamoja na; kukamatwa kwa kilo **83** za makome, vipande **111** vya nyavu haramu, michinji miwili (**2**), mifuko **12** ya mwani, vyombo nane (**8**) vya uvuvi, na fito**145** za mikoko iliyovunwa kinyume na sheria. Aidha, Wizara kupitia Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu imeendelea kutoa elimu kuhusu sheria na matumizi ya zana sahihi na uvuvi endelevu ili kuhifadhi rasilimali za bahari kwa vizazi vya sasa na vijavyo;

(ii) Maboya ya alama za mipaka (*demarcation buoys*) **16** yamewekwa kwenye Hifadhi ya Bahari ya Silikanti Tanga (**7**) na Hifadhi ya Bahari ya Kisiwa cha Mafia – Pwani tisa (**9)**;

(iii) Mafunzo kwa ajili ya kupima ufanisi wa malengo ya uhifadhi (*Integrated Management Effectiveness Tool* – IMET) yametolewa pamoja na ushirikishwaji wa jamii (Co-Management) kwa watumishi wa MPRU kwa ajili ya kuboresha usimamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa;

152. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kuboresha miundombinu na huduma za msingi kwa watalii kazi zifuatazo zimefanyika:-

(i) Kutengeneza mabanda ya kupumzikia na vyoo katika Maeneo Tengefu Dar es Salaam pamoja na Hifadhi ya Ghuba ya Mnazi na Maingilio ya Mto Ruvuma, kununua vifaa vya uwekaji kambi za kitalii katika Hifadhi ya Ghuba ya Mnazi na Maingilio ya Mto Ruvuma, pamoja na kutengeneza mabango elekezi ili kutoa taarifa za Hifadhi na vivutio vya utalii kwa watalii na wadau mbalimbali;

(ii) Maboya **10** ya kuegeshea boti (*mooring buoys*) yamewekwa kwenye maeneo Tengefu ya Dar es Salaam ili kusaidia boti za wageni kuweka nanga za kuegeshea na kuonesha mipaka ya maeneo hayo.

(iii) Jamii imeelimishwa kuhusu uhifadhi baharini na vivutio vya utalii vilivyoko katika maeneo yaliyohifadhiwa kupitia maonesho ya kitaifa na kimataifa ambapo imeshiriki katika maonesho ya **44** ya Biashara ya Sabasaba yaliyofanyika Dar es Salaam, Maonesho ya wakulima ya Nanenane yaliyofanyika Nyakabindi – Simiyu na Ngongo - Lindi pamoja na kujitangaza kwa kupitia vyombo vya habari kama magazeti, Televisheni na vipindi vya radio; na

153. ***Mheshimiwa Spika***, Katika mwaka 2021/2022 Serikali itaendelea kuimarisha Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu kutekeleza majukumu ya uhifadhi na kuimarisha utalii ikolojia.

Usimamizi wa Uvuvi katika Bahari Kuu

154. ***Mheshimiwa Spika***, itakumbukwa kuwa Sheria ya kuanzisha Mamlaka ya Usimamizi wa Uvuvi wa Bahari Kuu (*Deep Sea Fishing Authority – DSFA*), Sheria ya Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu Na.1 ya mwaka 1998 na Marekebisho yake ya Mwaka 2007 haikuorodheshwa katika Baraza la Wawakilishi Zanzibar kwa zaidi ya miaka 20 na kusababisha Mamlaka kufanya kazi zake katika mfumo wa mpito (*interim*). Baada ya Bunge lako Tukufu kupitisha Muswada wa kutungwa kwa Sheria Mpya ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu, Sura ya 388 ya mwaka 2020 tarehe 20 Mei, 2020, Sheria hiyo ilisainiwa na Mhe. Rais wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 15 Juni, 2020. Sheria hiyo ilianza kutumika rasmi tarehe 12 Oktoba, 2020 kupitia tangazo la Serikali (GN) Na. 883 la mwaka 2020.

155. ***Mheshimiwa Spika***, Ninayo furaha kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa tarehe 23/02/2021 Sheria ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu Sura 388 ya mwaka 2020 iliwasilishwa katika Baraza la Wawakilishi Zanzibar na kuorodheshwa kulingana na masharti ya ibara ya 132 ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 toleo la 2010. Kuorodheshwa kwa Sheria Mpya katika Baraza la Wawakilishi kutaiwezesha DSFA kuwa na Muundo wa Utumishi na kuweza kuajiri watumishi wake tofauti na sasa ambapo watumishi wake wanaazimwa kutoka Wizara zinazosimamia uvuvi (SMT na SMZ) na hivyo kuongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu yake.

156. ***Mheshimiwa Spika***, Kanuni mpya za Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu zimetayarishwa na kutangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 334 ya tarehe 23 Aprili, 2021. Kanuni hizi zitawezesha kutekeleza kikamilifu Sheria ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu, Sura 388 ya mwaka 2020 ambayo pamoja na mambo mengine imeweka mazingira bora ya uwekezaji kwenye uvuvi wa Bahari Kuu kwa kutoa vivutio kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi, masharti nafuu ya leseni kwa wazawa ikiwa ni pamoja na punguzo la gharama za leseni kati ya asilimia **33** na **84** ikilinganishwa na meli za uvuvi za kigeni ili kuongeza ushiriki wa Sekta binafsi katika Uchumi wa Buluu nchini.

157. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2020/2021 Serikali kupitia DSFA imeendelea kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na uvuvi wa Bahari Kuu ambapo hadi kufikia Aprili 2021, Mamlaka ilitoa leseni sita (**6**) za uvuvi wa Bahari Kuu kwa meli (**3**) zenye bendera ya Tanzania (ALMAIDA, ASHANI SHANIKA na SEHEWA 02) na meli tatu (**3**) za Ushelisheli na kukusanya jumla ya **Shilingi 288,677,014.70.** Meli hizo zilivua tani **437** za samaki aina ya Jodari na jamii zake zenye thamani ya **Shilingi 2,753,100,000** na tani **12** za samaki wasiolengwa (*by-catch*) wenye thamani ya **Shilingi 60,000,000**.

158. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kusimamia ulinzi wa rasilimali za uvuvi wa Bahari Kuu na kuhakikisha kuwa shughuli za uvuvi zinaendeshwa kwa kuzingatia Sheria na Kanuni. DSFA iliweka waangalizi watatu (**3**) wa shughuli za uvuvi melini (*Fisheries obsevers*) kwenye meli zinazovua Bahari Kuu, kufanya doria za anga siku tatu (**3**) kwa mwezi kwa masaa yasiyopungua manne (**4**) kwa siku. Aidha, DSFA imeendelea kuboresha mifumo ya udhibiti na ufuatiliaji wa mienendo ya meli (*Vessel Monitoring System - VMS,* na *Automatic identification System - AIS*) yenye uwezo wa kuona meli za uvuvi zilizopewa leseni na zisizo na leseni ikiwa ni pamoja na aina nyingine za meli za mizigo, abiria, mafuta na utafiti kwa muda halisi (*real time*). Vilevile, Mamlaka zingine za usimamizi wa rasilimali na ulinzi, hususan Polisi Wanamaji, Jeshi Wanamaji, KMKM na Idara za Uvuvi (SMT na SMZ) zimeunganishwa katika mfumo wa VMS ili kuongeza ushirikiano na uwazi katika kusimamia rasilimali za uvuvi Nchini.

159. ***Mheshimiwa Spika***, Katika mwaka 2020/2021 Mamlaka ilikamilisha tafiti za hali ya uchumi kwa samaki aina ya Jodari na jamii zake (*Economic profile of tuna and tuna-like species*) na upembuzi yakinifu wa uvuvi wa kutumia upondo na ndoano (*feasibility study of pole and line fishery*), na hali ya mazingira ya bahari inavyoathiri mtawanyiko wa samaki aina ya Jodari na jamii zake nchini (*Oceanographic factors influencing spatial and temporal distribution of tuna and tuna-like species in Tanzania marine waters*). Tafiti hizi zilibainisha kuwa Tanzania itanufaika na uvuvi wa Bahari Kuu iwapo uwekezaji utafanyika katika mnyororo wa thamani hapa nchini.

160. ***Mheshimiwa Spika***, Kupitia Mradi wa SWIOFish Mamlaka kwa kushirikiana na taasisi za utafiti wa uvuvi ndani na nje ya nchi ipo katika hatua za mwisho kukamilisha utekelezaji wa tafiti zingine **10** za uvuvi katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari (*Exclusive Economic Zone - EEZ*) ya Tanzania zinazotarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Juni mwaka huu. Aidha, katika kutoa mchango wake kwa jamii, DSFA imeendelea kufadhili utafiti wa kutambua maeneo yenye

samaki wengi (*Potential fishing zones - PFZs*) katika Maji ya ndani na kitaifa na kutoa taarifa kwa wavuvi wadogo wadogo ili kuongeza kiasi cha samaki wanaovuliwa na kuwapunguzia gharama na muda wa kutafuta samaki. Vilevile, Mamlaka imetoa jumla ya mizani **12** yenye uwezo wa kupima kilo **500** za samaki katika Halmashauri zilizopo katika ukanda wa pwani Tanzania Bara na Zanzibar.

161. ***Mheshimiwa Spika***, Katika mwaka 2021/2022 Serikali itaendelea kutoa elimu na kuimarisha utekelezaji wa Sheria na Kanuni za Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu, kujenga miundombinu wezeshi, kuvutia meli zaidi za ndani na nje kununua leseni za uvuvi wa Bahari Kuu na kutoa uelewa wa kutosha kwa wawekezaji na jamii kwa ujumla kuhusu fursa zinazopatikana kwenye uvuvi wa Bahari Kuu ili kuongeza uwekezaji katika uvuvi huo. Hivyo, katika kufanikisha azma hiyo Mamlaka itaendelea kushirikiana na Sekta binafsi na Umma ikiwemo Vituo vya Uwekezaji Tanzania (TIC na ZIPA), EPZA, TBS na TRA. Vilevile, Serikali itakamilisha tafiti zenye lengo la kutathmini rasilimali nyingine za uvuvi zinazopatikana katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu.

Ukuzaji Viumbe Maji

162. ***Mheshimiwa Spika*****,** Katika mwaka 2020/2021 Wizara imeviwezesha vituo vya Kingolwira (Morogoro), Ruhila (Ruvuma), Mwamapuli (Tabora), Nyengedi (Lindi) na Machui (Tanga) kwa kuboresha miundombinu ili viweze kuzalisha vifaranga vya samaki na kutoa huduma za ugani. Vituo vya Wizara vimezalisha vifaranga vya samaki **1,901,717** ikilinganishwa na vifaranga vya samaki **1,059,440** vilivyozalishwa mwaka wa fedha 2019/2020.

163. ***Mheshimiwa Spika*****,** Wizara imeendelea kuhamasisha uwekezaji wa sekta binafsi katika mnyororo wa thamani wa ukuzaji viumbe maji ili kuboresha upatikanaji wa vifaranga vya samaki na chakula bora cha samaki pamoja na uzalishaji endelevu wa mazao yatokanayo na ukuzaji viumbe maji. Idadi ya vituo vya kuzalisha vifaranga vya samaki vimeongezeka kutoka **18** mwaka 2019/2020 hadi **28** kwa

mwaka 2020/2021 **(Kiambatisho Na. 32).** Vilevile, vituo hivyo vimezalisha jumla ya vifaranga vya samaki **18,071,752** ambavyo ni sawa na ongezeko la asilimia **9.7** ya lengo la kuzalisha vifaranga vya samaki **milioni 16**.

164. ***Mheshimiwa Spika*****,** Wizara imeendelea kuhamasisha Sekta Binafsi kuwekeza katika uzalishaji wa vyakula vya samaki, hadi kufikia Aprili 2021 jumla ya viwanda **11** vya chakula cha samaki vimezalisha tani **875** ikilinganishwa na tani **58.45** kwa mwaka 2019/2020. Vilevile, Wizara imetoa vibali **24** vya kuingiza tani **472.47** za chakula kutoka nje ya nchi na kufanya kiasi cha chakula kilichotumika nchini kuwa tani **1,182.47** *(***Kiambatisho Na. 33**).

165. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kufanya ukarabati, upanuzi na ujenzi wa vituo vya kuendeleza ukuzaji viumbe maji ili kupanua wigo wa utoaji huduma za ugani na uzalishaji vifaranga vya samaki ambapo vituo vya Kingolwira, Mwamapuli, Nyengedi na Ruhila vimeanza kufanyiwa ukarabati na upanuzi kwa gharama ya shilingi **802,255,999.20**. Pia, Wizara inaendelea na ujenzi wa kituo cha Rubambagwe (Geita) kwa ajili ya kurahisisha upatikanaji wa vifaranga bora vya samaki na huduma katika mikoa ya kanda ya Ziwa Victoria.

166. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kuhakikisha kuwa vifaranga vya samaki wa maji chumvi vinapatikana, Wizara imekamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa michoro kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha Ukuzaji Viumbe Maji Bahari cha Kunduchi (Dar es Salaam) kupitia mradi wa SWIOFish. Vilevile, Wizara imepata eneo katika mkoa wa Mtwara kwa ajili ya kujenga kituo kipya kwa lengo la kuhamasisha ukuzaji viumbe maji bahari katika pwani ya Mikoa ya Kusini.

167. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutoa huduma za ugani kuhusu masuala ya ukuzaji viumbe maji ambapo idadi ya wananchi waliopatiwa mafunzo imeongezeka kutoka **7,072** mwaka 2019/20 hadi **11,275** mwaka 2020/21. Kati ya wananchi hao, **6,092** walipatiwa mafunzo ya ufugaji samaki katika vituo vya Wizara, **424**

wamepatiwa mafunzo ya uongezaji thamani wa mazao ya mwani katika Mikoa ya Tanga, Lindi, na Pwani. Aidha, maafisa uvuvi **42** kutoka Halmashauri za Wilaya zilizoko katika mikoa ya Iringa, Rukwa, Morogoro na Dodoma walipatiwa mafunzo rejea ya ufugaji samaki katika kituo cha Kingolwira kwa ajili ya kuboresha huduma za ugani katika maeneo yao. Vilevile, wananchi **4,717** walitembelea mabanda ya Wizara wakati wa maonesho ya Saba Saba, Nane Nane na Siku ya Chakula Duniani na kupata ushauri kuhusu masuala ya ukuzaji viumbe maji ambapo jumla ya vipeperushi **10,000** viligawiwa.

168. ***Mheshimiwa Spika,*** Kampuni ya Righa's Safina's Aqua Farming Ltd (*Big Fish*) iliyopo Kigamboni kwa kushirikiana na kampuni ya Skretting ya Uholanzi na TAFIRI na walitoa mafunzo ya ufugaji samaki kitaalam kwa washiriki **156**. Aidha, mafunzo haya ni sehemu ya ushirikishwaji wa sekta binafsi katika utoaji wa huduma za ugani na utekelezaji wa makubaliano (*Memorandum of Understanding* – MoU) kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Uholanzi.

169. ***Mheshimiwa Spika*****,** Wizara inaendelea na taratibu za ujenzi wa mashamba darasa Matano (**5**) ya ufugaji samaki katika Halmashauri za Mwanga, Mkuranga, Meatu, Njombe na Tandahimba ili kusogeza mafunzo ya ufugaji samaki kwa vitendo karibu na wananchi.

170. ***Mheshimiwa Spika*****,** Katika mwaka 2020/2021 Wizara imeendelea kuhamasisha uwekezaji katika tasnia ya ukuzaji viumbe maji ambapo idadi ya wakuzaji viumbe maji imeongezeka kutoka **28,009** mwaka 2019/2020 hadi **30,064**. Vilevile, idadi ya mabwawa imeongezeka kutoka **27,979** hadi kufikia **30,032** na vizimba vimeongezeka kutoka **431** mwaka 2019/2020 hadi **473** (Ziwa Victoria – **362,** Ziwa Tanganyika – **9** na Ziwa Nyasa - **1** pamoja na malambo - **101)**. Aidha, vibali **14** vya ufugaji mkubwa wa samaki kibiashara vimetolewa kwa wafugaji samaki. Kati ya hivyo, vibali **11** kwa ajili ya ufugaji samaki kwa njia ya vizimba, viwili (**2**) vya mabwawa na kimoja (**1**) kwa ajili ya ufugaji samaki kwa mfumo wa kuzungusha maji (*Recirculation Aquaculture System - RAS*).

Pia, kampuni saba (**7**) zilipatiwa vibali vya kununua mwani kutoka kwa wakulima wadogo na kuuza kwenye masoko ya nje.

171. ***Mheshimiwa Spika*,** Wizara imeandaa Mkakati wa Kudhibiti Magonjwa ili kuboresha na kulinda afya ya viumbe maji; na ubora wa mazao yake na kupunguza uwezekano wa milipuko ya magonjwa ambapo kutokana na uzoefu wa nchi nyingine unaonyesha kuwa milipuko ya magonjwa yanatokana na kuongezeka kwa shughuli za ukuzaji viumbe maji. Aidha, katika kutekeleza mkakati huo, Wizara imetoa mafunzo ya kudhibiti magonjwa kwa watumishi **29** wa vituo binafsi vinne (**4**) vya kuzalisha vifaranga vya samaki vilivyopo katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani ambavyo ni Big fish farm (**5**); Eden Agri Aqua Ltd (**7**); Ruvu Fish Farm (**10**); na Judasa Fish Farm (**7**).

172. Katika Mwaka 2020/2021 Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI) imepandikiza samaki **101,500** katika malambo ya Kongogo (Dodoma - **20,000**), Mwanduigembe (Singida - **15,000**), Mwalusho (Simiyu - **20,000**), Mahiga (Mwanza -**20,000**), Igigwa (Tabora **10,000**), Mpera (Shinyanga - **1,500**), Wanging'ombe (Njombe - **5,000**) na Kitanda (Ruvuma - **10,000**) ikilinganishwa na samaki **1,500** waliopandikizwa mwaka 2019/2020.

173. ***Mheshimiwa Spika*,**Katika mwaka 2020/2021 Wizara kwa kuhahikisha kwamba inaongeza ufugaji wa samaki nchini ilishirikisha Jeshi la Magereza na Jeshi la Kujenga Taifa. Kufuatia ushirikishwaji huo Kituo cha Kingolwira (Morogoro) kimetoa vifaranga vya sato **25,000** kwa Gereza la Kwamngumi lililoko Korogwe, Tanga. Gereza hilo limejipanga kutumika kama shamba darasa na kuzalisha vifaranga kwa ajili ya wananchi wa Tanga na mikoa ya jirani. Pia, Kituo cha Ruhila (Ruvuma) kimeanza programu ya kujengea uwezo Gereza ya Kitai – Mbinga na kambi ya JKT Mlale. Wizara itaendelea kutoa ushauri wa kiufundi katika ujenzi wa miundombinu ya kufugia samaki na vitotoleshi vya vifaranga vya samaki.

174. Katika mwaka 2021/2022, Wizara itaendelea kuwezesha vituo vitano (**5**) vya ukuzaji viumbe maji vya Mwamapuli (Tabora), Ruhila (Ruvuma), Kingolwira (Morogoro), Nyengedi (Lindi) na Rubambagwe (Geita) ili viweze kuzalisha vifaranga vya samaki **milioni 3** na kutoa mafunzo kwa wakuzaji viumbe maji **3,000.** Aidha, Wizara imepanga kuhamasisha matumizi ya mbinu bora za ukuzaji viumbe maji na udhibiti wa magonjwa kwa vitotoleshi binafsi **10**, viwanda vya chakula cha samaki vitano (**5)**, na wakuzaji viumbe maji **3,000**.

175. ***Mheshimiwa Spika*****,** Katika mwaka 2021/2022 Wizara itawezesha kutambua na kufanya upembuzi yakinifu kwa maeneo yanayofaa kwa ufugaji samaki kwenye vizimba (*Strategic Environmental Impact Assessment*) kwa lengo la kupunguza gharama za uwekezaji. Zoezi hili litaanza na kanda mbili (**2**) katika Ziwa Victoria. Aidha, Wizara itaendelea na upandikizaji wa vifaranga vya samaki katika malambo **10** yaliyopo katika Mikoa ya Rukwa, Arusha, Mtwara, Ruvuma, Kilimanjaro, Simiyu, Dodoma, Tabora, Manyara na Shinyanga kwa lengo la kuboresha usalama wa chakula na lishe pamoja na kipato kwa wananchi wa maeneo husika.

176. Katika mwaka 2021/2022 Wizara itaendelea kutoa mafunzo rejea kwa maafisa uvuvi **100** ili kuboresha na kupanua wigo wa huduma za ugani wa ukuzaji viumbe maji nchini. Pia, Wizara imepanga kuanzisha mashamba darasa **40** katika Halmashauri **40** nchini kwa kushirikiana na OR - TAMISEMI. Aidha, kaguzi zenye siku kazi **300** zitafanyika katika viwanda vya vyakula vya samaki, vitotoleshi vya vifaranga vya samaki na mashamba ya ufugaji samaki katika mikoa yote nchini ili kuhakikisha Sheria, Kanuni na Miongozo ya ukuzaji viumbe maji inafuatwa.

177. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2021/2022 Wizara itaendelea na jitihada za kusimamia uzalishaji na kutoa mafunzo ya kuongeza thamani katika mazao ya ukuzaji viumbe maji bahari kwa wakulima **2,000** katika mikoa ya ukanda wa Pwani. Aidha, Wizara itaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika uzalishaji wa vifaranga vya

samaki, vyakula vya samaki na uzalishaji wa samaki na mazao mengine ya ukuzaji viumbe maji ili kufikia lengo la kuzalisha tani **25,000** za mazao ya ukuzaji viumbe maji ifikapo mwaka 2025.

178. Katika mwaka 2021/2022 Wizara itaanza ujenzi wa vituo vipya viwili (**2**) vya ukuzaji viumbe maji katika Mikoa ya Mtwara na Dar es Salaam ili kuhamasisha ufugaji wa samaki, kambamiti, kaa, majongoo bahari, chaza wa lulu na kilimo cha mwani katika ukanda wa Pwani. Kituo cha Dar es Salaam kitaendeshwa kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambacho kitakuwa na jukumu la kubuni teknolojia mbalimbali za ukuzaji viumbe maji bahari. Aidha, Wizara itaendelea na ukarabati na upanuzi wa vituo vya Nyengedi (Lindi), Ruhila (Ruvuma), Kingolwira (Morogoro), Mwamapuli (Tabora) na Rubambagwe (Geita) ili kuongeza uzalishaji wa vifaranga vya samaki na huduma za ugani.

179. ***Mheshimiwa Spika*****,** Ukarabati huu utafanyika kupitia Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi (*Agriculture and Fisheries Development Programme – AFDP*) inayofadhiliwa na Mfuko wa Kimataifa wa Kuendeleza Kilimo (*International Fund for Agricultural Development - IFAD*). Vilevile, AFDP itawezesha uanzishwaji wa mfumo wa ukusanyaji taarifa za wakuzaji viumbe maji, uanzishwaji wa mashamba darasa na kongani za wafugaji samaki, ununuzi wa vifaa vya TEHAMA, uandaaji wa vipindi vya redio televisheni na majarida ya ugani, ununuzi wa vyombo vya usafiri pamoja na utoaji mafunzo kuhusu masuala ya jinsia na lishe bora kwa jamii za wakuzaji viumbe maji.

Huduma za Ugani wa Uvuvi

180. ***Mheshimiwa Spika***, Jumla ya vipindi **20**vya redio na **15** vya luninga viliandaliwa na kurushwa hewani pamoja na makala za magazeti **30** kuhusu ufugaji na upatikanaji wa vifaranga bora vya samaki ikijumuisha ufugaji wa samaki katika vizimba yaliandaliwa. Aidha, nakala **5,000** za machapisho yaliyohusu ufugaji bora wa samaki, athari za uvuvi haramu na uhifadhi bora wa mazao ya uvuvi

yalichapishwa na kusambazwa kwa wadau wa uvuvi kwa lengo la kutoa elimu na uelewa kuhusu Sekta.

181. ***Mheshimiwa Spika***, Katika mwaka 2020/2021 Wizara imeendelea kutoa mafunzo rejea kwa wavuvi na wakuzaji viumbe maji nchini ambapo jumla ya wadau **16,733** kutoka Halmashauri **21** nchini wamepatiwa mafunzo hayo. Halmashauri hizo ni: Ludewa, Tanganyika, Kalambo, Nkasi, Ilemela, Nyamagana, Sengerema, Misungwi, Bunda, Busega, Mtwara mji, Mtwara vijijini, Lindi Vijijini, Iringa vijijini, Mpwapwa, Chamwino, Missenyi, Muleba, Bukoba, Chato na Geita vijijini. Mafunzo hayo yanahusu matumizi ya zana bora za uvuvi, ufugaji bora wa viumbe maji, uhifadhi bora wa mazao ya uvuvi na uanzishwaji na uimarishaji wa vyama vya ushirika vya wavuvi na wakuzaji viumbe maji.

182. ***Mheshimiwa Spika***, Katika mwaka 2020/2021 Wizara imeendelea kuhamasisha uanzishwaji wa vyama vya ushirika vya wavuvi na wakuzaji viumbe maji katika Halmashauri mbalimbali ambapo jumla ya vyama vipya **45** vimeanzishwa na hivyo kufanya vyama vya ushirika vilivyotambuliwa hadi sasa kufikia **147.** Aidha, Wizara imeviwezesha Vyama vya Ushirika vya Wavuvi kwa kununua injini **10** za boti, kati ya injini hizo nne (**4**) zimegawiwa katika vyama vinne (**4**) vya ushirika vya Izigo (Muleba), Kasalazi na Zilagula (Buchosa) na Kikumba itale (Chato) na injini sita (**6**) zilizobaki zitatolewa kwa vyama sita (**6**) vya ushirika vya Kabwe (Nkasi), Mwamgongo (Kigoma Vijijini), Msangamkuu (Mtwara Vijijini), Kilwa Kivinje (Kilwa), Igombe (Ilemela) na Chembaya (Buchosa). Vilevile, Wizara imeendelea kuunganisha vyama vya ushirika na taasisi za fedha kupitia Dawati la Sekta Binafsi ili viweze kupata mikopo yenye riba nafuu.

183. ***Mheshimiwa Spika***, Katika mwaka 2020/2021 Wizara ilishiriki katika maonesho mbalimbali ya kitaifa na kimataifa ikiwa ni pamoja na Maonesho ya kimataifa ya biashara-Sabasaba, Nanenane, siku ya chakula Duniani na Mvuvi day ambapo zaidi ya wadau **37,062** walitembelea mabanda ya Wizara na kupata elimu na ujuzi kuhusu Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji pamoja na ufahamu juu ya Sera ya Taifa ya

Uvuvi ya mwaka 2015 na Sheria mbalimbali zinazosimamia Sekta ya Uvuvi.

184. ***Mheshimiwa Spika*,** Katika mwaka 2020/2021 Wizara imeendelea kutoa huduma za ugani nchini kwa kutumia Wagani **677** ikilinganishwa na hitaji la sekta la kuwa na wagani **16,000** na hivyo kuwa na upungufu wa wagani **15,323**. Aidha, Wizara imeendelea kuwasiliana na Ofisi ya Rais TAMISEMI ili kuzielekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa kuajiri Maafisa Ugani. Vilevile, Wizara imeendelea kuhamasisha Sekta Binafsi kuwekeza katika kutoa huduma za ugani ili kuongeza upatikanaji wa huduma hizo katika maeneo mbalimbali nchini.

185. ***Mheshimiwa Spika*,** Katika mwaka 2021/2022 Wizara itahamasisha na kutoa mafunzo rejea kwa wadau wa uvuvi **25,000** ili kuwa na uvuvi endelevu. Vilevile, Wizara itaendelea kusambaza matokeo ya tafiti za kiteknolojia kwa wadau wa Sekta. Aidha, Wizara itaandaa na kurusha hewani vipindi **30** vya redio na **10** vya luninga kuhusu masuala ya Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji.

186. ***Mheshimiwa Spika*,** Katika mwaka 2021/2022 Wizara itawezesha vyama vya ushirika vya wavuvi na wakuzaji viumbe maji **20** kwa kuvipatia vifaa na zana bora za uvuvi ili kuongeza tija katika sekta. Aidha, Wizara itaendelea kushiriki na kuhamasisha wadau kushiriki katika maonesho ya Kitaifa na Kimataifa (Sabasaba, Siku ya Chakula Duniani na Siku ya Mvuvi Duniani) ili waweze kujifunza teknolojia mbalimbali za uvuvi pamoja na kubadilishana uzoefu.

187. ***Mheshimiwa Spika*,** Katika mwaka 2021/2022 Wizara itawawezesha maafisa ugani kwa kuwanunulia pikipiki kwa Halmashauri nane (**8**) za mwanzo ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu yao ipasavyo. Vilevile, Wizara itawawezesha wanafunzi wa Uzamili watatu (**3**) na Uzamivu wawili (**2**) kufanya tafiti za kipaumbele zinazohusiana na masuala ya uvuvi na ukuzaji viumbe maji ili kuendeleza na kutekeleza Agenda ya Taifa ya Utafiti wa Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji "2020-2025".

Taasisi Zilizochini ya Sekta ya Uvuvi Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania – TAFIRI

188. ***Mheshimiwa Spika***, Katika mwaka 2020/2021 Wizara kupitia Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI) imefanya tafiti mbalimbali ambazo zimesaidia kuendeleza Sekta ya Uvuvi na kuchangia katika ukuzaji wa uchumi wa wananchi na Taifa kwa ujumla. Aidha, tafiti hizi ziligusa maisha ya wananchi moja kwa moja na nyingine zilisaidia kuishauri Serikali katika kuweka mikakati na miongozo madhubuti katika kusimamia rasilimali za uvuvi nchini. Tafiti hizo zilifanyika kwa samaki wa maji asili na ukuzaji viumbe maji, ambapo tafiti kwenye maji asili zilifanyika katika maeneo mbalimbali ikiwemo Bahari ya Hindi Maziwa Makuu, Mabwawa na Mito.

Utafiti Bahari ya Hindi

189. ***Mheshimiwa Spika*****,** Katika mwaka 2020/2021 TAFIRI imeendelea kufanya tafiti mbalimbali katika Bahari ya Hindi. Utafiti wa uvuvi wa Pweza na mazingira yake ulifanyika katika maeneo ya Mtwara (Msangamkuu na Mgao), Tanga (Kwale na Mtambwe), Pwani/Mafia (Bwejuu, Jibondo na Jojo) na Lindi (Songosongo). Utafiti huu umewezesha kutengenezwa kwa ramani ya miamba yote inayotumika kwa uvuvi wa Pweza na hivyo kusaidia kufanya tathmini ya hali halisi ya miamba hii na kiwango cha uvuvi katika maeneo haya. Aidha, matokeo ya utafiti huu yamesaidia katika kuboresha Kanuni za Uvuvi na usimamizi endelevu wa uvuvi wa pweza. Utafiti huu umesaidia sana katika mchakato unaoendelea wa kupata Nembo ya Kiikolojia (Eco-labeling) kwa zao la Pweza kupitia taasisi ya *Marine Stewardship Council* (*MSC*) ya Afrika ya Kusini.

190. ***Mheshimiwa Spika*****,** Nembo ya Kiikolojia husaidia kuonesha kuwa zao husika limevunwa kwa njia endelevu na hivyo kufanya zao husika kuwa na thamani zaidi. Hivyo, mchakato huu ukikamilika, zao la Pweza wa Tanzania litauzwa katika soko lolote duniani likiwa na thamani ya juu. Aidha, kuongezeka kwa thamani ya Pweza wa Tanzania

kutasaidia kuongeza kipato kwa wavuvi wa Pweza, kuongeza mauzo nje ya nchi na kukuza uchumi wa nchi kwa ujumla. Mpaka sasa mchakato wa kupata Nembo ya Kiikolojia umefikia asilimia **89**, hivyo kuvuka kiwango cha chini cha asilimia **81** kinachohitajika na kuwezesha zao hili kuingia kwenye hatua ya juu ya kupata nembo husika. Hii ni hatua nzuri sana na hivyo Taasisi kwa kushirikiana na wadau wengine, inaendelea kukamilisha utafiti huu ili kukamilisha mchakato husika.

191. ***Mheshimiwa Spika*****,** Utafiti wa kuangalia hali ya uvuvi wa Kambamiti kwa wavuvi wadogo na kwa njia ya kukokora kwa kutumia meli ulifanyika na matokeo yake kusaidia kuboresha Kanuni za Uvuvi za mwaka 2020 na hivyo kuchangia katika usimamizi na uvuvi endelevu wa Kambamiti nchini. Matokeo yanaonesha kuwa kuna aina tano (**5**) za kambamiti wanaovuliwa na wavuvi wadogo lakini aina mbili ndio zinazopatikana kwa wingi, ambazo ni *Metapenaeus monoceros* na *Fenneropenaeus indicus*. Aidha, matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa Kambamiti wanazaliana katika miezi ya Septemba mpaka Disemba, na wanaanza kuonekana kwenye mavuvi wakiwa wachanga katika miezi ya Januari mpaka Machi kila mwaka. Hivyo, usimamizi utaimarishwa kwenye maeneo husika ili lengo la kuwa na uvuvi endelevu wa rasilimali za Kambamiti liweze kutimia. Aidha, matokeo ya utafiti huu yanatumika katika kutengeneza mpango wa usimamizi endelevu wa uvuvi wa Kambamiti.

192. ***Mheshimiwa Spika***, TAFIRI inafanya utafiti wa kupunguza upotevu baada ya mavuno (*postharvest loss*) wa samaki aina ya jodari na jamii zake kwa kuongeza thamani na kuzalisha mazao mengine yanayotokana na samaki hao. Aidha, utafiti huu utasaidia kupunguza au kuondoa kabisa changamoto ya kuharibika na kupotea kwa ubora wa samaki aina ya jodari. Utafiti umejikita katika kutengeneza aina mbalimbali za mazao/bidhaa zitokanazo na samaki hawa kama njia mojawapo ya kuongeza thamani na kuongeza ulaji wa samaki hawa katika masoko ya ndani na

kuongeza mauzo katika masoko ya nje. Hii itaongeza mchango wa uvuvi katika uchumi wa jamii na Taifa kwa ujumla.

193. ***Mheshimiwa Spika*****,** TAFIRI inafanya utafiti wa kuchunguza virutubisho vilivyomo kwenye samaki aina ya Jodari kwa afya ya binadamu ili kuweza kuhamasisha jamii kuwatumia kama kitoweo, kuongeza biashara ya samaki hawa kwenye soko la ndani, kuongeza chanzo cha protini na virutubisho vingine vitokanavyo na samaki kwa afya ya binadamu, na kupunguza umaskini kwa kuongeza kipato hasa kwa jamii ya wavuvi na wafanyabiashara wa samaki.

194. ***Mheshimiwa Spika,*** TAFIRI kwa kushirikiana na Mamlaka ya Usimamizi wa Uvuvi Bahari Kuu Tanzania (DSFA) imefanya utafiti wa kutambua maeneo ya uvuvi (*Potential Fishing Zones* - PFZ) kwa kutumia setelaiti. Lengo la utafiti huu ni kuwezesha kutambua maeneo yenye viashiria vya kuwepo samaki kwa kutumia teknolojia ya setelaiti. Ufatifi huu unawahusisha wavuvi ambao wamenufaika kwa kupunguza muda wa kutafuta samaki na matumizi ya mafuta, hivyo kupunguza gharama za uvuvi na kuongeza tija na pia kuondokana na uvuvi wa kubahatisha au wa kuwinda samaki. Utafiti huu unaendelea na tayari umeonesha kuleta ahueni na uvuvi wenye tija kwa jamii ya wavuvi. Pia, utafiti huu ni muhimu hasa katika kipindi hiki ambapo tunawekeza katika uvuvi wa Bahari Kuu kwa kutumia vyombo/meli za ndani.

Utafiti Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika

195. ***Mheshimiwa Spika*****,** Utafiti kuhusu wingi na mtawanyiko wa samaki katika Ziwa Victoria unaonesha kuwa samaki aina ya Sangara wameongezeka kutoka tani **816,694** mwaka 2019 hadi tani **1,024,623** mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia **25**. Ongezeko hili limetokana na juhudi za Serikali katika kupiga vita na kupambana na uvuvi haramu.

196. ***Mheshimiwa Spika*,** TAFIRI inatekeleza mradi wa FISH4ACP unaohusu uendelezaji wa mnyororo wa thamani wa dagaa na migebuka kutoka Ziwa Tanganyika. Madhumuni ya mradi huu ni kuongeza thamani ya dagaa na migebuka na kujenga uwezo wa wavuvi, wachakataji na wafanya biashara wa dagaa na migebuka kutoka Ziwa Tanganyika ili waweze kuvua kwa uendelevu, kuchakata na kuongeza thamani, na hatimaye kuuza katika soko la nje. Kwa sasa utafiti wa kutambua mnyororo mzima wa thamani (*value chain mapping*) unaendelea kwa kuwahusisha wadau wote kwenye mnyororo wa thamani wa dagaa na migebuka katika wilaya zilizopo katika mwambao wa Ziwa Tanganyika na mikoa ya jirani.

197. ***Mheshimiwa Spika*,** Katika mwaka 2020/2021 Wizara kupitia TAFIRI imefanya tafiti za ufugaji wa samaki nchini ili kubaini aina na mbegu bora ya samaki iliyoratibiwa kijenetiki; vyakula bora vya samaki vilivyotokana na malighafi asili inayopatikana katika eneo la wafugaji samaki; teknolojia bora na rahisi ya ufugaji samaki katika maeneo mbalimbali ya Tanzania na ufugaji wa vizimba katika Maziwa Makuu (Victoria, Tanganyika na Nyasa) na maziwa ya kati na madogo. Aidha, TAFIRI inaendelea kuweka miundombinu bora ya kuzalisha mbegu bora za samaki ili kuchangia katika kuondoa nakisi iliyopo nchini.

198. Katika mwaka 2021/2022 TAFIRI itaendelea kufanya tafiti za kuendelea kujua wingi, aina na mtawanyiko wa samaki katika Maziwa Makuu (Victoria, Tanganyika na Nyasa), Maziwa ya Kati, Maziwa Madogo, mito, mabwawa na maeneo oevu. TAFIRI itafanya utafiti wa kujua wingi na mtawanyo wa rasilimali za uvuvi katika Ukanda wa Bahari Kuu ya Bahari ya Hindi ambapo utafiti husika haujawahi kufanyika, na kwenye Ziwa Tanganyika ambapo utafiti husika ulifanyika takribani miaka **30** iliyopita. Utafiti katika Bahari ya Hindi na Ziwa Tanganyika utasaidia Wizara kuweka misingi bora ya usimamizi endelevu wa rasilimali za uvuvi katika maeneo haya.

199. ***Mheshimiwa Spika*,** Katika mwaka 2021/2022 TAFIRI itafanya tafiti katika maji ya kitaifa (territorial waters) na katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari (*Exclusive Economic Zone, EEZ*) kuchunguza uhusiano wa vinasaba kati ya makundi ya samaki aina ya Jodari na jamii zake na mazingira ya bahari yanayovutia uwepo wa samaki hao. Aidha, utafiti huu utawezesha kujua kiasi na mtawanyiko wa samaki wa kibiashara waliopo kwenye EEZ na kutoa fursa ya uwekezaji kwa eneo hili.

200. TAFIRI itafanya utafiti wa kurejesha mazingira ya bahari yaliyoharibiwa na uvuvi haramu, hasa matumbawe ambayo yaliharibiwa na matumizi ya vilipuzi ili kurejesha uhakika wa mapato katika uvuvi mdogo mdogo. Utafiti huu, pia, unalenga kungeza maeneo ya mavuvi ya pweza, hasa katika miamba inayoweza kufikiwa kwa urahisi na akina mama katika ukanda wa pwani. Utafiti huu utaongeza mapato.

Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi – FETA

201. ***Mheshimiwa Spika***, Katika mwaka 2020/2021 Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA) imeendelea kutoa mafunzo mbalimbali ya muda mrefu (Astashahada na Stashahada) na mfupi katika Tasnia ya Uvuvi. Ili kuwezesha wahitimu wa mafunzo husika kujiajiri na kufanya kazi kwa ufanisi na kuleta tija kwa Taifa, mafunzo hayo yametilia mkazo masuala ya ujasiriamali, ubunifu na mafunzo kwa vitendo. Katika kipindi hicho FETA ilidahili jumla ya wanafunzi **1,257** kwa masomo ya Astashahada na Stashahada katika Kampasi za Mbegani (Pwani), Nyegezi (Mwanza) na Kibirizi (Kigoma), sawa na ongezeko la wanafunzi **154** ikilinganishwa na wanafunzi **1,103** waliodahiliwa mwaka 2019/2020.

202. FETA imeendesha mafunzo ya muda mfupi kwa washiriki **3,573** ambayo yaliendeshwa katika kampasi tano (**5**) za Mbegani (Pwani) **774**, Nyegezi (Mwanza) **819**, Kibirizi (Kigoma) **125**, Mikindani (Mtwara) **255** na Gabimori (Mara) **285** na katika mialo ya Maziwa Makuu (Victoria **102**, Tanganyika **722** na Nyasa **110**), Ziwa Rukwa **178** na Bahari ya Hindi **203**. Mafunzo hayo yalihusu masuala yafuatayo:

uendeshaji boti kwa usalama; mbinu bora za uvuvi endelevu; ufugaji wa samaki kibiashara; utunzaji wa mazingira na bioanuai katika maji; uhifadhi, ubora na uchakataji samaki viwandani; na mbinu za upunguzaji wa upotevu wa mazao ya uvuvi baada ya kuvuliwa. Aidha, mafunzo ya uhifadhi na ubora kwa Kitengo cha Mabaharia wanaofanya kazi kwenye meli za kusafirisha mizigo nje ya nchi yalitolewa ili kiwe na uwezo wa kuhudumia mazao ya uvuvi ipasavyo.

203. ***Mheshimiwa Spika***, Mafunzo yenye ithibati ya Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) kuhusu uendeshaji salama wa vyombo katika maji yametolewa kwa waendesha vyombo **453** wakiwemo wavuvi ili kuwapa uelewa na mbinu salama za kuendesha vyombo hivyo ili kupunguza ajali (kuzama na kugongana) na majanga mengine yanayoweza kutokea kama vile moto na hatuastahiki za kujiokoa inapotokea ajali.

204. ***Mheshimiwa Spika***, FETA imeendesha mafunzo yanayohusu upotevu wa mazao ya uvuvi baada ya kuvunwa (*post-harvest loss*) kwa washiriki **110** kutoka Ziwa Nyasa. Mafunzo hayo yameendeshwa kwa ufadhili wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) na yalifanyika Wilaya ya Nyasa katika mialo ya Mbamba-Bay na Linda. Lengo la mafunzo hayo ni kuwasaidia wavuvi na wachakata samaki kuwa na ujuzi wa kuhifadhi samaki na kupunguza uharibifu kabla ya kumfikia mlaji. Aidha, majiko ya aina tatu ambayo ni Charcoal, Altona na Thiaroye yalitumika kukaushia samaki aina ya dagaa, mbufu/mbofu na mbasa mtawalia. Majiko hayo yanatumia kuni kidogo na hivyo kutunza mazingira.

205. ***Mheshimiwa Spika*,** FETA ikishirikiana na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kupitia TASAC ipo katika hatua za mwisho za kuanza kutoa mafunzo ya kimataifa ya "*Standards of Training, Certification and Watch Keeping for Fishing Vessels Personnel* (STCW– F95)" kwa wafanyakazi wa meli zinazovua katika EEZ baada ya Itifaki hiyo kuridhiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mei, 2020. Kwa sasa kinachosubiriwa ni Shirika la Bahari Duniani (*International Maritime Organization* – IMO) kuja kukagua wakufunzi na

miundombinu kwa ajili ya kuanza mafunzo hayo. Mafunzo haya ni muhimu kwa mabaharia wazawa ambao wanatakiwa kuwa na cheti cha mafunzo husika kwa ajili ya kufanya kazi kwenye meli za uvuvi.

206. ***Mheshimiwa Spika***, FETA imeendelea kuboresha mitaala yake ili iendane na wakati na kukidhi matakwa ya wadau wa Sekta ya Uvuvi. Mitaala iliyoboreshwa ni mitatu (**3**) katika Kampasi ya Nyegezi ambayo ni *Fisheries Science and Technology, Fisheries Management and Technology* na *Aquaculture Technology* na mitaala miwili (**2**) katika Kampasi ya Mbegani ambayo ni *Fish Processing, Quality Assurance and Marketing* na *Environment and Coastal Resource Management*.

Mitaala hii imeboreshwa ili kuwapa ujuzi na weledi zaidi wahitimu katika masuala ya dhana ya uchumi wa Buluu (Blue Economy), ubunifu, ujasiriamali, kuongeza thamani ya mazao na mafunzo kwa vitendo. Mafunzo haya yamekusudiwa kuwawezesha wahitimu kujiajiri na kuleta tija kwa mtu binafsi na Taifa kwa ujumla.

207. ***Mheshimiwa Spika***, Katika Mwaka 2021/2022 Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi utajenga kumbi mbili (**2**) za mihadhara katika Kampasi ya Mbegani kwa ajili ya Programu mbili (**2**) za Shahada ya Kwanza; maabara na maktaba katika Kampasi za Mikindani (Mtwara) na Gabimori (Mara). Vilevile Wakala utajenga na kuboresha vitotoleshi vitatu (**3**) vya vifaranga vya samaki katika Kampasi za Mbegani (Pwani), Nyegezi (Mwanza) na Gabimori (Mara); Pia itanunua mitambo ya kuzalishia vyakula bora vya samaki kwa Kampasi za Mbegani (Pwani) na Nyegezi (Mwanza), mitambo ya kukaushia samaki katika Kampasi za Mbegani (Pwani) na Nyegezi (Mwanza). Aidha, Wakala umejipanga kukarabati meli tatu (**3**) za Uvuvi za kufundishia kwa vitendo za MV Mafunzo, MV Jodari na MV Mdiria. Pia wakala utakarabati mitambo ya kuzalishia barafu na vyumba vya baridi (cold rooms) vya kuhifadhia Samaki.

Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO)

208. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali inaendelea na hatua za kufufua Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO) ambapo majukumu yaliyotekelezwa ni pamoja na:-

(i) Kukamilisha uandaaji wa Muundo wa Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO) na kuwasilishwa kwenye Mamlaka husika;

(ii) Kufanya tathmini ya hali ya majengo yaliyopo Makao Makuu ya TAFICO ili kuyafanyia ukarabati. Aidha, taratibu za kumpata mzabuni kwa ajili kukarabati jengo la ofisi ya utawala ya TAFICO umekamilika na tayari Mkandarasi amepatikana na kusaini Mkataba; na

(iii) Kuendelea na zoezi la utambuzi na uhakiki wa awali wa mali za TAFICO zilizopo nje ya Mkoa wa Dar es Salaam.

209. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022, TAFICO inatarajia kuanza kutekeleza lengo kuu la kuanzishwa kwake la uzalishaji kama ifuatavyo:-

(i) Kuanza uzalishaji wa barafu na uhifadhi wa samaki kwa kutumia mtambo wa kuzalisha barafu (*Ice plant*) unaotarajiwa kusimikwa mwaka 2022 chini ya Programu ya ESDP. Mtambo huo unategemewa kuzalisha barafu tani **2** kwa siku ambayo itatumika na Shirika pamoja na wavuvi wadogo kwa ajili ya kutunza ubora wa samaki, kuongezea thamani na kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi. Aidha, uhifadhi wa samaki utaanza kwa kutumia ghala la ubaridi la kuhifadhia samaki (*Cold Storage facility*) linalotarajiwa kusimikwa mwaka 2022;

(ii) Kufanya ukarabati wa majengo ya TAFICO ikiwemo jengo la zamani la mtambo wa kuzalisha barafu, jengo la utawala la zamani na kuanza ukarabati wa gati la kuegeshea meli; na

(iii) Kuendelea kuhamasisha Sekta Binafsi kuwekeza katika miradi ya TAFICO.

MIRADI YA MAENDELEO YA SEKTA YA UVUVI

I. Mradi wa Kikanda wa Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi SWIOFish (*South West Indian Ocean Fisheries Governance and Shared Growth Project – SWIOFish*)

210. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/2021 Wizara imeendelea kutekeleza Mradi wa Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIOFish) ambao unatekelezwa kwa kipindi cha miaka Sita (2015 hadi 2021). Mradi huo unatekelezwa katika pande zote mbili za Muungano na Taasisi ya Kusimamia Uvuvi Bahari Kuu chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia. Lengo kuu la mradi huo ni kuimarisha usimamizi madhubuti wa uvuvi katika ngazi ya kijamii, kitaifa na kikanda.

211. ***Mheshimiwa Spika*,** Kwa upande wa Tanzania Bara mradi unatekelezwa kupitia Wizara yangu ambapo katika mwaka 2020/2021 kazi mbalimbali zimetekelezwa zikiwemo:-

(i) Kufanya tafiti za uvuvi wa kipaumbele; kuimarisha ushiriki wa jamii za wavuvi katika usimamizi na ulinzi wa rasilimali za uvuvi; kuwezesha ulinzi na usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi na kuwezesha Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU) katika shughuli za
ulinzi wa rasilimali za uvuvi;

(ii) Kuimarisha na kujenga uwezo wa kitaasisi ikiwemo TAFIRI kwa kuipatia vitendea kazi vya kufanya utafiti wa kubaini maeneo yenye samaki wengi ili kufanya uvuvi wenye tija;

(iii) Umewezesha mafunzo ya muda mrefu katika ngazi za shahada ya uzamili (**10**), uzamivu (**5**) na ya muda mfupi (**18**) ili kuimarisha uwezo wa kiutendaji;

(iv) Kuimarisha miundombinu wezeshi kwa Sekta ya Uvuvi hususan ujenzi wa Maabara ya Utafiti wa Uvuvi Dar es Salaam; ofisi ya Hifadhi ya Bahari ya Kisiwa cha Mafia; ukarabati wa miundombinu ya soko la Samaki Feri (Dar es Salaam); na ujenzi wa Kituo cha Ukuzaji Viumbe Maji Bahari (*National Mariculture Resource Centre*) Kunduchi, Dar es Salaam. Aidha, Mradi umewezesha kujengwa kwa ofisi tano (**5**) za Vikundi vya Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi (BMU) katika Wilaya tano (**5**) za Ukanda wa Bahari ya Hindi ambazo ni Mkinga, Pangani, Chalinze, Bagamoyo na Lindi Vijijini;

(v) Kuandaa Mipango ya Usimamizi wa Samaki wa Kipaumbele ambayo ni Usimamizi wa Pweza na Kambamiti;

(vi) Kuwezesha uanzishwaji wa maeneo **12** ya usimamizi wa pamoja wa rasilimali za uvuvi (CFMAs) katika wilaya tano (**5**) za ukanda wa Bahari ya Hindi;

(vii) Kuwezesha uanzishwaji wa vikundi **174** vya kiuchumi (VICOBA) vyenye wanachama **4,222** katika Halmashauri za Ukanda wa Bahari ya Hindi na kutoa elimu ya ujasiriamali; na

(viii) Kuwezesha uandaaji na uimarishaji wa mifumo ya kukusanya takwimu za uvuvi(*Fisheries Information System - FIS*) na taarifa za sekta ya Uvuvi (*Management Information System -MIS*).

212. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2021/2022 Wizara kupitia mradi wa SWIOFish itawezesha kuandaa mkakati endelevu wa Vikundi vya Ulinzi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi (BMUs) katika Ukanda wa Bahari ya Hindi kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI. Aidha, mradi utawezesha kuhuisha Mpango wa Usimamizi wa Samaki wanaopatikana katika tabaka la juu la maji ya bahari (Dagaa, jamii ya Jodari na Vibua) ili kuimarisha usimamizi wa rasilimali hiyo. Vilevile, mradi utawezesha kukamilisha ujenzi na kuboresha miundombinu mbalimbali ikiwemo: ujenzi wa jengo la ofisi ya MPRU (Mafia); ukarabati wa miundombinu ya soko la Feri (Dar es Salaam);

na ujenzi wa Kituo cha Ukuzaji Viumbe Maji Bahari (*National Mariculture Resource Centre*) Kunduchi, Dar es Salaam.

II. Mradi wa Kuwezesha Kufanya Mapitio na Kuandaa Mpango Kabambe wa Sekta ya Uvuvi

(The TCP/URT/3709* - Technical Assistance to Develop Tanzania Fisheries Master Plan*)

213. ***Mheshimiwa Spika***, Mradi huu unatekelezwa kwa kushirikiana na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) unaolenga kufanya mapitio na kuandaa Mpango mpya baada ya Mpango Kabambe wa Uvuvi wa mwaka 2002. Hadi sasa kazi zifuatazo zimetekelezwa:-

i. Kukusanya taarifa ya awali kuhusu hali ya Sekta (*Baseline Information*) itakayotumika kama mwongozo wakati wa kundaaa Mpango mpya ambapo taarifa husika imekamilika; na

ii. Kuandaa Rasimu ya Mpango ambayo itakamilika mwisho wa mwaka wa fedha 2020/2021.

CHANGAMOTO ZA SEKTA YA UVUVI

214. ***Mheshimiwa Spika*,** Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Sekta ya Uvuvi imeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo:-

(i) Kuendelea kuwepo kwa uvuvi na biashara haramu ya mazao ya uvuvi;

(ii) Uwekezaji mdogo katika uvuvi wa Ukanda wa Uchumi wa Bahari na usindikaji wa mazao ya uvuvi;

(iii) Ushiriki mdogo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau wengine katika kusimamia na kulinda rasilimali za uvuvi;

(iv) Kutopatikana kwa mikopo ya kutosha na yenye masharti nafuu kwa wavuvi na wakuzaji viumbe maji ikilinganishwa na mahitaji yao;

(v) Uhaba wa Maafisa ugani wa uvuvi na ukuzaji viumbe maji ikilinganishwa na mahitaji ya wataalam katika Halmashauri;

(vi) Ukosefu na uchakavu wa miundombinu ya uvuvi hususan mialo ya kupokelea samaki na masoko;

(vii) Uwezo mdogo wa rasilimali fedha wa kufanya tafiti za mara kwa mara ili kutambua rasilimali zilizopo kwenye maji yetu hususan katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari; na

(viii) Kuendelea kuwepo kwa upotevu wa mazao ya uvuvi baada ya kuvunwa.

215. ***Mheshimiwa Spika*****,** Katika kukabiliana na changamoto hizi Wizara imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali kama inavyoonekana kwenye ***(*****Kiambatisho Na. 34*****)***

MAENEO YA VIPAUMBELE KATIKA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2021/2022

216. ***Mheshimiwa Spika***, Katika mwaka 2021/2022 Wizara kwa kushirikiana na wadau itatekeleza vipaumbele mbalimbali ili kuifikisha nchi yetu kwenye Uchumi Shindani wa Viwanda kwa Maendeleo ya Watu. Vipaumbele hivyo ni pamoja na:-

(i) Kuimarisha ulinzi na usimamizi shirikishi pamoja na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi nchini;

(ii) Kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali yatokanayo na Sekta ya Uvuvi;

(iii) Kuimarisha ukusanyaji wa mapato yatokanayo na Sekta ya Uvuvi;

(iv) Kuimarisha usimamizi wa rasilimali na uwekezaji katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari;

(v) Kuimarisha usimamizi na uthibiti wa ubora, usalama na viwango vya samaki na mazao ya uvuvi;

(vi) Kuimarisha miundombinu ya uvuvi na kukuza biashara ya mazao ya uvuvi;

(vii) Kuboresha upatikanaji wa taarifa na takwimu sahihi za uvuvi;

(viii) Kuimarisha utafiti, huduma za ugani na mafunzo ya uvuvi; na

(ix) Kuongeza upatikanaji wa vifaranga na vyakula bora vya samaki.

D. MASUALA MTAMBUKA KATIKA SEKTA ZA MIFUGO NA UVUVI

Dawati la Sekta Binafsi la Wizara

217. ***Mheshimiwa Spika***, Dawati la Sekta Binafsi lilianzishwa rasmi tarehe Oktoba, 2018. Lengo la kuanzishwa kwa Dawati hili ni kufuatilia na kutatua changamoto zinazoikabili Sekta Binafsi na kuhamasisha uwekezaji; uvuvi na ufugaji bora; na biashara ili kuongeza ajira na Pato la Taifa**.**

218. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2020/2021 Wizara kupitia Dawati imesaidia kuunganisha kampuni zinazohitaji huduma ya mikopo hususani kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kwa kusaidia utayarishaji wa Maandiko ya Biashara (Bankable Business Plans) ambapo kampuni **15** zimefaidika zikiwemo 11 za mifugo na 4 za uvuvi. Aidha, hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2021 kumekuwepo na ongezeko la maombi ya mikopo katika benki ya TADB kutoka shilingi **bilioni 63.8** zikiwemo shilingi **bilioni 26.1** kutoka sekta ya mifugo na shilingi **bilioni 37.7** kutoka sekta ya uvuvi mwaka 2019/2020 hadi kufikia shilingi **bilioni 98.5** ikiwemo shilingi **bilioni 47.1** sekta ya mifugo na shilingi **bilioni 51.4** sekta ya uvuvi katika

mwaka 2020/2021 ambapo kiasi cha shilingi **bilioni 27** kimeidhinishwa ikiwemo shilingi **bilioni 25.2** sekta ya mifugo na shilingi **bilioni 1.8** sekta ya uvuvi. Kati ya fedha zilizoidhinishwa shilingi **bilioni 22.5** kimetolewa ikiwemo shilingi **bilioni 21.4** sekta ya mifugo na shilingi **bilioni 1.1** sekta ya uvuvi.

219. ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2020/2021 Wizara kupitia Dawati la Sekta Binafsi imefuatilia uanzishwaji wa Bima ya Mifugo ili kuwakomboa wafugaji na kurahisisha upatikanaji wa mikopo ambayo imeanza kutumika mwaka 2020. Aidha, Shirika la Bima la Taifa (NIC) limetoa bima kwa vyama vya ushirika vitatu (**3**) vya wafugaji wa ng'ombe wa shirikisho la TDCU Tanga ambao walinufaika na mikopo ya ng'ombe kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB). Vyama hivyo ni UWAKO, UWAMKI na UWADAKI.

220. ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Dawati la Sekta Binafsi itaendelea kuainisha, kuratibu na kufuatilia changamoto za sekta binafsi na kuzitafutia ufumbuzi na kuhamasisha uwekezaji katika viwanda vya kusindika mazao ya mifugo (nyama, maziwa na ngozi), vyakula vya mifugo, ufugaji samaki katika vizimba, mabwawa, uzalishaji wa vifaranga na vyakula bora vya mifugo na samaki.

221. ***Mheshimiwa Spika,*** vyama vya Ushirika vya Wavuvi vipo **145**, kati ya hivyo, vilivyohai ni vyama **106** na vyama Sinzia **39.** Aidha, uhamasishaji unaendelea ili wavuvi waweze kutumia fursa hii. Aidha, vyama vya Ushirika vitatu (**3**) vya Zilagula (Sengerema) na Bukasiga (Ukerewe) vimepata jumla ya mkopo wa shilingi milioni **300.7** kutoka TADB na vimeshaanza utekelezaji. Chama cha Kikumbaitale cha Chato kipo kwenye hatua za mwisho za kupatiwa mkopo ambapo kitapatiwa jumla ya shilingi **milioni 200**. Pia, Wizara kupitia Dawati la Sekta Binafsi inaendelea kuunganisha vyama vya Ushirika **39** vya Wavuvi.

222. ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Dawati la Sekta Binafsi itaendelea kuainisha, kuratibu

na kufuatilia changamoto za sekta binafsi na kuzitafutia ufumbuzi na kuhamasisha uwekezaji katika viwanda vya kusindika mazao ya mifugo (nyama, maziwa na ngozi), vyakula vya mifugo, ufugaji samaki katika vizimba, mabwawa, uzalishaji wa vifaranga na vyakula bora vya mifugo na samaki.

Utawala Bora, Jinsia na UKIMWI

223. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021 jumla ya watumishi **613** wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi wameendelea kuhamasishwa kupima afya zao kupitia vikao mbalimbali vya watumishi.

224. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021 vikao saba (**7**) vya Kamati ya Ajira vimefanyika vikiwemo vitatu (**3**) sekta ya mifugo na vinne (**4**) sekta ya uvuvi ambapo watumishi **39** wamethibitishwa kazini wakiwemo **25** sekta ya mifugo na **14** sekta ya uvuvi, Watumishi **13** wamebadilishwa kada wakiwemo watano **(5)** sekta ya mifugo na nane (**8**) sekta ya uvuvi na watumishi wapya wawili **29** wameajiriwa wakiwemo **27** sekta ya mifugo na wawili (**2**) sekta ya uvuvi. Pia, taarifa za watumishi **828** zimehakikiwa wakiwemo **450** sekta ya uvuvi na **378** sekta ya uvuvi. Aidha, ufuatiliaji wa utendaji wa watumishi walio katika vituo vya nje ya Makao Makuu ya Wizara umefanyika.

225. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/2022 Wizara itaendelea kuhamasisha watumishi **577** kujikinga na maambukizi mapya ya VVU/UKIMWI na kupima afya zao kwa hiari wakiwemo **517** sekta ya mifugo na **60** sekta ya uvuvi, kuwezesha vikao vinne (**4**) vya Kamati ya Maadili na kuwezesha utekelezaji wa Mfumo wa HCMIS, GSPP, OPRAS na Mkataba wa Huduma kwa Wateja.

Teknolojia ya Habari na Mawasiliano Serikalini

226. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021 Wizara imeendelea kutumia kwa ufanisi mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwenye utendaji kazi wa

kila siku. Aidha, Wizara imewekeza kwenye matumizi ya mfumo wa ofisi mtandao (e-Office) ambapo mfumo huu umeweza kuwaunganisha wadau wa Wizara kwa kuwawezesha kutuma taarifa au barua kwa njia ya kieletroniki kupitia barua pepe ya barua@mifugo.go.tz au barua@uvuvi.go.tz ambapo mdau anapata mrejesho kwa njia ya ujumbe mfupi wa maneno (SMS).

227. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutumia Mifumo ya TEHAMA kwenye usimamizi na ukusanyaji wa maduhuli. Katika utekelezaji huo, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya RaisTAMISEMI inakusanya maduhuli yatokanayo na vibali vya ukaguzi wa Afya ya Wanyama kupitia mfumo wa makusanyo wa *Local Government Revenue Collection Information System (LGRCIS)*. Kupitia mfumo huo wastani wa makusanyo umeongezeka kutoka Shilingi **3,795,970,430.02** kwa kipindi cha Julai hadi Aprili 2019/2020 hadi kufikia Shilingi **6,174,581,718.81** kwa kipindi kama hicho 2020/2021. Aidha, Mfumo wa Ukusanyaji wa Maduhuli ya *Uvuvi (Fisheries Revenue Collection Information System - FIRCIS*) umeboreshwa kwa kuingiza kasma ya leseni za uingizaji na usafirishaji wa mazao ya uvuvi ambapo leseni na vibali vya ukuzaji viumbe maji zitatoka kielektroniki. Pia, kutokana na matumizi ya Mifumo ya TEHAMA uwazi na uwajibikaji umeongezeka kwenye makusanyo ya maduhuli.

228. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021, Wizara kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo imeendelea kutoa elimu kwa wafugaji kupitia mfumo wa ugani kiganjani. Pia, Wizara imefunga Mfumo wa *Event Mobile Application (EMA-i)* kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa **119** kwa ajili ya kutoa taarifa za mapema na taadhari ya milipuko ya magonjwa ya mifugo.

229. ***Mheshimiwa Spika***, katika jitihada za kuimarisha mawasiliano na utendaji kazi kwa njia ya mtandao, Wizara imeboresha miundombinu ya TEHAMA katika vituo vilivyo chini ya Wizara ambapo mnada wa upili wa Pugu pamoja na Taasisi za nne (**4**) za sekta ya mifugo zilizopo Dar es Saalaam. Pia, Vituo vya Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi vya Mwanza,

Kigoma na Dar es Salaam vimeboreshwa kwa kufunga mtandao wa Serikali (*Govnet*).

230. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/2021 Wizara imeendelea kutoa taarifa mbalimbali kwa wadau wa mifugo na uvuvi kupitia vipindi mbalimbali vya radio na televisheni kwa kutayarisha na kurusha hewani jumla ya vipindi **22** vya televisheni na vipindi **34** vya redio kwa ajili ya kutoa elimu kwa umma.

231. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/2022, Wizara itasanifu na kutengeneza mfumo wa TEHAMA wa kusimamia vibali vya kusafirisha mifugo na mazao yake ndani na nje ya nchi, kujenga uwezo juu ya matumizi endelevu ya TEHAMA kwa watumishi wa Wizara na kusanifu na kutengeneza mfumo jumuishi wa TEHAMA wa Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji Mifugo, vituo vya ukusanyaji wa maduhuli kwa sekta ya uvuvi pamoja na utoaji wa huduma za ugani. Pia, Wizara itaendelea kutoa taarifa na maarifa kwa wananchi juu ya mambo mbalimbali yanayohusu sekta ya mifugo kupitia redio, televisheni na magazeti.

Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi

232. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/2021, Wizara imefanya uhamasishaji wa jamii za wafugaji na wakulima-wafugaji juu ya uzalishaji na utumiaji wa nishati ya kinyesi cha wanyama (Biogas) ambapo wataalam wa mifugo **90** kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa mikoa ya Manyara (**42**) na Tabora (**48**) wamepatiwa mafunzo juu ya umuhimu wa matumizi ya nishati hii mbadala ili waweze kwenda kuwajengea uwezo wafugaji na wakulima.

233. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/2021 Mafunzo kwa Wawezeshaji (ToT) kuhusu ufugaji unaohimili mabadiliko ya tabianchi (*Climate Smart Agriculture - CSA*) yametolewa kwa wawezeshaji **90** katika Halmashauri **7** za Mkoa wa Manyara (Babati Manispaa, Babati DC, Mbulu TC, Mbulu DC, Hanang DC, Kiteto DC, na Simanjiro DC) na Halmashauri nane

(**8)** za Mkoa wa Tabora (Tabora Manispaa, Uyui DC, Sikonge DC, Urambo DC, Kaliua DC, Nzega TC, Nzega DC na Igunga DC).

234. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia utunzaji na uhifadhi wa mazingira ambapo kwa kushirikiana na Baraza la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Wizara imetoa mafunzo yanayohusu ukaguzi wa masuala ya mazingira '*Environmental Audit'* kwa watumishi **11** kutoka Idara ya Uvuvi makao makuu na katika Kanda za Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Kanda ya Pwani, Kanda ya Kati na Bwawa la Nyumba ya Mungu.

235. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilifanya ufuatiliaji wa utunzaji wa mazingira kwa wafugaji wa samaki **11** kutoka katika Wilaya za Sengerema, Magu, Ukerewe, Bunda, Msoma Mjini na Rorya. Aidha, zoezi hili liliambatana na utoaji wa mafunzo kwa vitendo kuhusu ufugaji wa samaki unaozingatia utunzaji wa mazingira.

236. ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2021/2022, Wizara itawezesha mafunzo ya wawezeshaji **192** kuhusu utekelezaji wa mwongozo wa ufugaji unaohimili mabadiliko ya tabianchi (CSA) katika Mamlaka ya Serikali za mitaa **32** na kufanya tathmini ya athari za kimazingira na kijamii (*Environemntal and Social Impact Assesment - ESIA*) katika miradi mitano (**5**) ya uwekezaji katika Sekta ya Mifugo; kutoa elimu juu ya usimamizi na utunzaji wa mazingira, ambapo nakala **1,000** kwa ajili ya kuelimisha wananchi kuhusu utunzaji wa mazingira zitaandaliwa; na kuandaa miongozo kwa ajili ya kufanya ukaguzi wa kimazingira kwa wafugaji samaki kwenye vizimba na mabwawa.

Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa

237. ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2020/2021, Wizara imeendelea kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa ili kuendeleza sekta za mifugo na uvuvi. Kupitia ushirikiano huo, nchi yetu inapata fursa ya kushiriki na kutekeleza sheria, miongozo, mikataba, itifaki na taratibu mbalimbali za

kikanda na kimataifa zenye lengo la kuimarisha sekta za mifugo na uvuvi hususan udhibiti wa magonjwa ya mifugo na samaki; biashara ya mifugo na uvuvi na mazao yake.

238. ***Mheshimiwa Spika*****,** baadhi ya taasisi za kikanda na kimataifa tunazoshirikiana nazo ni pamoja na:Taasisi ya Usimamizi wa Uvuvi Ziwa Victoria (*Lake Victoria Fisheries Organization-LVFO*), Mamlaka ya Usimamizi wa Ziwa Tanganyika (*Lake Tanganyika Authority-LTA*), Kamisheni ya Usimamizi wa Uvuvi wa Jodari ya Bahari ya Hindi (*Indian Ocean Tuna Commission-IOTC),* Kamisheni ya Usimamizi wa Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (*South West Indian Ocean Fisheries Commision- SWIOFC*), Umoja wa Nchi zilizoko katika Mwambao wa Bahari ya Hindi (*Indian Ocean Rim Association* - IORA), *Western Indian Ocean Marine Science Association* (WIOMSA), Kamisheni ya Usimamizi wa Nyangumi (*International Whaling Commission-IWC*), Kamisheni ya Bahari ya Hindi (*Indian Ocean Commission-IOC*) na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Africa (SADC). Taasisi ya Wanawake wa Afrika katika Rasilimali za Mifugo na Kilimo-Biashara (*African Women in Animal Resource Farming and AgribusinessAWARFA*) na Shirika la Afya Duniani (WHO) na Shirika la Afya ya Wanyama (OIE).

239. ***Mheshimiwa Spika*****,** mashirika mengine tunayoshirikiana nayo ni Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD), Benki ya Dunia, Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Jumuiya ya Nchi Wanachama wa Umoja wa Ulaya (EU), *African Union Interafrican Bureau for Animal Resources* (AU – IBAR), Serikali ya Uholanzi na Serikali ya Japan kupitia Programu ya Uchumi na Maendeleo ya Jamii (*Economic and Social Development Programme – ESDP*), *Overseas Fishery Cooperation Foundation (OFCF) of Japan* na *Japanese International Cooperation Agency* (JICA).

240. ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2020/2021, Wizara imeshiriki katika vikao vya Jumuiya ya Afrika Mashariki na SADC ikiwemo kikao cha Kamati ya Sekta ya Biashara ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kujadili masuala ya biashara

ndani ya Jumuiya; mkutano wa uzinduzi wa Taasisi ya Wanawake wa Afrika katika Rasilimali za Mifugo na Kilimo-Biashara (*African Women in Animal Resource Farming and Agribusiness-AWARFA*); na Kikao cha Wakuu wa nchi za SADC katika ngazi ya wataalamu kilichofanyika mwezi Agosti, 2020 jijjini Dar es Salaam.

241. ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2020/2021 Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Chakula Duniani (FAO), Shirika la Afya Duniani (WHO) na Shirika la Afya ya Wanyama (OIE) imeendelea kufuatilia viashiria vya Ugonjwa wa Mafua Makali ya Ndege unaoambukiza binadamu kutokana na kugusana na ndege wenye virusi vya ugonjwa huo. Ili kufanikisha ufuatiliaji huo jumla ya sampuli 640 zilichukuliwa kwenye maeneo hatarishi wanakotua ndege kutoka Bara la Ulaya na matokeo ya kimaabara yanaonesha mpaka sasa hakuna virusi vya ugonjwa huo hapa nchini.

242. ***Mheshimiwa Spika***, Katika mwaka 2020/2021 Wizara imeshiriki kwenye mikutano na vikao mbalimbali vya Kikanda kama ifuatavyo:-

(i) Vikao vya Umoja wa Nchi zilizoko katika Mwambao wa Bahari ya Hindi (*Indian Ocean Rim Association-IORA*) ambavyo vililenga kuandaa Mpango wa Pamoja wa Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi katika Bahari ya Hindi na kujenga uwezo na kubadilishana uzoefu kwa watendaji na wataalam;

(ii) Mkutano wa sita (**6**) wa Tume ya Kudumu ya Pamoja kati ya Nchi yetu na Jamhuri ya Burundi kwa lengo la kuimarisha mashirikiano katika sekta mbalimbali ikiwemo Sekta ya Uvuvi. Katika Mkutano huo, rasimu ya Hati ya Makubaliano ya Mashirikiano (MoU) katika masuala ya uvuvi na ukuzaji viumbe maji kati ya nchi hizi uliandaliwa;

(iii) Mkutano wa Baraza la Mawaziri wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wenye dhamana na usimamizi wa Sekta ya Uvuvi Ziwa Victoria ili kujadili masuala mbalimbali ya uvuvi ikiwemo kudhibiti uvuvi

haramu na utoroshaji wa mazao ya uvuvi, biashara ya mazao ya uvuvi hususan zao la mabondo kwa lengo la kuhuisha taratibu husika; na

(iv) Mikutano ya Shirika la Biashara Duniani (WTO) ili kujadili namna ya kuwezesha wavuvi wadogo katika nchi zinazoendelea kunufaika na rasilimali zao.

(v) Mkutano wa Kamisheni ya Usimamizi wa Uvuvi wa Jodari ya Bahari ya Hindi (*Indian Ocean Tuna Commission-IOTC)* ambao ulijadili mfumo wa mgawanyo wa mavuno (*Quota system*) ya samaki katika Bahari ya Hindi na kuwezesha nchi kupata mgawanyo mkubwa utakaotuwezesha kufaidika na rasilimali za uvuvi kupitia Uchumi wa Buluu.

243. ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2021/2022 Wizara itaendelea kushirikiana na Taasisi za kikanda na kimataifa katika sekta za mifugo na uvuvi ili kuimarisha mahusiano katika kuendeleza sekta ya hizi.

Uwekezaji na Uwezeshaji katika Sekta za Mifugo na Uvuvi

Uwekezaji Sekta ya Mifugo

244. ***Mheshimiwa Spika*,** Wizara imeendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika sekta ya mifugo kwa kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji ikiwemo kuboresha Sheria na Kanuni katika sekta ya mifugo.

245. ***Mheshimiwa Spika*,** kutokana na kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji katika tasnia ya ngozi, katika mwaka 2020/2021 uzalishaji wa viatu vya ngozi umefikia jozi **2,855,600**ikilinganishwa na jozi **1,715,000** zilizozalishwa katika mwaka 2019/20. Aidha, ongezeko hili limesababishwa na Kiwanda cha *Kilimanjaro International Leather Company Ltd*kuanza uzalishaji. Pia, kiwanda cha ngozi cha *ACE Leather* cha Morogoro kimeanza kufanya kazi ambapo kitachangia kuongezeka kwa ngozi iliyosindikwa kufikia hatua ya mwisho (finished leather) kutoka futi za mraba milioni **9** zilizokuwa zikizalishwa hadi mwezi Desemba mwaka 2020 hadi futi za

mraba milioni **25** katika mwaka 2021/2022. Aidha, kwa sasa kuna viwanda vya kusindika ngozi vitano (**5**), viwanda vya kutengeza bidhaa za ngozi vitano (**5**) na viwanda vidogo **150** vinavyozalisha bidhaa za ngozi nchini (**Kiambatisho Na.15 na 16**).

246. ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2020/2021 vipo viwanda **10** vya kusindika nyama na machinjio **25** yanayofanya kazi. Aidha, machinjio saba (**7**) hazifanyi kazi. Pia, ujenzi wa machinjio/viwanda saba (**7**) unaendelea katika maeneo mbalimbali (**Kiambatisho 17-20**).

247. ***Mheshimiwa Spika****,* kwa ujumla ipo minada ya mifugo **530** ikiwemo minada ya awali **504**, minada ya upili **15** na minada ya mpakani **11**. Ili kuboresha mazingira ya biashara ya mifugo, Serikali imeendelea kujenga na kukarabati minada ya mifugo. Katika mwaka 2020/2021 ukarabati wa minada **6** upo katika hatua mbalimbali ikiwemo Mnada wa Ipuli-Tabora (**95%**), Igunga–Tabora (**90%**), Nata-Tabora (**70%**), Murusagamba–Kagera (**45**%), Kizota–Dodoma (**5%**) na uchimbaji wa kisima kirefu katika mnada wa mifugo wa mpakani wa Kirumi Butiama–Mara umefikia asilimia **45**. Pia, ujenzi wa mnada mpya wa Buzirayombo – Geita umefikia asilimia **35**.

248. ***Mheshimiwa Spika*****,** ili kuwa na chanjo za magonjwa ya mifugo za kutosha kulingana na mahitaji nchini, Wizara imeendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya kuzalisha chanjo za magonjwa ya mifugo ambapo katika mwaka 2020/ 2021 mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

(i) Upanuzi wa Kiwanda cha Uzalishaji Chanjo (TVI) Kibaha Mkoani Pwani unaendelea kwa kujenga jengo jipya litakalotumika katika utengenezaji wa chanjo za bacteria ambapo tayari ujenzi huo umefikia asilimia 90; na

(ii) Ujenzi wa kiwanda kikubwa cha kuzalisha chanjo za mifugo cha *Hester Biosciences Africa Limited* cha Kibaha chenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 18

(Shilingi bilioni 41.4) unaendelea ambapo ujenzi umekamilika kwa asilimia 98.

249. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa na sekta binafsi inawekeza katika ujenzi wa majosho ili kudhibiti magonjwa ya mifugo. Katika mwaka 2020/2021, ujenzi wa majosho **13** umekamilika katika Halmashauri za Wilaya **8** na majosho mengine **12** yanaendelea kujengwa kwa ushirikiano kati ya Halmashauri za Wilaya, wafugaji na wadau wengine (**Kiambatisho Na.21**). Aidha, katika mwaka 2021/2022 Wizara itajenga majosho **129** katika Halmashauri mbalimbali nchini.

250. ***Mheshimiwa Spika***, sekta binafsi inaendelea kuhamasika katika uzalishaji wa malisho na mbegu za malisho. Katika mwaka 2020/2021, jumla ya wawekezaji binafsi **36** wamewekeza katika eneo lenye ukubwa wa hekta **238** kwa ajili ya kilimo cha malisho. Aidha, jumla ya tani **32.8** za mbegu za malisho zimezalishwa na kusambazwa kutoka katika mashamba ya sekta binafsi.

Uwekezaji Sekta ya Uvuvi

251. ***Mheshimiwa Spika*****,** Serikali imeendelea kuhamasisha Sekta binafsi kujenga viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi na maghala ya kuhifadhia na kugandisha mazao ya uvuvi ambapo hadi sasa kuna maghala ya kuhifadhi mazao ya uvuvi **90,** viwanda vikubwa vya kuchakata mazao ya uvuvi **16,** viwanda vya kati vitano (**5**) na viwanda vidogo **33**. Vilevile, kuna viwanda nane (**8**) vya kuchakata mabondo ya Sangara na viwanda vitano (**5**) vya kutengeneza zana za uvuvi.

252. ***Mheshimiwa Spika*****,** Ili kuchochea uwekezaji katika uvuvi wa Bahari Kuu, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali itakamilisha upembuzi wa kina (*bathymetric, topographic and geotechnical survey*) katika eneo la Mbegani, Bagamoyo na kuanza ujenzi wa bandari ya uvuvi. Uwepo wa bandari utawezesha meli zinazovua Bahari Kuu

kuja kushusha samaki na hivyo kuchochea fursa za uwekezaji ikiwemo kujenga viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi na mitambo ya kuzalisha barafu.

253. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Programu ya Uchumi na Maendeleo ya Jamii (*Economic and Social Development Programme* – ESDP) inayofadhiliwa na Serikali ya Japan. Kupitia Programu hiyo, vifaa vya uvuvi ikiwemo meli moja yenye uwezo wa kuvua katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari vitanunuliwa. Hadi sasa, hatua za uundaji wa meli na ununuzi wa vifaa vya uvuvi zinaendelea kufanyika na uundaji wa meli unatarajiwa kukamilika mwezi Januari 2022.

254. ***Mheshimiwa Spika***, kupitia Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi (*Agriculture and Fisheries Development Programme* – AFDP) imepata mkopo wenye masharti nafuu kutoka Mfuko wa Kimataifa wa Kuendeleza Kilimo (*International Fund for Agriculture Development* - IFAD) kwa ajili ya kununua meli nane (**8**) za kuvua katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu ambapo meli nne (**4**) zitakuwa Tanzania Bara chini ya TAFICO na nne (**4**) Zanzibar chini ya Kampuni ya Uvuvi ZanzibarZAFICO. Kwa upande wa Tanzania Bara, meli mbili (**2**) za mwanzo zitanunuliwa mwaka 2021/ 2022 na meli zingine mbili (**2**) mwaka 2023/2024.

255. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2021/2022 TAFICO inatarajia kuanza kutekeleza lengo kuu la kuanzishwa kwake la uzalishaji kama ifuatavyo:-

(i) Kuanza kuvua kwenye Ukanda wa Uchumi wa Bahari (*Exclusive Economic Zone – EEZ*) na Maji ya Kitaifa (*Territorial Water*) kwa kutumia meli moja (**1**) ya uvuvi yenye urefu wa mita **22**. Meli inatarajiwa kuwasili mwezi Januari 2022 na kuanza uzalishaji; na

(ii) Kuanza uzalishaji wa barafu na uhifadhi wa samaki kwa kutumia mtambo wa kuzalisha barafu (*Ice plant*) unaotarajiwa kusimikwa mwaka 2022 chini ya Programu ya ESDP. Mtambo huo unategemewa kuzalisha barafu tani **2**

kwa siku ambayo itatumika na TAFICO pamoja na wavuvi wadogo kwa ajili ya kutunza ubora wa samaki, kuongezea thamani na kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi. Aidha, uhifadhi wa samaki utaanza kwa kutumia ghala la ubaridi la kuhifadhia samaki (*Cold Storage facility*) linalotarajiwa kusimikwa mwaka 2022.

256. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaimarisha uwekezaji katika Sekta ya Uvuvi kwa kuendelea na taratibu za kufufua Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO) na kuendelea na mpango wa kujenga Bandari ya Uvuvi ili kuwezesha uwekezaji katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari. Pia, imeendelea kuhamasisha Sekta Binafsi kuwekeza katika Sekta ya Uvuvi ambapo hadi sasa kuna viwanda vikubwa **16** vya kuchakata samaki na viwanda vitano (**5**) vya kutengeneza zana za uvuvi. Aidha, uwekezaji katika tasnia ya Ukuzaji Viumbe Maji umeongezeka ambapo hadi Aprili, 2021 kuna vizimba vya kufugia samaki **473**, mabwawa **30,032**, vitotoleshi **28** na viwanda **11** vya kutengeneza chakula cha samaki.

Gawio la Serikali katika Sekta ya Mifugo

257. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/2021, Taasisi, Bodi na Wakala zilizopo chini ya Wizara ambazo ni NARCO, LITA, TALIRI, TVLA, Bodi ya Nyama Tanzania, Bodi ya Maziwa Tanzania, TAFIRI, FETA na MPRU zimetoa gawio kwa Serikali lenye jumla ya shilingi **348,940,989.85** (**Kiambatisho Na.35)** ikilinganishwa na kiasi cha shilingi **1,492,500,000** kilichotolewa mwaka 2019/2020. Aidha, Wizara imeendelea kuhamasisha uwepo wa tija katika taasisi hizo ili kuweza kuchangia zaidi mapato katika mfuko wa Serikali.

Michango katika Shughuli za Kijamii

258. ***Mheshimiwa Spika,***katika mwaka 2020/2021, Taasisi, Bodi na Wakala zilizo chini ya Wizara zimetoa mchango wa shilingi **279,636,302.48 (Kiambatisho Na.35)** ikilinganishwa na shilingi **560,971,726** zilizotolewa mwaka 2019/2020. Michango hiyo ni kwa ajili ya kuchangia shughuli za maendeleo ya jamii ikiwemo uchanjaji mifugo, kutoa elimu kwa wafugaji,

kuendesha elimu ya uhifadhi katika vijiji nje ya eneo la hifadhi za Bahari na maeneo tengefu, kutoa misaada ya vifaa vya kielimu kwa shule za msingi katika Wilaya ya Mafia nk.

E HITIMISHO

Shukrani

259. ***Mheshimiwa Spika*,** kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wale wote waliochangia kwa namna moja au nyingine katika kuiwezesha Wizara kufanikisha majukumu yake. Mafanikio yaliyopatikana katika mwaka uliopita yametokana na ushirikiano na misaada ya kifedha na kiufundi kutoka kwa nchi wahisani, mashirika mbalimbali ya kitaifa na kimataifa, taasisi za fedha za kitaifa na kimataifa, taasisi za hiari zisizokuwa za kiserikali na mashirika ya kidini bila kusahau hamasa na ushiriki wa wananchi wakiongozwa na Waheshimiwa Wabunge na Madiwani.

260. ***Mheshimiwa Spika*,** napenda kuchukua fursa hii kuzitambua na kuzishukuru nchi za Japan, Korea Kusini, Uingereza, Jamhuri ya Watu wa China kwa kuchangia katika maendeleo ya Sekta ya Mifugo.

261. ***Mheshimiwa Spika***, napenda pia kutambua na kuzishukuru jumuiya za kikanda ambazo ni Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) na Umoja wa Nchi za Ulaya (EU). Aidha nashukuru taasisi za Kifedha na Wadau wa Maendeleo ambao ni Benki ya Dunia (WB), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Shirika la Kimataifa la Ushirikiano la Jamhuri ya Korea (KOICA), Shirika la Kimataifa la Ushirikiano la Jamhuri ya Japan (JICA), Shirika la Misaada la Ireland (Irish Aid), Shirika la Misaada la Marekani (USAID), Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (DfID), Taasisi ya Rasilimali za Wanyama ya Umoja wa Afrika (AU-IBAR), Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (OIE), Shirika la Maendeleo ya Uswisi (SDC), Shirika la Ushirikiano la Ujerumani (GIZ), United Nations University (UNU), Shirika la Maendeleo la Denmark (DANIDA), na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Sweden (SIDA); na mashirika ya FAO, WHO, IAEA,

UNICEF, UNDP, UNIDO, SIDA, ILRI, CIAT, ASARECA na CCARDESA. Pia, natoa shukrani kwa Mifuko ya Kimataifa ya GEF na IFAD kwa michango yao katika kuendeleza Sekta za Mifugo na Uvuvi.

262. ***Mheshimiwa Spika***, pia, napenda kushukuru Mashirika na Taasisi za hiari za *Bill and Melinda Gates Foundation, World Wide Fund for Nature (WWF), Indian Ocean Commission (IOC), South West Indian Ocean Fisheries Commission (SWIOFC), Heifer Project Tanzania (HPT), Overseas Fisheries Cooperation Foundation of Japan (OFCF), Vetaid, Care International, OXFARM, Welcome Trust, World Vision, FARM Africa, Land O' Lakes, Building Resources Across Communities (BRAC), World Society for Protection of Animals (WSPA), Global Alliance for Livestock and Veterinary Medicine (GALVmed), Institute of Social Studies (ISS), International Land Coalition (ILC), British Gas International, Sea Sense, Indian Ocean Tuna Commission (IOTC), International Whaling Commission (IWC), SmartFish, Marine Stewardship Council (MSC),* Mashirika na Taasisi mbalimbali za humu nchini zinazojihusisha na uendelezaji wa Sekta za Mifugo na Uvuvi.

263. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee nimpongeze na kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan,** kwa namna anavyoliongoza Taifa letu tangu alipokula kiapo tarehe 19 Machi, 2021 na anavyotusimamia katika kutekeleza majukumu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Nina imani kuwa ndani ya uongozi wake tutahakikisha kuwa llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 - 2025 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2021/2022 – 2025/202 inatekelezwa kikamilifu hususan katika sekta za mifugo na uvuvi.

264. ***Mheshimiwa Spika,*** pia napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza wadau mbalimbali katika sekta za mifugo na uvuvi wafugaji na wavuvi hususan wanaozingatia Sheria katika utendaji wa kazi zao kote nchini kwa kutunza, kuzalisha na kulinda rasilimali za Taifa. Napenda kuwaahidi kwamba Wizara yangu itaendelea kusimamia na kuunga

mkono juhudi za wafugaji, wavuvi, wasindikaji na wafanyabiashara wa bidhaa za mifugo na uvuvi.

265. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kurejea tena kutoa shukrani zangu za dhati kwa **Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega,** Mbunge wa Jimbo la Mkuranga, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa ushauri wake katika kusimamia kazi za Wizara. Aidha, napenda pia nitoe shukrani zangu kwa Katibu Mkuu Mifugo, **Prof. Elisante Ole Gabriel** na Katibu Mkuu Uvuvi, **Dkt. Rashid Adam Tamatamah**, Wakurugenzi pamoja na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi kwa kazi nzuri sana wanazofanya.

266. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa wananchi wa Jimbo la Maswa Magharibi ambao muda wote wameendelea kuniunga mkono katika kutekeleza majukumu yangu ya jimbo na kitaifa, nataka niwahakikishie kuwa nipo tayari kuendelea kuwatumikia kwa juhudi, bidii, maarifa na ujasiri mkubwa ili kuleta mabadiliko ya kimaendeleo katika jimbo letu na nchi kwa ujumla.

F. MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

267. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022, Wizara inaomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ya jumla ya shilingi **169,194,996,810.00** Kati ya fedha hizo, shilingi **47,844,949,810** kwa ajili ya Sekta ya Mifugo na shilingi **121,350,047,000** kwa ajili ya Sekta ya Uvuvi. Mchanganuo wa fedha zinazoombwa kwa kila Fungu ni kama ifuatavyo: -

Fungu 99: Sekta ya Mifugo

268. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaomba kutumia jumla ya shilingi **47,844,949,810** kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Sekta ya Mifugo. Kati ya fedha hizo, shilingi **30,973,208,810** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **16,871,741,000** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo**.** Mgawanyo wake ni kama ifuatavyo:-

(i) Fedha za Matumizi ya Kawaida shilingi 30,973,208,810

- Mishahara shilingi **19,269,097,810**
- **Matumizi Mengineyo (OC) shilingi 11,704,111,000**

(ii) Fedha za Matumizi ya Maendeleo shilingi16,871,741,000

- Fedha za Ndani, shilingi **16,871,741,000;** na
- Fedha za Nje shilingi - **Hakuna.**

Fungu 64: Sekta ya Uvuvi

269. ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2021/2022 Wizara inaomba jumla ya shilingi **121,350,047,000** kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Sekta ya Uvuvi. Kati ya fedha hizo, **shilingi 22,205,681,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **99,144,366,000** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Mchanganuo wake ni kama ifuatavyo:-

(i) Fedha za Matumizi ya Kawaida ni shilingi 22,205,681,000.

- Mishahara ni Shilingi **11,575,270,000**; na
- Matumizi Mengineyo(OC) ni **Shilingi 10,630,411,000**

(ii) Fedha za Matumizi ya Maendeleo shilingi 99,144,366,000

- Fedha za Ndani: shilingi **62,550,000,000;** na
- Fedha za Nje : shilingi **36,594,366,000**

270. ***Mheshimiwa Spika*****,** naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara: www.mifugouvuvi.go.tz

271. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Ahsante sana hoja imetolewa na imeungwa mkono, tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na uvuvi kwa kuwasilisha hotuba yako kwa umahiri mkubwa na tumeisikiliza mwanzo mwisho. Tunachotakiwa Waheshimiwa Wabunge sasa ni kuipokea hotuba hii na kujadili mawasilisho haya ya mapendekezo ya Wizara na Mifugo na Uvuvi kuhusu mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Sasa tunaingia kwenye *phase* ya uchangiaji na ni dakika kumi kumi.

Aah Mwenyekiti wa Kamati nilishakusahau sijui umekaa upande gani Mwenyekiti, anakuja Mwenyekiti mwenyewe wa Kamati basi baada ya mwenyekiti wa Kamati utatufungulia Mheshimiwa Charles Mwijage na Mheshimiwa Olelekaita atafuatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, karibu.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMDU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI: Mheshimiwa Spika, naomba taarifa pamoja na uvuvi yote ingie hansard.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) na Kifungu cha 6(7) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, taarifa inayowasilishwa inajumuisha mafungu mawili ambayo ni: Fungu 64- Sekta ya Uvuvi na Fungu 99 –Sekta ya Mifugo. Taarifa hii inafafanua mambo matano kama yalivyoainishwa kwenye taarifa ya Kamati ukurasa wa Pili.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Ushauri wa Kamati, wakati wa kuchambua Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Kamati ilitoa maoni na ushauri kwenye maeneo manne kama yalivyoainishwa kwenye Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, napenda kulialifu Bunge lako Tukufu kuwa, baadhi ya ushauri uliotolewa na Kamati umefanyiwa kazi. Hata hivyo, kasi ya utekelezaji imekua sio ya kuridhisha, hali inayopelekea sekta za Uvuvi na Mifugo kuwa na tija ndogo na kutoweza kuchangia kikamilifu katika Pato la Taifa kwa Maendeleo ya Uchumi na kipato cha wavuvi na wafugaji. Kamati inasisitiza Serikali ifanyie kazi ushauri ambao haujatekelezwa kulingana na maoni yaliyotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi uliofanywa na Kamati katika Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2020/2021 ulijikita katika kulinganisha kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge, kiasi cha fedha kilichopokelewa na kutumika hadi mwezi Aprili, 2021 na eneo la ukusanywaji maduhuli kwa kulinganisha makadirio yaliyowekwa na kiasi kilichokusanywa hadi Aprili, 2021.

Mheshimiwa Spika, Kiasi cha Fedha kilichoidhinishwa na kutolewa, Sekta ya Mifugo Fungu 99 na hapa nitaongelea fedha za maendeleo kwa fedha za maendeleo, kwa fedha za maendeleo hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2021, kiasi cha shilingi 6,902,623,129.68 sawa na asilimia 67 kilipokelewa na kutumika.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Uvuvi Fungu 64 nitaongelea kwa upande wa fedha za maendeleo, fecha

za maendeleo, hadi kufikia Mwezi April, 2021, jumla ya Shilingi 4,099,761,925.27 zilitolewa kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ambayo ni sawa na asilimia 31.4. Kati ya hizo shilingi 1,055,829,927.16 ni fedha za ndani na Shilingi 3,043,931,998.11 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitaka kujua sababu zilizopelekea utolewaji wa fedha kidogo za maendeleo kamati ilifahamishwa kuwa ni kutokana na mfumo wa manunuzi unaowataka Wakandarasi kutumia fedha zao katika kutekeleza miradi na baadaye kulipwa baada ya kuwasilisha hati ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara ya Mifugo kupitia Sekta ya Mifugo ilitarajia kukusanya kiasi cha shilingi 50,000,000,000:00. Hadi kufikia mwezi Mei, 2021 kiasi cha shilingi 32,779,275,605.06 kilikuwa kimekusanywa sawa na asilimia 66 ya lengo la makusanyo. Aidha, Sekta ya Uvuvi, ilitarajia kukusanya kiasi cha shilingi 33,000,000,000:00, hadi kufikia mwezi April, 2021 kiasi cha Shilingi 18,534,461,827.62 sawa na asilimia 56.2 ya lengo zilikuwa zimekusanywa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa sababu kubwa zilizopelekea ukusanyaji wa maduhuli kushuka ni pamoja na mlipuko wa ugonjwa wa *Covid 19* ambao umeathiri soko la mazao ya uvuvi na mifugo katika nchi za Ulaya.

Mheshimiwa Spika, Maoni na tathmnini kuhusu Mwenendo wa Utoaji Fedha za Miradi ya Maendeleo na Makusanyo ya Maduhuli. uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini kwamba; Kwa miaka mitatu mfululizo, Fedha za Miradi ya Maendeleo zinazoidhinishwa na Bunge hazitolewi kama zilivyoidhinishwa na hivyo kuchangia kutofikiwa kwa malengo yaliyopangwa; Sekta za Uvuvi na Mifugo kwa pamoja zilitengewa kiasi kidogo cha bajeti ya shilingi 23,400,500,865:25, kwa ajili ya maendeleo. Kati ya fedha hizo zilizotengwa, kiasi kilichotolewa ni shilingi 11,428,943,209:81, sawa na asilimia 49.

Mheshimiwa Spika, Kamati imesikitishwa zaidi na kiasi kidogo cha Fedha za Miradi ya Maendeleo zilizotolewa katika Sekta ya Uvuvi ambazo ni shilingi 4,099,761,925.27 sawa na asilimia 31.4 ya kiasi cha shilingi 13,059,214,000:00 zilizotengwa. Kamati ina maoni kuwa, bado Serikali haijafanya uwekezaji wa kutosha ili kuifanya sekta hii kuwa chanzo cha uhakika cha mapato ya Serikali; Pamoja na kutengewa bajeti ndogo, bado fedha inayotolewa ni kidogo. Hata hivyo sekta hizi zimeweza kukusanya kiasi cha shilingi 51,313,737,432:68 ambazo ni takriban mara tano ya fedha za maendeleo zilizotolewa katika kipindi husika.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini pia kuwa, Makusanyo ya Maduhuli kwa Sekta za Uvuvi na Mifugo katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2020/2021 yanaashiria kuwepo fursa kubwa za kuweza kuimarisha uzalishaji na kuinua pato la wavuvi na wafugaji na hivyo kuchochea sekta zingine; Tathmini ya Kamati imebaini kwamba uwekezaji wa kutosha katika sekta hizi una tija ya moja kwa moja katika kuimarisha uzalishaji. Hivyo Kamati inatoa rai kwa Serikali kutambua fursa zilizopo katika sekta ya Uvuvi na Mifugo na kuzitumia kikamilifu ili kuimarisha uzalishaji na kukuza uchumi wa wavuvi, wafugaji na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka 2020/2021 kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (1) inayoitaka Kamati kufanya ukaguzi wa Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Kamati ilipanga kukagua Mradi wa Ukuzaji Viumbe maji katika Kituo cha Kingolwira Morogoro; Mradi wa kuzalisha chanjo za Mifugo Kibaha; na Ranchi ya Taifa Ruvu.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Kamati ilitembelea na kukagua Mradi wa Kuendeleza Ukuzaji Viumbe kwenye maji katika Kituo cha Kinguruwira Morogoro ambacho kina jukumu la kutoa huduma za ugani kwenye ukuzaji viumbe maji na kuzalisha vifaranga na samaki wazazi kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa samaki.

Mheshimiwa Spika, katika ziara hiyo, Kamati irilidhika na maboresho yaliyofanywa yenye lengo la kuongeza uzalishaji wa vifaranga bora wa samaki kwa ajili ya kuuza na kutoa mafunzo kwa wafugaji wa samaki. Kamati inapongeza maboresho yaliyofanyika kwani ni hatua muhimu katika kuimarisha ukuzaji samaki kwenye maji ikiwepo mabwawa na vizimba.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, Kamati ilibaini Kituo cha Ukuzaji Viumbe Maji kinakabiliwa na changamoto mbalimbali kama zilivyoorodheshwa kwenye taarifa ya Kamati. Kamati ina maoni kuwa ufumbuzi wa changamoto hizi utatuliwa kwa kuongeza bajeti kwa ajili ya kuimarisha ufanisi kwenye ukuzaji viumbe maji.

Mheshimiwa Spika, maoni ya jumla kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2020/ 2021. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ulikabiliwa na changamoto mbalimbali wakati wa utekelezaji wake. Changamoto hizo ni pamoja na:-

(i) Upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kwa Sekta ya Mifugo na Uvuvi;

(ii) Uhaba wa Maafisa Ugani wa Uvuvi na Mifugo ikilingalishwa na mahitaji ya wataalam hao katika halmashari;

(iii) Kutopatikana kwa mikopo yenye masharti nafuu kwa wavuvi na wafugaji ikilinganishwa na mahitaji yao;

(iv) Kukosekana kwa bandari ya uvuvi na hivyo kupoteza fedha ambazo zingepatikana kutokana na meli zinazovua katika bahari kuu;

(v) Upotevu wa mazao ya uvuvi baada ya kuvunwa; na

(vi) Uwekezaji mdogo katika uvuvi wa bahari kuu na usindikaji wa mazao ya uvuvi kunaathiri mchango wa sekta katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, mpango wa bajeti ya mwaka 2021/2022 wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, imeandaliwa kwa kuzingatia masuala kumi 11 kama yalivyoainishwa kwenye taarifa ya Kamati ikiwa ni pamoja na Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa mwaka 2021/2022 na kuzingatia mwongozo wa utayarishaji bajeti. Kamati ilipitia Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2021/2022 na kutathimini endapo mpango huo umezingatiwa kwenye uandaaji wa bajeti inayoombwa.

Mheshimiwa Spika, dira na dhima ya mpango wa bajeti ya Wizara na Mifugo na Uvuvi unaakisiwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano wenye maeneo makuu matano ya vipambele. Katika eneo la kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma linajumuisha miradi ya viwanda inayolenga kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi, pamoja na kuzalisha bidhaa zitakazotumia malighafi na rasilimali zinazopatikana nchini.

Mheshimiwa Spika, vilevile Kamati imechambua bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kulinganisha na vipaumbele na kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ambayo lengo lake kuu ni kuiwezesha Tanzania kuwa na hadhi ya nchi yenye kipato cha kati na kuondokana na umaskini uliokithiri ifikapo 2025. Kamati imebaini kasi ndogo na isiyoridhisha na isiyowiana na Sera za Uvuvi na Mifugo hasa ikizingatiwa kuwa inatazamiwa ifikapo mwaka 2025 nchi yetu itakuwa na viwanda vya kisasa zaidi ambavyo vitatumia malighafi zinazopatikana ndani na zinazotokana na mazao ya kilimo mifugo na uvuvi na hivyo kuondoa umaskini kwa kuongeza ajira. Viwanda hivi vitaongeza thamani ya mazao na masoko ya mifugo na uvuvi yanayozalishwa hapa nchi.

Mhehimiwa spika, umuhimu wa sekta ya uvuvi. Nchi yetu ina fursa nyingi za kuendeleza uchumi kupitia rasilimali

zilizo katika bahari, maziwa, mito na mabwawa endapo Serikali itahakikisha shughuli za uvuvi nchini zinaboreshwa. Pamoja na fursa zilizopo, takwimu zinaonesha kuwa mchango wa sekta ya uvuvi kwenye pato la Taifa ni kidogo ukilinganisha na fursa zilizopo ambapo ni wastani wa asilimia 1.7 kwa mwaka. Aidha, sekta hii imekuwa ikikua kwa wastani wa asilimia 1.5 kwa mwaka. Vilevile sekta ya uvuvi inatoa ajira kwa Watanzania takribani milioni 4.5 na inachangia fedha za kigeni, kipato, chakula na lishe.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa sekta ya mifugo. Sekta hii ni miongoni mwa sekta muhimu katika ukuaji wa uchumi. Kutokana na umuhimu wa sekta hii ipo haja kwa Serikali kuimarisha ufugaji wa kisasa na kuchakata bidhaa za mifugo kwa ajili ya mahitaji ya ndani ikiwepo malighafi ya viwanda, lishe bora na usafirishaji nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, ili sekta ya mifugo ilete tija inayokusudiwa, Serikali haina budi kutekeleza mipango mikakati ya kuwezesha ufugaji wa kisasa na wenye tija. Vilevile sekta iongeze mkazo zaidi katika kushughulikia migogoro ya wafugaji na watumiaji wengine kwa ardhi hususani wakulima na maeneo ya hifadhi.

Mheshimiwa Spika, makadirio na mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Kwa ujumla kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Fungu 99 na 64 inaomba fedha kama ilivyoainishwa na Wizara kutoka kwa mtoa hoja. Aidha, Wizara inatarajia kukusanya maduhuli kiasi cha shilingi milioni 88 kutokana na vyanzo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Fungu 64 - Sekta ya Uvuvi. Katika mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara kupitia sekta ya uvuvi inaomba kuidhinishiwa fedha kama alivyosema mtoa hoja. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 22.2 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo shilingi bilioni 10.6 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 11.5 ni kwa ajili ya mishahara. Aidha, kiasi cha shilingi bilioni 99.1 zinazoombwa

ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi 62.5 ni fedha za ndani na shilingi 36.5 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, makusanyo ya madhuhuli kwa Sekta ya Uvuvi kwa mwaka 2021/2022. Sekta ya Uvuvi itakusanya jumla ya shilingi bilioni 33 zitakazopatikana kutokana na leseni na kusafirisha samaki na mazao yake kwa upande wa uvuvi, leseni za uingizaji mazao ya uvuvi, ushuru wa mrahaba, tozo ya maabara na faini zitokanazo na makosa mbalimbali ya ukiukwaji wa sheria za uvuvi.

Mheshimiwa Spika, Fungu 99. Katika mwaka wa fedha 2021/2022, Sekta ya Mifugo inaomba kuidhinishiwa fedha kama mtoa hoja alivyosema. Kati ya fedha hizi shilingi bilioni 30.9 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo shilingi 19.2 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 11.7 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Sekta ya Mifugo inaomba kuidhinishiwa fedha za ndani Sh.16,771,741,000 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, makusanyo ya maduhuli kwa Sekta ya Mifugo. Kwa upande wa maduhuli sekta hii inatarajiwa kukusanya shilingi bilioni 50 zitakazotokana na vyanzo mbalimbali vya mapato kama vilivyoonyeshwa kwenye hotuba ya mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, fedha zinazoombwa zimepanga kuteleza malengo na vipaumbele katika bajeti ya Wizara kama ilivyoelezwa na mtoa hoja katika hotuba yake ambayo imeeleza malengo na mikakati ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, tathimini ya malengo kwa bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022. Kamati imepitia, kuchambua na kutathimini malengo yaliyoainishwa katika mpango wa bajeti wa mwaka 2021/2022 na kuridhishwa nayo. Hata hivyo, changamoto kubwa imekuwa ni kasi ndogo ya utekelezaji wa vipaumbele vinavyopangwa kutokana na bajeti ndogo inayotengwa na kutolewa. Kufuatia tathmini hiyo, Kamati

inaishauri Serikali kupanga bajeti halisi inayowiana na malengo na vipaumbele vilivyoainishwa na Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na tathmini hiyo, uchambuzi wa Kamati umebaini mambo ya msingi yafuatayo:-

(i) Makadirio ya bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2021/22 imeongezeka kwa asilimia 57 ikilinganishwa na bajeti inayomalizika ya mwaka wa fedha 2020/2021;

(ii) Hakuna ongezeko kwa makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi;

(iii) Kwa upande wa bajeti ya miradi ya maendeleo kuna ongezeko la asilimia 80 ya fedha inayoombwa. Kamati inaipongeza Serikali kwa ongezeko hili. Hata hivyo, Kamati ina maoni kuwa pamoja na ongezeko hili bajeti asilimia 80 bado kiasi hiki ni kidogo na hakikidhi mahitaji ya kuwezesha mabadiliko ya kweli katika sekta hizo.

Mheshimiwa Spika, maoni na mapendekezo ya Kamati. Baada ya Kamati kufanya uchumbuzi katika maeneo mbalimbali ya majukumu ya Wizara ikiwa ni pamoja na maombi ya fedha kwa bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022, naomba kuwasilisha maoni na mapendekezo yafuatayo:-

(i) Kukamilisha maboresho ya sera na sheria za uvuvi na mifugo. Kamati imebaini kuwepo malalamiko ya wadau mbalimbali wa Sekta ya Mifugo na Uvuvi ikijumuisha wafugaji na wavuvi wenyewe, wafanyabiashara wa samaki, mawakala wa biashara na uvuvi na wenye viwanda vya kuchakata samaki mazao ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, msingi wa malalamiko yaliyopo ni kukosekana mazingira bora na yenye tija katika shughuli za biashara ya mifugo na uvuvi kutokana na sera, sheria na kanuni zinazosimamia sekta hizi kutokuwa rafiki na baadhi kupitwa na wakati. Serikali imeanza kuchukua hatua

mbalimbali kwa lengo la kuboresha sera, sheria na kanuni zinazosimamia Sekta za Mifugo na Uvuvi ili kuboresha mifumo ya uendeshaji biashara katika mnyororo wa thamani wa mazao ya mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Kamati ina maoni kuwa zoezi la kupitia upya sera, sheria na kanuni kwa ajili ya kufanya marekebisho ili kuakisi mahitaji ya kusimamia mazao ya mifugo na uvuvi imechukua muda mrefu na hivyo kukwamisha ukuaji wa sekta. Hata hivyo, tunashukuru Mheshimiwa Waziri kusema kuwa liko kwenye hatua linakwenda vizuri. Kufuatia hali hii, Kamati inaishauri Wizara kuharakisha mchakato huo kama Waziri alivyosema, kuhakikisha unakamilishwa mapema iwezekanavyo ili maboresho yatakayofanyika yaweze kujenga mazingira wenzeshi na kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza kikamilifu.

(ii) Kuimarisha bajeti inayotengwa na kutolewa kwa ajili ya Sekta ya Mifugo na Uvuvi. Sekta hii ni muhimu kwa uchumi na maendeleo ya nchi na Watanzania kwa ujumla. Sekta ya Mifugo inaweza kuchangia kwa kiwango kikubwa zaidi katika uchumi wa nchi kama uwekezaji utafanyika inavyotakiwa. Sekta hii inaajiri takribani asilimia 50 ya Watanzania na inachangia asilimia 7.9 kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonyesha Tanzania ina ng'ombe takribani milioni 33 idadi ambayo inaifanya Tanzania kuwa nchi ya tatu kuwa na ng'ombe wengi Barani Afrika baada ya Ethiopia na Sudan. Pamoja na wingi huu wa mifugo bado sekta ya mifugo haijatumika kikamilifu katika kuinua pato la Taifa na kumsaidia mfugaji kuondokana na umaskini kutokana na uwekezaji mdogo unaofanywa na Serikali. Kwa Mfano, katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2021/ 2022 Sekta ya Mifugo imetengewa Sh.16,871,741,000 tu kwa ajili ya kutekeleza miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati haijaridhishwa na kiasi kidogo cha bajeti kilichotengwa kwa ajili ya maendeleo ya mifugo. Hivyo inaishauri Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/

2023 kutenga fedha zinazoshabihiana na wingi wa rasilimali za mifugo zilizopo nchini ili kuweza kunufaisha wafugaji na kukuza uchumi wa Taifa. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya sekta binafsi kuwekeza kikamilifu kwenye sekta ya mifugo. *(Makofi)*

(iii) Uwekezaji katika uvuvi wa bahari kuu. Uchumi wa Bluu ambao unajulikana kama uchumi wa bahari unafungamanisha kwa pamoja sekta za uvuvi, ufugaji samaki, ujenzi wa viwanda vya samaki na matumizi bora ya rasilimali mbalimbali za bahari. Uchumi wa Bluu haukamiliki bila ya kuwepo kwa bandari za uvuvi na meli za uvuvi.

Mheshimiwa Spika, kukosekana kwa bandari ya uvuvi katika nchi yetu kunalikosesha taifa fursa ya kunufaika na uvuvi wa bahari kuu. Licha ya kuwa Tanzania eneo la uchumi wa bahari kuu lina kina kikubwa na samaki wengi lakini hawawanufaishi Watanzania kwa kuwa meli za nchi za kigeni hufika na kuvua samaki hao ambao kwa mujibu wa mikataba ya kimataifa halina mipaka.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu huo, kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Serikali imetenga fedha za ndani kiasi cha Sh.50,000,000,000 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa bandari ya uvuvi kama Waziri alivyosema. Kamati inapongeza Serikali kwa hatua hii. Hata hivyo, ni rai ya Kamati kuona fedha hizo zinatolewa kwa wakati ili ujenzi wa bandari ya uvuvi uweze kuanza.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 10.4 kwa ajili ya kununua meli nne za uvuvi lakini kwa kuanza na meli mbili katika bahari kuu. Fedha za ununuzi wa meli hizo zitatokana na mkopo wa masharti nafuu kutoka kwa Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo *(IFAD).*

Mheshimiwa Spika, Kamati ina taarifa kuwa taratibu zote za mkopo huo zimeshakamilika. Hatua inayofuata ni taratibu za ndani za kukamilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili fedha hizo zitoke na taratibu za manunuzi zifanyike

kwa ajili ya ununuzi wa meli hizo. Kwa kuwa suala la ununuzi wa meli za uvuvi ni la muda mrefu, Kamati inashauri Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kukamilisha mapema iwezekanavyo taratibu zinazohusika ili fedha za mkopo huo zitoke kwa ajili ya ununuzi wa meli hizo.

Mheshimiwa Spika, aidha, ukosefu wa bandari ya uvuvi huchangia kulikosesha taifa fedha za kigeni ambazo zingepatikana kutokana na mauzo ya samaki wengi wanaopatikana kwenye bahari kuu. Pia kunapelekea kuwakosesha ajira vijana.

Mheshimiwa Spika, kufuatia fursa nyingi zilizopo kwenye uvuvi wa bahari kuu, Kamati inaishauri Serikali kuona umuhimu wa kuchukua hatua mahsusi kwa kuweka mazingira wezeshi na kuwekeza katika uvuvi wa bahari kuu kwa kukamilisha mipango iliyopo na kuanza ujenzi wa bandari ya uvuvi sambamba na ununuzi wa meli hizo kwa ajili kuvua katika eneo la Bahari Kuu.

(iv) Kuimarisha usimamizi wa nyanda za malisho nchini. Mabadiliko ya tabianchi kama yanavyojidhihirisha mahali pengi duniani yana athari kwa mazingira na pia yamesababisha uhaba wa malisho ya mifugo hata kupelekea upungufu katika uzalishaji wa mazao ya mifugo. Ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kuimarisha sekta ya mifugo na mazao yake, Serikali ilianzisha mashamba ya kuzalisha mbegu za malisho ya mifugo kwa madhumuni ya kuzalisha mbegu bora.

Mheshimiwa Spika, pamoja na dhamira hii njema, bado mashamba ya malisho yanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo uhaba wa maji kwa ajili ya kunyweshea mashamba ya malisho. Ili mashamba ya malisho yalete tija, ni lazima yaendelezwe kwa kutumia kilimo cha umwagiliaji badala ya kutegemea mvua zilizoathiriwa na ukame kutokana na mabadiliko ya tabianchi. Kamati inaishauri Wizara kutekeleza yafuatayo: -

· Kuweka mazingira wezeshi na kuhamasisha sekta binafsi kuanzisha mashamba ya malisho;

· Kusambaza mbegu bora za malisho;

· Kueneza teknolojia za kujenga na kuendesha miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya malisho; pamoja na

· Kuweka na kuendeleza utaratibu wa kuwa na mashamba darasa ya nyanda za malisho katika jamii za wafugaji ili kuongeza tija na ubora wa mazao ya mifugo.

(v) Kuimarisha usimamizi wa Kampuni ya Ranchi za Taifa. Kampuni ya Ranchi za Taifa ilianzishwa kwa lengo la kuendeleza na kueneza ufugaji bora kwa kutumia mbinu za kisasa kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi. Takwimu zinaonyesha ranchi zilizopo zina uwezo wa kuhudumia na kuendeleza ng'ombe kati ya 80,000 - 90,000. Hata hivyo, ranchi zote zilizopo nchini, kwa takwimu za mwaka 2019/2020 zinakadiriwa kuwa na ng'ombe 12,681 tu ambayo ni sawa na asilimia 15 ya uwezo wake.

SPIKA: Mwenyekiti muda wako umeisha, naomba uhitimishe.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI: Mheshimiwa Spika, hitimisho; napenda kukushukuru wewe mwenyewe, Naibu Spika, Waziri Mifugo na Naibu wake, Makatibu Wakuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kutupatia ushirikiano kwenye Kamati hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuwatambua na kuwashukuru wanakamati kwa jinsi walivyojitoa katika kuchangia shughuli mbalimbali za Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kumshukuru pia wasaidizi wa Kamati na Mkurugenzi wa Kamati, Ndugu Athuman Pamoja na Ndugu Nenelwa...

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI: Nampa hongera tena kwa kuteuliwa kuwa Katibu wa Bunge. Nawapongeza Ndugu Virgil na Ndugu Rachel Nyega Makatibu wangu na Ndugu Kizingiti msaidizi kwa kuihudumia Kamati hii vizuri.

SPIKA: Ahsante Mwenyekiti.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI: Mheshimiwa Spika, nakushuru, naomba kuwasilisha na naomba ijadiliwe. *(Makofi)*

TAARIFA YA MAONI YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

SEHEMU YA KWANZA

1.0 MAJUKUMU YA KAMATI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) na Kifungu cha 6 (7) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, vilevile Kanuni ya 117 (1) inataka Kamati kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha unaoisha 2020/ 2021.

Mheshimiwa Spika, naomba nitangulie kusema Taarifa ninayoiwasilisha inajumuisha mafungu mawili (2) ambayo ni: -
Fungu 64- Sekta ya Uvuvi na Fungu 99 –Sekta ya Mifugo. Taarifa ninayoiwasilisha inafafanua mambo matano (5) kama yalivyoainishwa kwenye taarifa ya Kamati ukurasa wa Pili.

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI WA MASWALA MBALIMBALI

2.1 Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuchambua Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Kamati ilitoa maoni na ushauri kwenye maeneo manne kama yalivyoainishwa kwenye Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, napenda kulialifu Bunge lako Tukufu kuwa**,** baadhi ya ushauri uliotolewa na Kamati umefanyiwa kazi. Hata hivyo, kasi ya utekelezaji imekua sio ya kuridhisha, hali inayopelekea sekta za Uvuvi na Mifugo kuwa na tija ndogo na kutoweza kuchangia kikamilifu katika Pato la Taifa kwa Maendeleo ya Uchumi na kipato cha wavuvi na wafugaji. Kamati inasisitiza Serikali ifanyie kazi ushauri ambao haujatekelezwa kulingana na maoni yaliyotolewa na Kamati.

2.2 UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/ 2021

Mheshimiwa Spika, uchambuzi uliofanywa na Kamati katika Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2020/2021 ulijikita katika kulinganisha kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge, kiasi cha fedha kilichopokelewa na kutumika hadi mwezi Aprili, 2021 na eneo la ukusanywaji maduhuli kwa kulinganisha makadirio yaliyowekwa na kiasi kilichokusanywa hadi Aprili, 2021.

2.2.1 Kiasi cha Fedha kilichoidhinishwa na kutolewa

a) Sekta ya Mifugo - Fungu 99

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Sekta ya Mifugo iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 38,929,091,304:00.** Kati ya Fedha hizo, **Shilingi 28,585,804,439:00** ni fedha za Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 10,341,286,865.25** ni fedha kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kwa upande wa Fedha ya Matumizi ya Kawaida, hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2021, jumla ya **Shilingi 23,524,701,194:00** zilikuwa zimetolewa, ambazo ni sawa na **asilimia 82** ya bajeti iliyotarajiwa kwa miezi kumi na miwili. Kati ya hizo, **Shilingi 12,220,937,012:00** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara (PE) na **Shilingi 9,737,176,262.99** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

Aidha, kwa upande wa Fedha za Miradi ya Maendeleo, hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2021 kiasi cha **Shilingi 6,902,623,129.68** sawa na asilimia **67** kilipokelewa na kutumika. Hii ni sawa na **asilimia 85.2** kwa kipindi cha miezi kumi (10).

b) Sekta ya Uvuvi - Fungu 64

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2020/ 2021 Sekta ya Uvuvi iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 34,721,321,000:00.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 21,662,107,000:00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, ambapo kati ya fedha za Kawaida **Shilingi 9,630,411,000:00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 12,031,696,000:00** ni kwa ajili ya Mishahara. Aidha, **Shilingi 13,059,214,000:00** ziliidhinishwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 5,976,856,000:00** ni Fedha za Ndani na **Shilingi 7,082,358,000:00** ni Fedha za Nje**.**

Hadi kufikia 30 Aprili, 2021 fedha za Matumizi ya Kawaida, 2021 kiasi cha **Shilingi 17,074,256,595.63**, sawa na asilimia **78.82** zilikuwa zimetolewa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 8,332,914,095.63** ni kwa ajili ya mishahara ya Watumishi (PE) na **Shilingi 8,741,342,500** ni fedha za Matumizi Mengineyo. Kwa

upande wa fedha za maendeleo, hadi kufikia Mwezi April, 2021, jumla ya **Shilingi 4,099,761,925.27** zilitolewa kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ambayo ni sawa na **asilimia 31.4.** Kati ya hizo shilingi **1,055,829,927.16** ni fedha za ndani na **Shilingi 3,043,931,998.11** ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitaka kujua sababu zilizopelekea utolewaji wa fedha kidogo za maendeleo ilifahamishwa kuwa ni kutokana na mfumo wa manunuzi unaowataka Wakandarasi kutumia fedha zao katika kutekeleza miradi na baadae kulipwa baada ya kuwasilisha hati ya utekelezaji.

c) Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2020/ 2021

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mifugo kupitia Sekta ya Mifugo ilitarajia kukusanya kiasi cha **Shilingi 50,000,000,000:00**. Hadi kufikia mwezi Mei, 2021 kiasi cha **Shilingi 32,779,275,605:06** kilikuwa kimekusanywa sawa na **asilimia 66** ya lengo la makusanyo. Aidha, Sekta ya Uvuvi , ilitarajia kukusanya kiasi cha **Shilingi 33,000,000,000:00,** hadi kufikia mwezi April, 2021 kiasi cha **Shilingi 18,534,461,827.62** sawa na **asilimia 56.2** ya lengo zilikuwa zimekusanywa**.**

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa sababu kubwa zilizopelekea ukusanyaji wa maduhuli kushuka ni pamoja na mlipuko wa ugonjwa wa *Covid – 19* ambao umeathiri soko la mazao ya uvuvi na mifugo katika nchi za Ulaya.

d) Maoni na tathmnini kuhusu Mwenendo wa Utoaji Fedha za Miradi ya Maendeleo na Makusanyo ya Maduhuli.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini kwamba: -

i) Kwa miaka mitatu mfululizo, Fedha za Miradi ya Maendeleo zinazoidhinishwa na Bunge hazitolewi kama zilivyoidhinishwa na hivyo kuchangia kutofikiwa kwa malengo yaliyopangwa.

ii) Sekta za Uvuvi na Mifugo kwa pamoja zilitengewa kiasi kidogo cha bajeti ya **Shilingi 23,400,500,865:25**, kwa ajili ya maendeleo. Kati ya fedha hizo zilizotengwa, kiasi kilichotolewa ni **Shilingi 11,428,943,209:81**, sawa na **asilimia 49.**

iii) Kamati imesikitishwa zaidi na kiasi kidogo cha Fedha za Miradi ya Maendeleo zilizotolewa katika Sekta ya Uvuvi ambazo ni **Shilingi 4,099,761,925:27** sawa na **asilimia 31.4** ya kiasi cha **Shilingi 13,059,214,000:00** zilizotengwa. Kamati ina maoni kuwa, bado Serikali haijafanya uwekezaji wa kutosha ili kuifanya sekta hii kuwa chanzo cha uhakika cha mapato ya Serikali.

iv) Pamoja na kutengewa bajeti ndogo, bado fedha inayotolewa ni kidogo. Hata hivyo sekta hizi zimeweza kukusanya kiasi cha **Shilingi 51,313,737,432:68** ambazo ni takriban mara tano ya fedha za maendeleo zilizotolewa katika kipindi husika.

v) Uchambuzi wa Kamati umebaini pia kuwa, Makusanyo ya Maduhuli kwa Sekta za Uvuvi na Mifugo katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2020/2021 yanaashiria kuwepo fursa kubwa za kuweza kuimarisha uzalishaji na kuinua pato la wavuvi na wafugaji na hivyo kuchochea sekta zingine.

vi) Tathimini ya Kamati imebaini kwamba uwekezaji wa kutosha katika sekta hizi una tija ya moja kwa moja katika kuimarisha uzalishaji. Hivyo Kamati inatoa rai kwa Serikali kutambua fursa zilizopo katika sekta ya Uvuvi na Mifugo na kuzitumia kikamilifu ili kuimarisha uzalishaji na kukuza uchumi wa wavuvi, wafugaji na Taifa kwa ujumla.

2.3 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA 2020/2021

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (1) inayoitaka Kamati kufanya ukaguzi wa Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Kamati ilipanga kukagua Mradi wa Ukuzaji Viumbe

maji katika Kituo cha Kingolwira Morogoro; Mradi wa kuzalisha chanjo za Mifugo - Kibaha; na Ranchi ya Taifa Ruvu. Hata hivyo, Kamati ilitembelea na kukagua Mradi wa Kuendeleza Ukuzaji Viumbe kwenye maji katika Kituo cha Kingolwira – Morogoro ambacho kina jukumu la kutoa huduma za ugani kwenye ukuzaji viumbe maji na kuzalisha vifaranga na samaki wazazi kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa samaki.

Mheshimiwa Spika, katika ziara hiyo, Kamati irilidhika na maboresho yaliyofanywa yenye lengo la kuongeza uzalishaji wa vifaranga bora wa samaki kwa ajili ya kuuza na kutoa mafunzo kwa wafugaji wa samaki. Kamati inapongeza maboresho yaliyofanyika kwani ni hatua muhimu katika kuimarisha kuimarisha ukuzaji samaki kwenye vizimba.

Pamoja na mafanikio hayo, Kamati ilibaini kituo cha ukuzaji viumbe maji kinakabiliwa na changamoto mbalimbali kama zilivyoorodheshwa kwenye taarifa ya Kamati. Kamati ina maoni kuwa, ufumbuzi wa changamoto hizo utatatuliwa kwa kuongeza bajeti kwa ajili ya kuimarisha ufanisi kwenye ukuzaji viumbe maji.

2.4 Maoni ya jumla kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka 2020/2021

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 ulikabiliwa na changamoto mbalimbali wakati wa utekelezaji wake. Changamoto hizo ni pamoja na:-

a) Upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kwa sekta za mifugo na uvuvi;

b) Uhaba wa Maafisa ugani wa uvuvi na Mifugo ikilinganishwa na mahitaji ya wataalam katika Halmashauri;

c) Kutopatikana kwa mikopo yenye masharti nafuu kwa wavuvi na wafugaji ikilinganishwa na mahitaji yao,

d) Kukosekana kwa Bandari za Uvuvi na hivyo kupoteza fedha ambazo zingepatikana kwa meli zinazovua katika Bahari kuu;

e) Upotevu wa mazao ya uvuvi baada ya kuvunwa,

f) Uwekezaji mdogo katika uvuvi wa Bahari Kuu na usindikaji wa mazao ya uvuvi kunaathiri mchango wa sekta katika Pato la Taifa;

2.5 MPANGO WA BAJETI NA UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Bajeti ya Mwaka 2021/2022 wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeandaliwa kwa kuzingatia masuala kumi na moja kama yalivyoanishwa kwenye Taarifa ya Kamati.

2.5.1 Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/2022

Pamoja na kuzingatia muongozo wa utayarishaji bajeti, Kamati ilipitia Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/2022 na kutathimini endapo Mpango huo umezingatiwa kwenye uandaaji wa Bajeti inayoombwa.

Mheshimiwa Spika, Dira na Dhima ya Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi unaakisiwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano, wenye maeneo makuu matano ya vipaumbele ambapo katika eneo **la Kuimarisha Uwezo wa Uzalishaji Viwandani na Utoaji Huduma,** inajumuisha miradi ya viwanda inayolenga kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi pamoja na kuzalisha bidhaa zitakazotumia malighafi na rasilimali zinazopatikana nchini.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Kamati imechambua Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kulinganisha na

vipaumbele na kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ambayo lengo lake kuu ni kuiwezesha Tanzania kuwa na hadhi ya nchi zenye kipato cha kati na kuondokana na umaskini uliokithiri ifikapo 2025.

Kamati imebaini kasi ndogo na isiyoridhisha, isiyowiana na Sera ya Uvuvi na Sera ya Mifugo. Hasa ikizingatiwa kuwa, inatazamiwa ifikapo Mwaka 2025, nchi yetu itakuwa na viwanda vya kisasa zaidi ambavyo vitatumia malighafi zinazopatikana ndani na zinazotokana na mazao ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi na hivyo kuondoa umasikini kwa kuongeza ajira. Viwanda hivi, vitaongeza thamani ya mazao na masoko ya mifugo na uvuvi yanayozalishwa hapa nchini.

2.5.2 Umuhimu wa Sekta ya Uvuvi

Mheshimiwa Spika, Nchi yetu ina fursa nyingi za kuendeleza uchumi kupitia rasilimali zilizo katika bahari, maziwa, mito na mabwawa endapo Serikali itahakikisha shughuli za uvuvi nchini zinaboreshwa. Pamoja na fursa zilizopo, takwimu zinaonesha kuwa:- Mchango wa Sekta ya Uvuvi kwenye Pato la Taifa ni kidogo ukilinganisha na fursa zilizopo, ambao ni wastani wa asilimia **1.7** kwa mwaka. Aidha, Sekta hii imekuwa ikikua kwa wastani wa asilimia **1.5** kwa mwaka**.** Vilevile Sekta ya Uvuvi inatoa ajira kwa watanzania takriban Milioni **4.5** na inachangia fedha za kigeni, kipato, chakula na lishe.

2.5.3 Umuhimu wa Sekta ya Mifugo

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mifugo ni miongoni mwa sekta muhimu katika ukuaji wa uchumi. Kutokana na umuhimu wa sekta hii ipo haja kwa Serikali kuimarisha ufugaji wa kisasa na kuchakata bidhaa za mifugo kwa ajili ya mahitaji ya ndani ikiwemo malighafi za viwanda, lishe bora na usafirishaji nje ya nchi.

Ili sekta ya Mifugo ilete tija inayokusudiwa, Serikali haina budi kutekeleza mipango mikakati ya kuwezesha ufugaji wa kisasa na wenye tija. Vilevile sekta iongoze mkazo

zaidi katika kushughulikiamigogoro ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi, hususan wakulima na maeneo ya hifadhi.

2.6 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 Wizara ya Mifugo na Uvuvi Fungu 99 na Fungu 64 inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 169,194,996,810**:00 Aidha, Wizara inatarajia kukusanya maduhuli kiasi cha **Shilingi 88,000,000,000:00** kutokana na vyanzo mbalimbali.

2.6.1 Fungu 64: Sekta ya Uvuvi

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/ 2022, Wizara kupitia Sekta ya Uvuvi inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi**. **121,350,047,000:00** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 22,205,681,000:00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi 10,630,411,000:00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 11,575,270,000:00** ni kwa ajili ya mishahara**.** Aidha, kiasi cha **Shilingi 99,144,366,000:00** zinaombwa ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 62,550,000,000:00** ni Fedha za ndani na **Shilingi 36,594,366,000:00** ni Fedha za Nje.

2.6.1.1 Makusanyo ya Maduhuli kwa Sekta ya Uvuvi

Kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Sekta ya Uvuvi inatarajia kukusanya jumla ya **Shilingi 33,000,000,000:00** zitakazopatikana kutokana na Leseni za kusafirisha samaki na mazao yake (*Export Licences*), Leseni za uingizaji mazao ya Uvuvi (*Import Royalty*), Ushuru wa Mrahaba (*Export Royalty*), Tozo ya Maabara, na faini zitokanazo na makosa mbalimbali ya ukiukwaji wa sheria za uvuvi.

2.6.2 Fungu 99: Sekta ya Mifugo

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/ 2022, Sekta ya Mifugo inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi**

47,844,949,810:00. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 30,973,208,810:00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi 19,269,097,810:00** ni kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 11,704,111,000:00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC). Aidha, kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 Sekta ya Mifugo inaomba kuidhinishiwa fedha za ndani **Shilingi 16,871,741,000:00** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya Maendeleo.

2.6.2.1 Makusanyo ya Maduhuli kwa Sekta ya Mifugo

Kwa upande wa Maduhuli Sekta ya Mifugo inatarajia kukusanya **Shilingi 50,000,000,000:00** zitakazotokana na vyanzo mbalimbali vya mapato kama vilivyoelezwa kwenye hotuba ya Waziri.

2.7 MALENGO YA UTEKELEZAJI NA VIPAUMBELE KWA SEKTA YA MIFUNGO NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

Mheshimiwa Spika, fedha zinazoombwa zimepangwa kutekeleza Malengo na Vipaumbele katika Bajeti ya Wizara kama yalivyoelezwa na Mtoa Hoja katika hotuba yake ambayo imeelezea malengo na mikakati ya Wizara.

2.8 TATHIMINI YA MALENGO KWA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

Mheshimiwa Spika, Kamati imepitia, kuchambua na kutathimini malengo yaliyoainishwa katika Mpango wa Bajeti ya Mwaka 2021/2022 na kuridhishwa nayo. Hata hivyo, changamoto kubwa imekuwa ni kasi ndogo ya Utekelezaji wa Vipaumbele vinavyopangwa kutokana na Bajeti ndogo inayotengwa na kutolewa. Kufuatia tahimini hiyo, Kamati inaishauri Serikali kupanga bajeti halisi inayowiana na malengo na vipaumbele vilivyoanishwa na Wizara.

Mheshimiwa Spika, pamoja na tathimini hiyo, uchambuzi wa Kamati umebaini mambo ya msingi yafuatayo: -

a) Makadirio ya Matumizi ya Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 imeongezeka kwa **asilimia 57** ikilinganishwa na Bajeti inayomalizika ya Mwaka wa Fedha 2020/2021;

b) Hakuna ongezeko kwa Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

c) Kwa upande wa Bajeti ya Miradi ya Maendeleo kuna ongezeko la **asilimia 80** ya fedha inayoombwa. Kamati inaipongeza Serikali kwa ongezeko hili. Hata hivyo, Kamati ina maoni kuwa, pamoja na ongezeko hili la Bajeti la **asilimia 80,** bado kiasi hiki ni kidogo na hakikidhi mahitaji ya kuwezesha mabadiliko ya kweli katika sekta hizi.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati kufanya uchambuzi katika maeneo mbalimbali ya majukumu ya Wizara ikiwa ni pamoja na Maombi ya Fedha kwa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2021/2022. Naomba kuwasilisha maoni na mapendekezo yafuatayo: -

3.1 KUKAMILISHA MABORESHO YA SERA NA SHERIA ZA UVUVI NA MIFUGO

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwepo malalamiko ya wadau mbalimbali wa Sekta ya Mifugo na Uvuvi, ikijumuisha Wafugaji na Wavuvi wenyewe, Wafanyabiashara wa samaki, Mawakala wa biashara ya Uvuvi na wenye Viwanda vya kuchakata samaki na mazao ya mifugo. Msingi wa malalamiko yaliyopo ni kukosekana mazingira bora na yenye tija katika shughuli za biashara ya mifugo na uvuvi kutokana na Sera, Sheria na Kanuni zinazosimamia Sekta hizi kutokuwa rafiki na baadhi kupitwa na wakati. Serikali imeanza kuchukua hatua mbalimbali kwa lengo la kuboresha Sera,

3.1 KUKAMILISHA MABORESHO YA SERA NA SHERIA ZA UVUVI NA MIFUGO

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwepo malalamiko ya wadau mbalimbali wa Sekta ya Mifugo na Uvuvi, ikijumuisha Wafugaji na Wavuvi wenyewe, Wafanyabiashara wa samaki, Mawakala wa biashara ya Uvuvi na wenye Viwanda vya kuchakata samaki na mazao ya mifugo. Msingi wa malalamiko yaliyopo ni kukosekana mazingira bora na yenye tija katika shughuli za biashara ya mifugo na uvuvi kutokana na Sera, Sheria na Kanuni zinazosimamia Sekta hizi kutokuwa rafiki na baadhi kupitwa na wakati. Serikali imeanza kuchukua hatua mbalimbali kwa lengo la kuboresha Sera, Sheria na Kanuni zinazosimamia Sekta za Mifugo na Uvuvi ili kuboresha mifumo ya uendeshaji biashara katika mnyororo wa thamani wa mazao ya mifugo na uvuvi. Hata hivyo, Kamati ina maoni kuwa zoezi la kupitia upya Sera, Sheria na Kanuni kwa ajili ya kufanya marekebisho ili kuakisi mahitaji ya usimamizi wa mazao ya mifugo na uvuvi limechukua muda mrefu na hivyo kukwamisha ukuaji wa sekta. Kufuatia hali hii, Kamati inaishauri Wizara kuharakisha mchakato huo kuhakikisha unakamilishwa mapema iwezekanavyo ili maboresho yatakayofanyika yaweze kujenga mazingira wezeshi na kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza kikamilifu.

3.2 KUIMARISHA BAJETI INAYOTENGWA NA KUTOLEWA KWA AJILI YA SEKTA YA MIFUGO NA UVUVI

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mifugo na Uvuvi ni sekta muhimu kwa uchumi na maendeleo ya nchi na Watanzania kwa ujumla.

Sekta ya Mifugo inaweza kuchangia kwa kiwango kikubwa zaidi katika uchumi wa nchi kama uwekezaji utafanyika inavyotakiwa. Sekta hii inaajiri takribani **50%** ya watanzania na inachangia **7.9%** kwenye Pato la Taifa.

Takwimu zinaonyesha Tanzania ina ng'ombe takribani **milioni 30.5** idadi ambayo inaifanya Tanzania kuwa nchi ya

tatu kuwa na ng'ombe wengi barani Afrika baada ya Ethiopia na Sudan. Pamoja na wingi huu wa mifugo bado sekta ya mifugo haijatumika kikamilifu katika kuinua Pato la Taifa na kumsaidia mfugaji kuondokana na umaskini kutokana na uwekezaji mdogo unaofanywa na Serikali. Kwa Mfano; katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2021/2022 sekta ya mifugo imetengewa **16,871,741,000** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati haijaridhishwa na kiasi kidogo cha bajeti kilichotengwa kwa ajili ya maendeleo ya Mifugo. Hivyo inaishauri Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 kutenga fedha zinazoshabihiana na wingi wa rasilimali za mifugo zilizopo nchini ili kuweza kunufaisha wafugaji na kukuza uchumi. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya sekta binafsi kuwekeza kikamilifu kwenye sekta ya mifugo.

3.3 UWEKEZAJI KATIKA UVUVI WA BAHARI KUU

Mheshimiwa Spika, Uchumi wa Bluu ambao unajulikana kama uchumi wa bahari unafungamanisha kwa pamoja sekta za uvuvi, ufugaji samaki, ujenzi wa viwanda vya samaki, na matumizi bora ya rasilimali mbali mbali za bahari. Uchumi wa Bluu haukamiliki bila ya kuwepo kwa Bandari za uvuvi na meli za uvuvi. Kukosekana kwa bandari ya uvuvi katika nchi yetu kunalikosesha taifa fursa ya kunufaika na Uvuvi wa Bahari Kuu licha ya kuwa eneo la Tanzania la uchumi wa bahari kuu lina kina kikubwa na samaki wengi ambao hawawanufaishi watanzania kwa kuwa meli za nchi za kigeni hufika na kuvua samaki hao ambao kwa mujibu wa mikataba ya kimataifa halina mipaka.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu huo, kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 Serikali imetenga fedha za ndani kiasi cha **Shilingi 50,000,000,00000** kwa ajili ya kuanza ujenzi wa bandari ya uvuvi. Kamati inapongeza Serikali kwa hatua hii, hata hivyo ni rai ya Kamati kuona fedha hizo zinatolewa kwa wakati ili utekelezaji wa ujenzi wa bandari ya uvuvi uweze kuanza. Kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022

Serikali imetenga kiasi cha S**hilingi 10,407,145,906:00** kwa ajili ya kununua meli mbili za uvuvi katika bahari kuu. Fedha ambazo zitatokana na mkopo wa masharti nafuu kutoka Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (***INTERNATIONAL FUND FOR AGRICULTURE DEVELOPMENT*** – IFAD).

Mheshimiwa Spika, Kamati ina tarifa kuwa, taratibu zote za mkopo huu zimeshakamilika, hatua inayofuata ni taratibu za ndani kukamilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili fedha hizo zitoke ili taratibu za manunuzi zifanyike kwa ajili ya kununua meli hizo. Kwa kuwa suala la un unuzi wa meli za uvuvi ni la muda mrefu, Kamati inashauri Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kukamilisha mapema iwezekaavyo taritibu zinazohusika na ofisi yake ili fedha za mkopo huo zitoke kwa ajili ya ununuzi wa meli hizo.

Aidha, ukosefu wa bandari ya uvuvi huchangia kulikosesha taifa fedha za kigeni ambazo zingepatikana kutokana na mauzo ya samaki wengi wanaopatikana kwenye bahari kuu. Lakini pia kunapelekea kuwakosesha vijana ajira.

Kufuatia fursa nyingi zilizopo kwenye uvuvi wa bahari kuu, Kamati inaishauri Serikali kuona umuhimu na kuchukua hatua mahsusi kwa kuweka mazingira wezeshi na kuwekeza katika Uvuvi wa Bahari Kuu kwa kukamilisha mipango iliyopo na kuanza ujenzi wa bandari ya uvuvi sambamba na ununuzi wa meli za uvuvi kwa ajili kuvua katika eneo la Bahari Kuu.

3.4 KUIMARISHA USIMAMIZI WA NYANDA ZA MALISHO NCHINI

Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya tabianchi kama yanavyojidhihirisha mahali pengi duniani yana athari kwa mazingira na pia yamesababisha uhaba wa malisho ya mifugo hata kupelekea upungufu katika uzalishaji wa mazao ya mifugo. Ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kuimarisha sekta ya Mifugo na mazao yake, Serikali ilianzisha mashamba ya kuzalisha mbegu za malisho ya mifugo kwa madhumuni ya kuzalisha mbegu bora. Pamoja na dhamira

hii njema, bado mashamba ya malisho yanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo uhaba wa maji kwa ajili ya kunyweshea mashamba ya malisho. Ili mashamba ya malisho yalete tija ni lazima yaendelezwe kwa kutumia kilimo cha umwagiliaji badala ya kutegemea mvua zilizoathiriwa na ukame kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

Kamati inaishauri Wizara kutekeleza yafuatayo: -

(i) Kuweka mazingira wezeshi na kuhamasisha sekta binafsi kuanzisha mashamba ya malisho;

(ii) Kusambaza mbegu bora za malisho;

(iii) Kueneza teknolojia za kujenga na kuendesha miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya malisho; pamoja na

(iv) Kuweka na kuendeleza utaratibu wa kuwa na mashamba darasa ya nyanda za malisho katika jamii za wafugaji ili kuongeza tija na ubora wa mazao ya mifugo.

3.5 KUIMARISHA USIMAMIZI WA KAMPUNI YA RANCHI ZA TAIFA

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Ranchi za Taifa ilianzishwa kwa lengo la kuendeleza na kueneza ufugaji bora kwa kutumia mbinu za kisasa kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi. Takwimu zinaonyesha ranchi zilizopo zina uwezo wa kuhudumia na kuendeleza ng‘ombe kati ya **80,000 - 90,000**. Hata hivyo, ranchi zote zilizopo nchini, kwa takwimu za mwaka 2019/2020 zinakadiriwa kuwa na ng‘ombe **12,681 tu,** ambayo ni sawa na **asilimia 15** ya uwezo wake. Idadi hii ni ndogo ikilinganishwa na uwezo wa ranchi zilizopo. Hali hii inadhihirisha kuwa hakuna uwekezaji wa kutosha unaofanywa kutokana na ufinyu wa bajeti inayotengwa. Ili kuiwezesha NARCO kutekeleza majukumu yake kikamilifu, Kamati inaishauri Serikali: -

a) Kuimarisha kampuni ya Rachi za Tifa kwa kuipatia fedha za kutosha ili iweze kutumia rasilimali ya fursa zilizopo kikamilifu;

b) Serikali ifanye tathimini ili kubaini kama miongozo na namna uendeshaji wa Ranchi za Taifa unavyofanyika una tija inayokusudiwa katika mazingira ya sasa;

c) NARCO ichukue hatua za makusudi kwa lushughulikia malalamiko yaliopo kuhusu vitalu kutolewa bila kuzingatia wafungaji waishio pembezoni mwa Ranchi za Taifa. Aidha, Kamati inashauri mikataba inayotolewa iwe ya muda mrefu ili kuwezesha wamiliki wa vitalu kuviendeleza kwa kuweka miundombinu muhimu ya ufugaji wa kisasa.

4.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, (Mb), na Naibu Waziri Mhe. Abdallah Hamis Ulega (Mb), Katibu Mkuu – Uvuvi Dkt. Rashid Tamatamah na Katibu Mkuu - Mifugo Prof. Elisante Ole Gabriel pamoja na Wataalamu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa ushirikiano walioipa Kamati wakati ikichambua na kujadili Bajeti ya Wizara hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao waliyoitoa wakati wa kupitia na kuchambua bajeti ya Wizara pamoja na kuandaa taarifa hii hadi kukamilika kwake. Naomba majina yao yaingie kwenye kumb ukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard) kama yalivyo kwenye Tarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Nenelwa Mwihambi, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati Ndugu Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi sehemu ya Kamati za Fedha Ndugu Michael Chikokoto pamoja na Sekreterieti ya Kamati ambao ni Ndugu Virgil Mtui na Ndugu Rachel Nyega pamoja na msaizizi wa Kamati Ndugu Waziri Kizingiti kwa kuihudumia Kamati pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naliomba sasa Bunge lako lipokee, lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja iliyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita na naomba kuwasilisha.

Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, (Mb)
MWENYEKITI,
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO,
MIFUGO NA MAJI
27 MEI, 2021.

SPIKA: Ahsante sana, shukrani. *(Makofi)*

Mchangiaji wetu wa mwanzo, kama nilivyosema, ni Mheshimiwa Charles Mwijage, atafuatiwa na Mheshimiwa Edward Olelekaita na Mheshimiwa Aida Khenani atafuatia.

Ahsante, Mwenyekiti ameunga mkono hoja. Mheshimiwa Mwijage, utuanzishie.

MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa hii ya kuchangia sekta hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia rasmi, nitumie dakika moja kuliweka sawa jimbo langu. Kama

inavyojulikana, mimi ninazo *square kilometers* 7,000 ambazo ni maji na nina Kata tatu za visiwani. Nitumie fursa hii kuwaomba wananchi wa Bumbile hasa Iyumbo, mtulie. Mamlaka ya *TASAC* imewazuia wananchi wetu wasipande mitumbwi kwenda kwenye Mwalo wa Kamugaza kwa sababu haujajengwa gati, mtulie. Nimemjulisha Waziri mwenye dhamana, nimemjulisha Mwenyekiti wa Sekta. Sijapata pesa za kujenga gati, lakini nitaomba hata kuuza mali zangu, nitajenga gati. Shida zangu na wananchi wangu nazijui mimi, mwenye shibe hamjui mwenye njaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkurugenzi Mkuu wa *TASAC* ana shibe yake na wasaidizi wake wana shibe zao, mimi nafanya kazi na Waziri na ikishindikana nitakuja kwako Mheshimiwa Spika. Mwenye shibe hamjui mwenye njaa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naanzia ulikoishia juzi. Juzi wakati tunahitimisha Wizara ya Kilimo, ulitoa mahitimisho mazuri na haya yalitokana na michango mizuri ya Waheshimiwa Wabunge, lakini zaidi mzungumzaji wa mwisho, Mheshimiwa Balozi Dkt. Kakurwa. Katika mahitimisho tulikubaliana wote kwamba sasa hatuwezi kwenda na mwendo huu, ila tunapaswa kuchupa. Ukarejea, tulipofanya mageuzi makubwa katika sekta ya nishati na sekta ya miundombinu. Kwa ruhusa yako nami uniruhusu nianze hapo.

Mheshimiwa Spika, katika Dira yetu ya Taifa 2020 - 2025, tuna mipango mitatu ya miaka mitano. Mpango wa Kwanza dhima yake ilikuwa kuondoa vikwazo, tulipambana. Mpango wa Pili, dhima yake ilikuwa ujenzi wa uchumi wa viwanda ili kuchochea mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu. Mpango wa Tatu ni kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu. Kumbe tulikuwa tunafanya nini? Dhima ya kwanza tulikuwa tunajenga msingi; dhima ya pili, tukanyanyua boma na dhima ya tatu ni *finishing. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi Wabunge wa Bunge la Kumi na Mbili tunahusika kwenye *finishing. Finishing* ya kufanya nini? Kuipeleka nchi hii ifikapo 2025 watu wawe na kipato, waondokane na umasikini, wawe na *income per capita* ya

dola 3,000. Ama wasifike, angalau wafike Dola 1,700 kama alivyosema Mheshimiwa Prof. Muhongo. Pia tuwe na uchumi imara na shindani.

Mheshimiwa Spika, nizungumze la muhimu, siyo hiyo *income per capita* ya 3,000 ila muhimu ni uchumi jumuishi. Sasa unapotaka kwenda uchumi jumuishi, ni sekta za kiuzalishaji ambazo ndizo zinaweza kukupeleka kwenye uchumi jumuishi. Unaweza kuzidiwa mafuta, dhahabu, ukawa na *income per capita* kubwa, lakini kuna watu wanakula vumbi barabarani. Kumbe ukiimarisha kilimo, mifugo na uvuvi, ndipo unaweza kwenda kwenye sekta ambayo italeta uchumi jumuishi kwa Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siendi kwenye takwimu kwamba bajeti ni ndogo, hapana. Iwe kubwa ifanye nini? Nataka kuchupa. Bahati mbaya, tujifunze kwa wadogo zetu, lakini siyo bahati mbaya wadogo zetu ni rafiki zetu. Tujifunze Uganda, tujifunze Rwanda. Katika nchi zinazofanya vizuri kwenye mifugo Afrika, ni Mali, Ethiopia, *South Africa* na Uganda.

Mheshimiwa Spika, Uganda wanauza maziwa na bidhaa za maziwa nje na wanapata Dola milioni 100 kwa mwaka. Tanzania hatupati hata senti 50. Ukiuliza kwa nini? Wanasema ni sera. Kumbe siyo bajeti, kinachotangulia ni sera.

Mheshimiwa Spika, nikishamirisha ule mkakati wako wa kuchupa, tunapaswa tuanze kwa kubadilisha *mindset* ya ufugaji wetu, tutoke kwenye uchungaji twende kwenye ufugaji. Kwa hiyo, sera ninayoitaka ni sera ya kuwachukua hawa watu; kwa sababu nawasikia watu wanavyochangia. Watanzania na Wabunge walio wengi, hawataki uchumi wa kuwapeleka wachache juu na kuwaacha wengine. Mimi nakuwa makini ninapokuwa nachangia na ndugu yangu Mheshimiwa Balozi Dkt. Bashiru. Yaani ukileta sera ya kuwaacha walio wengi, unaona anaumia kweli. Kwa hiyo, sera inayotakiwa ni ya kuwachukuwa walio wengi.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia, *dairy industry* ya Uganda, imechangiwa na wananchi walio wachache, lakini Serikali ya Uganda ilikopa pesa nyingi na kulikamata lile eneo lililofanya vizuri na kuwekeza pesa pale. Ndiyo ikafanyika *local farming,* ikafanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, Uganda wanachakata maziwa lita milioni 2.8. Nilipokwenda Uganda ku-*understudy,* ile nafika walijua najua nakuja ku-*understudy.* Wakanieleza mambo yote, lakini wakasema Tanzania mna uwezo wa kuzalisha na kuchakata lita milioni nne. Nikasema mnajuaje? Wakasema habari zenu tunazijua. Mnaposema Tanzania nasi tunazalisha lita milioni 2.8, hoja siyo kuzalisha, hoja ni kuzichakata ili zifike kwa mteja. Unaposema unajenga uchumi wa Taifa, ujenzi wa uchumi wa Taifa ambao ni shindani, lazima uwe na kiburi cha kuuza. Hatuuzi nje. Tuna hali mbaya kwenye maziwa. Sasa tunachopaswa kufanya ni kukamata watu kuwafundisha njia mpya za kufuga kama walivyofanya Uganda.

Mheshimiwa Spika, watu wamezuiwa mambo ya kuhamahama; ndama anazaliwa Muleba, akija kuchinjwa ameshafika Lindi. Huyo ng'ombe ukimchinja, wastani wa kilo ni 100. Leo hii katika jimbo la Mheshimiwa Bashungwa kuna ndama wa miezi 18, ukimchinja unapata kilo 600. Waziri ulimwona, Katibu Mkuu wako alimwona na Wabunge niliokuwa nao; na Mheshimiwa Balozi Dkt. Bashiru alimwona na akaweka sahihi nikaiona sahihi yake. Tunapaswa kuipeleka sekta hiyo, ndipo tutakapoweza kuchukua walio wengi na kwenda kwenye *level* hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie *NARCO.* Waziri ameizungumza vizuri kwamba asilimia 20 ya *NARCO* ndiyo ranchi ambazo wanazimudu na kuweka ng'ombe hao. Katika kuchupa, nitoe ushauri kwa *NARCO;* ubaki na eneo la asilimia 20 uache kupangisha. Haya maeneo unayopangisha uwaachie Halmashauri na Waziri wa Ardhi wawapangie wananchi. Nitapendekeza tuje na kitu kinaitwa *Livestock Development Authority* ambayo itakuwa na idara ya maziwa na idara ya nyama, kusudi ninyi sasa muwe mna-

regulate na kuwaambia watu *pasture* ziko vizuri, *pasture* zinakwenda namna hiyo ili tuweze kuhakikisha kwamba sekta ya mifugo na sekta ya uvuvi zinachangia pato la Taifa zikiwa za kwanza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kaguta Museveni aliniambia, kufika 2022 kama sekta ya maziwa haitakuwa namba moja Uganda, Waziri anapoteza kazi. Leo maziwa ni sekta ya pili baada ya kahawa ukiondoa dhahabu, katika kuchangia uchumi wa Uganda. Waziri wa Mifugo (ni mjomba wangu) aliniambia kwamba 2022 maziwa yatakuwa yanaongoza. Sasa na sisi Taifa tujiwekee mpango kwamba samaki tuta-*export* kiasi gani? Maziwa kiasi gani? Sisi aibu tumezizoea, hata kwenye samaki; nusu ya Ziwa Victoria ni la Tanzania lakini Uganda wanatuzidi kwa ku-*export* samaki. Yaani unapata aibu, unakuwa mjinga mpaka unazoea ujinga. Sasa tuchupe. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakimbilia kwenye maamuzi yako kwamba tuchupe, hii hali tuliyomo siyo ya kwetu. Sina shida na bajeti, uwasilishaji mzuri, lakini hii tunaitumia kama maandalizi ya kuweza ku-*take off* na kuchupa kwenda kwenye anga tunazostahili zenye kipato kikubwa cha watu walioshikamana wenye utulivu, amani na utawala bora tulionao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Charles Mwijage. Umetuanzishia mjadala vizuri sana, tunakushukuru sana. Pamoja na mengine umesifia *NARCO,* lakini Mwenyekiti amesoma hapa kwamba *NARCO* ina ng'ombe kama 10,000 na kitu. *Capacity* yao ni 90,000. *NARCO* imeshashindwa. *(Makofi)*

Kenya kuna *NARCO?* Hayo mafanikio ya Uganda ni kutokana na *NARCO?* Rwanda kuna *NARCO?* Mheshimiwa Kimiti yuko hapa, *NARCO* imeshashindwa, twende *private.* Sisi ndiyo ushauri wetu; wagawiwe watu vipande vya ardhi, wapewe na hati, wataendeleza. *(Makofi)*

Hata hayo mashamba yaliyopo, siyo *range* ya mifugo. Inaitwa *NARCO* lakini imejaa misitu utafikiri ni hifadhi ya wanyamapori. Hifadhi ya wanyamapori na shamba la mifugo ni vitu viwili tofauti. *NARCO* imeshashindwa, huo ndiyo ukweli. Meneja wa *NARCO* upo, Bodi mpo, mmeshashindwa, kubalini kwamba mmeshindwa. Tunaendelea, maana ni mjadala huu. *(Makofi)*

Tunaendelea na mjadala kuona kama kuna wanaoweza kutetea, hebu watetee tuone leo na kesho. *NARCO* imekaa pale Kongwa hekta 40,000 na ndiyo *the best ranch in the country,* hakuna kitu. Siyo kwamba meneja hafai, haya mambo ya kufanya kipamoja pamoja haiwezekani. Twende *private;* ya mtu mmoja mmoja, *private* ya vikundi, *it is okay.* Ila hii ya *National Ranching,* tumeshashindwa.

Mheshimiwa Olelekaita, atafuatiwa na Mheshimiwa Aida Khenani.

MHE. EDWARD O. KISAU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Kwanza kabisa nampongeze Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu yao wote.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Balozi Dkt. Bashiru, juzi alituwekea *foundation* nzuri sana. Tunapozungumza habari ya kilimo au mifugo na uvuvi, kama asilimia 65 au 70 ya Watanzania wako huko; *we have no option,* lakini Bunge hili umenisaidia, kwamba baada ya miaka mitano Watanzania wanufaike na sekta hizi za mifugo, uvuvi na kilimo. Najua pengine tutakuwa tumechelewa mwaka huu, lakini tunaanza kutema cheche hapa ili sasa mwaka wa fedha ujao Serikali ijue kabisa, kama tunataka kuweka *legacy* kwenye kilimo, mifugo na uvuvi, ni lazima tu-*commit* pesa nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nasoma takwimu za Serikali hapa, tunaambiwa kuna mifugo karibu milioni 33.6. Ilani ya Chama cha Mapinduzi imeainisha vitu vingi sana ambavyo tumeahidi kufanya kwa miaka mitano ijayo. Hekta

za mifugo kutoka 2,788,000 hadi hekta 6,000,000. Kwa hiyo, maana yake tumeahidi kutenga hekta 3,211,000. Ili mifugo iweze kustawi ni lazima wawe na maeneo.

Mheshimiwa Spika, mzungumzaji aliyepita alikuwa anasema ng'ombe anazaliwa Kagera anaishia Lindi, *there is absolutely nothing wrong.* Ng'ombe kuhama ni *coping mechanism* ya magonjwa, wanatafuta maji na malisho. Wafanye nini sasa kama hifadhi zinachukuwa maeneo yao? Kuhama kubaya ni ile ya kusababisha migogoro na watumiaji wengine wa ardhi. Hiyo hapana, lakini kuhama ni *coping strategy.*

Mheshimiwa Spika, vile vile ilani inazungumza na nilikuwa nasoma hotuba ya Wizara hapa; inasema mtajenga majosho 129. Ni kidogo sana na hii inatokana na bajeti yenu kuwa ndogo sana. Kwa mfano, Kiteto peke yake majosho tunayohitaji ni 48, kwa sababu ilani inasema lazima katika kila kijiji chenye mifugo kiwe na josho. Sasa kama mnapewa bajeti ya kutengeneza majosho 129, Kiteto peke yake inahitaji 48, haiwezekani. *It is a very big joke.*

Mheshimiwa Spika, vile vile ilani imesema tutajenga mabwawa kama 400 hivi kwa miaka mitano. Kwa hiyo, *in average* ni mabwawa karibu 91 kila mwaka, lakini hapa ninyi mmepewa mabwawa manne tu. Kama siyo manne, Matano. *It is a very big joke.* Kwa Kiteto peke yake, pungufu ya malambo ni 44, halafu tunaweka kwenye bajeti manne.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tumedhamiria kwamba Bunge hili liwanyanyue Watanzania katika sekta hizi muhimu sana, nashauri; kwa sababu nilikuwa naangalia hapa, uvuvi na mifugo; na imetokea *trend* siku hizi ukichanganya mifugo na kilimo kuna sekta moja itapewa pesa nyingi kuliko nyingine. Ukichanganya maji na mifugo kuna sekta moja itapewa hela kutoka nyingine. Sasa maji tunafanya vizuri, kilimo tunaelekeaelekea hivi kidogo, sasa mmechanganya uvuvi na mifugo. Sasa uvuvi inachukua bajeti mmetenga hapa karibu shilingi bilioni 90 na kitu kwa uvuvi halafu mifugo shilingi bilioni 16.

Mheshimiwa Spika, tukitaka kufanya vizuri zaidi labda huko mbele tutenge kabisa, tuwe na Wizara maalum ya Mifugo, tuwe na Wizara maalum ya Uvuvi, tuwe na Wizara ya Kilimo. Tukitenga hivi tutaweza kuweka nguvu kubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, nami napendekeza tena, lazima tuji-*commit,* kuweka asilimia 10 ya mapato yetu kwenye uvuvi, kwenye mifugo na kilimo. Tukifanya hivyo tutaweka *investment,* lazima iwe *serious. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mzungumzaji aliyepita alikuwa anatoa mifano ya nchi nyingine kama Ethiopia, Rwanda na Uganda; na Botswana *by the way,* ndiyo inafanya vizuri zaidi kuliko nchi yoyote Afrika kwa ku-*export beef,* lakini angalia *investments* zao, ni kubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, nami nakubaliana nawe. Kuna siku nimetembelea *NARCO* hapo, kwenda kuangalia ng'ombe pale. Ni kweli, yaani hata majani yaliyoko pale hayawezi kumalizwa na ng'ombe walioko *NARCO.* Ni afadhali mngewapa wafugaji tu. Kwa hiyo, ni lazima tuangalie tija kwa miradi tunayowekeza kwenye sekta hizi.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa tunasoma ilani hapa; tani za kunenepesha mifugo nchi hii ni 900,000 peke yake na tuna ng'ombe milioni 33 na tumejiwekea malengo ya kutengeneza hizo tani milioni nane. Kwa hiyo, huo ni mfano tosha tu kwamba hatuja-*invest heavily* kwenye mifugo. Kwa hiyo, tusishangae sana.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, pato la Taifa asilimia 7.9 siyo kidogo. Wakati mwingine huwa nafikiri kwamba hatutengenezi mipango sahihi ya ku-*capture contribution* ya mifugo. Kama kuna wanywa bia hapa, hakuna mnywa bia hata mmoja asiyekula nyama. Nami sitaki kuvuruga Bunge lako, lakini ningesema leo wanyooshe mikono wanaokula nyama hapa, watasimama mpaka wale waandishi wa habari ambao wanapiga kamera hapa. Hiyo ni *contribution*

ya mifugo. Kwa hiyo, *I think* hamjaweza ku-*capture* kabisa *contribution* ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, kwa Jimbo la Kiteto peke yake tuna mifugo 500,000, mbuzi 500,000, siyo kidogo hiyo, ni *contribution* kubwa sana. Ripoti zeni zinasema kuna watu milioni nne wanategemea *direct income* kutoka kwenye mifugo katika nchi hii. Kwa hiyo, lazima tuwe *serious* katika ku-*invest,* tuweke pesa nyingi ili mifugo yetu iweze kuleta tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naangalia ripoti zangu za Kiteto hapa wataalam wanaohitajika, ukiangalia wataalam wanaohitajika kwenye sekta hii ni 106 halafu waliopo ni 35, pungufu 40. Kwa hiyo lazima kweli tu-*invest* kwenye mifugo na uvuvi kama tunataka kwenda mbele huko. Miaka miwili iliyopita sisi tumepata mvua kubwa sana na Kiteto sasa tuna wafugaji wanakula Samaki sasa.

MHE. ESTHER MATIKO: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Taarifa Mheshimiwa Esther Matiko nimekuona.

MHE. ESTHER MATIKO: Mheshimiwa Spika, ahsante nataka tu nimpe taarifa ndogo mchangiaji wakati anachangia amesema tukiamua kuazimia nakuchukua walau asilimia kumi ya mapato, tungeweza kufika mbali upande wa mifugo, uvuvi hata kilimo. Nimkumbushe tu kwamba ni Azimio la Malabo ambalo tumelisaini ambalo linatutaka walau tutenge asilimia kumi ya bajeti ya Serikali kwenye eneo la kilimo, mifugo na uvuvi. Kwa hiyo, siyo kwamba tuhiari tu kama mapato ila ni Azimio ambalo tumelisaini. Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Taarifa hiyo unaipokea Mheshimiwa Edward.

MHE. EDWARD O. KISAU: Mheshimiwa Spika, nakubali na napokea, lakini ninataka tu nimuambie kwamba hatuhitaji Malabo *actually* ili tuamue ku-*invest ten percent*. Malabo *declaration* ni kwamba tu wametusaidia, lakini kweli

kama tungekuwa tunasubiri Malabo *declaration* na Malawi na hata hivyo pamoja na *declaration* hiyo *investment* inayoenda kwenye kilimo ni less *than one percent*, less *than one percent.* Kwa hiyo, kwa kweli lazima, lazima tutoke huku tu-*invest every* kwenye uvuvi, tu-*invest every* kwenye mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivi, siku hizi Kiteto tumepata kama mabwawa mawili ya samaki na tumeanza kujifunza kula samaki na wilaya yangu kwa mara ya kwanza kwa mwaka fedha wamesema tutapata kodi kama milioni nane hivi inatokana na Samaki na wafugaji wameanza kutengeneza leseni kutoka kwenye halmashauri.

Mheshimiwa Spika, halafu anakuja mtu wa maliasili eti anawaambia wale wafugaji wale *brand new,* watu ambao wanataka kula samaki *for the first time,* halafu unawaambia tena eti hairuhusiwi, sijui nini, yaani tunawaongezeeni watu wa kula samaki ili tuongeze tija zaidi halafu mtu anatwambia mambo ya leseni yametoka wapi ni *confusion* na ndio ile Mheshimiwa Rais wetu alikuwa anasema *concept of one government.* Kwa hiyo, kwa kweli lazima tuwatetee, lakini baada ya kusema haya lazima sasa na ninyi mifugo muwe *serious* nilikuwa nasoma ripoti zenu hapa.

Mheshimiwa Spika, wanasema eti ng'ombe milioni sita zimekamatwa kwenye mapori tengefu, ng'ombe milioni sita ipo kwenye ripoti hapa, na kwanza nashangaa kwa sababu hawajaandika jimbo langu na kila siku wanakamatwa hapo na pori hili Tengeru linaitwa Mkongoroyo**,** lazima muwatete wafugaji hawa, ipo kwenye ripoti zenu. Naona Waziri anamuuliza mwenzake hapo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ukisoma ukurasa wa 205 nendeni mkasome *data* za mifugo kukamatwa kwenye mapori haya, ni lazima kama nchi tusimame huu ni uchumi hatutaki ng'ombe hizi zikamatwekamatwe hovyo ni uchumi wa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Edward Olelekaita, Mbunge wa Kiteto. Nilishakutaja Mheshimiwa Aida Khenani na Mheshimiwa Jasson Rweikiza atafuatia.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru nimepata hii nafasi kuweza kuchangia wizara hii muhimu na ninaomba niendelee alipoishia mchangiaji kwamba, pamoja na kwamba tunatambua kwamba wafugaji nao wanahaki na tunatambua kwa kwenda kuchukua ushuru kutoka kwao, lakini bado wafugaji hawajatendewa haki kama inavyostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Mifugo na Uvuvi zote zipo kwenye Serikali, leo ukiangalia namna wanavyotendewa wafugaji wa nchi hii, wakati tayari wizara inawajibu hamuwezi kuwa na haki ya kuchukua ushuru halafu mnashindwa kutimiza wajibu wenu kwa wafugaji, haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo jambo kwamba, pamoja na hizo wizara mbili ambazo nimezungumza, lakini bado kuna wafugaji ambao ng'ombe zao zilikamatwa bila utaratibu wakaenda mahakamani na mahakama ikaamua kwamba hao wafugaji warudishiwe ng'ombe zao, mpaka leo hawajapewa ng'ombe zao. Ni wajibu wenu wizara kwa sababu mnachukua ushuru na tozo mbalimbali kuhakikisha wafugaji wa nchi hii ambao mahakama imeshaamua wanapewa haki zao za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba wanatakiwa kurudishiwa mifugo bado mnawajibu kama wizara kuhakikisha kwamba hawa watu, minada pale panapostahili, nitazungumzia eneo moja tu, wafugaji wangu ambao wapo ziwani, Ziwa Tanganyika ili wafikishe mifugo yao mnadani lazima wapite kwenye hifadhi na wakipita kwenye msitu ule wanakamatwa sasa ni wajibu wa nani, lazima muwapelekee huduma jirani na kule waliko kwa

sababu ni haki yao na ni wajibu wenu Wizara kufanya hivyo. Kwa hiyo tunaomba minada kwenye maeneo ambayo yana wafugaji kwa sababu ni haki yao kupata huduma za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuzungumzia uchache tu kwa hao wafugaji, naomba niende kwa wavuvi, miongoni mwa changamoto ambao zinawakumba wavuvi wetu ni pamoja na kanuni zilitungwa 2019/2020, kuna changamoto kubwa kwenye eneo hilo, Mheshimiwa Ulega ulikuwepo kwenye utungaji wa hizo kanuni na wakati Mheshimiwa Rais anasema anakurudisha hapo alitamka maneno fulani. Hata hivyo, wakati naangalia *CV* zako nikagundua kwamba eneo hilo linakuhusu sana la uvuvi na akasema amekuleta urekebishe na sisi tunaimani kwamba Mama hakuja tu kwamba kukurudisha alikuwa amepitia na akagundua kwamba kuna shida. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa hicho alichokifanya tuna mategemeo makubwa kwa kuwa waziri ndio ameingia wewe ulikuwepo utamsaidia zaidi kuweza kuboresha yale makosa ambayo yalifanyika kipindi kilichopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitaanza kuzungumzia habari ya uvuvi haramu. Mimi Aida siyo muumini wa kuwasaidia wanaofanya uvuvi haramu, lakini kumekuwa na makatazo kadhaa kutoka kwa wizara na Serikalini, lakini makatazo hayo hayaendani na njia mbadala namna ya kuwasaidia wavuvi wetu kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia suala la nyavu, wakati waziri anawasilisha hapa amesema uvuvi haramu umepungua kwa asilimia 80 tunashukuru kwa sababu umepungua, lakini umepungua umewaacha wavuvi wetu kwenye hali gani kwenye Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara ilikuja na utaratibu wa kwamba wanahitaji kutumia nyavu ya milimita nane na kumekuwa na mkanganyiko kwenye hiyo taarifa, wengine milimita kumi, wengine milimita nane. Pamoja na milimita nane hiyo nyavu wanapokwenda kutumia hao wavuvi kuna

maeneo ambayo haizuii hiyo nyavu Samaki ambao wizara haitaki waingie kwenye ile nyavu, kinachotokea ni nini? Huyu mvuvi ambaye ni mtu wa mwisho kabisa ikitokea wale Samaki ambao inaonekana ni halali wapo robo tatu labda pale wamepenyeza Samaki kumi au watano hawa watendaji wanapofika kule wanawatoza faini, faini ambazo hazina uwiano, milioni mbili, milioni tano, milioni kumi.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hawa wavuvi pamoja na kuchangia pato la Taifa hizi nyavu zinapoingia nchini Serikali mpo, nyinyi ni wajibu wenu kuhakikisha mnafuatilia nyavu hizo zinazalishwa wapi. Kinachofanyika sasa hivi kwenye nchi yetu ni sawa na msafara wa ng'ombe, ng'ombe wa mbele akisimama anayepigwa ni ng'ombe wa nyuma ndiye anaye adhibiwa. Hawa wanao adhibiwa leo wavuvi wetu ni watu wa chini kabisa hizi nyavu zimepita sehemu ngapi mpaka kumfikia mvuvi wa chini. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri nikuombe sana, niwaombe sana na Mheshimiwa Waziri kuna haja ya kufanya utafiti wa kutosha juu ya jambo hili na kwa sababu tumekuwa na utaratibu tukiamini ndiyo njia halali, au ndiyo suluhisho la kuchoma nyavu ni vizuri tukajifunza. Nitatolea mfano wa Ziwa Tanganyika, Ziwa Tanganyika tuna-*share* zaidi ya nchi tatu, hivi mmejiuliza nchi nyingine ikiwemo Kongo, Burundi na Zambia wamefanya nini na wanatumia nyavu gani badala ya kuja kuwaadhibu hawa wavuvi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilizungumza kwenye Bunge lililopita na leo narudia kusema hawa Samaki wanavyokuwa mle ndani kwenye ziwa hawajui kwamba wapo Tanzania, wapo Kongo au wapo Burundi kwa hiyo kuna wakati mwingine tunatunga kanuni ambazo zinakwenda kuwanyonga wavuvi wetu bila kuangalia kwamba wenzetu wanafaidikaje na hilo jambo.*(Makofi)*

MHE. ASSA N. MAKANIKA: Mheshimiwa Spika, taarifa, hapa.

SPIKA: Mheshimiwa Spika, taarifa nakuruhusu.

MHE. ASSA N. MAKANIKA: Nipo hapa Makanika.

SPIKA: Sawa, endelea.

MHE. ASSA N. MAKANIKA: Mheshimiwa Spika, naomba kumpa taarifa mzungumzaji anayezungumza kuhusu nyavu hizi ambazo zinatakazwa na wizara ni nyavu aina ya Makira, hizi nyavu aina ya Makira neno lenyewe limetoka Kongo ni neno la kifaransa kwa hiyo linakatazwa huku kwetu Ziwa Tanganyika, lakini kule Kongo wanavua kwa kupitia nyavu hiyo, kwa hiyo, tunahifadhi samaki huku kwetu kule tunawaachia waweze kuwavua hao Samaki. Ahsante sana.

SPIKA: Unapokea taarifa hiyo Mheshimiwa Aida.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Spika, kwa maslahi ya wavuvi wetu ninapokea kabisa, kabisa hiyo taarifa na kuna haja ya wizara kujitafakari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwenye jambo hili twendeni tukafanye utafiti wa kutosha kwenye nchi ambazo tuna-*share* kwenye Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika, kuangalia wenzetu wanafanya nini kabla ya kuja na kanuni ambazo hazitusaidii. Lakini tuboreshe pia sera zetu na sheria ambazo tunaamini zitaleta manufaa kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uvuvi *ring net,* kulingana na umaskini wa wavuvi wetu wanatumia *ring net* utakuta mle ndani kwenye hicho kifaa kuna wavuvi kumi, kumi na moja mpaka kumi na tano. Sheria zetu zinataka kila mvuvi aliyopo kwenye kile chombo awe na leseni, hili jambo Mheshimiwa Waziri nataka tu kwamba, kama tuliweza kuangalia zile sheria au kanuni za wafanyabiashara wadogo ambazo zilikuwa ni kero twendeni tukaangalie na kwa wavuvi wetu jambo hili ni kero bado kwa wavuvi wetu, naamini inawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende kwenye jambo lingine kuhusu mikopo, mikopo kwa wavuvi. Pamoja na kuwachomea nyavu hawa watu wamekuwa maskini ni wajibu wa Serikali sasa tuende tukawapatie mikopo ambayo itawasaidia kuwa na nyavu halali ambazo zimeidhinishwa na wizara ziweze kuwasaidia watokane na uvuvi walionao leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba hili jambo ipo kwenye sera, nashukuru nimeona wizara mmeanza juzi Mwanza nilikuwa na Naibu Waziri yupo kule, tunataka kuwaona na wavuvi wa Ziwa Tanganyika wanapewa mikopo, mikopo ambayo itawawezesha waondokane na umaskini ambao mwingine ulitokana na maamizio na mambo yenu ambayo mlikwenda kuyafanya ambayo hayatatusaidia kitu chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda niende kwenye suala la mipaka ndani ya ziwa. Kama kuna sehemu kinatumika kama kichaka leo hii cha kukusanya kodi kwa wavuvi ni hicho kitu kinaitwa mipaka, hifadhi ndani ya ziwa. Hawa wavuvi wetu wanapoingia ziwani kuvua hakuna alama yoyote inayoonyesha kwamba hapa niihifadhi, matokeo yake wale watendaji badala ya kutoa elimu wamekaa pale kama mtego wanasubiri mvuvi aingie kisha wampe adhabu kwamba hapa umeingia kwenye hifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo hili halikubaliki, ni vizuri tukajikita kutoa elimu na kutimiza wajibu wetu wa kuweka mipaka, alama zinazoonyesha hii ndiyo mipaka hapa ni hifadhi, badala ya kwenda kuwapa nanii adhabu wavuvi wetu. Na hili jambo wapo watendaji wenu ambao siyo waaminifu, inawezekana zile fedha hazifiki kwa sababu hata wanapotoza hawatoi risiti, naamini Serikali hainufaiki na chochote kwenye jambo hili. Kuna kila sababu pamoja na sheria zenu ziwe wazi na mjikite zaidi kutoa elimu kwa wavuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la uvuvi ni suala ambalo watu wanataka kujikimu kimaisha yale maji yalivyo yasigeuke leo kuwa laana kwa wananchi wetu lazima maji yale kuwa karibu leo na Ziwa Tanganyika wananchi wanataka kunufaika iwe baraka, siyo leo inavyoonekana kuwa laana kuwa karibu na Ziwa Tanganyika, haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho, kuna wamama ambao wamejikita kuuza Samaki hawa Samaki ambao leo inaonekana ni haramu wanapita na mabeseni na sinia wanauza zile Samaki. Jambo ambalo linatokea leo Maafisa Uvuvi akikuta yule mama anauza Samaki, yule mama hajui kwamba huyu Samaki anaruhusiwa au haruhusiwi anakamatwa na sinia lake, anatozwa faini milioni moja, laki tano, laki nane, niwaombe wizara kuna kila sababu ya kuwaangalia...(*Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Aida Ahsante sana, nakushukuru, Mheshimiwa Jasson Rwekaiza atafuatiwa Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe.

MHE. JASSON S. RWEIKIZA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuchangia hotuba hii ya Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi, lakini Mheshimiwa Spika nakubaliana na wewe kwamba *NARCO* imeshindwa moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeambiwa hapa na Mheshimiwa Mwijage kwamba Uganda maziwa peke yake yanachangia shilingi dola milioni mia moja, mapato ya mauzo ya maziwa nje ya nchi, sisi Tanzania maziwa kwanza hatuuzi, lakini Wanyama wote *livestock* nzima siyo maziwa *item* moja inazalisha mapato ya ndani asilimia kumi, siyo ile *national product, gross GBP* mapato ya ndani asilimia kumi peke yake, ng'ombe ambao ni maziwa ndani yake, nyama,

ngozi, mbuzi, kondoo, nguruwe, kuku yaani kwa ujumla wote, *livestock* yote, asilimia kumi kwenye mapato ya ndani *gross domestic product*. Kwa hiyo kwa kweli hii ni kielelezo kwamba *NARCO* imeshindwa kabisa kazi, imekuwepo muda mrefu inafanya kazi ya kuendeleza mifugo ambayo haiiendelezi, nimesema, wabunge wamesema na wewe umesema *ranch* zote zimekuwa machaka, mapori imejaa miti hakuna Wanyama. Tunapoomba sisi kupewa hizo *block* tuanze kufuga hatupewi ili tuziendeleze ndiyo ile *private sector* kuingia kule kwenye ile *sector* wanabaki wana mapori ambayo hawayatumii.

Mheshimiwa Spika, hicho ni kielelezo kimoja cha kwamba wameshindwa, kingine kipo jimboni kwangu Bukoba nina kata mbili ambazo nashindwa kuelewa kwa nini *NARCO* inashindwa kuweka mipaka kati ya wananchi na hizo *ranch* au *block* hizo, wananchi wanapata shida kubwa sana. Kuna Kata ya Luhunga na Kata ya Kibirizi yaani watu wanaishi kwenye *ranch* humo, wanavurugana, juzi, juzi hapa katika Kata ya Luhunga *NARCO* ilitenga kipande hivi *block* hivi ikampa mtu mmoja, mfanyabiashara mmoja tena kiongozi mkubwa, akawaambia hiyo ni *block* yako, hiyo sehemu inawatu ndani yake, ina makazi ya watu, ina shule, ina makanisa, ina misikiti, ina maeneo wanaishi humo ndani, wakampa mtu aweke pale ng'ombe wake, akaweka ng'ombe wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi kwa hasira wakawaua hawa ng'ombe wote wale wakawaua zaidi ya mia, kwasababu wameingia kwenye makazi yao, wamekula mazao yao, mihogo, ndizi n.k. Sasa unashindwa kufahamu *NARCO* inafanya kazi gani inayofanya hii. Hii inaitwa *ranch* ya Mabale ipo pale karibu na Kata ya Luhunga vitongoji na vijiji vya Kayojwe, Tainoni, Kabanga, Milembe vipo mle ndani kwenye *ranch, NARCO* haiwezi kuweka mipaka ya wazi kwamba hili ni eneo la watu, hili ni eneo la mifugo hiyo ya *ranch* ambayo wameitenganisha. Hakuna mipaka inayoonekana wazi kwamba hapa ni watu hapa ni mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna Kata ya Kibirizi mwaka jana Disemba, mwezi wa kumi na mbili akaenda Meneja wa *ranch* pale, *ranch* ya Kagoma akaweka mpaka mpya kwenye maeneo ya watu, akateka kaya 170 ndani ya *ranch*, akaingiza kwenye *ranch*, akaziingiza, ambazo zilikuwa nje ya *ranch* akaziingiza katika mpaka mpya kwa kufanya hivyo akawa amechukua maeneo ya wakazi 1,138 hawana pakukaa, wamekumbwa na ranch ambayo haikuwepo leo wanasemekana kwamba wapo ndani ya *ranch*.

Mheshimiwa Spika, uamuzi ambao ameuchukua mwenyewe hakushirikisha viongozi, hakuhusisha wananchi amekwenda kuweka mipaka mipya na akachukua maeneo ya wakazi ambayo yalikuwa tayari yana makazi ya watu. Sasa hiyo ni matatizo ambayo yanaonyesha kwamba *NARCO* kwa kweli kazi haiiwezi imekuwa ngumu kwao tuangalie njia nyingine ya kufanya *NARCO* waachie hii kazi kama inawashinda. *(Makofi)*

MHE. RICHARD T. SANGA: Mheshimiwa Spika, taarifa, niko hapa Sanga.

SPIKA: Taarifa.

MHE. RICHARD T. SANGA: Mheshimiwa Spika, nataka kumpa taarifa pia mzungumzaji kwamba *NARCO* kwamba imeshindwa kuna mambo mawili ambayo pia yamejitokeza, kwenye hotuba ya Waziri ya mwaka 2016 na hata zilizofuata wanakiri wazi kwamba Serikali imeshindwa kuzalisha Mitamba kwa maana kwa mwaka 2015/2016 ilizalisha Mitamba 634, lakini *Private Sector* ilizalisha Mitamba 10,820 na kusambaza kwa wananchi kwa hiyo hicho ni kigezo mojawapo cha kwamba *NARCO* imeshindwa.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine cha pili Ranch ya Ruvu ambayo inasimamiwa na *NARCO* kuna mradi wa 5.7 billion ambayo hadi sasa umekwama, lakini mashine zimenunuliwa zipo pale zinaoza kwenye makontena kwa hiyo ni kweli *NARCO* imeshindwa.

SPIKA: Nakuunga mkono katika taarifa hiyo, wakati Olelekaita anasema katika Wilaya ya Kiteto wana ng'ombe laki kadhaa, umesema laki ngapi, laki tano, *NARCO* nchi nzima ina ng'ombe haizidi 16,000 *can you compare the two,* ni *wastage*, yaani *NARCO* mmeshindwa endelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rweikiza.

MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA: Mheshimiwa Spika, taarifa hiyo naikubali na naiunga mkono ni taarifa nzuri.

Mheshimiwa Spika, nashindwa kufahamu kwa nini Wizara inavumilia uozo huu wa *NARCO* kushindwa hasa kuchukua maeneo ya watu na kuwahamisha isivyo halali, watu wanauliwa, wanaua wanyama hawa, wanyama hawana hatia, hatia ni ya *NARCO.* Kwa nini Wizara inanyamaza na inafumbia macho jambo hili? Hatuwezi kuthamini wanyama kuliko watu, haiwezekani. Hili ni kosa kubwa linafanyika ni lazima litafutiwe ufumbuzi na tuweze kupata maelezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo navyozungumza hapa, hawa *NARCO* wako Karagwe katika Jimbo la Mheshimiwa Bashungwa wanapima kule, wanachukua maeneo ya watu wanawaingiza kwenye ranchi. Wako kwenye Kata inaitwa Lugela, wamechukua maeneo ya watu wameingiza kwenye ranchi, watu wako kule ndani, kuna shule na kadhalika. Sasa hawa watu wana nia gani? Wanaingiza watu kwenye ranchi maeneo ambayo hayakuwa ranchi hapo awali.

Mheshimiwa Spika, nafahamu kwamba miaka miwili iliyopita au mitatu Mheshimiwa Rais aliunda Tume au Kamati ya Mawaziri nane kwenda ku-*monitor* jambo hili nchi nzima. Wakazunguka maeneo ya ranchi na maeneo ya watu, wakaainisha kwamba watu wabaki huku na ranchi zibaki huku na nafikiri walitoa taarifa yao nzuri lakini *NARCO* au tuseme Wizara haitekelezi jambo hili ili shida hii iishe. Kwa hiyo, kwa kweli hili ni jambo kubwa linaathiri sana watu.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana kwenye kampeni pale kwangu ilikuwa patashika, wananchi wanasema hatukupi kura kwa sababu tunatishiwa na ranchi hizi, tutakupaje kura wewe na CCM kama hamuwezi kumaliza jambo hili? Kwa hiyo, jambo hili ni kubwa sana na ni la kisiasa, kisera, kiuchumi ni vizuri wananchi wakapata mipaka yao inayoeleweka. Kwa hiyo, niombe Wizara inapokuja kumalizia jambo hili itupe maelezo wanafikiria nini kulimaliza.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, wamesema Waheshimiwa Wabunge hapa ni la uvuvi, hata mimi linanihusu nina maeneo mengi ya uvuvi. Watu wanavua samaki wa ukubwa mbalimbali na wanatumia nyavu ambazo wanazinunua kihalali madukani. Nyavu zinalipiwa kodi na zinauzwa kihalalali, lakini wanakwenda kuchoma nyavu hizi kwenye mitumbwi kule ziwani, wanazikamata na kuzichoma moto. Samaki wanakamatwa, akina mama na wavuvi wengine wananyang'anywa, wamenunua kwa wavuvi ambao wamenunua nyavu zile kihalali.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa nini mnaruhusu nyavu hizi zitoke madukani au viwandani, watu wauziwe, halafu unasema hii sio halali. Mnakuwa wapi zinapotengenezwa, zinapoagizwa, zinapouzwa, usubiri mpaka zifike ziwani ndio uwazuie watu kutumia. Huu ni uonevu mkubwa ambao hauwezi kuvumiliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naunga mkono hoja lakini nataka majibu, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Jasson Rweikiza. Nilishakutaja Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe na utafuatiwa na Mheshimiwa Kirumbe Ng'enda.

MHE. TWAHA A. MPEMBENWE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuweza kuchangia katika Wizara hii muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nichukue fursa hii kuipongeza Wizara kwa wasilisho zuri ambalo

wameliwasilisha mbele yetu na sasa hivi tunalijadili. Kipekee nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa unyenyekevu mkubwa sana aliokuwa nao na ushirikiano ambao anauonesha kwa Wabunge wote ambao tunazungukwa na maeneo haya ya uvuvi.

Mheshimiwa Spika, vilevile nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Rais alivyoweza kumpa nafasi hii tena kwa kumtoa kwenye sehemu ya michezo, Mheshimiwa Rais alifanya maamuzi yaliyokuwa asilia. Kwa sababu Mheshimiwa Naibu Waziri yeye ni mzoefu na ni *institutional memory* katika Wizara hii. Ana uzoefu mkubwa sana na ni mtaalam katika sekta hiyo. Kwa hiyo, ni mategemeo yangu kwamba anakwenda kushirikiana na Mheshimiwa Waziri pamoja na wataalam katika Wizara husika ili kuweza kuleta mabadiliko makubwa zaidi kwa maslahi mapana ya wananchi wa Tanzania na bila kuwasahau watu wa Jimbo lake la Mkuranga pamoja na wajomba zake wa pale Kibiti.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie Wizara hii katika eneo moja tu la uvuvi. Mchango wangu utakuwa umegawanyika sehemu kubwa mbili, sehemu ya kwanza nitachangia kitaifa zaidi lakini sehemu ya pili nitarudi kule katika Jimbo langu la Kibiti pamoja na wajomba zangu wa Mkuranga ambao tuna adha kubwa sana kuhusiana na suala zima la mambo ya kamba.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli ulio wazi kabisa kwamba rasilimali tulizonazo sisi Tanzania katika maeneo yetu ya uvuvi ni rasilimali tosha kabisa kuonesha kwamba pato letu la Taifa linaloweza kuchangiwa na Wizara hii au na sekta hii liwe linakwenda juu siku hadi siku. Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ametuambia kwamba katika *GDP* tumepata asilimia 1.7 mwaka 2020 na amesema kwamba sekta hii imeongeza uzalishaji imekua kwa asilimia 6. Sasa sielewi tafsiri pana mimi niliyokuwa nayo katika watu wa uchumi tunasema ongezeko hili lime-*increase* katika *decreasing rate*.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu mwaka 2013 sekta hii katika suala zima la *GDP* lilichangia kwa asilimia

2.4, lakini leo tuko mwaka 2020 limechangia kwa asilimia 1.7. Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ametuambia kwamba kuna ongezeko zuri sana la uzalishaji katika sekta hii, sasa huu uzalishaji ongezeko lake liko *very questionable*.

Mheshimiwa Spika, Ziwa Victoria sisi tuna asilimia 51, tafiti zilizokuwa zimefanywa na wataalam zinatuambia kwamba tani za samaki zilizokuwa pale ni 3,495,914. Katika Ziwa Tanganyika sisi tuna asilimia 41, tafiti zilizokuwa zimefanywa na wataalam zinatuambia kwamba tani za samaki zilizoko pale tunazungumzia 295,000.

Mheshimiwa Spika, tukienda mbele zaidi kule kwa wakwe zangu katika Ziwa Nyasa sisi tuna asilimia 18.5 katika eneo la uvuvi, tafiti zilizokuwa zimefanywa na wataalam zinatuambia kwamba tani za samaki zilizokuwa pale ni 168,000. Hatujaishia hapo tukienda mbele zaidi kwenye *territorial area* yetu kule, tafiti zilizokuwa zimefanywa na wataalam tunaambiwa tuna tani 100,000 za samaki. Kule ndani zaidi hatukuweza kufika kwa sababu utafiti bado haujafanyika. *In totality* tani zote za samaki zilizopo Tanzania tunazungumzia 3,598,914. *GDP* tunaambiwa kwamba tumechangia kwa asilimia 1.7 hapa kuna shida tena kuna shida ya msingi.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Serikali, Mheshimiwa Waziri ametuambia hapa kuna mambo makubwa ambayo wanakwenda kufanya, mojawapo wanatuambia kwamba kuna meli tunaitegemea itapatikana kwenda kule *deep sea*. Hii iko *very questionable* kwa sababu tunachokifanya hapa tunanunua mbeleko wakati bado hata mtoto hajazaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hotuba hii Mheshimiwa Waziri ametuambia kwamba tunakwenda kutengeneza bandari pale Bagamoyo. Sisi ni wageni utatuvumilia vijana wako kwa sababu tunajifunza mambo mengi sana, mwaka 2012 kuna fedha ziliweza kutolewa katika Bunge lako hili karibia milioni 500 za kufanya tafiti jinsi ya kuweza kujenga bandari. Kutokana na taarifa tulizokuwa tumezipitia *library* huko

inasemekana kwamba kule Kilwa Masoko ndiyo bandari ilikuwa inakwenda kujengwa, nini kilichotokea mimi sijui.

Mheshimiwa Spika, leo Mheshimiwa Waziri anatuambia tunakwenda kujenga pale Mbegani safi sana mimi natokea Pwani na nina *interest* hiyo kwa Pwani lakini na Taifa kwa ujumla wake. Hata hivyo, tunaambiwa kwamba katika bajeti imetengwa shilingi bilioni 50 na sisi tunakwenda na mfumo wa *cash budget system* pale tunapokuwa tunakusanya ndipo tunapokwenda kutumia, sasa napata shida tunaagiza meli, halafu tunaambiwa tunakwenda kujenga kule Mbegani, tumetenga bilioni 50, *where are we going to get the money from?* Hapa mimi napata shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ni mhubiri mkubwa sana wa suala zima la *PPP*. Tukubali, tusikubali Serikali tusiwe tunaingia moja kwa moja kichwa kichwa katika mambo haya. Ni vizuri tukawa *tuna-regulate,* lakini tunajua kabisa kwamba kuna baadhi ya maeneo katika suala zima la tafsiri ya kiuchumi inaweza ikawa ni *controlled economy* ikawa *mixed economy*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali lazima tuwe tunaangalia jinsi ya kuweza kuingia pale. Ili tuweze kuwekeza jinsi inavyopaswa katika sekta nzima hii ya mambo ya *fishery,* ni lazima twende katika suala zima la *PPP*. Mheshimiwa Waziri na wataalam mkae kitako kuishauri Wizara kwamba twendeni kwenye *PPP* tuwaite watu waweze kwenda kujenga bandari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunavyozungumza kujenga bandari ya uvuvi hiki siyo kitu cha masihara tunazungumza bandari iwe na *infrastructure* zote zinazoweza kukubalika, ikiwemo suala zima la kutengeneza viwanda, meli inavyokuja inapaki pale, samaki zinaondolewa, kama utumbo unatolewa, watu wanaweka kwenye *cold room* mambo mengine yanaendelea. Sasa tunakuja kuzungumza kwamba tunakwenda kujenga Mbegani tumetenga shilingi bilioni 50, *this is a joke!*

SPIKA: Mheshimiwa unayetoka rudi kwenye kiti chako kwa sababu umekatiza kati ya mzungumzaji na mimi. Kwa hiyo, rudi ukae kwenye kiti chako. Nazidi kuwakumbusha kama mzungumzaji anazungumza usikate kati ya mstari wake na Spika. Mheshimiwa Mpembenwe endelea. *(Makofi)*

MHE. TWAHA A. MPEMBENWE: Mheshimiwa Spika, kwa tafsiri hiyo hiyo maana yake ni kwamba sisi ili tuweze ku-*move* kutoka hapa tulipo kama alivyosema *senior* wangu pale, kaka yangu Mheshimiwa Mwijage, ni lazima twende katika *concept* hii ya *PPP*.

Mheshimiwa Spika, narudia mara kwa mara na nitaendelea kulirudia kwa sababu kubwa moja, sheria ililetwa hapa. Sasa kama hii sheria ilikuwa imekuja kuja tu katika mazingira ya kuja, mimi napata shida. Sheria hii ilikuja hapa na ikafanyiwa *amendments,* lazima sasa tuweze kutumia sheria hii tuweze kuwaita wawekezaji ili sasa kwa namna moja ama nyingine twende tukajenge bandari na tuweze kuona sekta hii inakwenda kuchangia vile inavyopaswa sio tu asilimia 1.7 twende mbele zaidi. Mheshimiwa Waziri unatuambia kwamba kuna *growth* ya 6 *percent* katika *production* lakini *Growth Domestic Product* yenyewe imekwenda 1.7 wakati 2013 ilikuwa 2.4, hii ni *increase* katika *decreasing rate, we cannot be able to move in that way*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa tafsiri hiyo hiyo, naomba tena niishauri Serikali, ili tuweze kufanya vizuri zaidi katika eneo hili basi hakuna budi na sisi vilevile katika Wizara hii tutengeneze jeshi letu, kama kule *TANAPA* mifugo inaibiwa, watu wanachukua kila kitu. Kuna watu wanaitwa *DCA*, wanachokifanya wao hakuna kitu kingine zaidi ya kutoa tu *certificate* watu wa Spain au Malabar na meli kubwa kubwa wanatoa tu taarifa tunataka kuja kuvua kule kwenu. Watu wanachokifanya wanaambiwa bwana lipa ada akilipa ada meli inakuja inavua inaondoka. Sasa kuna zile meli nyingine haziwezi zikaja kufunga hapa, hatuna *ports* ya kuweza kufanya hawa watu waje kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mambo yako mengi, lakini naomba niende Jimboni kwangu sasa. Jimboni kwangu kuna shida ya msingi sisi tunavua kamba na hapa Tanzania wanavyozungumza suala zima la kuvua kamba wanapatikana pale. Mimi najua baba yangu mzee Mpembenwe siku moja aliwahi kuniambia, yule mnayemuona pale Spika wenu yule aliwahi kuwa Rufiji huku anaijua Rufiji vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niseme tu kwamba pale Kibiti na Mkuranga sisi tuna shida na Wizara hii, kikubwa wanachokifanya ni kuweka tu mambo ya kitaalam mengi, ma-*scientist* wanakuwa wengi. Mwaka 2017 wamezuia pale uvuvi wa kamba katika kipindi fulani, hivi ninavyozungumza kamba pale wanavuliwa katika kipindi siyo rafiki. Wakati sisi wananchi wanaomba kuvua kamba katika kipindi cha mwezi Desemba mpaka Mei wao wanatuambia tuanze kuvua kuanzia mwezi Juni kwenda mbele, kipindi hicho wale kamba wanakwenda bahari kuu, wanavyokwenda bahari kuu wananchi wetu hawana vyombo vya kwenda kule. Tafsiri yake ni nini? Tunawaweka wananchi wa Mkuranga na Kibiti katika maisha magumu. Kule ni *delta,* vile ni visiwa, hatuna zao tunaloweza kuzalisha sisi zaidi ya kamba wale kuweza kutusaidia. Kwa hiyo, hivi vitu lazima tuviangalie kwa upana wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine la kusikitisha zaidi, Mheshimiwa Waziri wiki iliyopita wakati nauliza swali hili Serikalini alisema kwa mapana marefu zaidi, katika kipindi cha miaka mitano mwaka 2015-2020 kamba waliopatikana katika Wilaya ya Mkuranga pamoja na Kibiti ni tani 1,200. Fedha zilizopatikana shilingi bilioni 16 Serikali walipata tozo shilingi milioni 600. Wilaya ya Mkuranga hawakupata senti tano, Wilaya ya Kibiti hatujapata senti tano, sasa mnatusaidia sisi watu wa Kibiti na Mkuranga? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba, Wizara lazima iweze kufikiria kutusaidia watu ambao tunaishi katika maisha ya delta, hatuna shughuli nyingine yoyote ya kilimo. Kule mimi niliko nina Kata 5 za Kiongoroni, Mbochi, Mapoloni, Msala

na Salale na kule kwa Mheshimiwa Waziri kuna Kata moja ya msingi sana kule...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. TWAHA A. MPEMBENWE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe. Waheshimiwa bandari anayoongelea ni bandari ya uvuvi, maana wako watu wakisikia neno bandari tu hatari wanaanza kuruka. Hiki nacho ni kitu kingine tofauti kina mambo yake nayo bandari ya uvuvi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Kilumbe Shaban Ng'enda, atafuatiwa na Mheshimiwa Tumaini Magessa.

MHE. KILUMBE S. NG'ENDA: Mheshimiwa Spika, naungana na waliotangulia kukushukuru sio tu kwa kunipa nafasi lakini kwa kuendesha Bunge lako vizuri kama walivyopongeza wengine katika siku hizi za karibuni tunajifunza kitu kipya kutoka kwa Ndugai tuliyemzoea, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi na wananchi wangu wa Kigoma Mjini unapozungumza habari ya uvuvi, unazungumza kiwanda kinachoajiri watu wengi na ambacho ni tegemezi kubwa la wananchi wa Kigoma Mjini. Hii inatokana na kwamba tunazo malighafi nyingi ambazo tungeweza tukaweka viwanda lakini kwa sababu hatujapata umeme wa *grid* ya Taifa bado malighafi hizo zinachukuliwa kwenda sehemu nyingine na nyingine hazijatumika kabisa na kwa maana hiyo uvuvi ndiyo eneo pekee ambalo tunalitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitamshukuru Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya uvuvi

na Wizara yake kwa ujumla. Hivi karibuni mimi na yeye tulifanya ziara Kigoma, ilikuwa mwezi jana Aprili na tukaongea na wavuvi. Napenda kutumia nafasi ya Bunge hili kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Uvuvi, kwa namna ambavyo ametatua matatizo ya wavuvi baada ya kupata ukweli na hali halisi ya manyanyaso wanayoyapata ambayo yana maeneo mawili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja ni eneo la Kanuni zilizotungwa zinazoongoza shughuli za uvuvi. Pili, ni utendaji wa ofisi yake kwa baadhi ya watu ambao wamekuwa hawana huruma kwa wavuvi. Siwezi kurudia mambo ambayo naona Mheshimiwa mwenzangu Aida ameyasema na wengine, lakini niseme, uzalishaji wa uvuvi uko chini karibu maeneo yote ya nchi yetu. Ukitafuta sababu kubwa ni mbili, sababu ya kwanza ni zana duni, lakini sababu ya pili, ni kanuni ambazo si rafiki kwa wavuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hili la Kanuni Waziri ametusaidia na namuomba aendelee kutusaidia. Kaja Kigoma pale katoa tamko la Serikali la kutaka wavuvi wa samaki wa migebuka watumie wavu wa inchi mbili, *ply* mbili badala ya maelekezo yaliyokuwa kwenye Kanuni ya wavu wa inchi tatu *ply* nne mpaka sita, ambao kwa kweli muda mrefu umewasumbua wavuvi kutokuvua. Kwa hiyo, nashukuru sana hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nimwombe Mheshimiwa Waziri asiishie hapo, kuna jambo pale tulisahau kuliweka sawa la tundu au macho ya wavu. Kanuni ya zamani ilikuwa inasema macho 144 kwa sababu wavu ulikuwa wa inchi tatu ulikuwa upana wa wavu sasa unakuwa mita 12.5. Sasa ukishapunguza upana wa macho yale kuwa ni ya inchi mbili ukiacha macho 144 ina maana kwamba wavu ule unakuwa sasa kina chake kwenda chini ni mita saba tu hauwezi kuvua. Kwa hiyo, wavuvi wanasema wanataka waende kwenye ile ile mita 12 kwa hiyo, lazima uongeze macho kwa sababu umepunguza ukubwa. Hili tulikwishalizungumza na Waziri akalielewa vizuri kwa hiyo, wameomba macho angalau

yafike 300 yawawezeshe kuvua vizuri na hasa katika ziwa hili lenye kina kirefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la zana duni za uvuvi, mimi nashangaa sana kwenye nchi yetu, tunapiga kelele ya mambo mengi lakini tunajizuia sisi wenyewe, tunasukuma gari halafu tunaweka gingi sasa itakwendaje? Ipo kampuni ya uvuvi ya wazawa wa Kigoma tangu mwaka 2015 maombi yao yako Wizarani, wametimiza vigezo vyote hamuwaruhusu kuingiza boti za kisasa za uvuvi.

Mheshimiwa Spika, baba yangu alikuwa mvuvi, kulikuwa na vyombo pale vya Wagiriki vinaitwa Angella wengine Yorobwe na kulikuwa hata na chombo cha Kibwedeko. Tulikuwa tunavua samaki mmoja wa nonzi na sangara anabebwa na watu nane leo hii hatuvui kwa sababu ya zana duni za uvuvi. Hata hivyo, urasimu uliopo wa kupata vibali vya zana za uvuvi, bora uombe kibali cha kwenda peponi utaingia haraka kuliko kupata zana za uvuvi. Haiwezekani lazima tubadilike Mheshimiwa Waziri tutoe hapo, hatuwezi kupata tija kwa zile zana zilizopo sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni ushuru katika mazao ya uvuvi. Bahati nzuri Mheshimiwa Waziri umelizungumza kidogo. Ushuru huu umekuwa tofauti sana katika mazao ya uvuvi ya Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika. Kwa mfano, kilo moja ya dagaa inayotaka kusafirishwa kwenda nje inadaiwa Dola 0.5 ambapo ikifika mahali unasafirisha kilo 100 ni zaidi ya Dola 50. Sasa hii kwa kweli unafika mahali unawakatisha tamaa hao wanaotaka kufanya biashara hii. Lazima tuangalie, ushuru uwe kidogo unaovutia biashara kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, muda mfupi hapa ulipokuwa unatambulisha wageni, umetambulisha wageni wangu na wako mpaka sasa kwenye *gallery* pale. Hawa walikuwa wananisubiri, tunakwenda nao Kigoma, wamewekeza kwenye kuchakata samaki Mwanza na tunataka kwenda nao Kigoma. Ila katika mazingira haya ya urasimu wa miaka mitano watu hawajapata vibali, haitawezekana.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme kitu kimoja, uwekezaji huu lazima tuujue uko wa aina mbili. Wapo wawekezaji ambao wanakuja kuwekeza katika nchi yetu, lakini soko lao wanategemea ndani ya nchi yetu. Wapo wawekezaji wanakuja kuwekeza katika nchi yetu, soko lao wanategemea nje. Hawa ndiyo wawekezaji bora zaidi. Kwa mfano, hawa nilionao mimi, Wachina wamefika mahali wamewekeza kule Mwanza. Wenyewe wanachukua yale matumbo ya samaki ambayo zamani yalikuwa yanatupwa. Wanachukua minofu, mapanki wanachukua Waswahili wenzetu wanakula, matumbo yalikuwa yanatupwa. Wenyewe wamechukua yale matumbo *(fishmonger),* wanafika mahali wanasafirisha huko nje na tunapata pesa nyingi. Huu ndiyo uwekezaji mzuri zaidi maana wanatoa hela nje kuingiza ndani ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikoni mtu ambaye ameleta *material* zake hapa anafika mahali anawekeza marumaru ambazo zinanunuliwa na Watanzania wenyewe humu humu wanachukua hela zetu. Kwa hiyo, nataka nisisitize lazima tutengeneze mazingira mazuri. Leo hao wawekezaji wa Mwanza...

SPIKA: Mheshimiwa Kilumbe, kumbe matumbo ya samaki nayo ni chakula!

MHE. KILUMBE S. NG'ENDA: Ohooo! Tena kina soko kubwa kuliko hata minofu ya samaki. Wapo hapa *(Kicheko/ Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la kushangaza hao hao wawekezaji ambao wapo hapa, wameomba vibali vya wafanyakazi wao wawili, leo miezi sita hawajapata na wameshalipa. Kila mmoja wamemlipia kama Dola 1,000 na risiti wamenipa wanazo hapa, lakini mpaka leo vibali vya wafanyakazi hao ambao wanakuja kuwekeza kwa ajili ya kuchukua matumbo ya samaki ambayo sisi hatuyatumii, wanayapeleka nje, sisi tunapata fedha. Mambo ya ajabu kabisa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka niseme kwenye Sekta hii ya Uvuvi sisi tunategemea Mheshimiwa Waziri na ndugu yetu Mheshimiwa Ulega, Naibu Waziri, mlete mapinduzi makubwa yaongeze pato la Taifa. Katika mapinduzi haya makubwa tunayotaka myatazame, kwanza ni hizi kanuni ambazo namshukuru Mheshimiwa Waziri ameanza kushughulika nazo. Pili, ni kuruhusu uwekezaji mkubwa kwa sababu mnaona leo tunalaumu hapa *NARCO.*

Mheshimiwa Spika, nami naungana nawe, jamani mwelekeo wa Sera za CCM katika miaka ya 1990 ni kutuondoa katika Sekta ya Umma kutupeleka kwenye Sekta Binafsi. Sekta Binafsi iweze kuchangia pato la Taifa kwa kiasi kikubwa. Sijui kwa nini hatuelewi hili? Kwa hiyo, leo Sekta Binafsi, tuisukume, tuitengenezee mazingira, sisi tukusanye kodi ili kodi zile zisaidie wananchi wetu. Mnakazana na Sekta ya Umma ambayo inafika mahali kila wakati inawekewa ruzuku na ruzuku zile zinayeyuka, kinachoendelea hakuna, mapori yamekaa. Hatuwezi kuendelea hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunataka kwenye uvuvi Sekta Binafsi imeonesha, hivyo viwanda vyote unasikia viko Mwanza, ingawa Mwanza kuna viwanda leo vya minofu mpaka hivi vya matumbo ya samaki, viko kama vinane tu, lakini nenda Uganda, viko 30 kwa sababu, Uganda wametengeneza mazuri ya uwekezaji.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Kilumbe, subiri. Mheshimiwa Amar.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Spika, nimpe taarifa mchangiaji. Siyo matumbo ya samaki. Yanaitwa mabondo kwa lugha nzuri.

SPIKA: Mheshimiwa Ng'enda unapokea Kiswahili hicho?

MHE. KILUMBE S. NG'ENDA: Mheshimiwa Spika, yaani hiyo taarifa ni sahihi na kama unavyojua Kiswahili

kimepanuka sana katika hivi vitu vya kisasa, maana hicho nilichotumia mimi ni cha Kigoma zaidi. Lugha sahihi ni mabondo na kwa kizungu wanaita *fish maws.* Kwa hiyo, nakubali taarifa hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nizungumzie suala zima la ushuru, kutazama ushuru. Nimeshalizungumza na ushuru usiwe na tofauti kubwa. Leo Ziwa Victoria, dagaa wa kilo 100 ushuru wake ni shilingi 38,000/=, lakini Ziwa Tanganyika 116,000/= kwa kilo 100. Tusiweke hii tofauti kubwa kiasi hicho.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo limelalamikiwa na wavuvi na wafanyabiashara wa mazao ya uvuvi, Mheshimiwa Waziri tukiwa pale Kigoma unakumbuka, dagaa zina *grade* kama ilivyo tumbaku. Sasa sijui hakuna *classifiers* wa ku-*classify* hii ni *class* gani na hii ni *class gani?* Haiwezekani *classes* zote ziwe bei moja tu ya ushuru. Kuna dagaa wanaitwa nyamnunga, walipigwa na mvua, hao ni kwa ajili ya chakula cha kuku...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. KILUMBE S. NG'ENDA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja.

SPIKA: Ahsante sana. Nilikuwa najiuliza kama matumbo ya samaki yanaitwa mabondo, maana Dodoma ukimwambia mtu mabondo hajui ni nini? Kwa hiyo, hivyo ndivyo, matumbo ya ng'ombe nayo ni mabondo pia; au yenyewe yanabakia kuwa matumbo? Inabidi mtutafutie neno pia. Isiwe matumbo ya samaki tu yana jina, wakati matumbo ya kondoo hayana jina. *(Kicheko)*

Kabla ya Mheshimiwa Tumaini Magessa ambaye atafuatiwa na Mheshimiwa Asia Mwadini Mohamed, niwatambue wageni wetu ambao niliwataja kabla wa Shule ya Sekondari ya Umonga. Kama mpo naomba msimame.

Umonga Sekondari. Ahsanteni sana watoto wetu. Hawa ni wageni wa Mheshimiwa Mama Toufiq, karibuni sana vijana wetu. Hii ni shule ambayo iko hapa hapa Dodoma Mjini na ni moja ya shule ambazo zinafanya vizuri sana. Hongereni sana, karibuni na mjitahidi katika masomo yenu. Tunafarijika sana kuwa nanyi watoto wetu. Inaitwa Umonga Sekondari. Umonga maana yake ni umoja. Umonga ni Kigogo, ni umoja. Kwa hiyo, karibuni sana ninyi ambao mnapenda umoja.

Mheshimiwa Tumaini Magessa, atafuatiwa na Asya Mwadini Mohamed.

MHE. TUMAINI B. MAGESSA: Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana kwa nafasi hii ya kuchangia Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Namshukuru sana Mwenyezi Mungu vile vile kunipatia nafasi hii. Niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wataalam kwa bajeti nzuri waliyoiwasilisha leo.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme mambo machache katika bajeti hii. Bajeti ya Uvuvi inaonekana kwenye utekelezaji, hela ya Serikali iliyokwenda mwaka 2020 ni asilimia 30 tu. Kwa hiyo, naishauri Serikali iongeze kupeleka pesa kwa ajili ya utengenezaji wa bajeti hii kwa sababu inawagusa sana wananchi wetu. Vile vile kwenye bajeti hii upande wa mifugo bado pesa iliyokwenda ni kidogo. Kila unapoangalia kwenye bajeti hizi utagundua mchango wa Serikali kwenye mchango ule ambao Serikali inatakiwa itoe, kwenye bajeti nzima ya nchi ni kama 0.08. Kwa hiyo, ni ndogo, haifiki hata asilimia 1 na hasa hizi za uvuvi na mifugo ni kama 0.03. Ni ndogo sana. Kwa hiyo, kama tunatarajia maendeleo makubwa na uchangiaji mkubwa wa pato la Taifa, tunategemea bajeti hizi ziongezeke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Waziri, kwenye uvuvi safari hii *development budget* ameiongeza mara saba; *seven point something* ambayo inaonesha kabisa kwamba kuna vitu vikubwa kwenye uvuvi vitakwenda kutokea japokuwa kwenye mifugo bado *development budget* ni

ndogo kwa hiyo, naamini hakutakuwa na mabadiliko makubwa sana kwenye Sekta ya Mifugo.

Mheshimiwa Spika, niungane na wewe ulivyosema *NARCO* ni kama imeshindwa hivi. Pamoja na kushindwa nitoe ushauri kwamba tunatakiwa tuunde sasa kitu kinaitwa *Livestock Development Authority.* Katika hilo, tukishakuwa na *authority* hii wao maeneo yao sasa kama wataya-*surrender* wayaache kwenye Halmashauri na Halmashauri iwape watu binafsi na vikundi mbalimbali kwa ajili ya kuhakikisha kwamba uzalishaji huu unaweza ukaongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunda hiyo *Livestock Development Authority,* tufanye kama Waganda. Tuwe na *Dairy Development Authority* ambayo itashughulika na maziwa na nyama. Kwa sababu, mpaka sasa hivi haya maziwa tunayosema yamezalishwa hapa yameshindwa kuuzwa nje kwa sababu hatuna chombo kinachoshughulika na haya. Kwa hiyo, tuunde chombo hicho, *Dairy Development Authority* ambayo itakuwa inashughulika na hii. Tutakapokuja kwenye bajeti nyingine, watatupa taarifa sahihi ya nini wameanzisha katika kuingia kwenye Soko la Kimataifa kuuza maziwa.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ambacho nataka nikizungumzie kwenye mifugo ni nyanda za malisho. Tunataka kufuga na sisi tupo atika tatu bora Afrika kama wafugaji wa ng'ombe. Mifugo hii tusipokuwa na malisho ya kutosha imekuwa ikisababisha mifarakano mikubwa katika jamii, wananchi wanagomba kati ya wakulima na wafugaji. Ugomvi huu unaotokea kati ya wakulima na wafugaji ni kwa sababu hakuna nyanda za malisho na hatujapanga matumizi bora ya ardhi kwa utaratibu mzuri ambao unaweza kutufikia nyanda za malisho wasigusane wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nitoe rai hapa kwamba tunazo sheria za kutosha. Tunayo Sheria Na.5 ya Mwaka 1999 ambayo inavikabidhi vijiji ardhi, inakuwa ni mali ya vijiji. Pia tunayo Sheria Na.7 ya Mwaka 2007 inayoshughulikia matumizi bora ya ardhi. Tunayo Sheria Na. 13 ya Mwaka 2010

inayozungumzia habari ya nyanda za malisho. Tuone ni namna gani bora tunaweza kufanya wakulima na wafugaji wasigombane kwa sababu hii ni kama Wizara moja. Kila mmoja azalishe lakini kwenye ardhi hii tuliyonayo.

Mheshimiwa Spika, nitoe ushauri tu kwamba tunapokwenda kwenye utekelezaji wa haya ambayo tunayafanya mwaka huu tuangalie namna gani tutaenda kushughulikia nyanda za malisho maana matumizi bora ya ardhi tuliyonayo yafanyike kwa wingi ndani ya maeneo tuliyonayo. Bahati mbaya sana jana ilikuwa Wizara ya Ardhi. Kwa hiyo, najua hili wao wanahusika na Wizara ya Mifugo nayo wanahusika kuhakikisha kwamba nyanda za malisho zinakuwepo ili ugomvi huu tunaousikia kila siku upungue. Migogoro ya ardhi inafifisha sana ukuaji wa Sekta hizi.

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Taarifa unapewa.

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba tatizo la Nyanda za Malisho halitokani na kutokuwa na mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa sababu vijiji vingi tayari vimeshapimwa. Kwa mfano, katika Jimbo langu la Longido kati ya viji 49, 30 vimeshapimwa na vina mpango wa matumizi bora ya ardhi, lakini kuna mashindano kati ya Wizara na Wizara. Wakati Wizara ya Mifugo haihangaiki ku-*secure* na kuhifadhi nyanda zake za malisho, maliasili wao wako kazini kutafuta nyanda za malisho za kuchukua na kuongezea kwenye hifadhi.

SPIKA: Taarifa hiyo Mheshimiwa Magessa.

MHE. TUMAINI B. MAGESSA: Mheshimiwa Spika, naipokea. Inaonekana tena kwamba kuna habari tena ya wanyamapori na siyo ya wakulima na wafugaji. Naipokea Taarifa hiyo. Najua kabisa Mkungunero pale kuna shida hiyo na kwa ndugu yangu Ngorongoro kuna shida hiyo. Hizi Wizara

zifanye kazi kwa pamoja kwa sababu ni Wizara ya Serikali. Kwanini zinashindana? Shida yetu kubwa ni kumtumikia mwananchi, hatuna haja ya kushindana. Nafikiri hili limeshazungumzwa sana kwamba Wizata zikutane kwa pamoja kujua nani anafanya nini na wakati gani ili wananchi waweze kupata maendeleo? Naomba niipokee Taarifa hiyo. Naikubali Taarifa yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme pamoja na ufinyu wa malisho kuna upungufu wa majisafi na salama kwa ajili ya mifugo hii. Kuna upungufu mno wa maji na mabwawa. Ningeomba sana mabwawa yaweze kuongezwa. Vile vile kumekuwepo na shida katika Sekta hii, kuna uwepo wa soko holela na bidhaa za madawa na vifaatiba vya mifugo. Sasa watu wanaleta tu dawa, badala ya kutusaidia ng'ombe wetu wakati fulani ng'ombe wanakufa. Pia kuna mwamko mdogo wa ufugaji wa kitaalam kwa kuzingatia idadi sahihi ya mifugo katika maeneo ya malisho. Hili nalo, tuna ng'ombe wengi lakini je, elimu imetolewa ya kutosha kuhakikisha kwamba wananchi wetu sasa wanaweza kufuga kitaalam badala ya hii ambayo inafanyika sasa hivi, inafikia mahali fulani watu wanagongana. Naamini kabisa hili likitolewa elimu, changamoto hizi zitapungua.

Mheshimiwa Spika, nijielekeze kwenye uvuvi sasa. Mimi kwenye maeneo ninayotoka...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. TUMAINI B. MAGESSA: Mheshimiwa Spika, hii kengele ya kwanza?

SPIKA: Ndiyo?

MHE. TUMAINI B. MAGESSA: Mheshimiwa Spika, kwenye maeneo ninayotoka nina mialo yapata karibu saba. Nina mwalo sehemu moja inaitwa Butunde, Kasamwa, Kageye, Bukondo, Busaka, Chankorongo na Kabugozo.

Maeneo yote haya ni sehemu ambayo nategemea wavuvi waweze kufanya kazi na kupata maisha. Bahati mbaya sana katika haya mazingira ya uvuvi, hawa wamekuwa wanafanya uvuvi huria tu. Akichukua mtumbwi wake asubuhi, anakwenda anakuja na samaki watatu au watano usiku mzima. Tunahitaji kuwawezesha hawa watu kwa kuwapa elimu na kuwafundisha.

Mheshimiwa Spika, kwenye kilimo tuna mashamba darasa, sijui kwenye uvuvi tutaita nini? Sijui tutaita uvuvi darasa, sielewi tutaita kitu gani? Ila tuwe na namna ambavyo hawa wavuvi wanaweza wakafundishwa. Sasa hivi dunia imehamia kwenye uvuvi wa vizimba. Nilimwona ndugu yangu mmoja alisimama hapa, ni mtaalam kwenye *cage* hizi (vizimba). Nimejaribu kuangalia kwenye maeneo yote hayo niliyoyataja, hakuna kizimba hata kimoja.

Mheshimiwa Spika, niseme tu, kwa sababu tuna kituo kikubwa kilichoko pale Chato, naamini kwamba kituo hicho sasa Wizara inaweza kukitumia kutusaidia sisi maeneo hayo kupata vizimba; kwanza vije vizimba vya mfano watu waone kinachofanyika; na wapatikane hao Maafisa Ugani wa kufundisha hiyo kazi kwa sababu hatunao sasa, lakini tuoneshe mfano halafu baadaye watu waingine kwenye vizimba. Watu wanasema kuna maeneo mengine yamechukuliwa kama *breeding area,* eneo tu la kufanya watu wazalie, lakini nafikiri tukifuga samaki maana yake hatuzuii *breeding* hiyo ambayo inafanyika sehemu nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naombe sana Wizara watusaidie kwa sababu tuna changamoto kubwa ambayo inaonesha ili uweze kuingia kwenye vizimba hivyo, inabidi ufanyiwe *environmental impact assessment.* Hii ni gharama kubwa. Inatakiwa *TAFIRI* waingie hapo, nao wana tozo yao; halafu Kata, Kijiji na Wilaya nayo ina tozo yake. Napendekeza sana, *TAFIRI* ambao wanashughulika na mambo ya samaki hawa ndio wachukue tozo moja tu. Wakishachukua wao ndio watai-*distribute* huko kwenye *environmental impact assessment.*

Mheshimiwa Spika, badala ya kuonekana huyu mtu mmoja mvuvi masikini anakwenda kulipa hizi na gharama yake ni kubwa, zinakwenda karibu milioni 10, ni nani mvuvi wa kawaida ana uwezo wa kuzilipa? Maana yake lazima Serikali iingie kuhakikisha kwamba tozo hizi zinapungua ili wananchi wa kawaida waingie kwenye hivyo vizimba na mwisho wa siku tutaona maendeleo yamekuja. Tumepata umeme sasa. Umeme huu utatumika wapi kama uvuvi wenyewe utaendelea kuwa wa mtu mmoja mmoja. Umeme huu utumike vizuri kuona viwanda vidogo vidogo vya samaki ili mapato haya yaweze kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, ninaamini kabisa Waziri na Naibu Waziri na Naibu Waziri wanajua, Kituo chao cha Nyamirembe kina uwezo wa kufanya kazi kubwa kwenye maeneo hayo na tukaona matokeo makubwa. Wananchi wetu tunategemea mifugo iliyoko. Kwa mfano, mifugo iliyoko Jimboni Busanda, mingi inabidi ipelekwe Misenyi. Sasa...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. TUMAINI B. MAGESSA: Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Asya Mwadini Mohamed atafuatiwa na Mheshimiwa *Eng.* Stella Manyanya.

MHE. ASYA MWADINI MOHAMED: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuweza kunipa nafasi nami niweze kuchangia hotuba hii ya Wizara muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naomba ninukuu Taarifa ya Kamati ya Bunge ya mwaka 2018 ambayo inasema kuhusiana na shughuli za uvuvi wa Bahari Kuu, kama utasimamiwa vizuri ipasavyo, basi Serikali tunaweza kuiingia pato la moja kwa moja shilingi bilioni 352. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika, Kamati ya Bunge leo hapa ilipokuja, imehakikisha na imezungumza pia bado Serikali haijafanya uwekezaji wa kutosha katika Sekta hii ya Uvuvi, hasa katika Bahari Kuu. Hili nimeliamini na limejidhihirisha pia; kwenye hotuba ya Waziri amesema pia kuwa wapo katika mchakato wa hatua ya kufufua Shirika la Uvuvi *TAFICO* ambalo Mheshimiwa Waziri ameliongelea zaidi kwenye ukurasa wa 119. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa sisi tumezaliwa na bahari tumeikuta, lakini leo ndio kwanza tunazungumza ufufuaji wa shirika. Kweli tumekuwa tuko tayari kwenye uwekezaji wa bahari?

Mheshimiwa Spika, ukiangalia bahari hii inaambiwa ina iwezo wa kuleta mapato shilingi bilioni 352. Sioni Serikali inakwama wapi kwa ajili ya kwenda kuwekeza, lakini kama Serikali nguvu hazitoshi kuna wadau wako tayari kuwekeza ambao tunawasema wawekezaji. Nadhani, nishauri, Wizara itoe wazo na iseme kwa bayana wawakaribishe wawekezaji kwenye bahari kuu waweze kuwekeza, ili tuweze kusaidia vijana wetu kupata ajira, lakini halikadhalika tuongeze pato la Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unapozungumza bahari huwezi kuacha kuzungumza uhifadhi wa maeneo ya mazalia ya samaki, nikimaanisha matumbawe. Haya matumbawe ambayo yapo yanazunguka ndani ya bahari yetu ndio sehemu salama na ndio muhimu kwa samaki wetu ambao wana uwezo wa kuzaliana, lakini pia samaki wanapata chakula kupitia hifadhi hizi muhimu za matumbawe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa matumbawe yetu yanapotea na yanaathirika kweli, kwa ambao wale wataalamu wa bahari wanakwenda baharini, nikiwemo mwenyewe nilishawahi kuangalia hayo matumbawe, unakuta matumbawe ambayo tayari yamefariki. Ukiwauliza wataalamu wanakwambia haya matumbawe yamefariki kwa sababu ya uchafuzi wa mazingira. Bahari inajaa joto kutokana na uchafuzi

mbalimbali ambao unafanywa wa kimazingira hivyo husababisha matumbawe yale kufariki. Yanapofariki yale matumbawe na kuondoka kabisa itabidi samaki hawa waweze kuhama sehemu ile ambayo hawawezi kuzaliana wala kupata chakula na kwenda kutafuta hifadhi mbali. Sasa maana yake wanavyokwenda mbali wana uwezo wa kutoka ndani ya bahari yetu ama kutoka ndani ya Tanzania na kwenda nchi jirani. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwadhibiti samaki hawa ambao wanatoka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, Serikali je, ilishawahi kukaa na nchi jirani na kutengeneza mikataba ya makubaliano juu ya usimamizi wa hifadhi za bahari na hasa samaki wetu wanavyotoka na kwenda kuhamia katika nchi jirani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna samaki wanaitwa Tuna, hao wana tabia kama ya nyumbu. Kuna msimu wanaondoka Tanzania, wanaondoka ndani ya bahari wanakwenda katika nchi jirani, wanakwenda kustarehe huko *then* wanarudi wanapenda kufanya *tour.* Kwa hiyo, samaki hawa wana uwezo wa kutoka na kwenda, lakini wakifika kule wakavuliwa *then* tunarudishiwa samaki hawa wanauzwa kwenye vikopo tunaambiwa nunueni Tuna kwenye makopo, lakini kumbe tunauziwa mali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu tunahitaji Serikali, nishauri, iwekeze zaidi ifanye mashirikiano na nchi jirani kuhakikisha wanasaini mikataba ambayo halali ya kusimamia samaki tuna na wengineo, ili kuweza kusaidia pato la nchi hii lisiweze kupotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halikadhalika kwenye uhifadhi, naomba niishauri tena Serikali, kuna kisiwa Zanzibar kinaitwa *Chumbe Island,* hiki kisiwa kwa wale wanaosafiri kwa boti mara kwa mara utakutananacho utakuta mnara pale wakati unaelekea Zanzibar. Hiki kisiwa kimepata tuzo ya uhifadhi wa utalii wa kimazingira mwaka 2019 kwa *East Africa* kimekuwa cha kwanza. Ni kwa sababu, kisiwa hiki kina muwekezaji kwa hiyo, wamewekeza vizuri, wana wataalamu wa kutosha na wanahifadhi vizuri yale matumbawe kwa

kushirikiana na Serikali ya Zanzibar. Kwa hiyo, wamefikia kupata hiyo tuzo, lakini pia sio hiyo tu, wamepata tuzo nyingine kuwa Wanautalii wa kihifadhi bora ndani ya miji ya kidunia yote wapo ndani ya namba 10. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, lisiwe tu kwa Chumbe na ukienda Chumbe kweli ni kweli hata kama hujui kuogelea wewe unaweza ukavishwa *mask* na ukasaidiwa na ukaona hayo matumbawe na jinsi roho yako itakavyoburudika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nishauri, matumbawe kwa jina jingine yanaitwa *coral reef* jamani. Niishauri Serikali kama Wizara ya Uvuvi imeona pia ni mzigo wa kuhifadhi kuna Wizara ya Utalii na Maliasili hawa ndio makonkodi wa uhifadhi. Kwa nini wasii-*move* hii *marine park* wakawapelekea Wizara ya Utalii na utalii ukaweza kuhifadhi vizuri? lakini nje na kwamba, tunatumia kupata samaki haya matumbawe, lakini vilevile ni utalii wa kimazingira ambao wageni walio wengi wanapenda kufanya utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukifika pale kwenye Kisiwa cha Chumbe unafanya *booking* mwezi mmoja kabla ukiwa unataka kwenda kuyaona matumbawe. Kwa hiyo, unaona jinsi gani pato linaongezeka na wageni wanapenda kwa hiyo, nishauri Serikali kama wao mzigo umekuwa mzito wawape Wizara ya Utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, pia nishauri hapo waongeze juhudi ya kuwatafuta wataalamu zaidi kwa sababu, tunahitaji samaki na bado samaki hawatutoshi wanakwenda mbali kwa hiyo, imekuwa ni shida na hasa kwa hawa Ndugu zetu ambao wanafanya kazi za bahari kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kwenye mafunzo kwa wavuvi wetu, tuna wavuvi ambao wanaamka asubuhi majumbani wanakwenda baharini, na wanakwenda kwa sababu ya njaa ya maisha, lakini hawaendi kwa sababu hii kazi wanataaluma nayo. Mwingine anakwenda kwa sababu

ameirithi, labda babu yake alikuwa mvuvi, leo atamchukua apige kasia, kesho wataingia baharini kwa hiyo na yeye anakwenda kwa kufikiri babu hapa alikuwa akitupa ndoana ndio wanapatikana samaki, lakini sivyo dunia imebadilika. Mabadiliko ya tabia ya nchi yapo mengi, halikadhalika bahari imekuwa na kina kikubwa cha maji, matumbawe ndio kama hivyo yanapotea kipindi hicho kulikuwa hakuna uchafuzi wa mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa wavuvi wetu wanakwenda kuvua wanarudi hakuna. Na wanarudi maisha yanaendelea kuwa magumu sana, lakini la pili pia wakipatiwa mafunzo wavuvi wetu itawasaidia watakwenda sehemu salama za kuweza kuvua, lakini la mwisho kabisa wakipatiwa mafunzo watakwenda sehemu ambazo wana uhakika leo tukienda siku ya leo tunapokwenda sehemu kadhaa basi hatuwezi kukutwa na changamoto yoyote ya kiuvuvi, lakini na watasikia moyo watasema kwamba, leo kama fulani ni mvuvi na mwingine atakwenda. *(Makofi/Vigelele)*

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Asya.

MHE. ASYA MWADINI MOHAMED: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Asiya Mohamed, sikujua kama wewe mtoto wa mvuvi, inaelekea umekulia katika matumbawe huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa *Eng*. Stela Manyanya, sijui kama yupo? Asante endelea, siku hizi sijui unakaa upande gani?

MHE. *ENG.* STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Spika, niko hapa mwisho kabisa. Naomba upaone kabisa, nimesimama. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kukushukuru sana kwa kupata hii nafasi na kwa kweli, wavuvi wana matumaini sana na wewe, hasa baada ya kuona jinsi ambavyo umeweka msisitizo katika Wizara ya Kilimo na leo kwenye

Wizara hii ambazo ulisema kabisa zote ziangaliwe kiundani kwa sababu, zinawaajiri wananchi wengi sana wa Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuwapongeza Waziri wa Wizara hii pamoja na Naibu wake, lakini pia Makatibu Wakuu wote wa Mifugo na Uvuvi wanajitahidi kwa kadiri inavyowezekana pamoja na timu zao zote.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo niseme pia, nawashukuru sana Wizara hii kwa kusikiliza kilio cha wananchi wa Jimbo langu la Nyasa ambao sisi tunatumia takribani ukanda wa kilometa 150 za Ziwa Nyasa. Kwa muda mrefu zaidi ya miaka 20 tumekuwa tukilia, tunalalamika kwa ajili ya kutuzuwia kuvua samaki wanaoitwa vitui, samaki wadogo ambao hawakui, lakini mwaka jana mwezi wa nane tulipata hiyo ruhusa na wananchi sasa hivi wanafurahi na wanasomesha watoto wao. Kwa hiyo, nafurahi kwamba, wamekuwa wasikivu katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwaombe kufanya tafiti kabla ya kutoa makatazo kwa sababu, watu wameteseka zaidi ya miaka 20 kwa sababu tu, kulikuwa hakuna taarifa za kutosha. Hata sasa hivi tulivyoruhusiwa hatujapata majibu kwamba, sasa yule kitui anakua au hakui? Kwa hiyo, tunaomba wakati mwingine tusiwe tunafanya makatazo kabla ya kuwa na taarifa za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kukuunga mkono na kuendelea kusisitiza juu ya umuhimu wa halmashauri ambazo zimeanza hivi karibuni na kipato chake ni cha chini, ziko pembezoni na kipato chake ni cha chini. Sawa na ile Wilaya yangu ya Nyasa, kuweza kuangalia upya namna ya kuziendesha halmashauri hizo. Kwa sababu, bila kufanya hivyo hizo halmashauri badala ya kuwa ni sehemu nzuri ya kuwahudumia wananchi inakuwa ni sehemu ya kuwa na kikwazo, kuwa na manyanyaso, kuwa na mateso kwa wananchi kwa sababu, ya kutafuta fedha za kujiendeshea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halmashauri nyingine zilizopata uwezo mkubwa kimsingi tumezijenga wote kwa sababu, inapotokea tunakubaliana kwamba, safari hii tutajenga barabara ya mahali fulani au tutajenga *fly-over* mahali fulani au tutajenga miundombinu mahali fulani, ina maana wengine wote tunasubiri ili kuwezesha hizo halmashauri zipate mapato na hatimaye tufaidike wote. Sasa zinapoenda tu kuhudumia hizo halmashauri zenyewe ambazo zimeshapata uwezo na wengine wakaachwa wanateseka si sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema hayo? Katika uvuvi, Halmashauri kwa mfano ya Nyasa, inakusanya ada ya leseni 20,000/= eti ili uende ukaingie kuvua mle majini ulipe kwanza 20,000/= kwa maana hiyo, kila mvuvi anayeenda kuvua lazima afanye hivyo. Na vijana wetu wengine ambao wako kule na wengi ambao kwa kweli, hawajasoma sana kwa sababu, hata nikiuliza sasa hivi kwenye Wizara wavuvi wangapi wana cheti angalau cha uvuvi, sidhani kama nitapata jibu. Nikiuliza wavuvi wangapi wana *degree* hatutapata jibu kwa hiyo, ni wale tu ambao wamekuwa wajanja wa kuzaliwanao ndio wanaenda kuvua kule halafu unamwambia ili uingie majini leta kwanza 20,000/= wewe umemsaidia nini mpaka yeye kujua kwenda kuvua? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna tulichomsaidia, wanahangaika tu wenyewe na vimitumbwi hivyo. Na kimtumbwi hata kikawa kidogo kiasi gani nacho kinachajiwa *(Charge)* leseni ya 20,000/= wakati ni hatari huko anakoenda, anaenda tu ilimradi ameenda. Ndio maana nasema kwamba, hata suala la elimu kwa wavuvi ni muhimu sana, lakini huko hatujaenda.

Mheshimiwa Spika, unakuta kwamba, kimazoea karibu wataalam wengi tunaokuwa tunawaandaa, vyeo vyetu vingi, ni kwa ajili ya kwenda kufanya udhibiti sio wao wenyewe kwenda kufanya ile kazi ambayo inaendelea kama kazi ya uvuvi. Ndio maana mwanafunzi akimaliza anasema sasa kazi iko wapi? Kwa sababu umemfundisha kazi za

kudhibiti hukumfundisha kazi za yeye kwenda kufanya shughuli ile kwa mfano ya uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala hilo linaumiza sana na ndio maana hata mara ya mwisho niliulizia kuhusiana na *engine* za maboti, kwa nini watu wakopeshwe kwenye vikundi? Lazima walazimishwe kuwa kwenye vikundi? Kwa sababu, mtu akiwa peke yake anajisikia acha nifanye hii kazi kufa na kupona niweze kupata faida, lakini unamwambia kwamba, lazima uende kwenye kikundi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halikadhalika tumeona hapa kwa upande wa kilimo, angalao tunasema kwamba, tani moja mtu apite bila kulipa ushuru, lakini mvuvi akishakuwa hapo na vidagaa vyake vichache, visamaki vichache, basi utakuta kila kona inamdai alipe, kila kona alipe. Huyo mvuvi lini atabadilika akawa ni mvuvi mwenye uwezo? Ndio maana mara nyingi katika maeneo ya fukwe wavuvi wengi bado ni masikini, hawajawa na kipato cha kutosha kwa sababu wanabanwa kiasi kwamba, hawawezeshwi vizuri, lakini nina imani kubwa sana na Wizara hii, nina imani kwa sababu, nyie ni wasikivu. Hata siku ile nimeuliza tu swali naona Naibu mara kwa mara unakuja tuna-*share,* tunashauriana, basi naamini kwamba, tutaweza kwenda vizuri kwa hiyo, niwaombe sana Wizara.

Mheshimiwa Spika, sitachangia katika mambo ambayo ambayo ni ya *macro, macro level* hayo ya kisera, sheria, nini, hayo nendeninayo ninyi. Wananchi wangu wamenituma nije nilalamikie hayo madogomadogo wanayoishinayo kila siku. Nachangia kwenye *micro level* ili ukitatua hilo tatizo lao dogo wao wanaendelea kuishi wakati mikakati mikubwa ya kitaifa inaendelea. Kwa hiyo, sitachangia kuhusu meli ya uvuvi kwa sababu meli ya uvuvi tutapata nne zitakuwa Bahari ya Hindi, hilo ni jambo jema sana kwa sababu, tumelalamika kwa muda mrefu kwa nini watu tunafikia mpaka tunakamata watu kutoka nje wanakuja kutuvulia kwenye maji yetu, lakini sisi wenyewe tunashindwa kuvua, hapo mmepiga hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hilo kwa sababu, najua kwamba, tukipata mapato hayo mapato tena yataondoka asilimia chache kwenda kusaidia kule kwa wavuvi wangu wa Wilaya ya Nyasa. Kwa hiyo, niwaombe sana tufanye hivyo, lakini na hizo *ranch* ambazo tumeambiwa hapa, ndugu zangu hata nilikuwa kule Rukwa, *ranch* ilikuwepo pale eneo la Namanyere, Nkasi, ng'ombe wachache tu na hata yule mwekezaji tuliyemuweka pale eneo la Sumbawanga mjini bado na yeye ng'ombe 150 kwenye eneo la zaidi ya hekta elfu kumi kwa hiyo, lazima tuangalie vizuri namna gani tunawekeza, namna gani tunasaidia kuona kwamba, yale tunayowekeza yanakuwa yenye tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni pamoja na kuwasaidia hao wananchi tunaosema kwamba, wao sasa sekta binafsi ndio iwe *engine* katika kuwezesha masuala ya kilimo, masuala ya mifugo, masuala ya uvuvi. Nimegundua kitu kimoja, *private sector* huwa sisi ni rahisi kumhamasisha aingie katika kutenda, katika kuwa kwenye mfumo tunaouhitaji, lakini akishaingia humo akapata kikwazo sisi Serikali, sisi watunga sera, sio rahisi sana kumsaidia, yaani tunataka aanze aingie likishampata huko atajijua mwenyewe na saa nyingine tunamlaumu kwa nini anafanya hivyo? Ameshindwa yule bwana.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu kuna mfano Hai. Hivi kile kiwanda cha pale Sumbawanga cha Mzee Mzindakaya kwa nini kimeshindwa kufanya kazi mpaka leo? Tatizo ni nini? Kama alichukua mkopo na mkopo ulikuwa ni wa Serikali kwa nini sisi Serikali tusichukulie ule mkopo ni sawa na *asset* yetu tuliyoiwekeza pale tukazungumza na mzee yule ili kukiona kile kiwanda kirudi katika hali yake ya uzalishaji?

Mheshimiwa Spika, kiwanda ni kizuri sana na yule mzee aliwekeza, mimi ninavyoamini aliwekeza kwa hamu kwamba, ngoja nikawekeze Sumbawanga angalao nako na sisi tuwe na kiwanda. Yaani alikuwa na ile kiu ya mafanikio, alikuwa na ile sifa kwamba, Sumbawanga kuwe

na kiwanda. Matokeo yake wakati ule anawekeza barabara kutoka Sumbawanga mpaka Tunduma ilikuwa ni ya vumbi, mashimo matupu. Alikuwa anasafirisha hizo nyama mpaka Dar-es-Salaam, hakukuwa na Kiwanja cha Songwe kinachofanya kazi, kiwanda cha ndege.

Mheshimiwa Spika, matokeo yake magari yale na mkopo wake ameutumia wakati akiwa na mazingira magumu ya uwekezaji, ame-*fail.* Kwa nini sasa hatumnyanyui? Tunaona kwamba, kama lile ni suala la Mzindakaya na sio suala la nchi, hela aliyotumia ilikuwa ni zile ambazo zilikuwa zinasaidia wajasiriamali wadogo wavuke kwenda kwenda kwenye ujasiriamali wa kati. Kwa hiyo, nasema kwamba, pale tutakapomuona huyu *private sector* ni ndugu, huyu *private sector* anawekeza kwa manufaa ya nchi, anawekeza kama kichochezi cha uchumi wa nchi, hapo ndipo tutakapoenda vizuri, lakini tukimchukulia yeye ni mtu binafsi, amekwama kodi, huyu ana miaka mingapi sasa halipi, mwizi, matokeo yake inakuwa kwamba, wengi wanakimbia kwenda kwenye *private sector.*

Mheshimiwa Spika, sisi wenyewe sasa kama Serikali tunarudi, acha tuwekeze na sisi kuwekeza kwetu ni ngumu kwa sababu, kwanza ili tukubaliane kuwekeza au kufanya jambo fulani lazima tukae vikao. Na tukitoka kwenye vikao pengine iundwe kamati na kamati na yenyewe kutoa majibu saa nyingine inaogopa inasema nitaambiwa nimekula fedha. Matokeo yake yote tunatoa majibu ambayo yanakuwa yako kati kwa kati. Haya ikitoka hapo sasa fedha zinapatikana vipi, miaka mitatu hatujafanya. Niwaombe sana Ndugu zangu tuiunge mkono sekta binafsi ili tuweze kuendeleza eneo letu la mifugo na uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge mtaona muda wetu, tutaendelea kwenye Saa Kumi na Moja, lakini mjadala umekuwa mzuri na unaendelea vizuri. Tunaendelea kuwashukuru sana Wizara ya Mifugo, kama

tulivyosema, kwa kweli Bunge hili la Kumi na Mbili, tungependa tujikite sana katika kilimo, mifugo, uvuvi, hizi sekta ambazo zinabeba watu wengi sana tuone kama tunaweza tukawa na *contribution* na sisi katika eneo hilo kwa kiasi ambacho tutaweza kusukuma, kuongeza bajeti na kuhakikisha kuna tija katika sekta hizi. *(Makofi)*

Ni sekta ngumu, muda mrefu tumeongelea mambo hayo, lakini hebu tujaribu, mbona wenzetu wanaweza, tunatoa mifano hapa ya wenzetu Waganda, Wakenya, Wanyarwanda na kadhalika.

Mheshimiwa Waziri wa Mifugo hii migongano ya wafugaji na hifadhi, ile sheria sijui ilipita wapi sijui tulikuwa tumelala au ilikuwaje, ile kwamba ng'ombe wakiingia kwenye hifadhi wanataifishwa wote hapana, hapana. Hii kitu sijui ilikuwaje? *(Kicheko/Makofi)*

Kama ni ya miaka ya karibuni sijui nilikuwa nimesafiri sijui nilikuwa nimeenda wapi, sikumbuki vizuri lakini ilipoanza utekelezaji wake tumepiga kelele muda mrefu kweli kwamba hii sheria ni tatizo, ni sheria dhulumati kabisa kwa sababu ng'ombe hawana akili, yeye hajui mpaka upo wapi. Siku hizi ukitazama wengi wanaochunga mifugo ni watoto wadogo au vijana wadogo wakati mwingine wanacheza mpira ng'ombe zimeshaingia kwenye mpaka wa hifadhi sasa wanachukuliwa wote wanauzwa yaani ni ukatili lakini tembo haohao kila siku anajibu maswali Mheshimiwa Waziri hapa na Naibu Waziri wa Maliasili wanazurura, wanakula mazao ya watu, sasa basi iwe *equal opportunity* kwamba tembo nao wakiingia kwenye shamba la mtu basi mali yake. *(Kicheko/Makofi)*

Hii ya upande mmoja tu, iko haja ya Serikali kuangalia jambo hili, Serikali ni moja. Katika *amendments* ambazo zitakuja baadaye kidogo huko hili nalo tulitazame, tuwe na jicho ambalo linaangalia suala hili.

Suala la pili, takwimu zetu za mifugo nimetafuta sana katika hii hotuba ya leo sijaona kutakuwa na mahali lazima,

Mheshimiwa Olelekaita wewe umeona, hivi wamesema Tanzania tuna ng'ombe wangapi?

MHE. EDWARD O. KISAU: Mheshimiwa Spika, tuna ng'ombe milioni 33.6.

SPIKA: Milioni 33.6. Mimi takwimu hii inanipa shida siyo kweli nina wasiwasi, Katibu Mkuu Ole Gabriel, kama takwimu hizi mnazipata kwa Maafisa Mifugo wenu wale kila mmoja anakuletea takwimu kubwa kwa sababu za kimkakati ili kama kuna mafungu basi muwaletee mafungu ya kutosha, ipo haya tufuatilie tuwe na takwimu *realistic* tuna ng'ombe wangapi. Nasema hivyo kwa sababu katika maeneo mengi ya nchi yetu ng'ombe waliokuwepo enzi zile na leo wamepungua sana ukiacha haya maeneo ambayo watu wamehamia kama ya Lindi, Mtwara, Pwani kwa sababu ni *new areas* lakini *traditional areas* za ufugaji ng'ombe wamepungua sana kwa sababu sehemu za malisho zimepungua kilimo kime-*expand* sana.

Kwa hiyo, nina wasiwasi na hii *figure* inaweza ikatudanganya, tuifanyie kazi. Kwa vile sensa ya watu inakuja basi tungejitahidi tutafute *methodology* ya kuwa na sensa ya mifugo. Sensa ya wanyamapori huwa ni *estimates* lakini sensa ya mifugo ni *total count,* sasa *total count has to be exactly* wakati ile kule ni *estimates.*

Kitengo cha Hifadhi ya Bahari nimeona hapa ukurasa wa 86 hadi 87 mmesema kidogo na ameeleza Mheshimiwa Asia kuhusu *Marine Parks and Reserves,* Serikali ni moja, ukweli ni kwamba *Marine Parks and Reserve* ziende Maliasili *(TANAPA)*. Huo ndio ukweli wenyewe na tumesema miaka mingi jambo hili mnaling'ang'ania tu lakini ni eneo moja ambalo lina kipato kikubwa pia, lakini utalii wake utangazwaji wake lazima uende na utalii wa nchi kavu, *Terrestrial and Marine* lazima iende pamoja. Hamuwezi kwenda ninyi peke yenu na wale peke yao watalii *almost* ni walewale wanaamua waende Mikumi wakitoka huko waende *Marine Park* ya Mafia au ya Mtwara au mahali pengine. Hizi hifadhi tulizonazo sisi ni nzuri sana za hayo

matumbao aliyokuwa anayasema Mheshimiwa Asia hapa, ni nzuri sana, ni *one of the best* Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Hata Kenya ni *Wildlife and Marine Services, is one unit* sisi tunatenga kwa nini? Hatuna sababu tuwaweke pamoja ili mpango wa utalii katika nchi yetu uwe *planned* pamoja. Hata wale watu wa misitu wana maeneo ya misitu wayaweke kwenye *plan* za utalii tuwe na utalii ambao unatangazika kwa pamoja siyo kila mtu kivyake. Ndio maana hapa hata mlichoeleza kuhusu *Marine Park* yaani ni hamna kitu kwa sababu ni kitu kama vile kipo *separate* kidogo. Mifugo, Uvuvi na Utalii kama vile siyo *main domain* yenu, kwa hiyo, bora tu siku zijazo mkawapa wale wanaohusika itasaidia. *(Makofi)*

Alisema Mheshimiwa Magessa kwamba zianzishwe *Development Authority Livestock, Dairy* sijui na nini. Mheshimiwa Magessa yalishakuwepo Makampuni siku za nyuma, ilikuwepo ya *Dairy* ilikuwa inaitwa nafikiri *DAFCO*, iko wapi? *DAFCO* ilikuwa inashughulika na masuala ya ng'ombe wa maziwa leo iko wapi, ilishakufa. Sasa tukisema tuanzishe tena sijui itakuwa na tija gani ilishakufa hiyo kwa sababu hizo hizo.

Tukawa na shirika la kuku, mnaikumbuka Waheshimiwa? Wengi ni vijana ninyi hamuwezi kukumbuka, tulikuwa na ya kuku inaitwa *NAPOCO,* iko wapi? Zamani hizo hata kuku walikuwa ni Shirika la Umma, *dairy* nao walikuwa ni Shirika la Umma lakini hawa wote walikufa. Tulikuwa na *TAFICO* lakini ilikufa. Waziri sasa hivi anasema anataka kufufua *TAFICO* simzuii wala hatumshauri kinyume lakini ilikufa sasa lazima ujiulize kwa nini ilikufa. *(Kicheko/ Makofi)*

Ukitazama hata kwenye kitabu chake hii *TAFICO* inayofufuka anataka kufufua mashine za barafu, majengo ya zamani sababu ya tatu kutafuta *private people* washirikiane kufanya kazi za *TAFICO.* Sijui labda wana mambo ya msingi zaidi atatueleza mwishoni.

Sasa binamu yao hawa wote *NAPOCO, DAFCO, TAFICO* ni *NARCO,* wenzie walishakufa siku nyingi, walishashindwa kabisa huyu yupo *ICU* miaka yote. Sisi wengine ni wadau kwa miaka mingi tumekaa tumenyamaza zimesomwa hotuba humu tukisema aah ngoja tusubiri tuone lakini tumefika mahali ambapo ukweli lazima usemwe *NARCO* hawezi kufufuka, hawezi. *(Makofi/Kicheko)*

Amewekwa pale Mzee Kimiti ni Mzee wa heshima lakini wanataka amalizie kwa sifa mbaya tu. Mngemtafutia Mzee Kimiti Bodi ya maana sio kumpa Bodi ya *NARCO,* mnataka kuharibu sifa yake nzuri ya miaka yote, ni ngumu sana, huwezi!

Mimi nimezaliwa pembeni ya Ranchi ya Kongwa najua ranchi ni kitu gani, ile siyo ranchi. Mkitaka tuibadilishe ile iwe Hifadhi ya Wanyamapori siyo ranchi kabisa, ranchi ni kitu kingine. Sasa ile ndiyo *the best* sasa hizo nyingine? Katika ng'ombe 16,000 walionao hawa karibu asilimia 90 ndiyo Ranchi ya Kongwa, nao yaani kwanza si mnapita Kongwa pale barabarani mliona ng'ombe? Mnapita, mnarudi miaka nenda rudi nyie mliwahi kuona ng'ombe pale? Wapo kidogo kidogo huko pembeni lakini hata Serikali inunue iende ijaze pale siyo kama Serikali inashindwa kununua na kujaza ng'ombe pale, hata mjaze hamtafanikiwa, Serikali kuchunga ng'ombe sio kazi yake, achieni wenye kazi yao. *(Makofi/ Kicheko)*

Sasa hivi mmetoa vitalu ni jambo jema kidogo pembeni pembeni katika baadhi ya ranchi lakini mnatoa kitalu kwa mwaka mmoja, hivi nani huwa anawekeza kwenye *contract* ya mwaka mmoja?

WABUNGE FULANI: Hamna.

SPIKA: Nani anawekeza kwenye ardhi ambayo haina hati, *you don't own* ardhi ni ya Serikali, wewe unawekeza akili yako iko sawasawa, haiwezekani! Lazima ufike mahali wakupe ardhi, Mheshimiwa Lukuvi yupo pale wakishaamua anawapatia watu ardhi watu wanaweka ng'ombe wanafanya maendeleo na tutayaona maendeleo na

wapewe Watanzania wala siyo mtu mwingine wa nje. Hiyo ndiyo fikra ambayo itatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri tembeleeni Uganda na Kenya mkatafute *NARCO* kama mtaikuta, hamtaikuta ni watu binafsi. Ndiyo maendeleo aliyokuwa anasema Mheshimiwa Mbunge wa Muleba Kaskazini ni watu wamewekeza *including President* Museveni mwenyewe ni *ranches***,** Kenya wana *ranches* za binafsi na *group ranches* na nimeshazitembelea. Pia Uganda, Botswana na Namibia nimefika nimeangalia ranchi zinavyokuwa na uendeshaji wake. Hizo zote za Namibia hakuna ya Serikali, wapi ipo ya Serikali, Botswana ni ya Serikali? Watu katika umoja wao wachache wachache katika ushirika au binafsi ndiyo wanachunga ng'ombe na ni ng'ombe wazuri kweli kweli. *(Makofi)*

Wewe una ranchi namba moja nchini haina fensi hata ya mita moja, hakuna popote pale. Ng'ombe wanaingia na kutoka sasa magonjwa ya mifugo na nini, yaani hiyo ranchi gani, hii siyo ranchi na hatuwezi ku-*fence ranches* zetu tulizonazo kwa bajeti hii tuliyonayo. Hatuwezi huo ndio ukweli lakini mkibisha nyie twendeni tutafika hapa mwaka 2025 hizo ranchi zitakuwa zipo hivyo hivyo hamuwezi kutoka pale mlipo.

Siyo kosa lenu siwalaumu ni kwamba huwezi ku-*run* hivi vitu katika utaratibu wa kiserikali, Serikali inakuwa na kitengo tu kwenye Wizara kule kinachoangalia masuala ya mifugo yote, ina mnaweza kubakiza maeneo machache kwa ajli ya *extension and research* na mambo ya namna hiyo kwa sababu madhumuni makubwa ya ranchi sio Serikali mfuge ng'ombe, madhumuni makubwa ya ranchi pamoja na kwamba itakuwa inafanya biashara iwezeshe wananchi na wafugaji wengine wote wawe na mifugo bora waweze kuiga wapate ng'ombe kama wale walionao, nitafutieni ni ranchi gani imeweza kufanya hilo? Bado Wagogo wanachunga ng'ombe zao wanavyochunga wenyewe na *breed* zao na nyie mko wenyewe.

Tangu mwaka 1967 tulipotaifisha maeneo haya mpaka leo ni miaka mingapi? Hivi hata kama ni *experiment* imeanza mwaka 1967 mpaka leo 2021 haijatoa majibu, hiyo ni *PhD* ya aina gani? Si majibu tayari kwamba hiki kitu *does not work. (Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, Wizara muangalie ili kwa nia njema kabisa tufike mahali kabla sisi watu wa Kongwa hatujaja moto sasa tudai ardhi yetu bora Serikali iangalie namna gani bora zaidi ya kufanya kwenye maeneo haya. Maeneo haya yamekuwa mzigo tu katikati ya vijiji mnatusababishia *under development* bila sababu. Kagera huko ni migogoro kila kukicha na hali hiyo ipo kila mahali.

Hata hivyo, tunawapongeza kwa kazi nzuri sana. Wizara kama hii ya Mifugo ni ngumu sana na hata Uvuvi yenyewe ni maeneo magumu kweli na matatizo ya wafugaji ni mengi sana tunahitaji tuwaongezee fedha kwenye majosho, dawa za mifugo na kuwasaidia wafugaji kadri inavyowezekana. Eneo hili la mifugo linaweza likatuletea fedha nyingi sana za kigeni, kwa hiyo, ni eneo ambalo tunawa-*support* sana. *(Makofi)*

Baada ya maelezo hayo, tutaendelea saa kumi na moja naomba nisitishe shughuli za Bunge hadi saa hizo. *(Makofi)*

(Saa 7.12 Mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)

Hapa Mwenyekiti (Mheshimiwa Najma M. Giga) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa tukae. Tunaendelea na majadiliano tutaanza na Mheshimiwa Nicodemas H. Maganga na baadaye Mheshimiwa Muharam na Mheshimiwa Omar Issa wajiandae.

MHE. NICODEMAS H. MAGANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na fursa hii niweze

kuchangia Sekta hii ya Uvuvi na Mifugo. Awali ya yote napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi niweze kuweka mawazo yangu kwenye hii Sekta ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka mwaka 2020 tulikuwa kwenye uchaguzi. Miongoni mwa vitu tulivyokuwa tukitembea navyo majukwaani, ukisoma ukurasa wa 52 ilani yetu ambayo ilikuwa andiko letu kuu kuweza kuwaomba ridhaa wananchi ili tuweze kuwaongoza katika Chama cha Mapinduzi, tuliahidi kwamba tutawasaidia wafugaji pamoja na wavuvi. Hata hivyo, kila kinachoendelea sasa hivi kwenye hili Taifa, leo ni mwezi wa Saba sasa, unaona kabisa kwamba bado hatujatekeleza huu ukurasa wa 52. Kwa hiyo, namwomba kaka yangu Mheshimiwa Mashimba pamoja na Mheshimiwa Ulega, kwa kuwa wao ndio wasimamizi wakuu wa Wizara hii, kwanza sheria zilizotungwa za hiyo sekta ni chonganishi, naweza nikasema hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kwamba hata Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano tulimchukia sana Kanda ya Ziwa wakati akiwa sekta hiyo, lakini ukweli ni kwamba baada ya kukua, nami kuingia kwenye michakato hii ya kisiasa na kuona kabisa sheria ziliwekwa vibaya; kwa maana hiyo mimi nikushauri Mheshimiwa Mashimba, ongea na Mheshimiwa Rais, kuna vipengele muhimu vya kuweza kufanyiwa marekebisho ili uweze kurudi hata Bungeni mwaka 2025, lazima sheria zibadilishwe, maana wafugaji kwenye hili Taifa wamekuwa kama wakimbizi. Wewe ni Msukuma mwenzangu tunaongea lugha moja na tumetoka sehemu moja, lakini kiukweli yaani ukisimamia hizo sheria lazima watu watakuchukia hata kama ni mtoto mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia wafugaji wanavyoteseka kwenye mapori hasa kwenye Jimbo langu la Mbogwe, kuna utitiri wa mapori, nilishaongea na Mheshimiwa Waziri tukiwa wawili na alisema atanisaidia, sasa leo nitashika shilingi ili anihakikishie kwamba Mbogwe katika bajeti yake atanisaidia mabwawa mangapi na

majosho mangapi ili niweze kuachilia kushika shilingi? Waheshimiwa Wabunge naomba mniunge mkono kwenye hili kama tutashindwana na kaka yangu ili kusudi tupinge, tusiwe tunapitisha tu kila bajeti bila hata kujua kinachoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kuzungumzia wafugaji wa Tanzania. Lazima tukubaliane kwamba; unajua katika maisha huwa kuna Kiswahili kinasema tunaishi kwa kutegemeana. Tukirudi kwenye historia ya nyuma, miaka ya nyuma huko, wakati wa utawala wa Mwinyi, ikumbukwe kwamba Wasukuma *professional* yetu sisi ni wafugaji. Ukiangalia Wamasai miaka ile tulikuwa tunagombana nao maporini, kazi yao ilikuwa kuja kutuibia ng'ombe ili nao waende wakafuge. Sasa hivi ukiangalia Wasukuma wengi wameacha biashara ya kufuga ng'ombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia Taifa tuna-*force* kuingia kwenye utajiri; na hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano alizungumzia kwamba hata Wabunge tutafute ubilionea. Kwa maana hiyo mimi kama Msukuma sasa, sheria za ufugaji zikirekebishwa vizuri, mimi nitarudi kwenye *professional* yangu. Hakuna haja ya kuhangaika na *network,* wala haya mamitandao sijui mara *M-Pesa* rusha huku, fanya hivi; maana sisi Wasukuma *professional* yetu ni wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma hata maandiko ya Neno la Mungu kulikuwa na Mfalme Daudi, alikuwa ni mchunga ng'ombe; hakuwa hata na Malaria maana alikuwa anakunywa maziwa ya ng'ombe. Hata mimi wakati bado sijaja mjini nilikuwa siugui *typhoid,* maana maziwa ya ng'ombe yale wale waliosoma sayansi wanaweza wakakuelezea ni nini maana ya kuwa na faida ya ng'ombe. Leo yanapokuja hata maziwa haya ya kiwandani, nakuwa sipati picha maana kila mara magonjwa yanazidi kuwa mengi na mpaka tunataka kuingia kwenye chanjo ambazo hazina sababu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kutokana na kuwadharau wafugaji na sisi Wasukuma tunaonekana washamba kwenye Taifa hili. Ni kweli sisi Wasukuma tuna sifa moja, yaani mkiingia pori moja ni kufyeka kwa kwenda mbele ili kusudi kujaribu kujitandanua kimaisha. Kwa kuwa sasa Chama cha Mapinduzi kiliahidi kwamba kwanza kwenye hizi hifadhi zetu tutapewa maeneo, tupewe sasa maeneo. Huu mwaka ni wa kwanza, bado miaka minne tuingie kwenye uchaguzi mwingine, tusiongee *story*. Binadamu sisi huwa tunasahau, yawezekana kabisa shida tuliyoipata kwenye kampeni watu wanaweza kuwa wameshasahau, lakini nataka niwahakikishie, tusipotimiza mambo haya, tutapata taabu sana mwaka 2025. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee upande wa uvuvi. Wananchi wangu wengi wako Ziwa Victoria. Nilishawahi kuongea na Mheshimiwa Mashimba na leo niongee naye nikiwa kwenye vyombo. Wavuvi wanapata taabu sana. Kuna mageti; ukitokea pale tulipokuwa na wewe Mheshimiwa Waziri na Rais wa Zanzibar, tulienda kwenye mwalo mmoja wa Mganza, ulisikia shida za wafanyabiashara wale na walikueleza changamoto wanazokabiliana nazo. Yamewekwa mageti mle njiani ya kipigaji. Wanahangaika wafanyabiashara wa dagaa, wafanyabiashara wa samaki wanafanyabiashara kwa shida, wanasumbuliwa na watu hawa wa misitu. Serikali ni moja lakini inakuwa kana kwamba Serikali ziko mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Mashimba, kaka yangu, Wizara hiyo kwa kuwa naye ameipenda na Rais wa Awamu ya Sita amemwamini, itendee haki hiyo nafasi. Kumbuka kwamba kuna mwenzio ambaye hata kwenye Ubunge wake amepita kwa wakati mgumu sana, nikimsikia sasa hivi *speech* zake kidogo saa hivi anatoa hotuba ambazo zina urafiki na wananchi kule anakotokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia wavuvi wengi wanakufa wakiwa wanakimbizana na *operation* za mle ziwani. Mwaka 2016 kuna marafiki zangu watatu walikufa

wakiwa wanafukuzwa na watu wa maliasili kwenye Kisiwa cha Rubondo walikuwa wanakaa Chakazimbwe. Kuna Visiwa vya Chakazimbwe, Mrumo, Iramba na Mjuno; Mheshimiwa Mashimba ukifanya ziara huko ukaongea na wale watu, utapata ukweli wangu, tarehe ya leo 27 nakushauri pamoja na Naibu wako mfanye ziara kwenye Visiwa vya Yozu, Nyamango humo, mkaongee nao. Wale wa *professional* yenu wawaambie na ili mje sasa siku moja mlete hata Muswada wa kufanya marekebisho ili kusudi nao waishi vizuri na waweze kuendelea vizuri na uvuvi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwenye Kamati ya Matumizi nishike shilingi ili kaka yangu anihakikishie bajeti yake atanisaidiaje kwenye Jimbo langu, tusiongee tu maneno maneno hapa halafu mwisho wa siku tusiweze kufanikiwa chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda jambo lingine tena niliweke sawa hapa. Namshukuru Mungu jana mchango wangu mwenyewe nilichangia na niliongea maneno mengi; namshukuru Mheshimiwa Lukuvi ameniahidi vitu vingi atanisaidia. Tukiangalia hii Sekta ya Uvuvi, tukaangalia na hii sekta ambayo tuliichangia jana, ni vitu viwili vinakaribiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, jana kwa kuwa Mheshimiwa Lukuvi alisema atakuja Mbogwe, ni vyema sasa tuje tupitie maeneo na mazingira ya Mbogwe yale ili kusudi tuangalie hata tunapokuja kubadilisha sheria mkaona na usumbufu ule wananchi wa Mbogwe wanaoupata kwenye yale mapori utakuwa umenisaidia sana kaka yangu. Sijui unanisikia Mheshimiwa Mashimba. Nakuona kama unanisikia, lakini naomba andika hiyo halafu uje uitolee maelezo kwenye kuhitimisha hotuba yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nikushukuru wewe, leo ni mara yangu ya tisa sasa kuchangia hapa. Mwanzoni niliongea vitu vingi na nikaiomba Serikali ya Awamu ya Tano iweze kutusaidia na isitubague sisi watu wenye elimu kidogo, lakini karama zetu zinakubali na kuweza

kufanya vitu vikubwa kwenye hili Taifa, naomba nawe maneno yangu uyasikilize. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoongelea neno viwanda, ni vyema na sisi tujitegemee na tujitambue. Tusitegemee tu kila kitu; nimemsikiliza mchangiaji wa kwanza anajaribu kutolea mifano Botswana, wapi na wapi; ni vyema tujiamini, kwa sasa tulipo hapa, tuko sawa sawa kabisa. Tukiwa tunachukua mifano Ulaya tu, kila kitu Ulaya, hatutaenda popote pale. Sisi tuliumbwa na Mungu, tuliwekwa kwenye ardhi ya Tanzania, Mungu alituamini, tena akatupa Taifa lenye makabila mengi na Taifa letu halijapata vita hata ya kikabila. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema kila mmoja sasa akithaminiwa; msomi amthamini ambaye hajasoma. Huyu ambaye hakusoma, amthamini msomi. Tunaishi kwa kutegemeana, maana hata sisi ambao hatujasoma hatuwezi kuingia kufanya *operation* kwenye hospitali yoyote, lakini tumekuwa na shida sasa hivi humu Bungeni, kumekuwa na mvutano fulani na kuchukiana sisi kwa sisi; ma-*professor* na wale wasio ma-*professor. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Wabunge, sote humu tuna akili timamu na tumevuka mishale mingi kufika kuingia kwenye jengo hili, tuheshimiane kuanzia leo. Naomba kwa kauli mniunge mkono, hiyo vita isiendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ahsante katika jina la Yesu.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Maganga. Naamini Mheshimiwa Waziri amekusikia vizuri na ninaamini ataweza kukusaidia vizuri.

MHE. NICODEMAS H. MAGANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaunga mkono akinifafanulia, maana nashika shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge na baadaye Mheshimiwa Omar Issa na Mheshimiwa Kavenjuru ajiandae. Kwa kuwa wachangiaji tunao wengi sana, tunaomba wote wachangie kwa dakika saba saba, lakini tutagonga kengele mara moja tu. Kwa hiyo, kengele ikilia mara moja, muda wako wa dakika saba umekwisha. Tuendelee.

Mheshimiwa Muharami, hayupo. Tuendelee na Mheshimiwa Omar Issa Kombo na baadaye Mheshimiwa Kavinjuru Felix ajiandae.

MHE. OMAR ISSA KOMBO: *Bismillah Rahman Rahim.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia fursa ya kuchangia nami katika hotuba hii ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ambayo ni muhimu sana kwa maslahi ya wananchi wetu, hususan wanyonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kukushukuru wewe, vile vile nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, pamoja na Naibu Waziri na baadhi ya watendaji wa Wizara hii. Kwa nini niseme baadhi ya watendaji, nitatoa ufafanuzi mbeleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wakati tunapochangia sekta tatu, lazima tuoneshe hisia za ukaribu zaidi; Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Kwa sababu sekta hizi zinawagusa asilimia kubwa sana ya Watanzania na hususan wenye kipato cha chini ambapo wengi wa Wabunge tunatoka katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitagusia kwenye Sekta ya Uvuvi. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kweli ameanza vizuri. Kwa nini ameanza vizuri, amekuwa tofauti na wale wengine ambao wanawachukulia wavuvi kama maadui zao. Baadhi ya wengine waliopita tuliwaona, walikuwa wanahisi kwamba kutekeleza majukumu yao ni kuwanyanyasa, kuwaadhibu wavuvi wetu, jambo ambalo

siyo sahihi. Mheshimiwa Waziri huyu amekuwa msaada mkubwa sana kwa wavuvi wetu, Mheshimiwa Waziri hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hongera hizo, lakini bado kuna changamoto kwenye Sekta hii ya Uvuvi na tunapozungumzia changamoto hizi, ni kwenye suala la kanuni. Kwa kweli kanuni ambazo zimetungwa hivi karibuni haziko rafiki na wala haziwasaidii wavuvi wetu. Kwa mfano, kuna kanuni ambayo inakwenda kuzuia uvuvi wa *ring net* kwamba uvuvi huu unaharibu mazingira. Nataka kusema kwamba siyo kweli kwamba uvuvi wa *ring net* unaharibu mazingira. Ila inaonesha kwamba kuna shirinikizo fulani, kuna watu ambao wanajaribu kuwaonea wavuvi kwa kisingizio cha uvuvi haramu au cha kuharibu mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tukubaliane kwamba shughuli zote za binadamu kwa njia moja ama nyingine zinaharibu mazingira. Tukizungumzia kilimo, kinaharibu mazingira, tukizungumzia uchimbaji madini, unaharibu mazingira, viwanda vinaharibu mazingira, utalii unaharibu mazingira, shughuli zote za binadamu zinaharibu mazingira; lakini hatuwezi kutumia kigezo hiki kuwadhalilisha wananchi. Licha ya kwamba shughuli za binadamu zinaharibu mazingira, lakini lazima maisha ya binadamu yaendelee. Ni lazima binadamu afanye shughuli zake za kujipatia kipato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kutoa ufafanuzi atueleze ni lini kanuni hii inakwenda kufanyiwa mabadiliko? Vinginevyo hapa patachimbika kwa sababu wavuvi wetu wanapata dhiki kubwa sana kutokana na kanuni hii. Lazima niseme kwamba tunapotunga kanuni au sheria lazima tuzingatie utekelezaji wa sheria hizo. Hivi unatunga kanuni ya *ring net* kwamba wavuvi wakavue maji mita 50, wapi na wapi? Ukiangalia wavuvi zana wanazotumia ni duni, au tunataka tupate mayatima wengi na wajane wengi? Kwa sababu mvuvi anapokwenda maji mita 50 ni kutafuta kifo tu, hakuna kingine, kutokana na zana wanazotumia, ni duni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ukisema labda *ring net* wafanye uvuvi wa usiku, haiwezekani kwa sababu samaki wengi wanapatikana muda wa mchana, usiku huwezi kumvua samaki kama aina ya jodari, lazima uvue wakati wa mchana. Vilevile wakati wa usiku unapomvua dagaa, mpaka asubuhi tayari ashaharibika; na ukizingatia *ring net* ndiyo uvuvi ambao unabeba wavuvi wengi. Boti moja ya uvuvi wa *ring net* wa mchana inachukua wavuvi kati ya 40 mpaka 100, lakini uvuvi wa usiku unachukua wavuvi 10 mwisho wavuvi 15. Hebu tuangalieni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi, tunapozungumzia Sekta ya Uvuvi, wananchi walio wengi wamejiajiri katika sekta hii. Mfano ulio hai, hebu tuangalieni soko la *ferry,* umati ambao uko pale; wote wale wanategemea Sekta ya Uvuvi. Nenda Mafia ukaangalie akina mama wanaojiajiri kwenye Sekta ya Uvuvi. Tunaweza kuiangalia Sekta ya Uvuvi kwa kuangalia mchango kwenye pato la Taifa, hii haiko sahihi. Pamoja na mchango ulioko kwenye pato la Taifa lakini Sekta hii ina tija kubwa kwa maslahi ya Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikupe mifano iliyo hai. Nenda katika Soko la *Ferry,* pale pana akina mama ntilie wanategemea Sekta ya Uvuvi, pana bodaboda wanategemea hii, pana daladala, hata *Ferry* inayovusha, abiria wengi wanakwenda kwenye Soko la *Ferry* kutokana na Sekta ya Uvuvi. Hata ukienda Kisiwa cha Mafia, akina mama walio wengi au wananchi walio wengi wa Mafia wanategemea Sekta ya Uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tujiulize tunapokwenda kuzuia uvuvi wa *ring net,* tunategemea wananchi wetu waishi katika maisha gani? Lazima tuzingatie. Kanuni hizi, nikwambie ukweli, inaonekana kuna shinikizo fulani. Watendaji wako Mheshimiwa Waziri wa ngazi za juu mara nyingi wanatuambia kwamba umeunda Tume ya kwenda kufanya utafiti, nakupongeza sana lakini katika Tume ikija kufanya utafiti inaonekana kuna vitu vitatu. (a) Tume hii haina elimu ya kutosha juu ya uvuvi huo. (b) kama siyo hivyo, Tume

hii haishirikishi wadau ipasavyo; na kama siyo hivyo, Tume hii haielezi ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi wa *ring net* hauvui samaki walio chini, wanavua samaki ambao wako juu. Isitoshe, uvuvi wa bahati kuu kama Bahari ya Hindi, hatuwezi kuzungumzia ufugaji wa samaki kama unayefuga samaki kwenye bwawa. Kwa sababu samaki wanatembea masafa ya mbali. Unaweza kufuga samaki Tanzania akaenda kuliwa Kenya. Sasa lazima tuangalie vizuri tunavyozungumzia masuala ya ufugaji wa samaki kwenye bahari kama Bahari ya Hindi.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Omar Issa Kombo kwa mchango mzuri.

MHE. OMAR ISSA KOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, naunga mkono hoja. Ingawa muda umekuwa mfupi, tutakutana na Waziri tuongee vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Kavejuru Felix na baadaye Mheshimiwa Nashon William ajiandae.

MHE. KAVEJURU E. FELIX: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na namshukuru Mungu kwa mara ya kwanza kusimama ndani ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie nafasi ya pekee kwanza kuwashukuru wananchi wapiga kura wote walionipigia kura nyingi kule kwenye Jimbo la Buhigwe. Ninawashukuru sana na ninawaahidi sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi ya pekee kutoka kwenye moyo wangu wa shukrani kuwashukuru

Waheshimiwa Wabunge wote waliotoka humu wakaja kunipambania. Ushindi wangu nilioupata ni wa sisi sote, ni wa Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru Chama changu Cha Mapinduzi, Kamati Kuu ya Chama Cha Mapinduzi iliyoniteua na hatimaye nikapeperusha bendera ya Chama Cha Mapinduzi na leo niko hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo, ninaomba sasa niende kwenye hoja mama. Kwenye wilaya yangu naenda kujikita kwenye suala la minada ya mifugo. Wizara ya Mifugo tunashukuru sana imetengeneza, imekarabati, imejenga mnada ambao unasimamiwa na wizara. Lakini huo mnada mpaka sasa hivi una zaidi ya miezi saba ulikwishakamilika, mkandarasi amekwishawaomba ili awakabidhi Wizara nao hawajafika. Ninaomba Wizara ije ifungue ili huo mnada ufanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wilaya ninayotoka iko mpakani, tunayo changamoto inayotokana na tozo ambalo inaonekana ni kubwa kwa wafanyabiashara wa mifugo. Ng'ombe mmoja anayesafirishwa nje na ni wafanyabiashara wadogo wadogo tu, tozo yake, ada yake ni 25,000. Hiyo imesababisha wafanyabiashara wa nchi jirani ambayo ni Burundi pale, hawaji kwenye minada yetu. Naomba Wizara ipunguze tozo hiyo ili waweze kuvuka na wanunue mifugo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao mnada wa halmashauri ambao uko mbali kwenye Tarafa ya Myama. Kwenye Tarafa ya Manyovu tuna ng'ombe wengi sana. Mifugo hio wanaenda kiholela, wanatoroshwa, hatuna mnada. Ninaomba tufungue mnada mwingine wa Halmashauri katika Kata ya Kibande ambayo ni karibu kabisa na iko mpakani mwa Burundi, ili Warundi waweze kuvuka wenyewe na wakishavuka wanunue wale ng'ombe na biashara nyingine zitaamka pale pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudi hapo hapo kwenye Idara ya Mifugo ninayo Tarafa ya Myama, ina kata saba. Kuna kata moja inaitwa Kata ya Kajana, ina mifugo wengi; hatuna josho. Naomba josho lijengwe pale. Nikirudi kwenye minada, tulikuwa na Afisa Minada mmoja lakini mpaka ninaposimama na kuzungumza hapa mbele ya Bunge lako Tukufu amekwishahamishiwa Pugu. Naomba mtuletee Afisa Minada ili aendeshe huo mnada ambao mmetujengea ulete tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea kuchangia hapo kwenye mifugo, tuna matatizo na tuna upungufu wa Maafisa Ugani. Hata wale waliopo hawana vitendea kazi. Tunaomba Wizara yako iwaone.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ni mara ya kwanza, naamini Wabunge wenzangu mtaendelea kunilea. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Felix. Naamini kabisa wananchi wa Buhigwe watakuwa wamefarijika kusikia kwa mara ya kwanza umeanza kufanya kazi vizuri sana katika Bunge. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Nashon William, Mheshimiwa Eric James na baadaye Mheshimiwa Furaha Matondo ajiandae.

MHE. NASHON W. BIDYANGUZE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia kwenye Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nimpongeze Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayofanya. Lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa jinsi alivyoweza kutatua mgogoro wa wavuvi katika Mkoa wa Kigoma kwa maana ya Majimbo matatu; Kigoma Kaskazini, Kigoma Mjini na Kigoma Kusini ambalo ndilo jimbo langu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli ametusaidia sana pale ambapo walikuja wale wavuvi na wakaja na agenda zao zilizosababisha Mheshimiwa Waziri kifuta baadhi ya kanuni ambazo hazikuwa rafiki. Mheshimiwa Waziri, nakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niipongeze Serikali kupitia Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa jinsi ambavyo mpango wa Serikali uliopo ni wa kuhakikisha kwamba inanunua meli za uvuvi katika Bahari Kuu ili nasi tuweze kufaidi samaki wale ambao watatusababishia kuongeza Pato la Taifa katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli tunasikitika sana wananchi tunapoona kwamba tunalo ziwa kuu lakini tumekuwa hatupati faida itokanayo na samaki wale katika ziwa kuu. Lakini inaonekana mpango wa Serikali ni kwamba sasa itanunua meli nne ambazo zitahakikisha kwamba zinavua samaki ambao watasababisha tupate mapato makubwa kutoka kwenye chanzo hiki cha mapato ambacho tumekiacha kwa muda mrefu. Hii naomba niwapongeze Serikali kupitia kwa Mheshimiwa Waziri kwa hii ambayo itakwenda kuongeza uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, alivyomaliza kutatua ule mgogoro katika zile kanuni kwenye jimbo langu pamoja na majimbo ya wenzangu wa Kigoma ambayo nafahamu kabisa utatuzi ule alikuwa anaendana na wavuvi wale wa Ziwa Tanganyika lakini katika Mkoa ule wa Katavi pamoja na Wilaya ile ya Tanganyika, na wenyewe walikuwemo katika ule ujumbe. Nina imani kwamba ukanda wote ule tatizo sasa hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo moja; naomba uige mfano wa Wizara ya Madini ambayo ina wachimbaji wadogo. Lakini wachimbaji wadogo wale wamewekewa utaratibu ambao Serikali imewatambulisha kwenye mabenki na sasa wanakopesheka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi wetu katika Ziwa Tanganyika wanatumia vifaa ambavyo ni duni. Na ndiyo maana wakati mwingine samaki hawawezi kupatikana vizuri kwa sababu hakuna utaalam wa kisasa. Naomba katika eneo hili wavuvi wa Ziwa Tanganyika, pamoja na maeneo mengine waweze kukopesheka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atengeneze utaratibu kama ambavyo Wizara ile ya Madini imeweza kufika mahali sasa wachimbaji wadogo wanaweza kukopesheka. Hii sekta ya uvuvi pia ni sekta muhimu. Wakopesheke. Pia Wizara iweke utaratibu namna ambavyo baada ya kupata samaki wale waweze kuhifadhika kwenye majokofu ili waweze kuuzwa hata baadaye, lakini samaki wanapopatikana bado wabichi wanalazimika kuwauza harakaharaka ili wasiweze kuoza. Sasa wanapoteza fedha kwa sababu hawawezi kuweka, lakini kama wataweka maana yake watauza wakati ambao soko lipo. Hili naomba Mheshimiwa Waziri ulichukue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwenye eneo la ufugaji wa ng'ombe kwa maana ya mifugo. Amezungumza mchangiaji mwenzangu kwamba Wasukuma ndio watu ambao kwa kweli wanajishirikisha na mifugo. Jimbo langu lina vijiji 61; wote wanaofuga ng'ombe pale wao wanaochunga ng'ombe kule katika vijiji vile ni Wasukuma, sisi Waha hatufugi ng'ombe. Kama vile Mheshimiwa Spika alivyokuwa akizungumza kwamba Serikali haifugi ng'ombe na sisi Waha hatufugi ng'ombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba, ng'ombe wale ni wengi. Katika wilaya yangu ile, kwenye jimbo langu, tuna ng'ombe takribani 200,000 na hawa ng'ombe wamezagaa. Hakuna mpango wowote lakini wanasumbua wananchi ambao wanajishirikisha na kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika eneo hili naomba nimshukuru Waziri kwa sababu alifika jimboni kwangu akaenda kutatua mgogoro ambao kwa kweli ulikuwa ni mkubwa katika eneo moja, ingawaje maeneo mengine

hakufika, pale ambapo aliruhusu kwamba kwenye eneo ambapo alitoa hekta 6,000 ziweze kutumika kwa wafugaji. Hilo ni jambo ambalo wananchi wamelifurahia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona bado kuna eneo lingine, kwa mfano kata nane za ukanda wa maji, bado hukufika na hukutoa maelekezo yoyote, na huko ndiko kwenye matatizo ya kuingiliana wale wafugaji wanapoingia kwenye maeneo ya wakulima. Kesi ziko nyingi mno na ng'ombe wakishaingia kwenye shamba, hata ungeenda mahakamani, kesi inaamuliwa kwamba ng'ombe ndio wamekula; sasa unashitakije ng'ombe? Inakuwa ni ngumu sana. Kwa hiyo, naomba katika eneo hilo Wizara iweze kuja na mpango wa kuhakikisha kwamba hizi ranchi ambazo zipo ambazo hazitumiki basi ziweze kutumika sasa katika kipindi hiki ambacho hazitumiki Wizara iweze kuwapa wananchi waendelee kuzitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tunajinasibu kwamba sisi nchi yetu ni nchi ya tatu katika mifugo. Sasa Serikali katika eneo hili imefanyaje? Imewatengea maeneo gani? Unakuta ni migogoro. Kwenye maeneo ya wakulima kuna migogoro ya wakulima, lakini kwenye maeneo ya ranchi wakati mwingine pia wakiingia kwenye *ranch* kuna matatizo tena katika maeneo hayo. Sasa nadhani Wizara ingekuja na mpango ikatenga maeneo kwa ajili ya hawa ambao nao ni wafugaji na ni eneo kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimalizie kwa kusema kuwa eneo hili Serikali bado haijawekeza. Kwa sababu jiulize; hawa ng'ombe 200,000 katika jimbo langu, kuna majosho mawili tu. Sasa tunasema nchi yetu ni nchi ya tatu katika mifugo kwa Afrika, sasa kwa nini tusifike mahali...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nashon.

MHE. NASHON W. BIDYANGUZE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Nashon. Tunaendelea na Mheshimiwa Eric James Shigongo na baadaye Mheshimiwa Furaha Matondo na Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge wajiandae.

MHE. ERIC J. SHIGONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nianze na pongezi kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi kubwa ambayo wameifanya kwenye Wizara hii. Nina siku mbili tu tangu nimerejea na Mheshimiwa Naibu Waziri kutoka Jimboni kwangu ambapo tumesafiri pamoja kwa mtumbwi mpaka kwenye visiwa ambako amekutana na wavuvi na kusikiliza kero zao; nampa pole sana kwa shida aliyoipata wakati tunapita ziwani kwani alijua asingeweza kurejea mahali hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi kubwa inafanyika katika nchi yetu kwenye suala zima la uvuvi ambalo nitachangia kwalo. Nataka nizungumzie sana suala la uvuvi kwa sababu eneo/Jimbo langu lina visiwa 32 na asilimia 35 ya watu wanaoishi eneo lile wameajiriwa kwenye uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nianze kwanza kwa kusema kwamba kama kweli kama Taifa tuna dhamira ya dhati kabisa ya kukuza uchumi wa nchi yetu, ni lazima sasa tuanze kutumia zawadi ambazo Mungu ametupatia; zawadi mojawapo ni uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imebarikiwa kuwa na vitu vingi sana, ukienda huko Liganga kuna mlima wa chuma, kando yake kuna mlima wa mawe; vyote hivyo Mungu alitupatia. Ni wakati wetu sasa kuanza kuvitumia vitu hivi, hatukuvinunua, Mungu alitupatia kama zawadi na ile sisi maisha yetu yabadilike ni lazima sasa tuanze kuvitumia, hilo ni jambo la kwanza ambalo nilitaka kuwakumbusha Watanzania wenzangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja kubwa na kama hotuba yangu/mchango wangu huu ungepewa jina ungeitwa *contribution of political will* kwenye *development.* Tunazungumza mambo mengi sana mazuri, nakaa hapa ndani nasikia michango mizuri najiuliza *what is wrong with us*; watu wanajua jinsi ya kutoka mahali tulipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachokikosa kabisa kwenye Taifa letu ni *political will,* utashi wa kisiasa. Bila utashi wa kisiasa hatutoki mahali tulipo na ndio maana nataka kusema ni lazima sasa tuanze kuwa na utashi wa kisiasa na *determination* na *commitment* ya kwamba ni lazima uvuvi ubadilishe maisha ya nchi yetu, ni lazima uvuvi utupandishe kutoka tulipo kwenda hatua ya juu zaidi; bila ya *political will* hatupigi hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nianze kwa kusema kwamba zawadi tulizopewa na Mungu zipo *underutilized,* ziwa letu na bahari yetu vipo *underutilized*; ni wakati wa sisi kuanza kuvitumia hivi vitu kuleta maendeleo ya nchi yetu. Kwa mfano, nataka nikupe *data* ndogo tu, mchango wa uvuvi kwenye *GDP* yetu kwa mujibu wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri ni *1.7 percent,* wakati huo tuna maziwa yote na bado kwenye bahari yetu tuna maili 200 kutoka ufukweni, zote ni za kwetu tunaweza kufanya chochote. Nchi ya Uganda ambayo ina asilimia 45 tu ya Ziwa Victoria na Tanzania ina asilimia 49, *GDP* yake ni asilimia 12 mchango wa uvuvi. Ukianza kuona hivyo lazima ujue hapa kuna tatizo/kasoro ndio maana nasema kuna mambo ambayo wenzetu wanayafanya sisi hatuyafanyi, tunahitaji *political will. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma Sheria ya Uvuvi ya Uganda ya mwaka 2018 na Sheria ya Uvuvi ya Tanzania yam waka 2003 nimegundua kwamba sheria yetu sisi imejielekeza zaidi kwenye ku-*control* lakini sheria ya wenzetu imejielekeza kwenye ku-*facilitate.* Hivyo basi, kama sheria yetu inaelekea kwenye ku-*control,* kila siku tutakuwa tunakamatana na wavuvi wetu, kuwachomea nyavu zao; jambo hili sio sahihi hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tujielekeze kwenye sheria ambayo ita-*facilitate* wavuvi wetu kuweza kuvua na kujipatia kipato na kuchangia kwenye *GDP* ya nchi yetu. Kama mambo haya hayawezi kufanyika nataka nikuhakikishie kabisa mchango wa uvuvi utaendelea kuwa mdogo kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, samaki wanachangia asilimia 20 ya protini ya wanyama katika nchi yetu. Kwa Uganda natolea mfano, samaki wanachangia asilimia 50 ya protini ya wanyama. Matumizi ya samaki wa Tanzania kwa mwaka kila Mtanzania anatumia kilo 5.5 tu lakini wenzetu ni kilo 15 mpaka 20. Ni lazima tufike mahali sasa tuamue kwa dhamira moja kabisa ya kuhakikisha kwamba watu wetu wanatumia samaki. Jimboni kwangu samaki imekuwa kitu *expensive,* watu wa kawaida hawawezi kumudu samaki kwa sababu gharama yake imekuwa kubwa sana. Sasa tufanye nini? Ili uvuvi wetu uchangie kwenye pato la Taifa letu, ili uvuvi wetu uwe na *impact* kwenye uchumi wetu ni lazima kama nilivyosema tuanze kuhakikisha kwamba kuna *political will* (dhamira ya kisiasa), tusije hapa kuzungumza tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunatoa michango mizuri sana, lakini kama hakuna *political will* hatupigi hatua. Kama Mheshimiwa Waziri hapa hawataachana na hofu na kuanza kutenda, hatupigi hatua hata kidogo. Tutabaki nyuma, tutaendelea *ku-lag behind* hatuwezi kukuza uchumi wa nchi yetu. Hatuwezi kuendelea namna hii, ni lazima tubadilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya nchi hii *TBS* wana kipimo chao cha nyavu na Wizara ina kipimo chake cha nyavu. Lazima hawa watu wawili wakae pamoja na wakubaliane...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. ERIC J. SHIGONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Furaha Matondo na baadaye Mheshimiwa Ally Mohamed na Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa, ajiandae.

MHE. FURAHA N. MATONDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia katika Wizara njeti ya Mifugo na Uvuvi. Pia napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipatia afya njema na kuweza kusimama siku ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza, napenda kumshukuru Waziri, Naibu Waziri, Makatibu wetu wote na wadau wa mifugo na uvuvi kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. Napenda sana kuishukuru Serikali kwa kazi nzuri ambayo imefanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoka Mkoa wa Mwanza, tumezungukwa na ziwa. Tulikuwa na changamoto moja kubwa sana. Wavuvi wetu hapo nyuma walikuwa wanapata shida sana, wakitoka wilaya moja kwenda wilaya nyingine ni lazima walipe. Tuna wilaya saba katika Mkoa wetu wa Mwanza, unamkuta mvuvi mmoja kwa mwezi mmoja analipa mara saba. Kwa kweli ilikuwa ni kero kubwa sana na iliwasumbua sana wavuvi wetu, lakini nipende kuishukuru Serikali kwa sababu kero ile iliweza kuondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naipongeza Serikali na kuishukuru kwa kazi nzuri ambayo ilifanya kwa wavuvi wetu; tulikuwa na desturi ya mvuvi mmoja ikifika Januari unatakiwa kulipa leseni na ukishindwa unapewa faini mwezi Januari huo huo au Februari. Sasa tumepewa kipindi cha miezi mitatu, mvuvi anajianda na kuweza kulipa kuanzia mwezi wa Kwanza mpaka mwezi wa Tatu wanalipa kwa hiari, lakini kama hatalipa, atakwenda kulipa kwa faini ifikapo mwezi wa Nne. Naishukuru sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuiomba Wizara ya TAMISEMI pamoja na halmashauri zetu, tuna kero kubwa sana katika Halmashauri zetu. Tuna wavuvi wadogo wadogo

ambao kwa Kiswahili kizuri, wanavua kwa kasia ambayo ni mitumbwi midogo ya futi 14; lakini tuna mitumbwi mikubwa ya futi 28 mpaka 30 ambayo inatumia *engine*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajikuta wavuvi wale wanalipa ada ya leseni sawa na mvuvi mwenye mitumbwi ya mashine. Ni kero na inawaumiza sana wavuvi wetu, hawawezi kujikomboa kutoka kwenye hali ya umasikini wakaenda kwenye kipato cha kati. Naomba sana Wizara husika iweze kuingialia kati na kuona hili suala. Napenda kuiambia Serikali, mchango wangu ni kwa wale wavuvi angalau kama Halmashauri inalipa 100,000/=, wavuvi wa kasia waweze kulipa shilingi 50,000/=. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ada ya ushuru kwenye mitumbwi. Wanapewa kulipa mitubwi sawa na mtumbwi wa mashine, kiasi kwamba mitumbwi ya kasia wala haiwezi kwenda sehemu yoyote mbali. Unaukuta mtumbwi wa mashine unatoka Mwanza mpaka Bukoba, lakini unakwenda kuleta mazao unakuja kuuza Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtumbwi wa kasia hauwezi kutoka hapa mpaka hata kisiwa kingine, kwa sababu ukipanda kwenye ule mtumbwi kwanza unayashika hata maji; ni mtumbwi mdogo, ni mtumbwi hatarishi, ni mtumbwi ambao watu wanajitafutia chakula. Naomba sana viongozi wetu na Serikali yetu iweze kuliona hili suala. Ushuru unaolipwa kwenye mtumbwi wa mashine wasipewe hata wale wengine kulipa kwenye mtumbwi wa kasia. Hii inawaumiza sana wavuvi wetu wadogo wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimechangia hapa hata muda ulioisha, nikaomba sana, wavuvi wetu wadogo wadogo waweze kutoka kwenye hali waliyonayo, Serikali iweze kuwatambua na kuwapatia mitaji waweze kutoka, lakini kila wakati wanabanwa. Wakitaka kujikwamua huku, wanabanwa, kweli watatoka? Hili suala ni gumu, lakini nina imani Serikali ikiingilia kati, hili suala litakuwa jepesi na watafanya kazi kwa weledi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba, tuna vijana wetu ambao wamemaliza vyuo vikuu, lakini hawajapata ajira. Ni wafugaji wazuri sana wa samaki, tunapata shida. Wananchi wengi wanatafuta jinsi gani ya kuweza kujikwamua kuchimba mabwawa hata kupata kipato, lakini hakuna wataalamu. Halmashauri zetu hazina wataamu wa ufugaji wa Samaki. Hebu niiombe Serikali iweze kuwachukuwa wale vijana, waweze kuji-*organize*, wapewe mtaji, wataweza kuwasaidia hata wananchi wetu ambao wanahitaji kufanya ile kazi, lakini hawana utaalamu. Unakuta hata kwenye Halmashauri husika, mtaalam ni mmoja, Halmashauri nzima inawezaje kuhudumiwa na mataalamu mmoja wa ufugaji wa Samaki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Wizara husika iweze kuliangalia hili suala angalau ipitie kila Halmashauri waweze kuajiriwa hawa vijana waweze kuleta weledi katika nchi yetu. Nina imani kubwa ufugaji wa samaki unaleta pato kubwa sana katika nchi yetu na walaji wetu wa samaki wanaweza kupata protein za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la ulinzi au salama wa wavuvi wetu wakiwapo ziwani. Wavuvi wetu wameachwa sana. Wavuvi wetu wanaliletea Taifa letu pesa nyingi sana, lakini hawajaliwi kabisa. Nikitoka Goziba nikija Ukerewe, Rolia, Muleba hakuna Kituo cha Polisi *(Police Marine)* cha kuangalia usalama wa wavuvi wetu na wafanyabiashara wanaoishi kandokando ya ziwa. Hii inaumiza sana kwa sababu wale watu wasipoangaliwa kila wakati wanavamiwa ziwani; kila wakati wananyang'anywa mashine; kila wakati wanaumizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iweze kufuatilia hili suala, iweze kuwapatia hawa watu waweze kuwa na ulinzi ambao utawasaidia hata wakiwa wanafanya kazi zao waweze kufanya kazi zao lakini wakiwa wametulia na akili zao zikiwa kabisa ziko vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wanawake wenzetu ambao wako katika hali ya kufanya biashara ndogo ndogo

katika mihalo. Wale akina mama ni wachakarikaji, nilishasema *last time* wakati naongea hapa. Naomba sana Serikali iweze kuona hili suala waweze kupatiwa mitaji wana biashara ndogo ndogo za kuchukua dagaa, lakini unawakuta wale akina mama wanaanika dagaa kwenye mchanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale dagaa wanakuwa ni wachafu na hata hawawezi kuliwa wakawa ni chakula cha binadamu. Naomba wapatiwe mitaji waweze kutengenezewa chanja. Zile dagaa wakianika kwenye chanja wanaweza kujipatia kipato kikubwa, lakini pia wakaingia hela Serikalini, nao wenyewe wakajikwamua kutoka kwenye umasikini walionao wakaingia hata kwenye hali nyingine. Wanahangaika sana siku hadi siku. Siku zinavyozidi kukatika lakini hawapati chochote, hali inakuwa ni ile ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, Serikali yetu ni sikivu, imejaribu kutusikiliza sana kila wakati. Kwa hiyo, naomba sana kuhusiana na hii kero ya wavuvi wadogo wadogo kutoa tozo. Kwa kweli inaumiza. Hata ukiuliza, yaani inaumiza sana. Waweze kutoka katika sehemu ya tozo ambazo ni sawa na mitumbwi mikubwa, angalau wapate tozo ambazo ni tofauti na wengine. Nina imani sana, ikiwa hivyo itasaidia sana wavuvi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi wetu wanakwenda ziwani, wanafanya kazi ngumu, wanafanya kazi kubwa, lakini wanapoleta mazao yao, hawana sehemu ya kuonesha kwamba tuna masoko yetu ya kuuzia samaki ambayo nikileta mzigo wangu, nikipeleka soko fulani nitapata faida.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. FURAHA N. MATONDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Furaha Matondo kwa mchango mzuri. Tunaendelea na Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge na baadaye Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa na Mheshimiwa Francis Mtinga wajiandae.

MHE. ALLY M. KASSINGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami nianze kuchangia Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kwanza kabisa kwa kupongeza uongozi wa Wizara ambao kwa ujumla umeanza kuleta matumaini mazuri kwa Watanzania hususan kwenye Sekta ya Mifugo na Uvuvi. Kwa hiyo, nawashukuru na ninawapongeza sana viongozi kuanzia Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Makatibu Wakuu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi ambalo linatupa matumaini ni kwamba uongozi huu umejikita kwenye ubobezi wa sekta wanazosimamia. Ukiangalia Katibu Mkuu wa Uvuvi, amejikita katika masuala hayo, Katibu Mkuu wa Mifugo kadhalika ni mzoefu wa masuala hayo. Ndugu yangu Mheshimiwa Ulega, Naibu Waziri ni mzoefu wa masuala hayo kitaaluma na pia kimakuzi. Kwa hiyo, Watanzania hatuna shaka katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ambalo nataka kuanza kuchangia katika hotuba hii, kwanza kabisa ijitambue kwamba ni Wizara ya Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi na siyo Wizara ya Mifugo na Kukwaza Uvivu Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza hivi kwa sababu mengi ambayo wachangiaji wenzangu wamezungumza, niwarejeshe tu katika kanuni za mwaka 2020, kanuni ya 66(1)(d)(f)(g). Vifungu hivi vinakwaza kabisa maendeleo ya uvuvi katika nchi yetu ya Tanzania. Sihitaji nidadavue vinakwaza vipi? Bahati nzuri wachangiaji wenzangu waliotangulia wameelezea. Naomba katika mabadiliko ya kanuni Mheshimiwa Waziri anayokwenda kuyafanya, azingatie haya ambayo kwenye vifungu nivyovitaja yanakwanza uvuvi Tanzania. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, naomba wataalam wa Sekta ya Uvuvi, wanapokwenda kutengeneza kanuni mpya, ziwe ni kanuni shirikishi na pia ziwe ni kanuni zinazoendana na mazingira husika. Kwa mfano, sisi watu wa Pwani, taratibu za uvuvi zinazingatia masuala ya nyakati, nyakati za pepo na miandamo ya miezi. Kwa mfano, unapokataza watu wasivue mchana kwa ujumla wake tu, wakati taratibu za uvuvi wa baharini zinazingatia mwandamo wa mwezi, kuna kipindi cha mwezi mchanga, kuna kipindi cha mwezi mpevu, kuna kipindi cha mwezi mwangavu, hilo lizingatiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kuna hawa samaki maarufu kama Kambakochi au Kambamiti. Kule Kilwa ni tofauti na Rufiji ambapo Kilwa uvuvi wa Kambakochi unatakiwa uanzie mwezi Januari, lakini leseni ambazo Wizara inatoa inaanzia mwezi Aprili. Maana yake ni kwamba mpira unapigwa huku, golikipa anaangukia huku; tofauti kabisa. Hapa tunaomba izingatiwe pia, ndiyo maana tunasema kwamba sheria hizi na kanuni hizi ziiwe shirikishi, ziulize wazoefu wa maeneo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninaomba ni kukuza Sekta ya Uvuvi na hususan katika Sekta ya Wilaya ya Kilwa, ni kuhakikisha kwamba pale Kilwa Kivinje ambapo nimejiridhisha kabisa samaki wengi ambao wanaliwa Tanzania wanatoka Kilwa; ukiona samaki wanaliwa Dar es Salaam wanatoka Kilwa, ukiona samaki wanaliwa mikoa mingine ya Kusini, wenzetu jirani zetu Mtwara na Ruvuma wanatoka Kilwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushahidi wa hili wale ambao wanatumia barabara hii maarufu kama ya Kibiti - Lindi, ukifika pale Somanga, ukinunua samaki unakuja Dar es Salaam au unakwenda Mtwara au unakwenda Ruvuma maana yake hao ndiyo samaki wa Kilwa. Kama hivyo ndivyo, kuna haja ya kuanzisha soko la samaki la kisasa pale Kilwa Kivinje ili wavuvi wetu wawe na uhakika wa soko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe taarifa tu kwenye Wizara hii, katika utaratibu usio rasmi jirani zetu wa Kongo wanakuja Kilwa kununua samaki tani za kutosha. Tumeandaa utaratibu gani wa kuingiza mapato ya Taifa kwa kuuza samaki nje ya nchi? Tuko katika utaratibu usiosimamiwa vizuri na Wizara. Nashauri katika eneo hili, Wizara isimamie inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine Mheshimiwa Waziri, matumizi ya nyavu zilizozuiliwa. Kimsingi nyavu hizi, wananchi wetu wavuvi hawa masikini wa Tanzania wanavua kulingana na aina ya samaki wanaovua. Kwa mfano, dagaa wote tunawafahamu, wanahitaji milimita kumi. Wote tunajua dagaa ni visamaki vidogo vidogo sana, vinahitaji milimita sita, ikizidi milimita saba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tangu kumetolewa zuio la kukataza zuio la kukataza uvuvi wa nyavu hizi, uvuvi wa mchana, wavuvi wetu wamebaki kuwa masikini, wamechomewa nyavu zao, wamechomewa vyombo vyao, vimeangamizwa, hii ni msiba mkubwa katika Taifa hili na siyo haki kufanya katika nchi ambayo iko huru. Malengo na matarajio ya Watanzania ni kuona kwamba kila sekta inasaidia wahusika. Kama ni Sekta ya Kulima isaidie wakulima, Sekta ya Uvuvi isaidie wavuvi, Sekta ya Ufugaji isaidie wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sihitaji nizungumzie kilio cha Wana-Kilwa cha kuchomewa nyavu zao, kuangamiziwa vyombo vyao vya uvuvi, kilichofanywa huko na Waziri ambaye amemaliza muda wake. Nina matarajio mazuri na Mheshimiwa Waziri wewe kaka yangu, hautafanya kama mwenzako aliyekutangulia. Utakuwa ni msikivu, utakuwa ni mwenye huruma kwa Watanzania masikini hususani wavuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, niseme tu kwamba katika mpango wa Wizara wa kuanzisha bandari za uvuvi, nimeona imetajwa Mbegani hapa, lakini mwanzoni Kilwa ilikuwa kwenye mpango. Tunaomba mpango huu kwa

miaka mitano hii, Kilwa isisahaulike. Kilwa Masoko pale kuna kina cha kutosha, kuna bandari ya asili. Kwa hiyo, ule mpango wa miaka mitano ubaki vile vile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Ally Mohamed. Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa, atafuatiwa na Mheshimiwa Francis Mtinga na baadaye Mheshimiwa Zuberi Kuchauka ajiandae.

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hii hoja ya Wizara ya Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuishukuru Wizara, kwa sababu katika kipindi cha mwaka wa fedha unaoisha, wameweza kutukarabatia bwawa moja kati ya mabwawa 27 ambayo ndiyo tegemo la Wanalongido katika Kata ya Kimokouwa. Ahsanteni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kwanza kuwapongeza kwa sababu najua kazi kubwa wanayoifanya na ugumu wa kazi hii, kwa sababu Wizara hii imeunganisha sekta mbili ambazo zote zinahitaji rasilimali kubwa sana katika kusimamia ili kuweza kufikia malengo ya kiuchumi kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kufanya ulinganifu kidogo wa bajeti iliyotengewa Wizara hii kwenye fedha za maendeleo. Nimeangalia bajeti ya mwaka huu unaoisha; mwaka jana wa fedha (2020/2021) ambao ndiyo unaisha mwezi wa Sita, fedha za maendeleo zilikuwa ni shilingi bilioni 23.4 na mgawanyo wake katika sekta zake mbili; Fungu 64 ambalo ni Uvuvi na Fungu 99 ambayo ni Mifugo ni kama ifuatavyo: mifugo walipewa shilingi bilioni 10.3 na uvuvi walipewa shilingi bilioni 13.05; na walijitahidi kufanya kazi walizozifanya na hizi ni fedha za maendeleo. *Returns* au maduhuli yaliyokusanywa katika hizo fedha

walizowekeza mpaka mwezi huu wa Tano, mifugo wanakaribia kufikia shilingi milioni 40, nadhani wameshafika shilingi milioni 40 kufikia sasa, lakini uvuvi wako chini ya shilingi milioni 18. Sasa utaona kwamba ni kwa jinsi gani hizi sekta zinaweza zikazalisha lakini haziwekezewi mtaji wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu wa fedha bajeti ambayo Waziri amewasilisha leo hotuba yake hapa, jamii yote ya wafugaji Tanzania pamoja na mimi tuna masikitiko makubwa. Kwa nini nasema hivyo? Kwa sababu mwaka huu mmeongeza bajeti ya maendeleo kwa asilimia 80 kutoka shilingi bilioni 23 mpaka shilingi bilioni 116.01, lakini katika mgawanyo kwenye mafungu yake yote mawili, mmeipendelea Sekta ya Uvuvi mkawapa shilingi milioni 99 ambayo ni sawa na asilimia 76 ya fedha yote ya maendeleo mkiaibakizia Sekta ya Wafugaji ambayo nayo ndiyo uti wa mgogo wa watu wengi katika nchi hii, asilimia 14 tu ambayo ni shilingi bilioni 16.8. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni masikitiko makubwa sana kwa sababu katika ukusanyaji wa maduhuli, bado mmeiweka sekta hii kwamba mnatarajia iwape shilingi bilioni 50 na uvuvi iwape shilingi bilioni 33 na wakati huo huo mmeshaona kwamba hata katika fedha kidogo za mwaka unaoisha wa fedha sekta hii ya mifugo ndiyo iliyokuwa inaleta *returns* zaidi kuliko uvuvi. Sasa imenifanya niungane na mwenzangu Mheshimiwa Olelekaita leo asubuhi akisema, kama mnaona kwamba hii Sekta ya Uvuvi ndiyo ina umuhimu mkubwa, basi ni bora Sekta ya Mifugo ipewe Wizara yake ijisimamie yenyewe ili tuweze kutafuta rasilimali za kuiendesha kwa ufanisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimeangalia katika ilani ya CCM ya mwaka 2020 mpaka 2025 ambayo ndiyo iliyounda Serikali inayoongoza nchi hii wameshabainisha vipaumbele na kwa masikitiko makubwa sidhani kwa bilioni hizi bilioni 16 tunaweza tukafanikisha masuala ya ugani na utafiti masuala ya uzalishaji wa mifugo na kutafuta masoko ya maziwa na nyama biashara ya nyama biashara ya mifugo

na mazao yake soko landani na la nje ukarabati wa miradi mbalimbali ya minada mambo ya kimkakati ya mpakani na mapitio ya ada na tozo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, hata wizara yenyewe waliweka malengo ambayo sijui watayatekelezaje na bilioni 16 kwenye hii sekta ya mifugo maana ndio ninayoisemea. Walisema kwamba tutasimamia kuimarisha afya ya mifugo ambayo ni mambo ya chanjo madawa majosho walisema watasimamia mambo ya vyakula vya mifugo na maji na wakati wilaya kame ndizo zenye wafugaji wengi kuliko wote nchi hii unakuta hawana vyanzo vingine wanategemea mabwawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Olelekaita yeye anahitaji mabwa 40 mimi nahitaji 27 wametengeneza moja tu na fedha sizioni hapa, lakini basi kwa masikitiko makubwa nipende tu kusema kwamba wizara imetuangusha katika kugawa hizi rasilimali na ninamuomba waziri atueleze ni utaratibu gani au ni kwa sababu gani ameamua kuwapatia uvuvu asilimia 75 ya fedha zote za maendeleo akawapatia wafugaji asilimia 15 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine kwa sababu ya uhaba wa muda nilimsikia Mheshimiwa Spika, asubuhi hii akiongea kwamba *NARCO* imeferi kweli imeferi, lakini mimi ninaomba tu nishauri Serikali sisi kama kamati niseme kwamba naunga mkono hoja ya kamati yangu yote na kazi tuliyoifanya. Tulishapendekeza kwamba ifanyiwe *review* kwa ajili ya kujua ilianzishwa kwa nini, kwani ni imeferi na kama malengo yako bado yanahitajika wakati huu miongozo na kanuni zilizoianzisha zipitiwe kabla ya kufikia hatua ya kusema tuifutilie mbali maana yake nadhani ndio shamba darasa la kuzalishia mbegu bora za kuendeleza wafugaji wa nchi kwa hiyo naomba wapewe nafasi ya pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu la mwisho, napenda kuongelea huu mtafaruku ulioko wa migogoro ya ardhi kati ya wafugaji na wakulima na watumiaji wengi, katika jimbo langu la Longido sisi hatukuwahi kuwa migogoro

na wakulima kwa sababu sisi ni wafugaji kwa asilimia 95 na maeneo ya hifadhi lakini pia hatujawahi kuwa na migogoro na hifadhi. Isipokuwa katika kipindi hiki kililchopo kuna pendekezo nadhani liko mezani halijaingia katika Bunge hili lakini limeshapita kwenye Baraza la Mawaziri la kutaka kumegua eneo la Wilaya ya Longido kuwa pori la akiba na ile ni ardhi *prime land* ya wafugaji ndio inaenda kuchukuliwa kuwa pori la akiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati marais wote wa Awamu ya Tano Hayati Dkt. John Joseph Magufuli na wa Awamu ya Sita mama yetu mpendwa Samia Suluhu Hassan wana tuahidi kwamba ardhi ya ufugaji inakwenda kuongezwa ifikie hekta milioni sita sasa inakuwaje leo kuna wizara inanyemelea tena nyanda zetu za malisho na kuzipunguza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Waziri wa Mifugo ebu angalia kutana na mwezako wa maliasili kwamba utaratibu huo wa kwenda kutwaa ardhi ya wafugaji ,ardhi ambayo imepimwa ni ya vijiji, na maeneo ambayo yametenga ili kuyafanya hifadhi iangaliwe upya kwa sababu inaenda kinyume na matarajio katika maeneo ya wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache naunga mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa tunaendelea na Mheshimiwa Amour Hamis baadaye Mheshimiwa Zuberi Kuchauka na Mheshimiwa Joseph Mkundi wajiandae.

MHE. AMOUR KHAMIS MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nikupongeze kwa namna unavyotuongoza, lakini pia niwapongeza sana Waziri wa Wizara hii na Naibu wake kwa kazi nzuri sana wanayoifanya ndani ya nchi yetu na kwa kufuata llani ya Chama chetu Cha Mapinduzi.

WABUNGE FULANI: Badilisha mic.

MBUNGE FULANI: Nenda nyingine.

MWENYEKITI: Badilisha *mic*.

MHE. AMOUR KHAMIS MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunazungumzia habari ya wavuvi na wafugaji, mimi ni mvuvi niliwahi kuvua kwa miaka mingi sana. Kwa hiyo, najua kwamba wavuvi hawana elimu maalum, wavuvi wetu wengi sana wanavua kwa mirathi yani kwa elimu ya mirathi. Jinsi mtu alivyomkukuta baba yake anavua ndivyo hivyo anavyovua na yeye na sina hakika kwamba wizara hii imeweka siku kwamba itakutana na wavuvi ana kwa ana kuwasiliza changamoto zao kule waliko au wataandaa mafunzo juu ya uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimwa Mwenyekiti, ni kwamba hawa wavuvi wengi hawavui kwa sababu ni kazi anayoipenda kwa sababu uvuvi ni kazi hatari sana, ni sawasawa na mtu anapopanda mnazi yaani wakati wowote unaweza kusikia chochote na hasa kwa kuzingatia vyombo wanavyovitumia, kuelekea katika mazingira hayo ya uvuvi. Kwa hiyo, naiomba Serikali sana, badala ya kuchukua maamuzi ya kuchoma tu nyavu au kutunga tu sheria ngumu walikuwa wafikirie sana namna ya kuwaendeleza wavuvi. Nasema hivyo kwa sababu, kwa mfano, Serikali inapotaka kupitisha njia eneo inapitisha barabara wanafika mahali wakikuta kibanda cha mtu kwa sababu ya kuthamini binadamu yule wanaamua kumlipa fidia. Lakini kwa bahati mbaya sana mvuvi hafanyiwi hivyo inachukuliwa tu nyavu kwa sababu ya kigezo cha uvuvi haramu inachomwa au kitu kingine chochote kinaangamizwa bila kufikiria kumbe Serikali ilitakiwa ikinunue kile kwa sababu na yeye ndio maisha yake. *(Makofi)*

Mheshimwa Mwenyekiti, sawa sawa na nyumba au ardhi inayopatikana wakati inapopitishwa barabara. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali iwahurumie sana wavuvi wanafanya kazi hatari sana na sisi kama Serikali hatujafikia kiwango cha kuwaendeleza moja kwa moja. Huwa

nachukulia mfano ingekuwa yule mvuvi ni mtoto wangu siningempa mtaji nikamnunulia chombo kizuri sana mashine nzuri, mitego mizuri lakini Serikali inatakiwa ijue kwamba wale wavuvi ni kwa ajili ya mapato ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo na wao ipo haja ya kuwaandalia utaratibu wa kuendesha maisha yao lakini pia na pato kwa Serikali. Jimbo langu sehemu kubwa sana imepakana na bahari ya Hindi na pale kuna wavuvi na mara nyingi sana wavuvi hawa wanaenda kuvua mbali sana lakini Serikali bado haijaweza kuweka ulinzi huko wanakokwenda, sina hakika kwamba Serikali hapa Tanzania Bara kwa mfano imeweka vyombo maalum huko baharini kwamba wavuvi wakipata tatizo lolote wanaenda kuokolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hilo halipo naomba sana Serikali ifanye hivyo kwa sababu uvuvi ni kazi hatari sana na sisi wote naamini kila anayemsomesha mwanae uvuvi hampi chombo kwenda kuvua baharini bali anamtafutia eneo zuri kwenye Serikali awe mhudumu ofisini ili awasimamie wavuvi. Kwa hiyo, bado uvuvi na changamoto kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ndipo tunapotakiwa sasa kutumia sayansi yetu tumesoma sayansi kwa muda mrefu sana na Tanzania wanasifiwa sana kwa wanasayansi, na hapa ndio tunatakiwa kuitumia vizuri sana kwa kuelewa ni eneo gani lina Samaki ili Serikali ipate faida kubwa zaidi, kama hautujaweza kutengeneza vifaa vitakavyotuonesha kwamba hapa hili eneo kuna, Samaki tukawatayarisha wavuvi wetu wawe katika utaratibu huo, elimu hiyo, basi tusitegeme kwamba sekta hii ya uvuvi itakuwa nzuri. Kwa sababu mpaka sasa hivi wavuvi wetu wanavua kwa kubahatisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu ana *ring net* anaenda kuzungusha anavua hamna kitu mara mbili tatu, bado tunabahatisha. Haya maeneo tajiri sana sisi watanzania Mwenyezi Mungu ametubariki sana maeneo haya ya uvuvi tuna maziwa mengi, lakini tuna bahari kubwa sana ya Hindi.

Kwanini hadi leo hatujafikia mahali bahari ya Hindi ikatuneemesha? Na kila mtu anajua kwamba bahari ni tajiri mbali ya Samaki kuna mambo mengi sana ambayo ni ya kufanya nchi yetu iwe tajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, bado Serikali haijafikia maamuzi ya kuandaa utaratibu wa kuwanufaisha wavuvi, na wahudumu wengine wa bahari lakini pia kwa kupata mapato makubwa zaidi. Naomba sana Serikali iwafanye wavuvi ni watoto wao lakini pia ni waajiwa wao kama vile wanavyohudumiwa walimu sisi Wabunge na wafanyakazi wengine ndivyo wahudumiwe wavuvi, kama kweli tunahitaji wavuvi walete tija ndani ya nchi hii vinginevyo tutawapelekea wavuvi hasara ndio maana hapa nina tarehe 3 Novemba, 2018 kuna wavuvi walikamatwa kesi yao haijulikani iko wapi lakini walipelekwa mahakami ni watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwaelekeze lakini pia Serikali kuna wavuvi walipigwa mpaka risasi kwa nini?

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa!

MHE. AMOUR KHAMIS MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana naunga mkono hoja na nawatakia heri sana Waziri na Naibu wake na wewe mwenyewe, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Amour Khamis tunaendelea na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka Mheshimiwa Joseph Mkundi na Mheshimiwa Silyvestry Francis wajiandae.

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi, lakini nianze kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri Naibu Waziri na watendaji wote kwenye wizara hii na mimi nina mada moja tu ambayo

nitachangia mada ya mifugo nitajikita kwenye mifugo, baada ya mifugo kufanya vibaya kwenye bonde la Ihefu, Serikali ilifanya maamuzi ya makusudi kupeleka mifugo ile kwenye Mkoa wa Lindi na sisi Mkoa wa Lindi kuna wilaya mbili ndio tumepokea wafugaji Wilaya ya Kilwa na Wilaya ya Liwale. *(Makofi)*

Mheshimies Mwenyekiti, Wilaya ya Liwale tulitenga vijiji vitatu; Kijiji cha Lilombe Ngapata na Kimambi ndio vijiji viliidhinishwa kupokea wafugaji, lakini kutokana na sababu sitofahamu ninyi wenyewe mnajua wafugaji sasa hivi Liwale nzima kuna wafugaji. Jambo ambalo nataka kuliongelea hapa Serikali hapakufanywa maandalizi ya kawaida au maandalizi mahususi ya kupokea mifugo. Hapakuwa na miundombinu yoyote ya kupokea mifugo ile naninavyoongea mpaka leo hakuna majosho hakuna malambo hapakuandaliwa lolote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, palihitaji maandalizi kwanza ya kimuundo mbinu, halafu maandalizi ya kielimu kwa maana kwamba watu wa kuandaa saikolojia kwa sababu sisi kwa asili sio wafugaji. Leo ninavyozungumza hapa ni zaidi ya miaka 10 mifugo iko Liwale lakini Halmashauri ya Wilaya ya Liwale haijawahi kunufaika na chochote kutokana na mifugo ile, hii ni kwa sababu hapakuandaliwa na miundombinu yoyote na vilevile sisi wenyewe wafugaji wana Liwale hatukuandaliwa kupokea mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikwambie jambo moja mwaka 76 mzee Rashindi Mfaume Kawawa waziri wa kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alituletea ng'ombe sisi Liwale kila Kijiji ng'ombe 20 na kila shule tulipata ng'ombe ishirini lakini ng'ombe wale walidumu miezi sita tu sababu ni nini hakuna mzazi aliyekubali mwanae kumpeleka kuchunga ng'ombe ilikuwa ni adhabu. Kwa hiyo, Mwalimu akimpangia kwenda kuchunga ng'ombe huyo Mwalimu haamki, lakini ng'ombe wa kijiji nao walikufa kwa mtindo uleule hakuna mtu aliyekubali kwenda kuchunga ng'ombe akiwa na akili timamu. Ukimwona kwetu mtu anachinja ng'ombe basi ujue dishi limeyumba. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo ng'ombe wale walikufa sisi kwetu mfugaji anafuga bata tena dume kwa hiyo kwa msingi huo kwetu tulikuwa tuandaliwe kisaikolojia namna ya kuwapokea wale ng'ombe vilevile tuandaliwe kwa miundombinu. Sasa nini kinatokea hatuna wataalam wakutuelimisha namna ya kukuaa na wafugaji wale na vijiji vyetu havikuingia kwenye matumizi bora ya ardhi. Jambo hili linatuletea migogoro sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua jukumu la matumizi bora ya ardhi ni jukumu la halmashauri lakini halmashauri inaingia kwenye jukumu hili kwa faida ipi ambayo tumeipata kutokana na mifugo ile? Naiomba sana Serikali, ije Liwale ije itusaidie kuanza kuhakikisha vijiji vile ambavyo tayari vina wafugaji vinaingia kwenye matumizi bora ya ardhi ili kutupunguzia migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi pia tunatakiwa tuwe na malambo kwa ajili ya wafugaji wale, jambo linalofanya sasa Liwale nzima isambae mifugo, kwa sababu wafugaji wanatafuta maji, hawana mahali pa kupata maji, kwa hiyo, tumeruhusiwa vijiji vitatu sasa vijiji vyote 70 vina wafugaji na miaka mitano, sita ijayo idadi kubwa ya wafugaji itakuwa kubwa kuliko wenyeji wa pale kwa hiyo tunaomba tuletewa wataalam kwa ajili ya miundombinu tuletewe wataalam kwa ajili ya kutuelemisha namna ya kufuga mifugo ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kuhusu minada tunaomba sana tupate mtu *specific* ambaye anajua mambo ya minada, aje atufunguliwe mnada Liwale, Kilwa ng'ombe wanakwenda Mtwara wanakula ng'ombe Mtwara wanakula ng'ombe Songea wanakula ng'ombe wapi lakini ng'ombe wanachukuliwa kutoka Liwale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwambia, Halmashauri ya Wilaya ya Liwale haijawahi kupata hata shilingi, tunahitaji juhudi za makusudi ili na sisi tuone faida ya kuwepo ile mifugo pale Liwale. Hilo ndio jambo mahususi niliyokuwa nimeomba nafasi hii kulizungumzia kwa siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa dakika tano hizi. *(Makofi/Kicheko)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Kuchauka umetumia vizuri dakika zako. Tunaendelea na Mheshimiwa Joseph Mkundi...

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MHE. ESTHER N. MATIKO: Kulikuwa na kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Joseph Mkundi atafuatiwa na Mheshimiwa Sylivia Francis na Mheshimiwa Osca Kikoya ajiandae.

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi ya kuchangia nitakuwa na mambo machache sana kwenye wizara hii na kimsingi kwa leo mchango wangu utajikita kwenye eneo la uvuvi, na nina sababu ya msingi. Natoka visiwa vya ukerewe na katika *square* kilomita 6400 ni asilimia 10 tu ya nchi ya kavu zaidi nimezungukwa na maji kwa hiyo watu wangu wengi ni wavuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwapongeze viongozi wa wizara Mheshimiwa Waziri, naibu na watendaji wote wa wizara hii, wamejitahidi sana kuitendea haki wizara hii na niombe mwenyezi mungu aendelee kuwasimamia kama mjadala ulivyoendelea kwa siku chache zilizopita uchumi wa Taifa hili unategemea sana sekta ya kilimo ikihusisha uvuvi na mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, zaidi ya asilimia 90 ya wavuvi wetu ni wavuvi wadogo. Kwa hiyo, katika mambo ya msingi ambayo tunapaswa kuyafanya ni kujenga msingi, hasa kuwezesha sekta hii ya uvuvi kupitia wavuvi hawa wadogo ili kuweza kuifanya sekta hii ya uvuvi iweze kuwa na *impact* kwenye uchumi wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka michache iliyopita wavuvi wetu walikuwa na shida sana na watumishi wa Wizara ya Uvuvi. Walikuwa kama wanawindana hivi, kama watu mahasimu. Sasa ili tuweze kujenga msingi imara kwenye sekta hii ya uvuvi, lazima kwanza tuanze kujenga mazingira mapya kwenye sekta ya uvuvi. Tu-*harmonize* hali tofauti na mazingira yaliyokuwepo kipindi cha mwaka mmoja au miwili iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma ilitokea operesheni, kama ambavyo nimekuwa ninasema, watu wengi sana walipoteza mali zao. Sasa ni wakati ambao tunahitaji tujenge mazingira ambayo watumishi, wataalam, wavuvi, wataaminiana ili kama nilivyosema, sekta ya uvuvi iweze kuwa na *impact.* Kwa sababu tukiweza kuimarisha sekta hii; na kama nilivyosema, zaidi ya asilimia 90 ya wavuvi wetu ni wavuvi wadogo; na kwa maana hiyo sekta hii itatusaidia kutengeneza ajira, itaongeza kitoweo na vitu vingine kama hivyo ili kuweza kusaidia watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa jambo la kwanza ambalo nafikiri nichangie kwenye eneo hili, kwanza naomba Wizara yetu itambue kwamba wavuvi wetu wanahitaji sana elimu. Kuna matatizo kadhaa yamekuwa yanajitokeza, lakini hasa ni kwa sababu wavuvi wetu wanakosa elimu kutoka kwa wataalam. Watu wanapotoka Wizarani kwenda kutoa tu adhabu kwa watu wale kwa sababu wamefanya makosa, haijengi dhana iliyo nzuri kuwawezesha watu wetu kuwa imara na kuimarisha mitaji yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutolee mfano wakati ule Wizara inatuma watu kwenda kuchoma makokoro na mitumbwi, hebu *imagine* mwananchi wa kawaida amejikokota kapata mtaji wake, kaanzisha biashara yake ya shilingi milioni 10 au shilingi milioni 15, siku moja tu ule mtaji unaporomoka. Lazima atakuwa *frustrated.* Kwa hiyo, kwanza tujikite kwenye kutoa elimu. Tuwe na kitengo maalum kwa ajili ya kuzunguka kwenye maeneo yetu kutoa elimu kwa wavuvi wetu ili yale wanayoyafanya, basi yaendane na miongozo, taratibu na mambo mengine kama hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana Wizara, kupitia hotuba yao, nimeona wako kwenye hatua nzuri ya kutafsiri sheria, miongozo na kanuni zetu kwa Lugha ya Kiswahili. Ni jambo jema kwa sababu wavuvi wetu wengi hawaelewi lugha hii tunayotumia kwenye sheria zetu. Kwa hiyo, kama itatafsiriwa kuwa Lugha ya Kiswahili itatoa fursa kwa wavuvi wetu kuweza kusoma na kuelewa miongozo, kanuni na sheria zinazohusu kazi wanazozifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu, kazi hii itakapokamilika, basi sheria hizi kwa Lugha ya Kiswahili iweze kusambazwa kwenye wilaya zetu ili wavuvi wetu waweze kuzipata na kuzisoma, waweze kuzielewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni juu ya tozo. Mwaka juzi, 2019 tulifanya marekebisho ya sheria hapa Bungeni; na katika sheria hizo tulipunguza baadhi ya tozo zilizokuwa zinakabili wavuvi wetu. Kwenye eneo hili, ni kweli baadhi ya tozo zile zimeondolewa, lakini bado kuna tozo ambazo ni kero kwa wananchi wetu. Naomba Serikali iendelee kuziangalia kupitia Wizara, iangalie tozo nyingine ambazo siyo za msingi sana tuweze kuzitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile naiomba Wizara, wavuvi wetu hawa wa kawaida wanasumbuliwa sana pale ambapo mamlaka zinapoenda kukusanya tozo. Kwa mfano, kuna tozo za *TASAC,* ushuru wa mitumbwi, leseni na kadhalika. Mbaya zaidi ni kwamba tozo hizi zinatozwa kwa nyakati tofauti tofauti, jambo linaloleta usumbufu kwa wavuvi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ione uwezekano wa kuunganisha tozo hizi ili zote ikiwezekana ziwe zinatolewa kwenye *center* moja halafu sasa Serikali inaweza kuchambua tozo zile kama ni ya *TASAC* au sehemu nyingine, kuliko kila wakati taasisi inakwenda kuwatoza wavuvi wetu, inakuwa ni usumbufu kwa watu hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nafikiri nilichangie ni kwenye uvuvi wa vizimba. Tumekuwa

tunahamasisha sana wavuvi wetu kufanya uvuvi wa vizimba; ni jambo jema. Kupitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri, inaonekana kwenye Ziwa Victoria kwa mwaka mmoja; mwaka 2019/2020 vizimba vilikuwa 431. Mwaka huu kwa mujibu wa utafiti wao, vizimba ni 473; ni jambo jema. Bado kwa mtazamo wangu tunahitaji kufanya zaidi. Tunahitaji tuwekeze zaidi kwenye uvuvi wa vizimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namna pekee ambayo tunaweza tukawasaidia watu wetu, kwa sababu moja kati ya changamoto zilizopo kwenye uvuvi wa vizimba ni gharama za kuanzisha shughuli hizi za ufugaji wa samaki. Kwa mwananchi wa kawaida kwa gharama zilizopo hivi sasa, ili mtu aanzishe kizimba anahitaji zaidi ya shilingi milioni 10. Ni wananchi wachache sana wa kawaida wenye uwezo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya sana kumekuwa na shida sana kupata vifaranga vya samaki. Hata chakula cha samaki hawa kimekuwa na shida kubwa. Kwa hiyo, naomba Serikali kupitia Wizara, ione uwezekano ili chakula cha vifaranga hawa kiweze kupatikana kwa bei nafuu. Vilevile vifaranga wazalishwe kwa wingi wapatikane. Pia zile gharama nyingine kwa mfano za kufanya *Environmental Impact Assessment,* angalau zake zipungue ili mwananchi wa kawaida awe na uwezo wa kuanzisha kizimba akafuga samaki, jambo litakalotusaidia kuondokana hata na ile migogoro ya uvuvi usio halali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo machache, nashukuru sana kwa nafasi, Mwenyezi Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Mkundi. Tunaendelea na Mheshimiwa Sylivia Francis, baadaye Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo na Mheshimiwa Tunza Malapo wajiandae.

MHE. SYLIVIA F. SIGULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa nami niweze kuchangia. Nianze

kwa kuiongeza Wizara, hasa kumpongeza Waziri na timu yake. Wakati uliopita nilitoa kero zangu hapa kuhusu wavuvi wa Ziwa Tanganyika, lakini Waziri alifika Kigoma akaongea na wavuvi na baadhi ya kero akazitatua. Wavuvi wa Kigoma na wavuvi wa Mwambao mwa Ziwa Tanganyika wanaipongeza sana Serikali Sikivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi leo nitakuwa na uchangiaji mdogo sana; na leo nina kero chache ambapo naamini Serikali yetu ni sikivu itakwenda kuzifanyia kazi. Namwomba Mheshimiwa Waziri wakati wa majumuisho aweze kutupatia ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia nilieleza umuhimu wa Ziwa Tanganyika. Kwa tafiti zetu zilizofanyika, nilisema Ziwa Tanganyika lina kina kirefu ambacho ni mita 1,470. Masikitiko yangu makubwa ni kwamba hili Ziwa Tanganyika ni kama Serikali hailioni. Naongea haya nikiwa na masikitiko makubwa kwa sababu moja. Ziwa Victoria lina urefu wa kina cha mita 120, na Ziwa Tanganyika ni mita 1,400 lakini tunaona kwamba kuna kanuni kandamizi kwa wavuvi wetu wa Ziwa Tanganyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na tafiti zilifanywa na *TAFIRI* zinasema kwamba uwezo wa samaki kuishi, *oxygen* inayopatikana ni mita 150 kutoka kwenye *water surface* (kina kile cha juu). Leo wavuvi wa Ziwa Tanganyika wanaruhusiwa kutumia nyavu ambazo zinakwenda kwa mita saba tu. Mbali ya kuwa na kina kirefu, wavuvi wa Ziwa Victoria wanaruhusiwa kwenda mpaka mita 16. Hii siyo sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana Wizara watueleze sisi wavuvi wa Ziwa Tanganyika, watuambie ni vigezo gani vinavyotumika ili sisi wavuvi tujue, maana tunaona kwamba hiki kitu siyo sahihi. Kwa hiyo, wavuvi wa Ziwa Tanganyika wanaomba angalau waweze kupatiwa nyavu ambazo zitaweza kwenda hata mita 20 au 25.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero namba mbili ya wavuvi wa Ziwa Tanganyika, wanatumia taa lakini kanuni zinawataka wasitumie taa zinazozidi *watt* tano; na kwa chombo kimoja zisizidi *watt* 50. Sasa kulingana na urefu wa kina cha Ziwa Tanganyika, hiyo taa ya *watt* 50 kwa chombo inaweza kwenda chini, yaani *light intensity* kwenda chini ni mita 20 tu. Sasa hao samaki ambao tunasema wako kwenye mita kuanzia moja mpaka 150 tunawapata vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Wizara iingilie kati jambo hili kwa sababu linakuwa ni kikwazo na linasababisha upatikanaji mdogo wa samaki katika Ziwa Tanganyika. Leo hii ukienda Kigoma, kilo moja ya dagaa ni shilingi 28,000/= mpaka shilingi 30,000/=. Hebu ona, mwananchi wa kawaida huyu masikini hatakuwa na uwezo wa kula dagaa ilhali wanavuliwa wanapoona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba sana Wizara itueleze mambo haya wakati wa majumuisho kwamba ni kwa nini tunawazuia wavuvi wasitumie taa ambazo zitaweza kuangaza chini sana? Mapendekezo ya wavuvi wanasema, angalau wapatiwe ruhusa ya kutumia taa ambazo zinaweza kwenda hata mita 200. Kwa hiyo, naomba sana, wavuvi wanasema kama watatumia taa zenye *watt* 200 wanaweza kwenda chini kuona mpaka mita 70 au 80. Kwa hiyo, naiomba sana Wizara, Waziri wewe ni msikivu na Naibu Waziri wako pia ni msikivu, tunaomba sana jambo hili liangaliwe kwa umakini mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa sababu leo sikuwa na mambo mengi. Wavuvi wa Ziwa Tanganyika wana masikitiko makubwa sana. Mbali ya kuwa ziwa la pili duniani lenye kina kirefu, lakini wamesahaulika. Waziri amesema kwamba Serikali imepeleka zaidi ya shilingi milioni 505 katika Ziwa Victoria, lakini ni aibu, Serikali haijapeleka hata shilingi 100/= kwa wavuvi wa Ziwa Tanganyika. Sasa tuambiwe: Je, wavuvi wa Ziwa Tanganyika ni sehemu ya nchi hii au siyo sehemu ya nchi hii? Kwa sababu tunaona hawanufaiki na Ziwa hili Tanganyika ilhali wanaliona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema haya kwa sababu mimi ni mwakilishi wa vijana na wanaojishughulisha na uvuvi, wengi ni vijana. Nisiposema haya nitakuwa sijawatendea haki vijana wenzangu. Nitaomba sana Mheshimiwa Waziri, atuambie kwa sababu kwa taarifa nilizonazo, mbali ya kupatiwa hiyo shilingi milioni 505 *plus,* bado kuna vikundi 20 vya Ziwa Victoria tayari uthamini umekamilika na muda wowote wanapewa mikopo hiyo. Ila Ziwa Tanganyika hatuoni. Kama shida ni vigezo, mtuambie tufanye nini ili tu-*qualify* kupata hiyo mikopo. Haiwezekani tuachwe ilhali tunateseka na sisi ni Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba sana Wizara, watakapokuja kufanya majumuisho, watupatie majibu hayo. Kama sitaridhika na majibu hayo, kwa kweli nakusudia kutoa shilingi kwenye mshahara wa Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumze kidogo sana kuhusu mifugo. Mkoa wetu wa Kigoma una mifugo mingi, lakini huwezi kusikia inasemwa kokote kwa sababu moja tu. Miundombinu ya Mkoa wa Kigoma ni hafifu. Kigoma kuna ng'ombe wengi, lakini leo nikitaka kumsafirisha ng'ombe kumpeleka sokoni ni gharama, yaani ng'ombe mmoja naweza nikatumia zaidi ya shilingi 200,000/=. Kwa hiyo, kama nitamnunua ng'ombe Kigoma kwa shilingi 300,000/= ili nimpeleke sokoni, nitahitaji kuongeza shilingi 200,000/=, mpaka anafika sokoni ni shilingi 500,000/. Je, mimi sokoni nitamuuza kwa shilingi ngapi? Kwa hiyo, siyo kwamba Kigoma hakuna mifugo; ipo, lakini miundombinu siyo rafiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanzoni kulikuwa kuna mabehewa yanabeba ng'ombe, lakini leo mabehewa yamekufa. Kwa hiyo, naomba kwa sababu jambo hili ni mtambuka, Wizara zishirikiane; Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Mifugo, tutakapokuwa na miundombinu ya uhakika tutasafirisha mifugo yetu, tutasafirisha samaki wetu na pia tutaweza kuongeza mzunguko wa fedha katika Mkoa wetu wa Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanzoni wakati Waziri anawasilisha, alielezea vizuri...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. SYLIVIA F. SIGULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Sylivia kwa kuwasemea vizuri wavuvi wa Ziwa Tanganyika. Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo na baadaye Mheshimiwa Tunza Malapo na Mheshimiwa *Eng.* Ezra Chiwelesa wajiandae.

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi nami nichangie hoja ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na jambo moja dogo. Asubuhi wakati Mbunge mmoja anachangia, aliongelea Wizara kutaifisha mifugo wa watu wetu. Katika wilaya yangu ninakotoka, natumaini Mheshimiwa Waziri ananisikia, kuna mwananchi tangu mwaka 2017 ng'ombe wake 111 na kondoo tisa walitaifishwa kwa kisingizio kwamba wameingizwa kwenye Hifadhi ya Burigi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kesi ilikwenda Mahakamani, akafunguliwa Kesi Na. 155 ya 2017 akashinda. Huyo mwananchi siku hiyo hiyo akakamatwa tena akafunguliwa Kesi Na. 56 ya mwaka 2017, akashindwa. Akakata rufaa Na. 35 ya 2019 Bukoba, Mahakama ikaamuru arudishiwe mifugo wake. Mpaka leo tunavyoongea, tangu mwaka 2017 hadi leo anafuatilia ng'ombe wake 111 na kondoo tisa, hajapewa mifugo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Waziri anatoa majumuisho, nitaomba kauli ya Serikali, hiyo mifugo iko wapi?

Kwa nini Wizara haitaki kumrudishia mwananchi ng'ombe wake?

MHE. JERRY W. SILAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Oscar, subiri. Taarifa Mheshimiwa Silaa.

TAARIFA

MHE. JERRY W. SILAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumpa taarifa mzungumzaji kwamba kama mwaka 2017 walikuwa ng'ombe 111 watakuwa wamezaa. Kwa hiyo, madeni ya huyo mwananchi wake aweze kuyaongeza na wale ndama watakaokuwa wamezaliwa kwa muda huo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Oscar, unapokea taarifa hiyo?

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea na huko ndiko nilikotaka kuelekea. Mheshimiwa Waziri huyu mwananchi anaitwa Dunstan kutoka Kata ya Kyebitembe. Naomba wakati unatoa majumuisho utupe kauli ya Serikali. *Whether* Serikali iko juu ya sheria au utatuambia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa mjadala wa asubuhi ilikuwepo hoja ya *NARCO.* Wakati Mheshimiwa Spika anasitisha shughuli za Bunge asubuhi, naye ametoa maoni yake kuhusu *NARCO.*

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Oscar, subiri. Taarifa; Mheshimiwa Esther.

TAARIFA

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa mzungumzaji kwamba hoja anayoiongea ni *valid* sana; na siyo mwananchi wake tu. Tukitaka kusimama hapa kila mmoja, kuna wananchi wengi sana ambao wanapitia hiyo adha. Kwa hiyo, Serikali tu labda ije na mkakati madhubuti kuhakikisha kwamba wale walioshinda kesi warudishiwe mali zao, ikiwezekana na fidia juu. Siyo kwa Muleba tu, ni karibia nchi nzima kuna matatizo kama haya. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Oscar.

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ni suala la kisera na Kitaifa, naipokea taarifa yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Spika anasitisha shughuli za Bunge asubuhi, naye alitoa maoni yake kuhusu *NARCO* na Mheshimiwa Rweikiza amesema asubuhi. Katika Wilaya ya Muleba tunao mgogoro mkubwa na shirika letu la *NARCO.* Katika Wilaya ya Muleba pekee, katika Kata ya Rutoro, tuna mgogoro na *NARCO* wa hekta 50,000. Katika kata zipatazo sita katika Jimbo la Muleba Kusini; Kata za Kyebitembe, Karambi, Mbunda, Kasharunga, Kakoma na Ngenge, tuna mgogoro na *NARCO,* mgogoro wa Mwisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anafahamu, tumeliongelea hili kwa muda mrefu, lakini kutokana na *remarks* alizotoa Mheshimiwa Spika leo asubuhi, namwomba Mheshimiwa Waziri, hii ardhi hekta 50,000 ukiongeza hekta 70,000 ambazo tuna mgogoro nazo, atuachie Wilaya ya Muleba tukapange matumizi bora ya ardhi. Wao kama *NARCO* wabaki kama *regulator* watupe *regulatory oversight* tukapange matumizi bora ya ardhi yetu, tukalete wafugaji ambao tunao katika Wilaya ya Muleba, wanatosheleza. Hatutaki wafugaji kutoka nje, tunao wa kutosha na tutafuga...

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Oscar, pokea taarifa.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kikao pia cha Waziri Mkuu cha tarehe 26 Februari, 2016 pale Kagera alitoa maelekezo kwamba *NARCO* wabainishe mpango bora wa matumizi ya ardhi na kama *NARCO* imeshindwa kuendesha waweze kuipendekeza Serikali wananchi waweze kugawiwa, hasa hilo nilikuwa naomba kumpa taarifa mzungumzaji.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Oscar.

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba ulinde dakika zangu ninaona nina taarifa nyingi leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba wizara na kwa maana hiyo tunaiyomba Serikali suala la Mwisa II kwa Mkoa wa Kagera watuachie, uwezo tunao, watu tunao, na ng'ombe tunao. Wakatupatie utalaam na uangalizi kidogo na ushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Muleba inazungukwa na Ziwa Victoria, nashukuru mzungumzaji wa mwisho amesema Kagera, Ziwa Victoria tumepewa pesa kwa ajili ya mikopo kwa wavuvi wetu, niishukuru Serikali kwa hilo. Lakini Waziri wa Fedha yupo hapa Tanzania tumebarikiwa kuwa na fursa nyingi kwa upande wa bahari, maziwa, lakini ukiingalia tunavyotumia hizo fursa ni aibu ni aibu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa bahari tuna fukwe yenye urefu wa zaidi ya kilometa 1424 zenye kufaa kwa uvuvi ni kilometa 854 ambayo ni sawasawa na asilimia 60 zinafaa kwa ufugaji wa Samaki. Kwa upande wa Ziwa Victoria ninakotokea, tuna ufukwe wa kilometa 3450 ambapo

kilometa 2587 sawasawa na asilimia 75 zinafaa kwa ufugaji wa Samaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia shughuli za uvuvi zinazoendelea na mazao tunayoyapata ni aibu, mahitaji ya Samaki kwa upande wa Tanzania kwa mwaka tunahitaji kati ya tani 700,000 mpaka 800,000 kwa mwaka. Lakini pamoja na fursa tulizonazo, pamoja na bahari tuliyonayo, pamoja na maziwa tuliyonayo tunazalisha tani 389,455 hata hatutoshelezi soko la ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, walichukua dakika zangu, naomba niongezee mbili.

MWENYEKITI: Dakika moja na nusu nakupa.

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaagiza Samaki kutoka nje mpaka sasa na tunalo tatizo la vijana kukosa ajira, sasa tunaomba wizara ituambie ina mkakati gani kuhakikisha kwamba hilo *gap* la Samaki tunaoagiza kutoka nje kwa pesa ya kigeni tunalipunguzaje na kuhakikisha kwamba tuna-*involve* vijana wengi zaidi ili tuweze kwanza ku-*create* ajira, wakati huo huo kupunguza uagizaji wa Samaki nje wakati tuna maziwa, tuna bahari ambavyo vipo, tumepewa tu na Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameongezea suala la kanuni na tozo, niliongelea hapa wakati nachangia Mpango wa Tatu, nimuombe wizara wapitie tozo zote ambazo tunatoza kwenye mazao ya uvuvi wa Samaki. Lakini tunapoongelea tozo tuangalie tunalinganisha na nchi jirani za Kenya na Uganda ambao wote tuna-*share* kwa mfano Ziwa Victoria kwa upande wa bahari tuna-*share* na Kenya na wenzetu Msumbiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusiishi kama tunaishi kwenye kisiwa, tunapotengeneza kanuni tuangalie na wenzetu, mchangiaji aliyemaliza kusema, amesema kina cha Ziwa Victoria na kina cha Ziwa Tanganyika vinatofautiana, kwa

hiyo tunapotengeneza kanuni, tusitengeneze kanuni kwa nchi nzima tuangalie na mazingira ya maziwa yetu, tuangalie mazingira ya bahari, havifanani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja, lakini naomba Waziri atakaposimama atuambie hatma ya ng'ombe wa wampiga kura wangu 111 na Kondoo 9 wapo wapi? na wameshazaa wangapi? na faida yake ni nini? na anamrudishia huyo mpiga kura lini hao ng'ombe wake. Nashukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Oscar tunaendelea na Mheshimiwa Tunza Malapo baadaye Mheshimiwa *Engineer* Ezra na Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah ajiandae.

MHE. TUNZA I. MALAPO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa zawadi ya uhai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati napitia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi nimepata mshituko wa moyo, kwa nini nimepata mshituko, ukiangalia kwa miaka mitano mfululizo wanatenga pesa za maendeleo, lakini haziendi. Kwa mfano nakupa ya miaka mitatu huko nyuma sitaki kurudi, mwaka 2017/2018 walitengewa bilioni nne haikwenda hata sumni, mwaka 2018/2019 Sekta ya Uvuvi peke yake ilitengewa bilioni saba ikapewa bilioni nne, 2019/2020 ilitengewa bilioni 14 ikapewa bilioni tatu, mwaka huu ambao tunaumaliza kesho kutwa 2020/2021 walitengewa bilioni 13 mpaka leo wamepewa bilioni nne.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kilichonishtua nini? leo wametengewa bilioni 99, ikiwa bilioni nne, bilioni 13 zinawashinda kupeleka, hizi bilioni 99 wanazitoa wapi? Ndio maana nakwambia nimeshituka, sasa Mheshimwa Waziri atakapokuja kuhitimisha atueleze mkakati wao, kutengwa kwa pesa nyingi maana yake tunaraji tukapate maendeleo makubwa kwenye hizo sekta kwa sisi ni furaha yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, furaha hii inakwenda kuingia huzuni kwa sababu walikuwa wanatengewa kidogo, lakini haziendi mpaka huu mwaka tuliopo sasa hivi tupo mwezi wa tano tunaumaliza wamepewa asilimia 31 tu katika bilioni 13, leo wanapata wapi *courage* ya kutenga bilioni 99, nataka akija hapa atueleze ni kitu gani hicho kilichowapelekea wao kufikiria watapata bilioni 99, hatutaki maneno, maneno tunakata vitendo. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mshtuko wangu wa pili, sisi Watanzania tuna maziwa makubwa, tuna Ziwa Victoria, tuna Ziwa Nyasa, tuna Ziwa Tanganyika, sisi watanzania tunaukanda mrefu sana wa bahari, sisi Watanzania tuna *deep sea*, bahari kuu maana yake. Unaamini kwamba kwa mwezi tunaagiza samaki tani 24,000 zinaingia nchini kwetu, pamoja na kuwa na hivyo vitu vyote, nimepata mshituko kwa sababu safari hii wakati naelekea kuchangia Wizara hii niliamua nijipe muda kidogo nisome, kwa hiyo huo mshituko wangu wa pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshtuka kwa sababu sisi kama Taifa tunatumia takribani bilioni 58 kwa mwezi kuagiza samaki nje, tuna Bahari ya Hindi, tuna Ziwa Victoria, tuna Ziwa Tanganyika, tuna Ziwa Nyasa. Mheshimiwa Waziri akija kuhitimisha atupe majibu tunakwama wapi? na kwa nini tunakwama? Mwenyezi Mungu atupe nini? kwa kiasi cha maji tuliyokuwa nayo sisi na hivyo nimekutajia makubwa, tunayo madogo karibia kila mtu kwao hapa utakuta kuna bwawa, ukienda Morogoro bwawa Mindu sijui huko wanavua, sijui nini, kuna mito midogo midogo watu wanavua, nimekutajia haya makubwa. Tuna sababu gani ya kuagiza Samaki wengi hivyo kutoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati naendelea kutafuta baadhi ya sababu ndiyo hizi zingine kwa sababu hela haiji, hela kama haiji wizara inashindwa kuwekeza, ama wizara haina mikakati thabiti kwa sababu gani, binafsi yangu sifikirii mpaka leo wavuvi wetu waingie baharini wakatafute Samaki wakati, yaani wakienda na ile kwamba Mungu akipenda

nitapata. Kuna vifaa vya kisasa vinavyotambua tu kwamba ukiingia baharini sehemu fulani ndiyo Samaki wapo wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unamwomba Mungu, lakini Mungu huyo ndiyo katupa sisi maarifa, Mheshimiwa Ulega wewe hii ni taaluma yako na unaijua, unatakiwa uwe *serious my brother* sasa hivi tunatakiwa twende kwenye uvuvi wa kisasa, jamani Samaki tunawaacha huko baharini kama mnakumbuka ile meli iliyokuwa inaitwa meli ya Magufuli hivi wale walivua Samaki kiasi gani? wenye ukubwa gani? nyinyi wote hapa ni mashahidi, lakini leo sisi tunavua Samaki ndio hao wanakujaga kupimwa na *ruler* hapo kwenye kantini. Maana yake hata kile kimo hajafika kwa sababu gani, kwa sababu ya kukosa zana bora za uvuvi, Serikali iwekeze hapo ndipo tunapofeli haya matatizo yote yanatokea hivyo, leo mwenzangu hapa jirani yangu wakati anachangia alikuwa anasema matumbawe yanaharibiwa, lazima yataharibiwa si wanatafuta mabomu, akipiga pale anapata samaki wake anarudi nao nyumbani, hana zana bora unategemea atavuaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, twendeni tukawekeze hapo. Uchafuzi huu wote watu kuhangaika kukimbizana na samaki wadogo wadogo hakuna mtu anayetaka apate samaki kidogo ama apate samaki wadogo ni kwa sababu anakosa dhana bora za uvuvi. Badala ya kukimbizana kuchoma nyavu fanyeni jitihada za makusudi mwambie mtu nyavu hii usivulie, vulia kifaa hiki, hakuna mtu anayependa maisha magumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa jambo moja dogo, lakini lina umuhimu wake. Sisi wanawake tuliowengi ndio wafugaji wa kuku, tuliowengi, iwe wale wa kisasa iwe wa kienyeji hata mwenyewe nafuga kwa kiasi kidogo, lakini nafuga. Kuna changamoto kubwa sana kwenye sekta hiyo na wanawake wengi ndio wanaponea huko, hiyo mikopo ya halmashauri ya asilimia kumi sijui nini wengine wanachukua kwenda kufuga. Hata hivyo, tunapata changamoto, kwanza upatikanaji wa vifaranga siyo wa

uhakika, unaweza kutafuta kifaranga leo mwezi wa tano ukaambiwa *order* utaipata mwezi wa tisa, jiulize tangu leo mpaka mwezi wa tisa hapo hiyo hela unaifanyia nini. Ukipata kifaranga chakula bei juu, ukipata chakula chanjo hazieleweki, unaweza kuweka kuku bandani umewapiga chanjo zote wakaja kufa usitoke hata na kuku mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Serikali iweke mkakati wa makusudi wa kunusuru wanawake na hata wanaume ambao wanafuga kwa kuhakikisha wanapata huduma bora za usaidizi, wanapata chakula kwa bei nzuri ili kusudi iendane na soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo mengi yenye umuhimu, nakushukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Tunza Malapo kwa mchango wako tunaendelea na Mheshimiwa Eng. Ezra Chiwelesa na baadaye Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah na Mheshimiwa Yustina Rahhi wajiandae.

MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii pia niweze kuchangia kwenye hotuba hii ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, nadhani nianze kwanza kwa kuipongeza Wizara kwa hotuba nzuri ambayo wameitoa, lakini pia niseme tu jambo moja, nitapenda zaidi kujikita kwenye sehemu ya mifugo hasa kwenye masuala ya ng'ombe kwa sababu mwenyewe historia yangu nimezaliwa kwa wafugaji, nimechunga sana ng'ombe nikiwa mdogo, kwa hiyo, kidogo ni kitu ambacho nakielewa na nimekiishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa haraka kuna jambo moja ambalo nimekuwa najiuliza alichangia mwenzangu bwana Maganga hapa tangu zamani hata kabla sijaingia kwenye siasa nimekuwa najiuliza kuhusu wafugaji wa Tanzania. Yaani wafugaji wa Tanzania wamekuwa kama yatima *always* ni watu ambao ni watu wa kufukuzwa fukuzwa, ni watu ambao wanaonekana

wanakosea kosea kwenye vitu vyao vingi wanavyovifanya, sasa nikawa niwaza Wizara ya Mifugo mnajua kwamba mna mtoto ambaye ni mfugaji na bado anakimbikizwa kimbizwa, lakini bado hamchukui hatua ya kum-*protect*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayasema haya kwa sababu wafugaji hawa sijui wanamakosa gani, kwa mfano kwa upande wa Biharamulo ni eneo ambalo tuna mifugo mingi sana na baada ya kuingia hasa wakati wa kampeni nimekuwa nikiuliza maelekezo ilikuwa ni kwamba tuna-*ranch* zimetengwa Karagwe, *ranch* zimetengwa Misenyi sasa nikawa najiuliza Mkoa mzima wa Kagera tutaenda kufugia Karagwe na Misenyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba labda tusaidiane kwenye jambo moja, wafugaji wetu wa Kata ya Kaniha kuna Kijiji pale kinaitwa Kijiji cha Mpago, wiki mbili zilizopita bwana mmoja wamemkamata ng'ombe wake akatozwa faini shilingi milioni saba, mwingine naye akatozwa faini ya shilingi milioni tano, *reason* ng'ombe wameingia kwenye hifadhi ya *TFS.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikawa najiuliza swali moja wewe ni mfugaji, *let say* ni mfugaji, nafuga kule kwa sababu tumehamasishwa kufuga, nipo Bungeni hapa sasa hivi vijana wanaochunga ng'ombe wapo karibu na hifadhi ng'ombe wameingia mle, mtanzania yule anatozwa shilingi milioni saba *at per* kama hajatoa milioni saba ng'ombe wote sabini wanaondoka najiuliza hata Waheshimiwa Wabunge tumo ndani leo tukimnyanyua mtu milioni saba ambayo haikutegemea papo aitoe hapa sidhani kama kuna mtu yupo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe wale watu wapo maskini, wapo vijijini kule ni maskini kabisa, faini ya kumtoza mtu shilingi milioni saba mtu ambaye juzi Kijiji cha Mpago kamati iliyoundwa wamesogeza mipaka, hawajaweka alama *TFS*, lakini wafugaji wetu wameshaanza kukamatwa wanatozwa hela yote hiyo, lakini hawa ni Watanzania tunahamasisha kwamba ufugaji uendelee,

mnalenga leo kutengeneza maziwa kutoka lita bilioni 2.7 mpaka lita bilioni 4.5 yatatoka wapi kama hawa watu wapo *disturbed* kiasi hiki na hawana sehemu ya kulishia ng'ombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya CCM imeahidi ukurasa wa 51 kwamba tunataka tuongeze malisho, sehemu ya kulishia kutoka hekta milioni 2.7 mpaka hekta milioni sita. Sasa hizi hekta milioni 2.7 na hekta milioni sita kutoka hapo hiyo *range* tunaipata wapi? sisi wananchi tunaipata wapi kama siyo Wizara ya Mifugo ndiyo itabidi ifanye kazi hiyo ya kuitafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo maeneo ambayo mnataka muyaongeze nani anayamiliki, tungekuwa tunamiliki wananchi wenyewe tungepeana, lakini yanamilikiwa na Serikali kupitia *TFS.* Sasa tunachowaomba ndugu zangu wa mifugo, ninachowaomba kwa niaba ya wananchi wangu sisi tuna eneo kubwa sana Kata ya Nyantakara pale tunaomba mfunge safari mje Biharamulo muwaambie wafugaji wa Biharamulo kwamba eneo lipo hapa kaeni na *TFS,* maana Biharamulo kwa sehemu kubwa tumezungukwa na mapori, kwa nyuma huku tumezungukwa na hifadhi ya Burigi Chato ambayo *off course* tunashukuru Mungu watalii wataanza kuja tutapata fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine yamehifadhiwa wananchi hatuwezi kwenda kuomba *TFS* hawatatuelewa ila wewe *custodian* wa mifugo ni kazi yako kuwatafutia wafugaji wako maeneo. Nyie mwende mkaongee na Serikali maana Serikali kwa Serikali mnashindwanaje? Ila wananchi huku wanaumia, nayaongea haya kwa uchungu kwa sababu wakazi wa Biharamulo tunajua tulivyoteseka na haya mapori. Sasa mnavyoyaacha mnataka wale jamaa warudi tena waanze kutuimbisha mtaji wa maskini nguvu zake mweyewe, tumeteseka mno tulikuwa tunashushwa kwenye magari usiku tunapigwa viboko, leo tumeshakaa vizuri sasa maeneo haya iyambieni *TFS* nyie watu wa mifugo wawakatie maeneo wafugaji wa Biharamulo wapate eneo la kufugia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina haja ya kushika shilingi, lakini ninachoomba sasa nyanyukeni mkae na wenzenu wa maliasili kwa sababu maliasili hatuwezi kuomba sisi, waombeni nyie watenge maeneo ili wakazi wa Biharamulo wapate maeneo ya kufugia, nina wafugaji wengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa imekuwa ina-*prompt* watu maliasili wapo hapa, mwezi wa pili nadhani walikuja wakamfukuza mkuu wa *TFS* pale na viongozi wengine, wafugaji wa Biharamulo wamekuwa wanalipa pesa, wanachanga, pesa nyingi mpaka milioni 50 wanawalipa viongozi, viongozi halafu wanawaruhusu wanaingiza ng'ombe, angalia mfugaji huyu anavyodhulumika, kwamba hana eneo la kuchungia inabidi amlipe mtu wa *TFS* amruhusu aingie yaani Mtanzania mwenyewe hata eneo la kuchungia ng'ombe unanunua, lakini bado Serikali ipo hapa inasema inataka ikuze ufugaji, kwa hiyo naomba hili jambo mliangalie nyanyukeni mkatusaidie na hapo. Sina haja ya kuendelea sana kwenye masuala hayo nadhani mmenielewa, rafiki yangu Mheshimiwa Ulega unaniangalia umenielewa vizuri njoo unisadie ili wakazi hawa wa Biharamulo wapate eneo la kufugia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo jambo moja nimekuwa naliangalia kuhusu ufugaji wa Samaki, kwangu kule mwanzo watu walihamasishwa wafuge samaki, watu wengi sana wamechimba mabwawa kwa ajili ya kufuga samaki mabwawa yale yamekauka hayana maji na watu wengi sana wamepata hasara, sasa ameongea sana bwana Mheshimiwa Mwijage hapa asubuhi Mheshimiwa Mwijage ni mtaalam sana wa mambo ya samaki kwa sababu mpaka anaandaa na vyakula *issue* ya kufuga kwa kutumia *cage*, lakini si kila mtu yupo karibu na ziwa, kutoka kwangu Biharamulo mpaka nifike Chato ziwani ni kilometa 50 siwezi kuwaambia wakazi wote wa Biharamulo sasa washuke Chato kwenda kufuga *cage* fifty kilometers unaenda ukaweke cage pale ukatafute eneo *its difficult.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba sana Serikali mnisikilize katika hili bado tunaingiza Samaki *all most fifty-eight billion* tunaingiza *value,* lakini kwenye Ilani ya CCM ukurasa wa 55 tumesema tunataka tuongeze idadi ya vifaranga vinavyofugwa katika vituo vyenu vile vinne vya Ruvuma, Iringa, Morogoro na Tabora ifike vifaranga milioni tatu, sasa hao vifaranga milioni tatu tunamuuzia nani kama watu wanajenga mabwawa, wakishajenga mabwawa maua yanakauka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichokuwa naomba nataka nitolee mfano, kwa mfano Biharamulo tulikuwa na mradi mkubwa wa maji ambao umekuwa *design* kwa ajili ya kutuhudumia pale kwa sababu tupo mbali na ziwa na hatuna *access* ya maji. Mwanzoni walikuwa wame-*design* wachimbe bwawa kubwa ambalo bwawa litakuwa linakusanya maji ya mvua kwa mwaka mzima, lakini bahati nzuri tutapata maji ya maziwa ambayo yatakuja kama Ilani ilivyoahidi, kwa hiyo mpango wa bwawa umeisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikaja na hii *idea; Don Consult* ndiyo *wali-design* ile kitu. Sasa nilitaka mfanye *pilot project* kwa kuanzia kwangu. Mje mwombe pesa, ongeeni na Don mchimbe lile bwawa pale kwetu Biharamulo. Bwawa lile litumike kwa ufugaji. Watu waliokuwa wanataka kufuga kwa kutumia vizimba sasa kule ziwani waje wafugie pale, *then you will be charging them.* Kwa sababu, kukuza wale vifaranga mnakosema, mtapata wateja pale. *Is a business mind,* mnaweza mkaja pale mkachimba lile bwawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkishachimba bwawa, maji yanaingia pale; watu wa kufuga kwa *cage* waje, lakini mtawa-*charge* kadri mnavyowakatia maeneo. Watafuga pale, mtakapokusanya fedha mnahamia sehemu nyingine, mnatengeneza bwawa lingine, maana yake tunatengeneza samaki *fresh,* hata mtu asiyekuwa karibu na ziwa aweze kupata samaki *fresh,* siyo wa kwenye friji. Maana samaki wanasaidia hata kukuza *brain* za watoto. Wote ni mashahidi hapa, kwa wenzangu wanaotoka Ukerewe kwa Kanda ya Ziwa, waliozaliwa mle visiwani, huwa tunasema kwa Kanda

ya Ziwa watu wa Ukerewe wana *ma-professor* wengi sana. Kwa sababu gani? Samaki wanaoishi nao mle ziwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba hili jambo mliangalie, mtusaidie, mje mjenge mabwawa. Mabwawa muwakodishe wafugaji, ambao watafuga na watakuwa wanalipa *as time goes on* huku mkikusanya fedha mnapeleka sehemu nyingine. Tunafungua watu kibiashara na vile vile tunapunguza fedha ambazo tunaagiza sato na samaki wengine kuwatoa nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, kwa sasa yalikuwa ni hayo mawili, niseme kwamba naunga mkono hoja. Nategemea haya ambayo nimeyasema, tutapata majibu sahihi na ya uhakika ili wananchi hawa walioniagiza mambo ya ufugaji wapate *solution* kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Eng. Ezra. Tunaendelea sasa na Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah na baadaye Mheshimiwa Justina na Mheshimiwa Shally Raymond wajiandae.

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja iliyopo mezani ya Wizara ya Uvuvi na Mifugo. Kwanza nianze kumpongeza Waziri pamoja na Naibu wake na timu nzima ya Wizara yake kwa kuwasilisha bajeti yao ya kipindi hiki cha mwaka 2021/2022 katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kutuunganisha Wabunge wote wa mikoa hii ambayo tunatoka maeneo ya ukanda wa bahari na kuweza kufanya kikao cha pamoja na kuchambua changamoto mbalimbali zinazowakumba wavuvi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Bashiru, aliyekuwa Katibu wa Chama cha Mapinduzi Taifa kwa kusimamia vizuri uandishi wa Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi. Ilani yetu imeeleza vizuri katika eneo hili la sekta ya mifugo na uvuvi kwa lengo la kutaka kuleta mapinduzi makubwa na kuzifanya sekta hizi ziweze kukuza uchumi, kukuza ajira, kuendelea kuwekeza kwenye viwanda vidogo vidogo na kuendelea kuleta ustawi wa wananchi wetu ambao wamejiajiri katika sekta hizo na hatimaye kuongeza kipato na kuleta mapato makubwa kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Waziri na timu yake kwa sababu mengi wameyazingatia, lakini nina mashaka makubwa sana katika utekelezaji wake. Kwa sababu fedha ya maendeleo inayoletwa katika sekta hizi ni ndogo sana. Pamoja na kwamba kuna mipango mizuri ya utekelezaji wa kipindi hiki cha 2021/2022, kama fedha hazikuja kama ambavyo tunatarajia, maana yake yale yote mazuri ambayo tunayategemea katika kuleta mapinduzi makubwa katika sekta hizi itakuwa ni kazi bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba sana Wizara ya Fedha, kumekuwa na changamoto kubwa sana ya utolewaji wa fedha katika sekta mbalimbali. Namwomba sana Waziri wa Fedha Mheshimiwa Mwigulu Mchemba aangalie namna gani atahakikisha anasimamia Sheria ya Fedha kupeleka fedha kwa wakati ili Wizara hizi ziweze kusimamia utekelezaji wa mambo ambayo tunayapanga na kuhakikisha kwamba tunaleta maendeleo kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kwamba Mpango wa Tatu wa Taifa umeelekeza nguvu kubwa sana katika uwekezaji wa uvuvi wa bahari. Naipongeza Serikali kwa sababu wameanza kwa kasi nzuri ya kuwekeza Bandari ya Mbegani na kwa kununua meli ya kuanza kufanya kazi katika sekta hii ya uvuvi. Hata hivyo, tukumbuke tuna wavuvi wadogo wadogo katika maeneo yetu; na sekta hii watu wengi wamejiajiri kwa sababu, sisi wazaliwa wa maeneo ya

Pwani tangu wazee wetu, kazi kubwa ilikuwa ni shughuli ya uvuvi. Kwa hiyo, vijana wetu, watoto wetu, baba zetu, wamerithi kutoka kwa mababu zetu kufanya shughuli hii kuweza kujipatia kipato na kuweza kuendelea kumudu maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo iliyopita, kumekuwa na changamoto kubwa sana ya kupata manyanyaso makubwa kwa wavuvi wetu. Hatutegemei kutokea yaliyotokea. Ndugu yangu Naibu Waziri, Mheshimiwa Ullega alikuwepo anayajua na ndugu zake wa Mkuranga, Lindi, Pwani na maeneo mengine Dar es Salaam anajua changamoto ambazo zimewakumba wavuvi wetu. Tunaiomba sana Serikali kuzingatia kwa sababu, wavuvi wetu wengi wamepoteza Maisha, wavuvi wengi *wame-paralyze* kwa kupata *pressure,* wavuvi wengi ndoa zao zimeharibika kwa sababu ya maisha yao kutoenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mvuvi mdogo ni mtu masikini sana, anapoingia baharini anapata samaki wa kumwezesha yeye kupata kipato na kuweza kumudu kuendesha maisha yake. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali kuhakikisha kwamba tunasimamia kwenye eneo hili ili wavuvi wetu wasibughudhiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapotunga sheria na kanuni tuzingatie katika maeneo husika. Unapomtaka mvuvi mdogo akavue mita 50 kwenda chini ya bahari na boti yake aliyokuwa nayo ni dhaifu, hana vifaa vya kisasa, hivi unategemea huyu unamtakia maisha mema kweli! Naiomba Serikali kutazama namna bora ya kuhakikisha kwamba tunawasaidia wavuvi wetu wadogo wadogo ili kutengeneza ajira na waweze kumudu maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kuhakikisha kwamba tunawaweka sawa wavuvi wetu wadogo kwa kuwapa elimu, lakini kuwawezesha kupata mikopo waweze kununua vifaa vya kisasa na waweze kuingia baharini

kuweza kufanya shughuli zao. Huwezi kuanza jambo kubwa kama hujaboresha katika jambo dogo. Kwa hiyo, naiomba Serikali kusimamia katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mara nilikuwa namfuata Waziri karibia miezi mitano sasa, kila tukikutana ajenda inakuwa moja ya ujenzi wa Chuo Kikuu cha Masuala ya Uvuvi na Usafirishaji Majini. Sisi pale Lindi Manispaa tumetoa tayari ekari 150. Kwa hiyo, naiomba Serikali, Waziri atakapokuja *ku-wind-up* atuambie ni lini wataanza kujenga chuo hiki ili tuwekeze katika rasilimaliwatu kuhakikisha kwamba baadaye tutapata wataalam watakaokuja kusimamia sekta hii ya uvuvi na usafirishaji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Lindi tumebahatika kupokea wafugaji. Wafugaji hawa mmetuletea lakini hamjawatengenezea mazingira ya wao kuweza kuishi vizuri. Imekuwa mwenye nyumba anaombwa na mtu mmoja kwamba nina familia ya watu 20, naomba niwalete kwako. Unapowaleta unawaacha, huwahudumii, huwatengenezei mazingira yoyote. Wafugaji hao wanahangaika, hawana maeneo ya kulisha mifugo yao na badala yake wanavamia mashamba ya watu na kusababisha migogoro mbalimbali. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kuhakikisha kwamba wafugaji waliokuja katika Mkoa wetu wa Lindi, watengenezewe mazingira mazuri ya kuishi ili waweze kufanya shughuli zao za ufugaji. Pale Lindi hatuna shughuli za ufugaji, sisi tumezoea kuishi kwa kuvua, tunakula samaki, lakini bado tunahitaji kula nyama ili tuendelee kuboresha afya zetu. Kwa hiyo, Serikali ifanye kila namna ya kuona namna gani wanaweza kuboresha wafugaji waliowaleta kwetu Lindi. Wana familia zao, wanahitaji kuishi vizuri, watoto wao wanahitaji kusoma, kwa sababu maisha yao hayaeleweki, hawana uhakika wa kuishi;

mara leo wako hapa, kesho pale, kesho kutwa kule. Kwa hiyo, hali siyo shwari. Naomba Serikali isimamie suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti...

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa. Nimekuachia kidogo umalizie, muda wako ulikuwa umeisha. *(Makofi)*

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Justina Rahi, baadaye Mheshimiwa Shally Raymond pamoja na Condester Sichalwe, wajiandae.

MHE. JUSTINA E. RAHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa takwimu ya sasa ni kweli kwamba Tanzania ni ya pili katika Afrika kuwa na mifugo mingi baada ya Ethiopia. Mifugo hii mingi hii, asilimia 90 ni kosafu ya asili; na kwamba asilimia 96 ya mifugo hii huchungwa na wafugaji wa kuhamahama na wafugaji wakulima. Hata hivyo, mifugo hii katika tasnia ya nyama inachangia asilimia 90 na maziwa inachangia asilimia 70; na kwamba takribani inatoa vipande vya ngozi milioni tano, kwa maana kutoka ng'ombe vipande milioni 2.6 na wanyama hawa wadogo mbuzi na kondoo vipande milioni 2.6. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na baraka ya namna hii, Tanzania ambayo ni ya pili Afrika kwa kuwa na mifugo mingi, lakini ni ya tatu kwa utapiamlo wa udumavu. Inasikitisha, kwa sababu asilimia 45 ya Watanzania wana udumavu; na athari ya udumavu ni kuathiri ukuaji wa akili pamoja na ukuaji wa mwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimehusisha hizi kwa sababu gani? Lengo la msingi la ufugaji halijaweza kutimizwa kwa sababu tunapofuga lengo la kwanza ni kujitosheleza kwa chakula, ni lishe; na lengo la pili ni ziada sasa ili tupate fedha kwa ajili ya kujipatia maisha bora; elimu bora, maji salama, makazi salama na afya nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukija kwenye lishe ndiyo tunaona, kwa mfano, Watanzania wanakunywa wastani wa lita 47 ya maziwa kwa mwaka, badala ya kiasi kinashoshauriwa cha lita 200 kwa mwaka. Watanzania hawa wanakula wastani wa nyama kilo 15 badala ya kilo 50 kwa mwaka kwa mtu mmoja na wanaweza kula mayai takribani 106 badala ya mayai 300 kwa mwaka kwa mtu mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ziko nyingi na changamoto. Unaona kwamba upatikanaji wa bidhaa hii ya mifugo ni mdogo, lakini kwa nini? Kwanza, tunakuja kwenye changamoto ya kosafu, hatuna sehemu yoyote ya kumlaumu huyu mchungaji au mfugaji. Atatoka asubuhi na mifugo yake ataenda kuchunga akirudi jioni anakamua lita moja au lita mbili ya maziwa. Atachunga ng'ombe wake huyu miaka mitano, sita akienda kuuza anaishia kwenye kilo 60, 70 anauza kwa shilingi 200,000/= pamoja na muda wote anaoupoteza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri sasa mkakati wa kwanza ni kwenye kwenda kubadilisha kosafu ya mifugo. Hii mifugo haina tija. Haya mambo yanawezekana. Nitoe mfano mdogo tu kwa wakulima. Hata hao wakulima zamani walikuwa wakitumia mbegu zao za kienyeji, lakini baada ya Serikali kuleta mbegu ya ruzuku kupitia vocha, wakulima wametoka kwenye kuzalisha ile gunia tano au nane kwa ekari, sasa wanazalisha gunia 15 mpaka 20, hawatarudi huko nyuma. Kubadilisha kosafu faida yake ni kwamba, wakulima watapunguza kundi kubwa la mifugo ambalo halina tija na linaharibu mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ziko nyingi za kuweza kuboresha mifugo; kuna magonjwa ya mifugo ambayo sisi tunaweza kuepukana nayo, ukiacha magonjwa ya milipuko. Kwa mfano, kupe na minyoo ni tatizo kubwa kwa mifugo, lakini kumbe mwarobaini wake ni kuwa na majosho. Tufanye *proper dipping*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji siku hizi wengine wanapaka paka tu mifugo kwa kutumia *spray*, lakini ile sheria ya zamani kwamba ng'ombe wote wa Kitongoji, ng'ombe wote wa Kijiji wanaogeshwa kwa pamoja sasa hivi wameacha. Kwa hiyo, wakiogeshwa kaya fulani, kaya nyingine hawajaogeshwa, ina maana lile tatizo la kupe lipo na ndilo linalosumbua. Ndiyo maana tunaona asilimia ya vifo vya mifugo ni kutokana na magonjwa ya kupe. Kwa hiyo, tuna uwezo mkubwa sana wa kuangamiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna majosho ya toka zamani ya wakoloni, yamechakaa huko vijijini, ni mabovu. Ni kwa nini sasa Wizara isihakikishe kwamba maeneo yote ya wafugaji wana majosho ya kuogesha mifugo yao ili kuachana na tatizo la kupe na kuondoa minyoo kwa mifugo ambayo pia inachosha mifugo yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni hili la wafugaji wetu kuhangaika kwa ajili ya ukosefu wa wataalam wa mifugo. Mfugaji siku hizi anatibu mifugo yake mwenyewe, lakini tunatengeneza *u-resistance* wa magonjwa. Kwa sababu, wanapiga *dose* kubwa, wanachanganya madawa haya kwa ajili ya kukosa maelekezo. Kuna umuhimu sana wa kuboresha huduma za ugani na wataalam wa mifugo wakakaa karibu. Hili siyo kundi la kudharau, kundi la wafugaji ni wakubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ifikirie namna gani sasa kurejesha; kwanza tulikuwa na *veterinary centers* kwenye kata, zimekufa; mfugaji hawezi kujua hata mahali pa kwenda, anabahatisha tu. Marafiki wa karibu wa wafugaji sasa wamekuwa *ma-agrovet*. Akifika kwenye maduka ya wakala ndio ashauriwe dawa hii na dawa hii; na wale ni

wafanyabiashara, anaweza akamshauri mfugaji dawa ni hii akachanganya dawa za aina nyingi pengine bila kujijua. Kwa hiyo, utaalam bado ni muhimu kama tunataka kuwasaidia hili kundi kubwa. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hatupati tija kwa sababu usindikaji unafanyika kwa kiwango kidogo sana. Tuna viwanda takribani 81 vya kusindika maziwa; na vingekuwa na uwezo wa kusindika lita hata milioni 276, lakini kwa sasa vinasindika lita milioni 56 hivi kama sikosei. Ni kwamba maeneo ya wafugaji ni maeneo yapo ndani, hizi lita mbili, mbili au lita tano, tano, kama tungeweka *collection centers* huko kwenye maeneo ya wafugaji vijijini au kwenye Kata, hizi zingeweza kukusanywa, zikapelekwa kiwandani na tukawa na maziwa mengi, tukaongeza hata hiki kiwango cha unywaji wa maziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hebu tuwaambie kuwa Halmashauri pengine kwa Wakurugenzi, maeneo ya wafugaji mara nyingi wanakaa mbali na soko. Soko ni miji ile midogo, hakuna mtu anaweza kutembea kilomita 30, 40 kupeleka lita mbili au tatu ya maziwa. Kungekuwa na *collection center* wapeleke maziwa, bado ingekuwa ni kipato kizuri tena hasa kwa akina mama. Maana anajua ukipeleka maziwa kuanzia Jumatatu, Jumanne, Ijumaa anapokea hela yake ya lita tano, tano; ni nyingi ingeweza kufanya kitu kikubwa.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. JUSTINA E. RAHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hizi *collection centers* ni muhimu kwa ajili ya... *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umeisha.

MHE. JUSTINA E. RAHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. tunaendelea na Mheshimiwa Shally Raymond na baadaye Mheshimiwa Condesta Sichalwe pamoja na Mheshimiwa Godwin Kunambi wajiandae.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Kipekee namshukuru Mungu kwa zawadi ya uhai. Niunge hoja mkono nisije nikasahau kwa sababu hii Wizara ni muhimu sana kwangu japo siku zote naishia kuomba kuomba, lakini wananchi wangu hawafikishiwi maombi yangu wala hawajibiwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo ni Wizara ambayo kwa kweli kila mtu anastahili kuwa karibu kwa sababu, sisi kina mama tukishajifungua siku hizi unaambiwa miezi sita wasinyonyeshe, lakini baada ya hapo mtoto anaweza akapewa maziwa mengine kidogo; na kama wewe ni Mtanzania mzuri, basi utamchanganyia maziwa ya ng'ombe au kama kuna wale wenye mbuzi wazuri, maziwa ya mbuzi kidogo, mtoto anaendelea kunyonyeshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mara chache sana utakuta mama wa Kitanzania anapenda maziwa ya unga. Sasa naomba kuiambia Wizara hii kwamba, hiyo mifugo tunayohesabiwa kwamba iko ranchi, ng'ombe milioni 33, lakini sasa tunaambiwa ng'ombe wa maziwa ambao ni mitamba itasambazwa milioni moja na ushee. Sasa naangalia, hivi hiyo milioni moja na ushee itakayosambazwa Tanzania kwa ruzuku, itawafikia wafugaji wangapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hiyo *figure* iangaliwe vizuri, kwa sababu Kilimanjaro, wakati amekuja kuzindua kampeni, Waziri Mkuu aliombwa; tunaomba mitamba ya ng'ombe, tunaomba mbuzi wa maziwa na pia aliombwa, vifaranga wa kuku wa kienyeji kwa kila mwanamama. Huko Kaskazini Kilimanjaro sisi hatujui kusweka ng'ombe, wanafuga kwenye *zero grazing*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwombea sana Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Mungu amlaze mahali

pemba Mbinguni kwa sababu peke yake ndiye aliwafanyia wale watu wakafuga kwa faida kwenye miaka ya 85 mpaka 87. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, alitoa mitamba bora na leo nimemsikia hapa ametajwa Mheshimiwa Kimiti, alikuwepo kwenye Bunge hilo. Mitamba ile ikasambazwa ndiyo wakabadili kutoka kwenye ile *indigenous breed* wakaja kwenye *hybrid.* Kuanzia wakati huo, wakaweza kukamua maziwa lita 20 kwa ng'ombe mmoja kutoka lita mbili kwa ng'ombe. Sasa, ni kipindi kirefu na mpaka sasa wameshapoteza ile mbegu. Kwa hiyo, uzalishaji umeshuka, namuomba sana Waziri wa Mifugo ambaye amezoea ng'ombe wengi lakini sijui wanakamua kiasi gani atufikirie tena Kaskazini tupate hiyo mitamba mizuri. Kopa ng'ombe, lipa ndama! Na hapo ndiyo tutaweza kuboresha tena mifugo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba kama zoezi hilo litafanikiwa basi hata uchumi wa wananchi kule utabadilika. Lakini sio hiyo tu kwa ajili ya ng'ombe wa maziwa. Hata hawa ng'ombe wanaofugwa nje, nadhani hali sio nzuri. Ng'ombe ana kilo 100 hadi 120. Ng'ombe mzuri anatakiwa awe na kilo 300, mzungumzaji aliyezungumza kabla yangu ameeleza vizuri sana na mimi nasisitiza kwamba ni bora sasa tukaingia katika ufugaji wa tija kuliko ufugaji huu wa kuangaliangalia tu kubahatisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii nihame sasa kwenye ng'ombe lakini nimalizie kwa kusema ng'ombe wakiwepo nyumbani tunapata samadi ambayo inaboresha mashamba yetu ikiwemo kahawa. Ni juzi tu kimefunguliwa kiwanda cha viatu vya Ngozi pale Karanga. Tunategemea ng'ombe hawa hawa wa Tanzania watupe Ngozi nzuri na sio tukaagize ngozi kuja kutengeneza viatu hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nihamie sasa kwenye eneo ambalo nina *passion* nalo. Kuku wa kienyeji. Niwapongeze sana ALVI wameweza kuja na mbegu ya Horace, katika ule ukurasa wa 11 tumeelezwa ambayo itaweza sasa

kutengeneza kuku wa asili ambao ni wazito na ambao wanaweza wakatoa kilo nyingi na mayai mengi.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Ninachoomba tu...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Shally subiri taarifa ya Mheshimiwa Dkt. Mwigulu.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO; Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mchango mzuri anaotoa mama yangu Mheshimiwa Mbunge pale. Kama ilivyo na ndizi Moshi, Bukoba, mchele wa Kyela na Shinyanga kuku wote wale anaowasema wa kienyeji ni kuku wa Singida na Dodoma, hiyo ni Fahari ya Makao Makuu. Akisema wa asili inaanza kuonekana kama dawa ya kienyeji hivi. Kwa hiyo, aseme kuku wa Singida na Dodoma. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Shally.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea Taarifa, lakini nataka tu nimwambie kwamba kisayansi hilo jina la mkoa alioutaja bado halijaingia na nachangia kutokana na hotuba ya Mheshimiwa Waziri na haya majina ninayoyatamka ndiyo yaliyoandikwa. Lakini, Tanzania tunajua. Hata ukifika Chako ni Chako unauliza kuku wa Singida wapo, lakini kwenye vitabu bado kuku wa Singida hamna. Kwa hiyo nishukuru sana kwa hilo na atakapopelekewa maombi kwamba anigawie kidogo ili wafike kule Kilimanjaro basi asiwe mchoyo kwa vile yeye ndiyo mwenye fungu lote lile la fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe pia pongezi kwa ugunduzi wa chanjo mpya inayoitwa tatu moja. Chanjo hii iko kwenye ule ukurasa wa 37 ni ya kuzuia magonjwa matatu, mdondo wa kuku, ndui ya kuku, mafua ya kuku na hiyo *dose* kichupa kimoja cha shilingi 6,800 kinatibu kuku 200. Kwa hiyo, mtu wa kawaida akinunua kichupa kimoja amemaliza kazi.

Kwa hiyo, naomba sana kwa kweli niwapongeze watafiti hawa walioweza kuleta chanjo hiyo na hivyo basi niseme nmtakaopatiwa vifaranga hao kwa wale wanawake wa Kilimanjaro hata hatutakuwa na uoga wa maradhi ya kuua hao kuku. Pia tutapata samadi ya kuku au inaitwa kinyesi cha kuku lakini mbolea ya kuku kwa ajili ya mashamba yetu na bustani zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme wazi, hakuna bajeti iliyopita hapa, huu ni muongo wangu wa tano bila kuomba vifaranga hivyo. Swali nimeuliza nikaambiwa nikanunue hivyo vifaranga kwa shilingi 2,500 bei ya ruzuku. Sasa sitaki wa kwangu, nataka Wizara ifanye *pilot scheme* mkoani Kilimanjari akina mama wale wafuge kwenye nyumba zao na pia iweze kufanana katika hali ya ufugaji wa kawaida. Nimechoka kusikia tunahesabiwa mifugo iliyo kwenye mashamba darasa, iliyo kwenye *ranch,* sasa inafanya nini huko? Yaani tutaje *figures* za nini? Niseme wazi kwamba kwa kweli...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Kengele ya kwanza eh?

MWENYEKITI: Kengele ni moja tu. Malizia sentensi yako.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Mwenyekiti, oh! Basi niulize tu swali moja. Nilikuwa na swali moja ili nisije kusema nashika shilingi nikakosa hata haya mambo ninayoomba. Bodi ya Wizara kwa umoja wao mwaka huu walitoa gawio la shilingi 348,940,989 ukilinganisha na trilioni 1.5 iliyotolewa mwaka wa 2019 ambayo ni anguko la asilimia 77. Ni nini kilichosababisha hiyo? Nilidhani sasa wangetoa gawio kubwa lakini wameshuka. Naomba watakapokuja kujibu nijibiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono tena. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Shally Raymond. Tunaendelea na Mheshimiwa Condester Sichalwe na mwisho tutakuwa na Mheshimiwa Godwin Kunambi.

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Kwanza kabisa nianze kuipongeza Serikali yetu na kuishukuru kwamba tunashukuru kwa kutusaidia kutujengea soko la Kimataifa la mifugo na mazao ambalo lipo pale Kakozi ambalo lipo mpakani kabisa kati ya nchi ya Tanzania na Zambia ni kilometa moja tu kutoka Tanzania kuingia Zambia. Soko hili liligharimu karibu, Serikali iliidhinisha pesa karibu bilioni 8.645 na mpaka sasa hivi tumepewa kiasi cha pesa bilioni 3.09. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe kwa kusema hivi kutokana kuwepo kwa soko hili la mifugo na mazao pale ni soko kubwa sana ambalo ninaamini kwamba Serikali wakati inaidhinisha kiwango hiki cha pesa na kutafuta mpango huu mzuri kwamba soko likajengwe pale ni mahsusi kabisa walizingatia kwamba ni kwa sababu tupo mpakani ina maana kwamba tutawahudumia Watanzania wa mikoa yote lakini pamoja na nchi zote ambazo zinatupaka kwenye lile eneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa basi, ombi langu kwa Serikali, iko sababu kubwa sana Wizara hii iweze kufika kwenye lile soko ambapo tunaendelea na ujenzi japokuwa tunashukuru limeshakamilika kwa kiasi fulani na tumeshaanza kufanyia kazi. Ifike ili tuweze kushauriana muweze kuona miundombinu namna gani tumejipanga katika kuboresha kwenye hilo eneo la ufugaji na eneo lingine ambalo litakuwa linahusu Wizara ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo kwa kuwa soko hili ni kubwa kwa kiwango hiki, naiomba Serikali ipo haja na sababu ambayo tunaweza tutakapoweka kiwanda cha kusindika nyama mahali pale inaweza ikatunufaisha sana. Itatunufaisha sana kwa sababu karibu mikoa yote ya Katavi, Rukwa na mikoa mingine iliyoko karibu

nasi ya Nyanda za Juu Kusini na mikoa mingine itaenda kwenda kutumia soko hili kwa sababu kua mnada kabisa wa kisasa ambao unatarajiwa kujengwa mahali pale, machinjio ya kisasa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wasiwasi wangu tunaweza, wakati tutakuwa tunafanya shughuli hizi za ufugaji tukawa tunawanufaisha wenzetu wa nchi za jirani. Sasa twende kuongeza thamani kwenye haya mazao ambayo yatatokana na ufugaji. Kwa hiyo, tukipata kiwanda cha kusindika nyama mahali pale, kuna soko kubwa sana la nyama kwenye nchi ya Kongo, Zambia na nchi zote ambazo ziko kwenye zile nchi za *SADC. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo liko andiko ambalo nimeziandikia baadhi ya Wizara hapa kuona kwamba kama tuko mpakani na soko lile liko pale mpakani kuna hati hati ya kwamba chochote tutakachokuwa tunazalisha pale kinaweza kikawa kinaenda nchi ya Zambia kinyume na utaratibu. Kwa hiyo, nimeiandikia andiko Wizara ya Fedha, Kilimo, Viwanda na Biashara, Uwekezaji, Mifugo yenyewe na Wizara ya Ulinzi na Usalama kwamba ninaiomba Serikali yangu Sikivu wkae wajadiliane waone kuna umuhimu wa sisi kutupatia geti pale ili tuweze kulinda mapato yote ambayo hayatapaswa kutoka pale kwa sababu soko litakapoanza kufanya vizuri na muingiliano wa watu utakuwa mwingi. Kwa sababu kuna njia zaidi ya 10 ambazo zinaizunguka lile soko ambazo zinatoka pale sokoni kuingia nchi ya Zambia na wakati mwingine huwa tuanzitumia hizo njia kupita ambapo wakati mwingine inakuwa ni kipindi cha Masika, barabara hazipitiki. Kwa hiyo, sitatamani kuona tunaenda kuzinufaisha nchi za wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niingie kwa kuwasemea watu wa Momba kwenye suala la mifugo. Kwenye sensa ambayo ilikuwa imefanyika mwaka 2012 tulionekana tulikuwa na ng'ombe 128,218, mbuzi 78,522, kondoo 10,071 na kuku 155,233 na kwa ajili ya muda pamoja na mifugo mingine. Kwa miaka ya karibuni ambayo imeongezeka sasa tumeonekana kuwa na ongezeko la mifugo hii karibu mara

tano kwa sababu tumepokea wenzetu wengi wa Jamii ya wafugaji, Wasukuma na Wamaasai ambao wamekuwepo maeneo yale. Sasa, kutokana na ongezeko hilo, kumeonekana uhitaji mkubwa sana wa kuhitaji malambo pamoja na majosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na lambo ambalo lilikuwa limeanza kujengwa kwenye Kata ya Mkomba ambapo Shirika hili la *Debit* kwenye mwaka 2016/2017 liliweza kutupatia kiwango cha pesa milioni 150 ambapo lambo hili lilikuwa linapaswa kukamilika kwa thamani ya milioni 800. Ombi langu kwa Serikali, kama mnaweza kufika, kupitia na kuliona lambo hili ili tuweze kuwasaidia wafugaji hawa wasiendelee kunung'unika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hayo yapo baadhi ya malambo ambayo yalikuwa yanatumika, lakini hayana ubora na yanahitaji kurekebishwa kwa sababu ongezeko la wafugaji limekuwa kubwa mara tano kama ambavyo nimesema. Naomba ukarabati wa malambo yafauatayo; lambo ambalo liko Kata ya Ivuna, Mkomba, Mpapa, Chitete, Msangano. Pia ombi langu kwamba kama tunaweza tukapata majosho kwenye Tarafa ya Ndalambo ambayo pia kwenye Bonde la Mto wa Kasinde pamoja na Tesa kuna ongezeko kubwa sana la watu hawa ambao ni wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo kwenye suala la ufugaji tunaomba kuboreshewa vifaa vya uimarishaji ili kwa ajili ya kuboresha koo za mifugo ambazo ziko pale. Hii imeonekana ni changamoto lakini na vifaa vya hawa Maafisa Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la uvuvi naomba niende tu moja kwa moja niziongelee changamoto ambazo zinawapata wavuvi ambao wako ndani ya Jiji la Momba. Wavuvi ambao wako ndani ya Jimbo la Momba wanaomba jambo moja kama sio matatu au manne. Tunaomba tupate *engine* za boti kwa sababu mpaka sasa tunaendelea kuvua kwa kutumia uvuvi wa kienyeji kwa

kutumia tu mitumbwi. Kwa hiyo, tukipata *engine* hizi tutaweza kutengeneza maboti ambayo angalau yanaweza yakawa ni ya kisasa.

Mheshimiwea Mwenyekiti, pia tunaomba kupata mikopo kwa wavuvi. Pia tunaomba kupata soko zuri ambalo liweze kutusaidia kuweza kukusanya mapato ndani ya halmashauri pia kukusanya mapato kwenye Serikali Kuu. Kwa sababu, pamoja na kwamba tunavua kienyeji, tunaweza kuvua kuanzia tani 7,000 mpaka tani 100,000 na pamoja na kuvua huku, tunalitosheleza soko la Mbeya Mjini, Tunduma, Vwawa na Mlowo. Kwa hiyo, tutakapokuwa tumepata hivi vifaa tunaweza kuzalisha tani kubwa na kwa wingi lakini pia tutaongeza mapato ndani ya halmashauri yetu pamoja na mapato kwa Taifa letu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Condester kwa mchango wako mzuri. Nilifikiria labda utaomba Waziri na Naibu waje kwa jinsi ambavyo umejipanga vizuri.

Tunamalizia na mchangiaji wetu wa mwisho, Mheshimiwa Godwin Kunambi. Hayupo?

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Godwin Kunambi ambaye hayupo alikuwa ndiyo mchangiaji wa mwisho. Lakini kabla hatujamaliza kazi zetu tuna wageni pale ambao ni wanafunzi 100 kutoka Chuo Cha Mipango hapa Mjini Dodoma. Tulikuwa nao muda wote huu wa jioni. Tunawakaribisha sana na tumefurahi kuwa nanyi katika kujifunza. Karibuni sana katika Bunge letu. Kila mara mnapohisi kwamba mnataka kujifunza. Naamini mmeona michango wa Wabunge wenu ambao wanawakilisha wananchi. Karibuni sana katika Bunge letu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia niwapongeze sana wachangiaji wote waliotumia muda wao kwa siku ya leo kwa kutoa michango katika Wizara hii ya mifugo na uvuvi.

Naamini Mheshimiwa Waziri na Naibu hapo wameyasikia mengi na kesho watatoa majibu mazuri ambayo naamini yatawafurahisha sana.

Baada ya kusema hayo basi kwa vile shughuli zetu zimeisha, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

(Saa 1.35 Jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa, Tarehe 28 Mei, 2021, Saa Tatu Asubuhi)